

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI

Kikao cha Nane – Tarehe 8 Februari, 2018

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulla Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

HATI ZA KWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE,
KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:**

Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevy ya mwaka 2016.

**MHE. ESTER M. MMASI (K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI
YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo Kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2017.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria Kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2017.

MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH (K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA):

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa Kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2017.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Katibu.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

MASWALI KWA WAZIRI MKUU

NAIBU SPIKA: Maswali kwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge, Kiongozi wa Upinzani Bungeni leo hayupo kwa hivyo tutaanza na Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri Mkuu swali hasa linalohusu pamba. Mheshimiwa Waziri Mkuu mwaka jana ulipata nafasi ya kuwaita Wakuu wa Mikoa inayolima pamba mara mbili, ukawapa maelekezo mazuri na maelekezo hayo wakayapeleka Mikoani mwao hadi Wilayani kwenda kufufua zao la pamba ambalo ni jambo jema sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu, wananchi wengi katika Mikoa hiyo, Mwanza, Simiyu na Mara, wameitikia sana wito huo na wamelima pamba nyingi sana.

Swali langu kwako Mheshimiwa Waziri Mkoo, Serikali imejipangaje endapo wanunuzi, kufuatana na pamba itakuwa nyingi sana watashindwa kuinunua pamba yote, kuwasaidia wananchi hawa ambao wameitikia wito wa Serikali wa kulima pamba, kuinusuru pamba ambayo itabaki bila kupata wanunuzi?

Swali la pili, kwa sababu ya muitikio huo kwa mfano, katika Wilaya ya Kwimba mwaka jana walitegemea kupata tani, kilo 6,000 mwaka huu ni mategemeo ni kilo milioni 30, lakini tatizo ni dawa ya viuwadudu mpaka sasa hivi hawajapeleka dawa. Mheshimiwa Waziri Mkoo wananchi kwa sababu, wameitikia wito wako, Serikali inasemaje kuhusu dawa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkoo majibu kwa maswali hayo.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kujibu swalii la Mheshimiwa Ndassa, lakini Mheshimiwa Ndassa ameuliza maswali mawili, sasa kama najibu yote basi Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu nijibu yote.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkoo, ameuliza mawili hatapewa maswali ya nyongeza kwa hiyo, yote unaweza kuyajibu sasa.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Ndassa, Mbunge wa Kwimba, kama ifuatavyo:-

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mbunge wa Sumve.

WAZIRI MKUU: Mbunge wa Sumve, samahani Mheshimiwa Ndassa. Mheshimiwa Ndassa, Mbunge wa Sumve kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali tunaendelea na kusimamia kuyafufua kikamilifu mazao makuu matano kwa kuanzia, mazao hayo pamba ikiwepo

pamoja na mazao mengine kama vile korosho, chai, tumbaku na kahawa. Ni mazao ambayo tumeyapa nafasi kubwa kwa sasa kufuatia historia yake kuwa ndiyo mazao makuu ambayo yalikuwa yanatuongeza pato kubwa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazao haya wakulima kadhaa wamepunguza uzalishaji kwa sababu mbalimbali. Moja ni kukosekana kwa usimamizi thabiti wa kilimo cha mazao haya ikiwemo na pamba. Kwa hiyo, kuwaita Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, Wenyevitii wa Halmashauri pamoja na Wakurugenzi ni kuwapa mkakati wa Serikali wa kwenda kusimamia mazao haya ili sasa mkulima anapolima apate kushauriwa kitaalam kuto ka ngazi ya awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba mwaka huu baada ya hamasa na kuwaita viongozi wa Serikali na mimi nataka nitumile nafasi hili kuwapongeza sana Wakuu wa Mikoa wa Mikoa yote inayolima pamba, Wakuu wa Wilaya, maendeleo haya tayari yameonesha kuwa, wamefanya kazi kufuatoa maelekezo yetu na mwaka huu tunatarajia kuzalisha sana. Sasa Serikali imajipangaje kununua pamba yote au kuhamasisha wanunuzi kununua pamba yote kama pamba itabaki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme tu kwamba mionganoni mwa mikakati ambayo tumeiweka, pamoja na kulima kitaalamu, lakini kuihudumia ni pamoja na masoko yake. Kwa hiyo, katika tarehe 15 na tarehe 17 mwenyewe nitakuwa Mkoani Mwanza, nakutana na wafanyabiashara wote wa pamba nchini, wanaofanya kazi ya kusokota nyuzi, wanaofanya kazi ya kukamua mafuta ya pamba, lakini hata wale wanaochambua pamba na yejote ambaye huwa ananunua pamba, ili tuweze kuweka mpango endelevu wa kununua zao hili la pamba msimu huu na misimu ijayo, ili tuweze kuza pamba yote na kuweza kuwatia hamasa wakulima waweze kununua zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mpango huo bado pia tumetoka nje ya nchi kuona kama tunaweza kupata masoko kutoka nje ya nchi. Wizara ya Kilimo pamoja

na taasisi inayoshughulikia masoko (*Commodity Exchange Department*) yenewe pia inafanya mawasiliano na mataifa ya nje kuona kama kuna taifa lolote ambalo linaweza kununua pamba kwa kiasi kikubwa ili tujue msimu huu tunaweza kuuza pamba kwa kiasi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana Mheshimiwa Mbunge wa Kishapu alitoa hoja binafsi ya kuhusu pamba, ametoa mawazo mengi, mawazo yale yote tutayazungumza kwenye kikao chetu cha wadau siku ya tarehe 15 au 16 nitakapokuwa Mwanza ili sasa yote haya na ushauri wenu ambao mtakuwa mnautoa tuweze kuhakikisha kwamba pamba yote inachukuliwa. Sasa kama pamba itabaki tutaona kwa sababu tayari hamasa kwa wanunuzi ni kubwa na ya kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la dawa wakati huu ambao pia kilimo kinaendelea dawa ni sehemu ya mahitaji ya kilimo cha pamba. Nimeona wiki moja iliyopita, Mkurugenzi wa Bodi ya Pamba akipokea dawa zaidi ya chupa milioni moja na nilimsikia akisema kwamba, wameleta mzigo wa awali na mzigo mwingine unakuja zaidi ya chupa milioni mbili ama tatu. Kwa hiyo, tunaamini dawa zinakuja na ni jukumu la bodi na tumeigiza Wizara ihakikishe wakulima hawa wanapolima wanapata pembejeo zote, mbolea, dawa za maji na kama ni dawa za kupuliza, zote hizo lazima Wizara sasa iweze kuratibu ili wakulima wasipoteze nguvu zao, huo ndiyo mkakati wa Serikali. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Devotha Mathew Minja.

MHE. DEVOTHA M. MINJA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, hivi karibuni tulikuwa kwenye uchaguzi mdogo katika Kata takribani 43. Uchaguzi ule uligubikwa na hila, vitisho, manyanyaso, hali ambayo ilisababisha uchaguzi ule kutokuonekana kuwa ni wa haki na huru. Katika hali isiyokuwa ya kawaida, wagombea walioshinda katika baadhi ya Kata Tume ya Uchaguzi

iliwatangaza walioshindwa badala ya watu walioshinda. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, iko mifano katika baadhi ya Kata chache tu nitakazokueleza, Kata ya Sofi - Malinyi, CHADEMA ilipata kura 1,908, CCM ilipata kura 1,878. Kata ya Siuyu - Singida CHADEMA ilipata kura 1,358 na CCM ilipata kura 1,304.

Je, ni sera ya Serikali kuwanyang'anya ushindi watu walioshinda kihalali na kuwatangaza waishindwa? (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa waziri Mkuu majibu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Devotha Minja, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Morogoro, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka niseme sitarajji kama Tume inafanya kazi ya kutangaza walioshindwa wakawaacha walioshinda kuwa ndio washindi. (*Makof*)

Kwa masuala haya ya Tume Serikali imeweaka utaratibu, tumeunda chombo kinachoshughulikia chaguzi zote nchini, Tume ya Uchaguzi, lakini chombo kingine kule kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa ajili ya chaguzi za Serikali za Mitaa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na vyombo hivi ambavyo tumeviunda, lakini tunazo sheria pia zinazosimamia uchaguzi na zote hizi zinasimamiwa na Tume, sheria hizi zote zinaipa mamlaka Tume kukutana na vyama kuweka taratibu za chaguzi zake zote. Moja kati ya taratibu hizo pale ambako inaonekana mionganii mwa vyama shiriki vya uchaguzi kutoridhika na matokeo, iko sheria inayowaruhusu, inayotoa muda na ni muda wa miezi mitatu kama sijakosea ya kukata rufaa dhidi ya hizo namba ulizoisoma, mimi sina uhakika nazo. (*Makof*)

Sasa Mheshimiwa Mbunge kama una uhakika na

takwimu ulizozisoma kwamba, hao uliowaona wenye namba nyingi ndio walioshinda lakini ametangazwa mwagine bado unayo fursa ya kukata rufaa kwa mujibu wa sheria za Tume. (*Makofi*)

Kwa hiyo, nikushauri kufuata chombo chetu na kwa kuwa sheria zipo na wewe pia unayo fursa ya kufuata sheria ile ili kupata haki yako ya msingi. Kwa hiyo, huo ndio utaratibu wa Serikali. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, sasa mtakumbuka Mheshimiwa Spika, alishafanya utaratibu mzuri kwamba, kwa kuwa, majina yanakuwa ni mengi, Waheshimiwa Wabunge wanaouliza maswali kwa Waziri Mkuu watauliza halafu..., yaani wanaouliza swali halafu hawapewi fursa nyingine isipokuwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni. Leo, Mheshimiwa Ndassa ameshauliza maswali mawili.

Kwa hiyo, tunaendelea na Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, swali kwa Waziri Mkuu.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nimuulize Mheshimiwa Waziri Mkuu maswali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na migogoro inayoendelea ya mipaka katika mapori ya Hifadhi za Misitu katika maeneo mbalimbali nchini, baadhi ya migogoro hiyo imo katika vijiji ambavyo vimesajiliwa na kwa kuwa kulikuwa na agizo la Serikali la kupima mipaka yote ya hifadhi zetu ifikapo tarehe 31 Desemba, 2017.

Je, Serikali imeweka utaratibu gani na mikakati gani ya kumaliza migogoro iliyopo hasa kwa kuwa wananchi wanahitaji maeneo zaidi kwa ajili ya shughuli zao zikiwemo kilimo na mifugo?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Waziri Mkuu. Je, pamoja na kazi zako nyingi unaweza kupata nafasi

ya kuja Urambo ukajionea migogoro hai katika Kata ya Nsenda, Runyeta, Uyumbu, Tebela na Ukondamoyo? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu, maswali yameulizwa mawili, utajibu swali la kwanza pekee.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margaret Sitta, Mbunge wa Urambo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye misitu ya hifadhi yote nchini kuititia Wizara ya Maliasili na Utalii, lakini tunayo misitu iliyoko chini ya Mamlaka za Hal mashauri za Wilaya, lakini tunayo misitu ambayo iko chini ya Mamlaka za Vijiji kulingana na mahitaji yao. Misitu hii yote Serikali tuliiitolea maelekezo baada ya kugundua kwamba tuna migogoro mingi kati ya wananchi walioko kwenye vijiji jirani na misitu yetu iliyohifadhiwa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, misitu yote ya Serikali Kuu imehifadhiwa kisheria, ramani ziko, michoro, mipaka na kila kitu inaonekana na ndio eneo kubwa ambalo limeonekana kuwa na migogoro mingi. Misitu hii tulitoa maagizo kwa Wizara kuiwekea mipaka ya vizingi (*beacon*) kwenye maeneo yote yanayozunguka misitu hiyo, ili kuweka alama itakayopunguza migogoro ya kuingiliana kati ya wananchi walioko kwenye vijiji na wahifadhi wetu kwenye maeneo ya hifadhi za misitu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua kabisa kwamba wanapoendelea na zoezi hili inaweza kujitokeza, wanapoweka mipaka kikajikuta kijiji kiko ndani ya mipaka, kuwa labda kiko ndani ya hifadhi, kunaweza pia kukatokea kutolewana kati ya wanavijiji na wenye mamlaka ya hifadhi ile. Tuliwasih wanakijiji wakati zoezi hili linaendelea na hata kama kijiji kitajikuta kimezungukwa na hizo *beacon*, hizo alama, wanakijiji watulie ili kazi ya awali ikamilike na pale kwenye mgogoro tutarudi tena kuja kuuangalia mgogoro huo nakufanya tathmini ya kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliiagia Wizara ya Maliasili wanapofanya kazi hii ya kuweka vizingi lazima washirikishe Mamlaka za Halmashauri husika, Mamlaka iliyoko kwenye Kijiji husika na wao washiriki katika uwekaji huu ili kuondoa migogoro isiyokuwa ya lazima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro hii ambayo inaendelea kwenye maeneo tullyopima bado nirudie tena, kwa kuwa kazi ya upimaji imekamilika muda mfupi uliopita tarehe 30 Desemba, sasa ni jukumu la Wizara kurudi kwenye maeneo yote yenye migogoro waungane na Halmashauri za Wilaya ili waweze kutoa majibu kwa wananchi na kama kuna kijiji kiko ndani kiangaliwe kama kijiji hicho kimesajiwu na Serikali, kama kimesajiliwa sasa tutafanya tathmini kuona mahitaji ya Serikali kwa kijiji chenyewe au kuendelea kuwa na hifadhi kulingana na malengo ya hifadhi hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, najua Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Margaret Sitta wewe unatoka Urambo na mimi nilikuwa Mkuu wa Wilaya pale, najua mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Urambo iliyozungukwa na misitu kwa zaidi ya asilimia 60.

Kwa hiyo, Wizara bado itakuja Urambo hata pale Kaliua jirani ambako kuna misitu mikubwa inayokwenda mpaka kule Kahama na Shinyanga ili wafanye mapitio kwenye mipaka yake, na kwa kufanya hilo sasa hii migogoro yote itakwisha.

Kwa hiyo, hakuna sababu ya kuendelea kugombana wasubiri kwanza taratibu za maliasili zikamilike, waweke mipaka halafu tuje tufanya tathmini ya vijiji vilivyoingia kwenye mipaka, baada ya hapo zoezi linalofuata sasa ni kutoa elimu ya wanavijiji walioko jirani kutoingia na wanapoingia wafuate utaratibu gani, naamini tukifuata hivyo wote tutaweza kuondoa migogoro isiyokuwa muhimu. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka swali kwa Waziri Mkuu.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, baada ya zao la korosho kufanya vizuri sana kwenye soko la Kimataifa Serikali msimu uliopita ilikuja na tamko kwamba pembejeo la zao hilo litatolewa bure. Na kwa sababu tamko lilitolewa katikati ya msimu Bodi ya Korosho wameshindwa kulitekeleza ipasavyo, jambo hili lilipelekea pembejeo za zao la korosho kuja zimechelewa, mbolea zilikuja zikauzwa zaidi ya mara mbili ya bei iliyyotarajiwa na tulipofika kwenye msimu sasa wa kuuza korosho vifungashie vikawa ni vya shida jambo lilipelekea korosho nyingi zikashindwa kufika mnadani kwa wakati.

Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu unawaambia nini wakulima wa korosho kwamba msimu ujao changamoto hizi zitakuwa zimetatuliwa kwa kiwango gani?

Vilevile tumepeata taarifa kwamba korosho zetu zilizokwenda Vietnam zimekwenda na mawe. Mheshimiwa Waziri Mkuu, unataka kuwaambia nini wakulima wa korosho ambao kwa uadilifu mkubwa nina hakika hawakufanya dhambi hii? Ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu utajibu swali moja linalohusu pembejeo.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Kuchauka, Mbunge wa Liwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kuchauka anataka kujua mfumo wa utoaji pembejeo kwenye mazao na hasa zao la korosho ambalo msimu uliopita pembejeo aina ya *sulphur* ilitolewa bure kwa wakulima wote. Kwa miaka mingi zao hili lilipoteza mwelekeo na halikuwa linalimwa na watu walilacha mikorosho porini. Sasa Serikali katika mipango yake ilikuwa ni kutafuta hamasa ya kulirudisha ili wakulima waweze kulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kati ya njia ya kuhamasisha wakulima Serikali kwa mwaka ule msimu huo wa kilimo, msimu uliopita ilitoa dawa ya *sulphur* bure kwa wakulima wote. Jambo hili kwa msimu huu ambao sasa tunakwenda nao kila mkulima sasa anatakiwa kujivekea akiba yake ili aweze kujinunulia pembejeo hiyo ya *sulphur* kwa ajili ya msimu ujao unaokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zote ambazo zimejitekeza wakati wa utekelezaji wa zoezi hili kwa uharaka, labda kwa kukosa umakini wa uongozi, moja kwanza tulichukua hatua ya kuvunja bodi na kuweka bodi mpya. Kwa hiyo, inawezekana moja ya changamoto iliyosababisha bodi hii isifanye kazi yake vizuri kwa sababu ilikuwa ngeni.

Lakini mbili, tulikuwa tunaunda tena na kusimamia ushirika na uaminifu wa uendeshaji wa zao hili kwa hiyo, maeneo mengi tulifanya mabadiliko kidogo ya viongozi wake ili kuweka viongozi waaminifu waweze kuratibu na ilikuwa katikati ya msimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru kwamba viongozi waliopo sasa wameweza kusimamia vizuri zao la korosho kwenye ushirika kwenye vijiji, ofisi za Wilaya mpaka Wakuu wa Mikoa na hatimae tumeypata mafanikio makubwa sana. Kwa hiyo, huo ndio mpango mkakati wa Serikali wa kupata mafaniko kwenye mazao haya na ndiyo ambao tunaupeleka kwenye mazao mengine pamba, chai, tumbaku na kahawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, msimu huu bodi imeanza mapema kuratibu kupata *sulphurna* tayari juzi niliwaita kwa bahati nzuri kutaka kujua utaratibu wao wa kupata *sulphur* wameeleza, *sulphurhii* itakapokuja basi wananchi watakuwa wanunuua kulingana na mahitaji yao ili waweze kupulizia kwenye mikorosho yao, kama kutakuwa na aina yoyote ya mahitaji kwenye mtiririko mzima wa kufikia hatua ya kuuza zao la korosho, ikiwemo ununuzi wa magunia kuandaa maghala, lakini pia kuhamasisha wanunuuzi, kazi hiyo itakuwa inafanywa na bodi na ninaamini watakuwa wamejipanga

vizuri ili kupata mafanikio makubwa zaidi msimu ujao wa kilimo. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Buberwa Kamala swali kwa Waziri Mkuu.

MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA: Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa kumekuwepo na migogoro ya muda mrefu katika Ranchi za Taifa pamoja na vijiji vinavyozunguka *ranch* hizo, na kuwa Serikali iliunda Kamati ya kupitia migogoro hiyo na kuja na mapendekezo kwa Waheshimiwa Wabunge ili waweze kutoa maoni yao kwa nia ya kupata ufumbuzi wa kudumu.

Je, ni lini taarifa hiyo italetwa hapa Bungeni ili Waheshimiwa Wabunge tuweze kutoa maoni yetu ya kupata ufumbuzi wa kudumu? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Kamala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kamala amezungumzia uwepo wa migogoro ya wafugaji na maeneo ya malisho ikiwemo mashamba yetu makubwa ya kufugia mifugo yetu *NARCO* yaliyoko nchini kote na hasa kule Wilayani Misenyi kwa Mheshimiwa Mbunge. Nakumbuka nimefanya ziara mpaka Misenyi tumekuta mgogoro mkubwa wa wafugaji kukosa maeneo na huku tukiwa na *NARCO* ambazo hazina mifugo kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilitoa utaratibu wa mashamba yote yaliyohifadhiwa kwa ajili ya malisho yaliyokuwa yanashikiliwa na *NARCO* chini ya Wizara ya Kilimo, huku wananchi wengi wana mifugo mingi hawana maeneo ya kufugia na maeneo yale yako wazi, tulitoa maelekezo kwamba maeneo yote ya *NARCO* yapimwe kwenye *blocks*, kwenye vieneo ambavyo vitawezesha kujua idadi ya ng'ombe halifu tuwaruhusu wafugaji waende kufugia

ng'ombe zao huko badala ya kubaki vijjini ambako tena kuna migogoro kati ya wakulima na wafugaji. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua Bunge, Wizara iliunda Tume kufanya uhakiki wa maeneo yale na *blocks* zile kwa kutambua nani anamiliki *block* hiyo na je, ana mifugo hiyo na alipewa kihalali au vinginevyo, ili tuweze kujua tuna maeneo mangapi yaliyo wazi ili wafugaji wetu wakubwa wote tuwapeleke kwenye maeneo haya na Serikali tunataka maeneo haya tuyahudumie kwa kushirikiana na Halmashauri za maeneo na Wizara yenewe kwa kuchimba malambo, majosho, lakini Maafisa Mifugo wetu sasa wawe wanajua mahali pa kwenda kwa ajili ya tiba ya mifugo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili ni nzuri na tunaendelea nalo sasa ametaka kujua lini taarifa tunaileta Bungeni. Kwa kuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi amenisikia ni jukumu lake kukamilisha sasa taarifa hiyo ili iletwe Bungeni kama ilikuwa inatakiwakuja Bungeni ili Waheshimiwa Wabunge na wafugaji wote sasa wapate dira ya Serikali na mwelekeo wa Serikali wa namna ya kufuga mifugo hii ili wapate ufugaji endelevu kwa ajili ya kuwaletea tija wafugaji wenyewe na Serikali pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa zaidi ni kuondoa ile migogoro kati ya wakulima na wafugaji ambayo inaendelea huku kwenye ngazi ya vijiji. Wizara imeweka utaratibu na utaratibu ule ukifuatwa hatutakuwa na migogoro hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge taarifa zitakuja na Waheshimiwa Wabunge wote taarifa tutawaletea kwa utaratibu ambao umewekwa kuanzia awali na Wizara husika. Ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu unaweza kwenda kukaa sasa. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali kwa Waziri Mkuu umekwisha kwa hiyo tutaendelea na maswali ya kawaida. Ahsanteni sana. Katibu. (*Makof*)

NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Maswali ya kawaida, tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini, sasa aulize swalii lake.

Na. 99

Mradi wa Maji Haydom

MHE. FLATEI G. MASSAY aliuliza:-

Mradi wa Maji wa Hydom umechukua muda mrefu kumalizika na wananchi wanasubiri maji huku muda wa mkataba na mkandarasi ukiwa umeisha.

Je, kwa nini Serikali isimfukuze mkandarasi huyo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa maji wa Mji wa Haydom ulianza kutekelezwa mwaka 2014 lakini kutokana na changamoto ya fedha utekelezaji ulisimama mwaka 2015/2016. Hata hivyo, pamoja na mkataba wa mkandarasi kuisha muda wake, napenda nimsifu na kumshukuru Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, kwa kushirikiana na Mkuu wa Wilaya Mheshimiwa Chelestino Mofuga na Mkurugenzi wa Halmashauri Ndugu Hudson Kamoga kwa kufanya kikao kati yao na mkandarasi chini ya Uenyekiti wa Katibu Mkuu wa Wizara ya maji Profesa Kitila Mkumbo tarehe 2/11/2017, ambapo muafaka wa mkandarasi kuendelea kutekeleza

mradi huo unaotarajiwa kukamilika mwezi Aprili, 2018 ulipatikana. Kwa maana hiyo, wakazi wa vijiji vya Haydom na Ng'wandakw vinyavounda Mji wa Haydom wenye wakazi 17,406 wataanza kupata maji baada ya mradi huo kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyongeza yangu kuhusu taarifa tulizozipata usiku wa leo zinazohusu changamoto za Mkandarasi zinazohitaji utatuzi wa haraka namwomba Mheshimiwa Flatei Massay na mwenzangu Naibu Waziri wa Maji tukutane hapa Bungeni baada ya kipindi cha asubuhi ili tupate utatuzi wa haraka wa mradi huo. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Flatei Massay swali la nyongeza.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kueleza masikitiko yangu kuhusiana na mradi huu, mwaka 2014 alikuja Katibu Mkuu wa Chama akadanganywa kuhusu mradi huu. Akaja Waziri Kamwelwe Januari mwaka jana akadanganywa kuhusu mradi huu, mimi nimekuja Ofisi na hao uliowasema mwaka jana Desemba mradi ulikuwa uishe tukadanganywa tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, nahitaji muda gani na mara ngapi kuja hapa kuuliza maswali haya na uwongo wa kudanganywa namna hii, wananchi kule umetaja 17,000 hawana maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa miradi ya maji katika Jimbo la Mbulu Vijiji iko mingi, nayo hakuna muda ambao umetajwa wa kumalizika na mikataba imeisha, na mimi kule sina fundi kabisa au Mhandisi wa Maji ndani ya Halmashauri yangu.

Je, unanisaidia pamoja na kwamba tutakaa baadae kuhusu ya watumishi katika Wizara hii au katika sekta ya maji?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

MHE. JOSEPH J. KAKUNDA - NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema wakati ninajibu swalii la msingi kwamba mradi huu kimsingi umeshatekelezeza kwa asilimia 90 bado asilimia 10 tu, zikazuka changamoto ambazo zilzungumzwa kwenye kikao, zikaonekana kwamba zinatatulika, lakini usiku wa leo nimepata mwendelezo unaohusu changamoto za ziada ambazo tunahitaji kuzitatua baada tu ya kikao hiki.

Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wote wa Haydom na Jimbo la Mbulu Vijijini kwamba mradi huu kama tutatatua hizi changamoto ambazo amekumbana nazo mkandarasi ninaamini ndani ya wiki mbili hadi tatu hii asilimia 10 itakuwa imekamilishwa, ndio maana tumesema ifikapo mwezi Aprili, tutakuwa tumekamilisha mradi huu.

Swali la pili, kuhusu watumishi, napenda nimwakikishie ndugu yangu Mheshimiwa Flatei kwamba tunaiangalia Wilaya ya Mbulu kwa ujumla na Halmashauri yake ya Mbulu Vijijini kwa uangalifu mkubwa kutokana na mazingira ya eneo lenyewe na *physiology* ya eneo lenyewe la Wilaya ambalo nimefika ni juu na tambarare zimechanganyika na kwa hiyo tutampatia Mhandisi wa Maji hivi karibuni. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mashimba Ndaki swalii la nyongeza.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo Mradi wa Maji wa Haydom, Mradi wa Maji wa Chujio Wilaya ya Maswa na wenyewe umekuwa wa muda mrefu sana. Mkandarasi amepewa *extension* ya kwanza hakumaliza, akapewa ya pili, hakumaliza akapewa ya tatu hakumaliza.

Je, Serikali inaonaje kumwondoa huyu mkandarasi na kuweka Mkandarasi mwenye uwezo zaidi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji majibu.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa Mkandarasi yule amechukua muda mrefu katika utekelezaji wa mradi, lakini mradi ule uliharibiwa tangu wakati wa usanifu wake. Walisanifu kujenga chujio sehemu ambayo siyo yenye, baadaye walivyoingia katika eneo la mradi ikabidi tena wakae kubadilisha, lakini hali m ulipofikia kwa sasa amebakisha sehemu ndogo sana, ameagiza vifaa kutoka nje ya nchi, hatuoni kwamba kwa sasa itakuwa ni busara kumsimamisha kwa sababu vile vifaa vikishafika ni kazi ya kufunga tu na mradi unaanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, na nishukuru hata bwawa ambalo litahudumia lile chujio sasa hivi mvua zimenesha maji yameja. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge ninakuomba uwe na subira baada ya muda kidogo tu huo mradi utaanza kufanya kazi. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lucia Mlowe swali la nyongeza.

MHE. LUCIA M. MLOWE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniona.

Kwa kuwa, katika Halmashauri ya Njombe Mji kuna tatizo kubwa la maji na Serikali imekuwa ikiahidi kuwasaidia wananchi kutatua tatizo hili la maji kupitia mradi wa Hagafilo lakini hakuna dalili yoyote.

Je, ni lini sasa Serikali itaanza kutekeleza mradi huo ambaao imekuwa ikiwahaidi wananchi siku zote? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji majibu.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Njombe ni mionganoni wa Miji 17 itakayofaidika na mkopo kutoka Serikali ya India wa dola milioni 500, kwa hiyo nikukuakikishie pamoja na wananchi wa Njombe kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeshajipanga tayari, mwaka wa fedha unaokuja tutasaini mikataba na kuekeleza mradi wa kuchukua maji kutoka mto Hagafileo na kuhakikisha kwamba Mji wa Njombe sasa unakuwa na maji.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Deo Sanga, swali la nyongeza.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi nami niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa nia ya Serikali ni kumtua mama ndoo, kumsogezea huduma jirani ili kuweza kupata maji hasa vijijini na mijini; na kwa kuwa kuna miradi 17 mikubwa ya maji hasa fedha za kutoka India ambazo zilipitishwa kwenye bajeti hapa; na kwa kuwa Mji wa Makambako umekuwa ni mionganoni mwa miji ya kupata mradi huu mkubwa wa maji katika miji ile 17.

Je, Serikali inawaambia nini wananchi wangu wa Mji wa Makambako ili waweze kupata maji, ni lini miradi hii itaanaza?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji majibu.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Deo Sanga kwa kufuatilia mradi huu wa mkopo wa dola milioni 500 kutoka Serikali ya India. Hata jana tulizungumza naye na alinituma niende kwa Waziri wa Fedha na majibu niliyopewa na Waziri wa Fedha ni haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu sasa zinakamilishwa ili tuweze kusaini mkataba wa fedha (*financial*

agreement) na baada kukamilisha kusaini basi moja kwa moja Wizara ya Maji na Umwagiliaji itaanza kutangaza tender kumalizia usanifu ili pamoja na hiyo miji 17 bwawa lako la Tagamenda litajengwa ili Mji wa Makambako upate huduma ya maji.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maji, Wabunge bado wamesimama hapo, kila mtu mahali kwake kuna taabu. Naomba uangalie Wabunge waliosimama tafadhali ili ushughulike na matatizo yaliyoko kwenye Majimbo yao.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda, sasa aulize swali lake.

Na. 100

Uchafuzi wa Mazingira katika Mto Rubana

MHE. BONIPHACE M. GETERE aliuza:-

Je, ni kwa nini mikakati ya dhati ya Serikali katika kunusuru na kuzuia uchafuzi wa mazingira ya Mto Rubana ambao unaingiza maji yake katika Ziwa Victoria na ni chanzo kikubwa cha maji katika Vijiji vya Tingirima, Kyandege, Mugeta, Mariwanda, Sarakwa, Kihumbu na Hunyari katika Jimbo la Bunda.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano na Mazingira, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MUUNGANO NA MAZINGIRA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), napenda kujibu swali la Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mto Rubana ulioko katika Halmashauri ya Wilaya ya Bunda ni chanzo muhimu cha maji kwa wananchi wa vijiji vilivyoko maeneo unakopita mto na pia kwa shughuli za uhifadhi. Maji ya mto huu hutumiwa na wananchi kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, kunyweshea mifugo, kilimo na uvuvi. Aidha, maji ya Mto Rubana hutumiwa na wanyamaporι kutoka Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na Pori la akiba la Grumeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa Mto Rubana kama chanzo cha maji na shughuli za uhifadhi, Serikali imechukua hatu zifuatazo ili kunusuru na kuzuia uchafuzi na uharibifu wa mazingira katika mto huo:

(i) Kuziagiza Halmashauri za Serengeti, Bunda na Bunda Mjini kuzingatia na kutekeleza kikamilifu Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji wa mwaka 2006 na Mkakati wa Hatua za Haraka za kuhifadhi Mazingira ya Bahari, Ukanda wa Pwani, Maziwa, Mito na Mabwawa wa mwaka 2008 katika maeneo yao ili kuzuia uharibifu wa Mto Rubana.

(ii) Kuendelea kutoa elimu ya uhifadhi wa mazingira kwa viongozi wa Halmashauri za vijiji na wananchi wote wa Kata za Hunyari, na Mugeta kuzingatia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Namba 20 ya mwaka 2004, Sheria ya Misitu Namba 14 ya mwaka 2002 inayozuia ukataji miti ovyo na Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamaporι Namba 5 ya mwaka 2009.

(iii) Kufanya doria za mara kwa mara na kukamata wanaokaidi na kukiuka sheria na kusababisha uharibifu wa mazingira ya mto kwa kukata miti ovyo na uchomaji wa mkaa.

(iv) Kuendelea kujenga na kuboresha miundombinu ya kunyweshea mifugo ili kuzuia wananchi kunyweshea mifugo kwenye mto.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa wito kwa wadau

wote ikiwemo viongozi katika ngazi ya Halmashauri, Waheshimiwa Wabunge, viongozi wa Kata na Vijiji na wananchi wote katika maeneo hayo kushirikiana katika kutekeleza mikakati ya Serikali ili jitihada za kunusuru Mto Rubana na kuzuia uchafuzi zifanikiwe kikamilifu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere swalii la nyongeza.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya ndugu yangu Kangi Lugola nuru ya wanyonge, Jimbo la Mwibara, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa chanzo kikubwa cha maji ya binadamu, mifugo na wanyamapori katika eneo hili la vijiji tisa ni Mto Rubana, na kwa kuwa hakuna chanzo kingine mbadala kwa wananchi wa maeneo hayo, na kwa kuwa ardhi haiongezeki na watu wanaongezeka na mifugo inaongezeka. Je, ni lini sasa Serikali kwa kupitia Wizara yake ya Mazingira itapeleka mradi mkubwa wa maji katika vijiji hivi viwili ili kuviokoa na tatizo la maji?

Swali la pili, kwa kuwa Mto Rubana, ndiyo mpaka kati ya vijiji tisa vinavyopakana na pori hilo la akiba, la Grumeti. Je, ni lini agizo lako ulilolitoa miezi miwili iliyopita, ulipotembelea maeneo hayo kwamba mita 500 za eneo la wazi kutoka eneo la mpaka kwenda vijijini na mita 500 kutoka eneo la mpaka kwenda porini wataweka *beacon*?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,
MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana Mheshimiwa Getere wapiga kura wako wanakuwa Tingatinga la maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiri kwamba baada ya uteuzi wangu nilitembelea Jimbo la Mheshimiwa Mbunge na kuweza kufanya mikutano miwili Maliwanda pamoja na Hunyari, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali yetu tayari kwa kuzingatia kwamba wananchi walikuwa wanatumia maji ya Mto Rubana kunyweshea mifugo, uvuvi pamoja na matumizi ya nyumbani, tayari katika Kijiji cha Kyandege, Kijiji cha Mugeta na Kijiji cha Mariwanda Serikali tulishawajengea malambo ya kunyweshea mifugo na mabirika ya kunyweshea mifugo yanafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna taasisi inaitwa *Rubana Corridor Environmental Development Strategy* wako mbioni na wamekamilisha mchoro wa kujenga bwawa moja kubwa katika Kijiji cha Kihumbu. Pia Halmashauri ya Wilaya Bunda, katika mwaka wa fedha wa 2017/2018 wametenga jumla ya milioni 30 kukarabati lambo la Kihumbu na pia *Foundation for Civil Society* kushirikiana na asasi niliyoitaja mwanzo, tayari wanataka kujenga visima viwili vya maji katika Kijiji cha Kihumbu, ikiwa ni pamoja na kuongeza lambo moja kubwa kwa ajili ya kunyweshea mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha uvuvi uliofanyika Rubana usiendelee na kuchafua mazingira, tayari *Foundation for Civil Society* wameendesha mafunzo ya vijiji vinne kwa ufugaji wa nyuki na sasa watasambaza mizinga 100 kwa ajili ya kuwafanya wananchi wasiende kuchafua mto.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili kuhusu changamoto ya mita 500. Ni kweli kabisa Sheria namba 5 ya mwaka 2009 kifungu cha 74 kinazungumzia kuweka *buffer zone* ya mita 500 kwenda kwa wananchi. Nimhakikishie Mbunge tayari Ofisi ya Makamu wa Rais, imeshawasiliana na Mkurugenzi Mkuu wa *TAWA* pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii, kwamba wanashughulikia masuala ya *beacon*. Pia nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba *beacon* zinazohusu wanyama na wanadamu ni *beacon* ambazo siyo endelevu, leo utaweka *beacon* ya mita 500 kwa wananchi,

na hawa wanyama wao hawajui kama kuna *beacon* ya mita 500, baadae watasogea tena kwenye mita 500, baadae wananchi watasema wanyama wamesogea tuweke tena *beacon* za mita 500, mwishowe vijiji vyote vitaisha kwa kuwa *beacon* ya hifadhi. Hiyo ndiyo changamoto ili yopo. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hawa Subira Bananga Mwaifunga, swali la nyongeza.

MHE. HAWA S. MWAI FUNGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru.

Tatizo liliopo katika Jimbo la Bunda linafanana kabisa na tatizo liliopo katika Jimbo la Tabora Manispaa, chanzo cha maji cha Mto Gombe kinasumbuliwa sana na tatizo la mazingira katika eneo hilo.

Je, Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira ina mpango gani wa kusaidia wananchi wale kunusuru afya zao za maji ambayo wanatumia wakati tukisubiri maji ya Ziwa Victoria?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,
MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba nchi yetu ina changamoto ya uharibifu na uchafuzi wa mazingira, kwenye vyanzo vingi vya maji. Ndiyo maana mkakati mmojawapo wa kunusuru vyanzo vya maji nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa January Makamba alishatoa agizo kwa Halmashauri zote nchini kuhakikisha wanaorodhesha vyanzo vyote vya maji katika maeneo yao, vikiambatana na changamoto ambazo zinakabili vyanzo hivyo ili Serikali ijipange katika kunusuru vyanzo hivyo, hili la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, katika llani hii ya CCM

ambayo naamini Mheshimiwa Hawa Mwaifunga anaiamini na kuisimamia itekelezwe katika maeneo yake, katika ukurasa wa 212 mpaka 213 llani hii inaagiza Halmashauri zote katika nchi yetu, kuhakikisha kila mwaka wanapanda miti ya kuhifadhi mazingira na kwenye vyanzo vya maji isiyopungua milioni 1.5.

Hivyo kupitia swali hili, naziagiza Halmashauri zote nchini, zitekeleze llani hii na baada ya Bunge hili wajue wana deni ambalo dawa ya deni ni kulipa nitaenda kukagua kuona sasa miaka miwili kwamba wana miti si chini ya milioni tatu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Alex Gashaza swali la nyongeza.

MHE. ALEX R. GASHAZA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa uchafuzi wa mazingira ni pamoja na uchomaji misitu hovyo unaosababisha uzalishaji hewa ya ukaa, na kwa kuwa tayari Halmashauri ya Wilaya ya Ngara kupitia Mbunge wao tulishandaa andiko la mradi kwa ajili ya kupambana na uchomaji moto Mradi unaoitwa *Participatory Community Based bush Fire Management and Livelihood Improvement* na tukawasilisha Wizara ya Muungano na Mazingira kwa ajili ya kuanza na vijiji 15 kati ya vijiji 75.

Je, ni lini Wizara yenye dhamana itawezesha ili Halmashauri tuweze kutekeleza mradi huu ambao unaonekana kuwa na tija, kwa sababu tutapanda miti ni *macadamia* na ufugaji wa nyuki vitakavyopelekea kutoa ajira lakini na kudhibiti mazingira, ni lini Wizara yenye dhamana itawezesha mradi huu? (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira yameulizwa maswali mawili, jibu moja lilitangulia.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,

MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Mheshimiwa Alex Gashaza amekuwa akifuatilia sana juu ya andiko lake katika ofisi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwakikishie Waheshimiwa Wabunge na nitoe wito kwa Watanzania wote na hasa ambao wanamiliki viwanda, suala la hewa ya ukaa ambalo Mheshimiwa Mbunge amelizungumzia ambalo ndio msingi na chimbuko la andiko lake, mabadiliko ya tabianchi ambayo yanatokea sasa yanaanza kuandama nchi yetu, ni kutokana na hewa ya ukaa inayozalishwa kwenye nchi zilizoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika nchi yetu tumeanza kuwa na maendeleo ya viwanda, kwa hiyo viwanda vihakikishe vinadhibiti hewa ya ukaa isije na vyenyewe vikaendelea kuongeza ukubwa wa tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Gashaza hewa ya ukaa, pamoja na kwamba upandaji wa miti utasaidia sana kwa sababu mchana miti inavuta hewa ya ukaa, kwa hiyo, ni kweli kwamba tukipanda miti kwa wingi tutaweza kudhibiti uzalishaji wa hewa ya ukaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hewa ya ukaa ni bidhaa ambayo ni adimu sana inauzwa kupitia Mfuko wa Mazingira Duniani. Ukiwa na hewa ya ukaa ukaivuna takwimu zile ukizipeleka kule ni fedha nyingi sana.

Kwa hiyo andiko lako Mheshimiwa Gashaza, Ofisi yetu inaendelea kulifanyia kazi, ili kuhakikisha maandiko ambayo tumeomba fedha kwenye mifuko ya Mazingira Duniani itakapopatikana basi andiko lako ambalo wataalam wetu wameliona ni zuri sana tutakwenda kulitekeza. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Mali Asili na Utalii, Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swalii lake.

Na. 101

Kuondoa Sintofahamu iliyopo katika Matumizi ya Ardhi

MHE. MWANTUMU DAU HAJI aliuliza:-

Kumekuwa na sintofahamu ya matumizi ya ardhi pamoja na masharti maalum yanayotakiwa katika mapori yetu hususan kwa wawekezaji na wananchi wanaozunguka hifadhi na mapori tengefu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza tatizo hili?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya hifadhi na mapori tengefu yametengwa kwa mujibu wa Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009.

Aidha, uwekezaji katika hifadhi, mapori ya akiba na tengefu, maeneo ya wazi yenye wanyamapori, maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi na Wanyamapori (*WMAs*) husimamiwa na sheria hiyo. Sheria na Kanuni husika hutoa taratibu za usimamizi wa maeneo hayo muhimu kwa maslahi ya uhifadhi, maliasili na mazingira, ukuaji wa uchumi na ustawi wa wananchi kuititia matumizi endelevu. Mwekezaji anapaswa kupata kibali na leseni ya kumruhusu kuendesha shughuli za utalii kutoka mamlaka zinazohusika kabla ya kuanza biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na tatizo hilo Serikali inapitia upya kanuni na taratibu za uwekezaji katika maeneo ya hifadhi na mapori tengefu, mionganoni mwa kanuni zinazopitiwa ni pamoja na Kanuni ya Jumuiya za Hifadhi Wanyamapori (*WMAs*).

Aidha, Serikali iko katika hatua za mwisho katika maandalizi ya kanuni za maeneo ya mapito (shoroba) ya wanyama na mtawanyiko wa wanyamapori.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa wawekezaji na wananchi wanaozunguka maeneo yaliyohifadhiwa. Aidha, natoa wito kwa wawekezaji kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizopo ili kupekuna na migogoro ya ardhi baina ya wanavijiji, wawekezaji na Mamlaka za Hifadhi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwantumu swali la nyongeza.

MHE. MWANTUM DAU HAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa wananchi, wanaendelea kunyanyasika katika maeneo hayo, je, Serikali ina mpango gani wa kutoa muda maalum kwa kumaliza mgogoro huo wa kitaifa? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo tumekuwa tukitoa majibu kwa muda mrefu kwamba sasa hivi tunayapitia matatizo na changamoto zote zilizopo katika hifadhi zetu, ikiwa nia pamoja na maeneo yale yanayosimamiwa na jumuiya za wananchi, naamini kabisa kwamba baada ya muda mfupi na baada ya Serikali na wadau wengine kukaa kwa pamoja tutaleta ufumbuzi wa suala hili na haya matatizo yatapungua kwa kiwango kikubwa. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Joyce Mukya swali la nyongeza.

MHE. JOYCE J. MUKYA: Mheshimiwa Naibu Spika,

ninakushukuru. Tatizo hili linafanana kabisa na tatizo la pori tengefu la Loliondo ambalo limedumu kwa kipindi cha miaka 25 sasa au zaidi, tokea nchi hii imepata uhuru ni awamu nne zimepita za uongozi na zote zikiongozwa na Serikali ya CCM. Kila awamu ilikuwa inapeleka uongozi wake kule kwa ajili ya kuongea na wananchi kwa ajili ya mgogoro huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata Waziri Mkuu Mheshimiwa Majaliwa ametoa agizo juzi kwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha aunde Kamati ya kwenda kushughulika na tatizo hili. Amepeleka ripoti na Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla amepeleka ripoti lakini mpaka sasa hakuna ambacho kimefanyika;

Naomba kujua je, ripoti hizi, zinasema wananchi wale waendelee kuteseka au ni nini ambacho kiko chini ya *carpet* ambacho kinasababisha wananchi hawa wasipiwe suluhu, na haki yao kupitia mgogoro huo ambao umeikumba Serikali hii na nchi hii kwa muda mrefu kwa muda wa miaka 25 na zaidi? (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwa muda mrefu kumekuwa na tatizo na mgogoro huko Loliondo na mgogoro huu umedumu kwa miaka mingi. Hivi sasa Serikali kama ulivyosema mwenyewe imechukua hatua za kuunda kamati mbalimbali ikiwemo kamati ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha ambayo ililetu mapendekezo na mapendekezo hayo yamepitwa na Serikali, Serikali imefanya uamuzi ambao tumeufikia ni kutaka kuwa na chombo maalumu kitakachosimamia lile pori la Loliondo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Serikali inafanya mchakato wa kuanzisha hicho chombo au mamlaka ambayo itahusika na usimamizi wa pori hilo la Loliondo kwa usimamizi na ushirikiano wa wananchi wenyewe wa Loliondo. Hii ndiyo tunaamini kwamba itakuwa suluhu ya

tatizo ambalo limedumu kwa muda mrefu katika lile eneo. Kwa hiyo, ni hivi karibuni tu tutaleta huo mwongozo na tutaleta hiyo mamlaka au tutaleta chombo hicho ambacho kitakwenda kusimamia tatizo hilo la Loliondo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe swali la nyongeza.

MHE.DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kunipatia nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ameongea kuhusu maeneo ya hifadhi ambayo yamekuwa yakihifadhiwa na Serikali lakini pia vyanzo vya maji. Kwa kuwa, wananchi wangu kwa kupitia Halmashauri ya Mpimbwe, Jimbo la Kavuu, wananchi wangu wa Kata ya Itobanilo; vijiji vya Senta Unyenye, Amani na Lunguya wamekuwa wakitumia maji ya Mto Kavuu ambao unapakana na mbuga ya Katavi na askari wa Katavi wamekuwa wakiwanyanya wananchi wakati vijiji hivyo hawana maji na tumekuwa na ujirani mwema wa kutumia.

Je, Serikali inasema nini kuhusu hawa watu wa *National Park* kupiga wananchi hivyo wakiwa wanaenda kutafuta huduma za msingi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli wananchi wa kata hizo alizozitaja pamoja na hivyo vijiji vimekuwa vikitegemea sana maji ya eneo lile ambalo amelisema karibu na mbuga yetu ile ya Katavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Sheria zetu za Wanyamaporu Sheria Na. 5 ya mwaka 2009 hairuhusu wananchi kuingia katika maeneo ya hifadhi bila kibali. Kwa hiyo, hivi sasa ambacho kinaweza kufanyika ili kunusuru

matatizo hayo, kwa sababu tuna sera ile ya ujirani mwema nitaomba tukae na Mheshimiwa Mbunge, tukakae na wananchi wenyewe ili tuweze kuangalia ni namna gani tunawapelekea maji katika maeneo ya vijiji vinavyohusika badala ya kuingia kwenye hifadhi ambapo wanakuwa wanahatarisha maisha yao na pia hali wataharibu hifadhi kitu ambacho ni kinyume na sheria. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge tushirikiane katika kutatua tatizo hili.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Mheshimiwa Hamad Salim Maalim, Mbunge wa Kojani, sasa aulize swalii lake.

Na. 102

Uhuru wa Faragha kwa Raia

MHE. HAMAD SALIM MAALIM aliuliza:-

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lbara ya 16 inatoa uhuru wa faragha kwa raia.

Je, kwa nini Jeshi la Polisi linapokwenda kupekua kwenye nyumba yenye mume na mke hutumia askari wa kiume peke yao?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Hamad Salim Maalim, Mbunge wa Kojani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la upekuzi ni jukumu ambalo sheria imelipa Jeshi la Polisi na utaratibu wake umeainishwa wazi namna ambavyo upekuzi utafanyika kwenye maeneo mbalimbali. Kifungu cha 38 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Sura ya 20 inatoa masharti na utaratibu wa kuweza kufanya upekuzi kwenye maeneo mbalimbali ikiwemo nyumba, majengo na vyombo vyaya usafiri

kama magari, boti na kadhalika endapo Afisa wa Polisi atakuwa amehisi na amejiridhisha pasipo na shaka kwamba kuna sababu ya kutosheleza kuwa kuna uwezekano wa kosa kutendeka au ushahidi kupatikana kuthibitisha kosa lillilotendeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, upekuzi wa makazi ya nyumba yenye mke na mume sheria haijaweka masharti ya ni askari wa jinsia gani anatakiwa kufanya upekuzi. Hata hiyo, Jeshi la Polisi kwa kutumia Kanuni ya Kudumu za Jeshi la Polisi (*PGO*) pia kwa kuzingatia busara na utu wa mwanadamu huwa inazingatia utaratibu wa kupeleka askari wa kike na wa kiume pale upekuzi unapofanyika kwenye makazi ya mume na mke.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hamad Salim Maalim swalii la nyongeza.

MHE. HAMAD SALIM MAALIM: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo hayaridhishi pia nina maswali mawili ya nyongeza.

Katika jibu la msingi Mheshimiwa Waziri amesema kwamba busara na utu wa mwanadamu huwa unazingatiwa, lakini naomba niseme kwamba siyo kweli kwamba busara na utu wa mwanadamu unazingatiwa.

Mimi binafsi nimefanyiwa tendo hili na nilipodai kwamba kwa nini hamkuja na askari wa kike wakalazimisha kutumia nguvu. Sasa naomba niulize Jeshi la Polisi, je, tabia hii mbaya itamalizika lini?

Swali la pili, je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuniletea orodha ya malalamiko ya matendo haya yaliyotendeka? Ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri swali la pili anataka orodha, kikanuni unaweza kuomba kujibu baadae kwa sababu ni swali la takwimu.

Waheshimiwa Wabunge, muwe mnazisoma kanuni sawasawa, orodha hawezi kuwa nayo hilo ni swali la nyongeza na kanuni hizi hapa, mimi ninao uwezo wa kuagiza hivyo. Someni vizuri mligawiwa mna miaka miwili humu ndani, mzifahamu vizuri hizi kanuni.

Mheshimiwa Waziri jibu swali la kwanza, swali la pili linataka takwimu utamjibu baadae, utampelekea hiyo orodha anayotaka.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake la kwanza kwamba inawezekana kuna tukio ambalo Mheshimiwa Mbunge anathabitisha lilimtokea binafsi la kufanyika upekuzi bila kuhusisha askari wa kike, naomba hili tulichukue ili tuelewe ni sababu gani iliyosababisha hilo litokee, halafu tuone sasa mimi na yeye Mheshimiwa Mbunge labda baadae tukae tuweze kulijua suala hili lilikuwaje ili tuone hatua gani ya kuchukua. Orodha tutampatia lakini siwezi kumpatia hapa kama Mheshimiwa Naibu Spika alivyosema.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jaku swali la nyongeza.

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, lakini kabla ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kumpongeza aliyekuwa Kaimu Waziri Mkuu Mheshimiwa Mwakyembe kwa kazi nzuri aliyoifanya Kukaimu Kiti cha Waziri Mkuu.

Baada ya hapo nichukue fursa hii swali la msingi linahusu mwanamke na mwanaume, je, kuna sheria gani iliyopitishwa na Bunge kama mtu kafanya kosa mume akakamatwa mke kuna utaratibu gani au kuna sheria iliyopitishwa?

Vilevile ninavyoju mimi utaratibu...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jaku swalni moja, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Jaku anataka kujua kama kosa la mwanamke anakamatwa mwanamume. Kosa aliyefanya ndiye atakayekamatwa, kwa hiyo, haiwezekani Mheshimiwa Jaku kosa akafanya mtu mwingine ukakamatwa wewe.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Madini Mheshimiwa Anna Joram Gidarya, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swal lake.

Na. 103

Maafa Mererani – Simanjiro

MHE. ANNA J. GIDARYA aliuliza:-

Mgodi a Tanzanite ulioko Mererani, Wilaya ya Semanjiro ni mgodi wenye idadi kubwa ya vijana wanaofanya kazi katika mgodi huo na kumekuwa na historia ya matukio ya maafa kila mwaka ya vifo vyatatu wengi.

(a) Je, Serikali imefanya utafiti gani ili kubaini chanzo cha maafa hayo yanayolikumba Taifa kila mwaka na kusababisha kupoteza nguvu kazi ya Taifa letu?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuanzisha utaratibu maalum kwa wamiliki wa vitalu vyatatu Tanzanite kuwalipa kifuta jasho wahanga wote wanaopatwa na maafa wanapokuwa kazini?

NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. DOTO M. BITEKO)
aliibuu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anna Joram Gidarya, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya taarifa za ajali yanaonesha kuwa ajali nyngi husababishwa na wachimbaji wadogo kutokuzingatia tahadhari ya usalama wanapotekeleza majukumu yao ya uchimbaji madini. Hivyo, Serikali imekuwa ikifanya juhudzi za ukaguzi wa maeneo ya uchimbaji na kuwa elimisha wachimbaji kuchukua tahadhari za usalama wakati wa kufanya kazi pamoja na kuwahamasisha kuunda timu za wakaguzi katika maeneo yao kutoka mionganoni mwa wachimbaji ambao hupewa elimu ya ukaguzi na wataalam wetu wa Wizara ya Madini. Hivyo, nawasihi wachimbaji wa madini kutambua umuhimu wa kuzingatia taratibu na usalama wa kazi kwa uchimbaji ili kulinda afya na uhai wao.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali imeanzisha Mfuko wa Fidia ya Wafanyakazi kupitia Sheria Namba 20 ya mwaka 2008 ya Fidia ya Wafanyakazi. Wizara itahamasisha wamiliki wa leseni na wachimbaji kuijunga na mfuko huu ili kupata kifuta jasho wanapopatwa na maafa wanapokuwa kazini.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Anna Joram Gidarya swali la nyongeza.

MHE. ANNA J. GIDARYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, pamoja na majibu ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na utaratibu wa Serikali pindi tu mawe yanapotoka kulazimisha wamiliki kuitisha mawe hayo kwenye chumba maalum (*strong room*) kabla ya kuuzwa mnadani, jambo ambalo limesababisha usumbufu mkubwa kwa wamiliki wa vitalu kutokuwalipa wafanyakazi hao kwa wakati.

Je, ni nini sasa kauli ya Serikali ili kuondoa usumbufu huu kwa wamiliki wa mgodi huu wa Tanzanite?

Swali la pili pamoja na wamiliki wa migodi wa Tanzanite kuwa na vibali halali kumekuwa na utaratibu wa Serikali kuuza mawe hayo kwenye mnada kwa bei ya kutupa; je, Serikali haioni kama wamiliki hawa wa migodi wanapata hasara kubwa pamoja na kuwa wanalipa kodi ya Serikali?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Madini majibu.

NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. DOTO M. BITEKO): Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nataka nieleze tu kwamba tunawalazimisha watu kupitisha mawe kwenye *strong room* kabla ya kuuzwa, lengo letu ni moja tu kutaka kujuua uhakika wa kiasi gani cha mawe yamezalishwa ili Serikali iweze kupata kodi zake na tozo zake mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili hatuwezi kurudi nyuma madini haya ya Tanzanite yamekuwa yametoroshwa na nchi hii imepata aibu kubwa. Asilimia 20 tu ya madini yote ya Tanzanite yanayochimbwa ndiyo tunaweza kuyaona yameingia kwenye mfumo wa Serikali. Kwa hiyo, tumeweka nguvu kubwa ya udhibiti na usimamizi na hili Mheshimiwa Anna ninamwomba aunge mkono juhudzi za Serikali kwenye jambo hili tusirudi nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili utaratibu wa kuza mawe haya kwenye mnada ni utaratibu ule ule na umekuwepo kwa muda mrefu, bei iliyopo pale sio bei ya kutupwa ni bei ya ushindani wale wanaotaka kununua wote wanakwenda kwenye eneo la mnada wanatoa bei zao yule anayeshinda anapewa kwa bei nzuri. Hili tunataka kulifanya kwa uzuri zaidi na litakuwa katika Mkoa wa Manyara ili lisimamiwe vizuri zaidi Serikali iweze kupata kodi zake. Ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Constantine Kanyasu swalii la nyongeza.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni tulifanya mabadiliko ya Sheria ya Madini na katika kudhibiti na kusimamia *CSR* tulielekeza Halmashauri husika kushirikishwa katika mipango. Inaonyesha kwamba huko nyuma taarifa ambazo zipo kwenye Halmashauri zetu ni miradi hii ilikuwa inakuwa *inflated* na mingi ilikomea njiani.

Ni nini maelekezo ya Serikali kwa sababu migodi itaendelea kusimamia yenye na kutangaza kazi yenye katika sheria ijayo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Madini majibu.

NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. DOTO M. BITEKO): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze tu kwa kueleza kwamba Mheshimiwa Kanyasu kwa muda mrefu amekuwa mtu ambaye ana kilio kikubwa juu ya matumizi ya hizi fedha za *CSR* zinazotolewa na migodi hapa nchini, wananchi wa Geita wanajua hilo na amekuwa akilisema hata hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli sheria mpya ya madini, marekebisho mapya kwenye Sheria yetu ya Madini ya mwaka 2010 imetoa utaratibu maalum kwa watu wote wenye migodi kutengeneza *plan* ya matumizi ya *CSR* na kuipeleka kwenye Serikali ya Halmashauri ili iweze kupata *approval*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna changamoto imejitokeza kwenye migodi mingi ambapo ni kweli kabisa kama alivyosema Mheshimiwa Kanyasu *inflation* ya bei ya vitu imekuwa kubwa mno na miradi mingi imekuwa miradi ambayo haifiki mwisho. Sasa kama Wizara tunaandaa utaratibu wa kukagua *CSR* ambazo zimekwishakutolewa ili tuone kama kweli fedha hizi zilizotolewa ziliwafikia wananchi na halikuwa jambo la kutegeshea tu. Ahsante. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ruth Mollel swali la nyongeza.

MHE. RUTH H. MOLLEL: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali ndogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachimbaji wadogo wadogo wamekuwa wakipata maafa makubwa sana kwenye migodi na ukaguzi mnasema unafanyika, ningependa kujua huu ukaguzi unafanyika kwa mfano kila mara baada ya miezi mingapi ili tujue kwamba kweli hawa watu wanasmamiwa ili kusudi kuepusha hizi ajali zinazotokea mara kwa mara.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Madini majibu.

NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. DOTO M. BITEKO): Mheshimiwa Naibu Spika, ukaguzi kwenye migodi ni utaratibu maalum wa Wizara yetu ya Madini kukagua mara kwa mara na hatuna muda maalum, wakati wowote kwenye migodi tunakwenda tunakagua kujiridhisha kama kuna *compliance* ya kufuata sheria yetu ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye migodi yote ziko Kamati ndogo ndogo za ndani kwenye hiyo migodi ambazo zinafanya kazi ya ukaguzi. Niwaombe wamiliki wote wa leseni kuzitumia Kamati hizi za ukaguzi ili tuweze kupunguza maafa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la msingi nimueleze tu Mheshimiwa Mbunge kwamba wachimbaji wadogo wenyewe waangalie usalama mahali pa kazi, kwa sababu mtu wa kwanza wa kuangalia usalama wake ni yeye mwenyewe mchimbaji kabla ya Serikali kuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji. Mheshimiwa

Deogratias Francis Ngalawa, Mbunge wa Ludewa, sasa aulize swali lake.

Na. 104

**Miradi ya Makaa ya Mawe Mchuchuma
na Chuma Liganga**

MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA aliuliza:-

Miradi ya Makaa ya Mawe ya Mchuchuma na Chuma Liganga imekuwa ikizungumzwa na Serikali kwa Awamu hii ya Tano na imewekwa katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016-2021).

(a) Je, ni lini miradi hii itaanza?

(b) Je, ni lini Serikali italipa fidia kwa wananchi wa Mundindi na Mkomang'ombe waliota maeneo yao kupisha miradi hii?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA
UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deogratias Francis Ngalawa, Mbunge wa Ludewa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa miradi unganishi ya Mchuchuma na Liganga inazungumziwa sana na Serikali na imeainishwa katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano kama moja ya miradi ya kipaumbele. Kutohana na umuhimu wa miradi katika uchumi wa Taifa, Serikali imejipanga kuhakikisha miradi hii inaanza kwa kufuata utaratibu sahihi na kwa kuzingatia manufaa mapana ya Taifa wakiwemo wananchi wa Mkoa wa Njombe, hususan Wilaya ya Ludewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakumbuka kuwa mwezi

Mei, 2017 wakati nikijibu swalii la Mheshimiwa Ngalawa kuhusu miradi hii, nililieleza Bunge lako Tukufu kuwa Kamati ya Wataalam ilikuwa imekamiliisha kupitia vivutio alivyoomba mwekezaji ili viwasilishwe Serikalini kwa lengo la kuhakikisha Taifa linapata faida zaidi.

Hata hivyo, mwezi Julai, 2017 Bunge lako Tukufu lilifanya marekebisho ya Sheria ya Madini ya mwaka 2010 pamoja na kutunga sheria mbili mpya za *The Natural Wealth and Resources Permanent Sovereignty Act, 2017* na *The Natural Wealth and Resources Contract (Review & Re-Negotiation of Unconscionable Terms) Act, 2017*. Maelekezo ya sheria rejewa hapo juu yanakinzana na baadhi ya vifungu vya mikataba ya ubia (*joint venture agreement*) na mgawanyo wa hisa (*Shareholding Subscription Agreement-SSA*) iliyokuwa imeingiwa kati ya mwekezaji na *NDC* mwaka 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ukinzani wa kisheria uliojitokeza, Serikali imeunda timu ya wataalam ya kufanya majadiliano na mwekezaji ili kutafuta ufumbuzi. Timu hiyo iliyokwishaanza kazi imepewa jukumu la kufanya mapitio ya mikataba yote na vivutio alivyoomba mwekezaji ili kuainisha maeneo yenye ukinzani na kujadiliana na wabia wenza ili kuepuka kutekeleza miradi kinyume na maelekezo ya sheria za nchi. Ni imani yangu kuwa baada ya makubaliano ya mwekezaji mwenza kwenye maeneo kinzani, Serikali itatoa baraka za mwisho na mradi utaanza mara moja ikiwemo kulipa fidia kwa wananchi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Deogratias Ngalawa swalii la nyongeza.

MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nipende kuipongeza Serikali kwa kuanza na miundombinu wezeshi ili miradi hii ya Makaa ya Mawe Mchuchuma na Chuma Liganga iweze kuanza. Mfano ni ile barabara ya kutoka

Mchuchuma kuitia Kijiji cha Ibumi - Amani mpaka Mundindi ambako Liganga ipo. Sasa maadam kuna timu ya wataalam ambayo imeundwa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wanaongea na mwekezaji.

Je, timu hii ya wataalam itachukua muda gani kumaliza mazungumzo yao na kufanya miradi hii ya Mchuchuma na Liganga ianze ikiwa ni pamoja na kulipwa na fidia?

Pili, kwa nini Serikali isichukue jukumu la kulipa fidia ili kuwafanya hawa waliopisha huu mradi wa Liganga na Mchuchuma waendelee na shughuli zao huku yenyewe ikiendelea na mazungumzo na mwekezaji? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianzie kumshukuru sana Mheshimiwa Deogratias Ngalawa kwa pongezi alizotumpa Serikali, lakini pia tumshukuru na kumpongeza yeye mwenyewe kwa jinsi ambavyo amekuwa akifuatilia mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee kabisa nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wanachi wa Ludewa hususani katika maeneo ya Mchuchuma na Liganga kwa uvumilivu wa kuona kwamba mradi huu unaendelea kushughulikiwa kwa manufaa ya nchi wakati wakisubiri fidia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Mchuchuma na Liganga ni mradi ambao ni wa kimkakati, kuna maliasili kubwa sana ambayo ipo pale. Mlima wa Liganga ambao ni chuma tupu, mimi mwenyewe nimeshafika pale, lakini pia na makaa ya mawe ambayo yapo Mchuchuma ni kiasi kikubwa sana cha rasilimali ya nchi ambayo majadiliano yake lazima yafanyike kwa kina na tuweze kuona kwamba tunapata haki kwa ajili ya manufaa ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa misingi hiyo nikijibu kwa pamoja, niseme tu kwamba Serikali imekuwa ikitoa fidia katika baadhi ya maeneo, lakini sasa tunaona fedha nydingi ya Serikali imekuwa ikikaa mahali wakati mwekezaji anakuwa bado hajapatikana, kiasi kwamba ingeweza kutumika pia katika kutengeneza miundombinu wezeshi maeneo mengine.

Hivyo mkakati wa Serikali sasa hivi ni kuona kwamba tunamshawishi mwekezaji achukue pia na dhamana ya kulipa fidia kwa wananchi katika maeneo ya uwekezaji. Kwa misingi hiyo nikupe tu uhakika kwamba tutajitahidi kwa kila hali kuhakikisha kwamba majadiliano yanaenda kwa kasi, lakini sio kasi tu kuwa yenye tija kwa faida ya wananchi wa Tanzania.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Jesca Kishoa, swali la nyongeza.

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatumia fedha nydingi sana za kigeni kuagiza chuma kutoka nje kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa reli ya katii.

Je, Serikali haioni haja ya kutumia fedha hizo kununua chuma kutoka Liganga na Mchuchuma badala ya kuendelea kupoteza fedha za kigeni kutoka nje?

Na kama alivyoelezea...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kishoa umeshauliza swali. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa reli unaoendelea sasa ni kwamba upo katika kuanza, lakini hatua za kujenga kiwanda kwa ajili ya kutegemea chuma

cha Liganga ni kazi ambayo inahitaji hatua katika vipindi mbalimbali na chuma kile ni tofauti na vyuma vingine, pale tuna *tinanium*, tuna *vanadium* zote ni madini ambazo ni aghali sana na muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachofanyika ni upembuzi yakini fu katika kuwapata wataalam watakaoweza kuifanya kazi hiyo kwa utaalam wa hali ya juu unaowezekana na hivyo lazima tufate taratibu zote. Kwa hiyo, hatuwezi kusimamisha miradi mingine wakati tukisubiri mradi wa Liganga na Mchuchuma.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 105

Kuwasha Umeme Kijiji cha Itengelo

MHE. NEEMA W. MGAYA aliuliza:-

Ni muda mrefu tangu *transformer* katika Kijiji cha Itengelo, Kata ya Saja imefungwa lakini umeme haujawashwa.

Je, ni lini Serikali itawasha umeme katika kijiji hicho?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kijiji cha Itengelo ni mionganoni mwa vijiji vilivyonufaika na mradi wa *REA Awamu ya Pili uliotolekezwa na Mkandarasi Kampuni ya M/S Sengerema Engineering Group Limited* ambaye alipewa kazi ya mradi kwa Mkoa wa Njombe. Kazi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa kilometra 8.5 za njia za umeme msongo wa

kilovoti 33 na kilometra sita za njia za umeme msongo kilovoti 0.4 kwa gharama ya shilingi milioni 564. Maradi ulikamilika mwezi Desemba, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kijiji cha Itengelo kiliwashiwa umeme tarehe 22/08/2017 kwa kufungiwa *transformer* mbili pamoja na kuwaunganisha umeme wateja 56 walolipia.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa, Neema Mgaya, swalı la nyongeza.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri katika Jimbo la Njombe Mjini kuna vijiji ambavyo vimepitiwa na mradi wa Makambako - Songea na mradi huu haujaingia kwenye vitongoji, haujaingia kwenye zahanati, shule ikiwemo shule ya sekondari ya Anne Makinda; na kwa kuwa mradi huu ni wa muda mrefu sana na vijiji vinaendelea kupanuka.

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika vijiji hivi vilivyoipitiwa na mradi wa Makambako - Songea?

Swali langu la pili, Jimbo la Lupembe lina vijiji 45, kati ya vijiji 45, vijiji 34 havina umeme ikiwemo Kijiji cha Ninga na kwa kuwa wananchi wa Kijiji cha Ninga wameamua kuunga mkono sera ya viwanda kwa kununua mashine ya kusaga yenye uwezo wa kusaga sembe zaidi ya tani 12 kwa siku, kwa nia ya kuanzisha kiwanda.

Je, Serikali itapeleka lini umeme katika vijiji hivi hususani Kijiji cha Ninga ili ndoto yao ya kiwanda chao kiweze kufanya kazi? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa, Naibu Waziri Nishati, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika,

ninakushukuru kwa kunipa fursa ya kujibu maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge Neema pamoja na Wabunge wa Viti Maalum kwa namna ambavyo wanaauliza maswali katika sekta yetu ya nishati.

Swali lake la kwanza amerejea kwamba mradi unaoendelea wa ujenzi wa msongo wa KV220 Makambo - Songea; kwanza awali ya yote nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kutuwekea jiwe la msingi katika mradi huu. Mradi huu unaendelea vizuri mpaka sasa umefikia asilimia 70, na utaunganisha vijiji 120 katika Mikoa ya Njombe na Ruvuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika maeneo ambayo ameyataja Mheshimiwa Mbunge Neema na naomba nimtaarifu mpaka sasa Vijiji vitano katika Mkoa wa Njombe vimeshawasha umeme kupitia mradi huu na kwamba katika maeneo ambayo ameyataja hayajafikiwa na mradi huu, nataka nimwambie tu pia Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa *densification* na kwa mkoa wa Njombe peke yake mpaka sasa hivi vijiji 12 vimeshaunganishwa.

Kwa hiyo nataka nimwambie maeneo ambayo yatakakuwa mradi huo haukuyafikia yatafikiwa na miradi ambayo inaendelea *REA* Awamu ya Tatu pamoja na *densification* ambavyo kama nilivyosema na kama ambavyo Serikali imekuwa ikitoa maelekezo, taasisi za umma ikiwemo shule ya sekondari na hapa amerejea sekondari ya Mama Anne Makinda viunganishwe katika miradi hii inayoendelea. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili amekitaja Kijiji cha Ninga, nataka nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kama alivyosema Jimbo la Lupembe lina vijiji 34 kati ya vijiji hivyo, vijiji 24 viro katika mradi wa *REA* Awamu ya Tatu pamoja na kijiji ambacho amekitaja, na naomba niwapongeze vijiji vyote ambavyo vinatekeleza sera ya viwanda na kwa kuwa Serikali yetu ya Awamu ya Tano imedhamiria kutekeleza mapinduzi ya viwanda, nishati ya

umeme itafika katika Kijiji cha Ninga pamoja na vijiji vingine kwa Awamu ya Tatu ambayo inaendelea. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hussein Amar swali la nyongeza.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa uzinduzi wa *REA* Awamu ya Tatu kimkoa wa Geita ulifanyika kwenye Wilaya ya Nyangh'wale, Kijiji cha Nijundu, mwenzi wa sita mwaka jana, lakini cha ajabu mpaka leo hii hata kijiji kimoja kati ya vijiji 35 vya Wilaya ya Nyangh'wale havijapelekewa nguzo.

Je, ni lini sasa Serikali itaanza kupeleka nguzo hizo katika hivyo vijiji ambavyo tumepewaa vijiji 35?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Amar kwa swali lake zuri, katika Mkoa wa Geita mkandarasi wake ni *JV White Service Limited* ambaye ameshaanza kazi, na kwa kuwa ameeleza kwamba mpaka sasa katika Wilaya yake, nataka niseme wakandarasi hawa walipoteuliwa unakuta Mkoa mmoja una mkandarasi mmoja, na Mkoa huo unaweza ukawa na Wilaya mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maelekezo ya hivi karibuni katika Mkoa wa Geita mkandarasi alikuwa ameshaagiza nguzo takribani 3,000 na tulimpa maelekezo aende kila Wilaya. Kwa hiyo, kama mkandarasi mpaka sasa hivi hajafika katika Wilaya ya Nyang'wale naomba nimuelekeze na nimpe agizo kwamba kama vile tulivyotoa maelekezo tulivyokutana kikao cha tarehe 13 Januari, wakandarasi wote wafanye miradi Wilaya zote, wasijielekeze katika Wilaya moja.

Kwa hiyo, ninamuagiza mkandarasi JV White wa Mkoa wa Geita aelekee kwenye Wilaya zote na afanye kazi ya kuunganisha kupeleka hii miundombinu ya umeme kama ambavyo tulikubaliana katika Kikao cha tarehe 13 Januari, 2018.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nadhani maelekezo kasema ni Wilaya zote bado tuna maswali ya nyongeza. Mheshimiwa Lucy Magereli, swali la nyongeza.

MHE. LUCY S. MAGERELI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa fursa niulize swali la nyongeza.

Changamoto ya umeme kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Kigamboni bado ni kubwa sana pamoja na kwamba mwaka jana wakati wa bajeti, wakati Waziri akijibu swali la Mheshimiwa Dkt. Ndunguille, alieleza bayana ya kwamba tatizo la msongo mdogo wa umeme eneo la Kigamboni litakuwa limekwisha mwaka jana mwezi Agosti, lakini hadi tunapozungumza leo bado changamoto ya umeme mdogo Kigamboni ni kubwa, lakini ukiachilia hilo umeme huo unakatika mara 15 kwa siku.

Je, Serikali ina maeleo gani kuhusu suala hili na kuchelewa kwa kutekelezwa kwa mradhi huu wa kufunga transforma kubwa yenye msongo wa kutosha kutupa huduma ya umeme eneo la Kigamboni?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nishati majibu.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Lucy kwa swali lake zuri na ni muhimu sana. Kupitia Bunge lako Tukufu, napenda nitoe taarifa ya Serikali kuhusiana na utekelezaji wa miradi ya umeme muhimu sana kwa wananchi wa maeneo ya Kigamboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa wananchi wa Kigamboni hivi sasa hawana umeme wa uhakika, lakini hatua madhubuti tunayofanya ni kujenga *substation*

itakayowapelekea umeme sasa wananchi wa Kigamboni wote, mradi huu utakamilika mwezi tarehe 25 Mei tutakuwa tumeshawapelekea wananchi wa Kigamboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya haraka tunachofanya hivi sasa tunakamilisha utekelezaji wa mradi wa kabambe katika Jiji la Dar es Salaam kwa eneo la Mbagala. Mradi tunategemea kuuwasha kati ya tarehe 20 mwezi huu kuanzia tarehe 12 tutakuwa tumeshawasha na tarehe 20. Mradi huu utahudumia wananchi wa Mbagala, Kurasini, Kigamboni pamoja na maeneo mengine ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge, kazi hiyo inafanyika na wananchi wa Kigamboni watarajie kwamba umeme utapatikana kufikia mwisho wa mwezi huu. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko swalil ya nyongeza.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, shida iliyoko huko Njombe inafanana sana na iliyoko huko Kigoma. Mkoa wa Kigoma tuna mkandarasi ambaye ana mgogoro, sasa mgogoro huu umeendelea kati ya REA na Wizara ya Ujenzi. Tungependa kujua kwa Wilaya za Kigoma, Buhigwe, Uvinza na Kasulu, mgogoro kati ya mkandarasi na Wizara unamalizika lini ili mradi wa REA Awamu ya Tatu uweze kuanza? Nakushukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nishati majibu.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine tena ninapenda kumshukuru sana Mheshimiwa Nsanzugwanko anavyofatilia masuala ya umeme katika Mkoa wa Kigoma kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwa upande

wa Mkoa wa Kigoma, Mkandarasi kwa ajili ya kutekeleza mradi wa REA Awamu ya Tatu mchakato umekuwa ukiendelea, lakini nitumie nafasi hii kusema kuwa, kweli wakandarasi walishakiana, shitaka linaendelea mahakamani na kwa taratibu za Kisheria, jambo linapokuwa mahakamani huwezi kuliingilia kwa sababu ni muhimili mwininge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa taarifa tu kwamba Serikali imeshaanza kuwapelekea umeme wananchi wa Kigoma, wiki iliyopita tulizindua mradi wa utekelezaji wa umeme vijiji katika Wilaya ya Kibondo na tayari mkandarasi ameshawasha Kijiji cha Mabamba. Lakini katika Jimbo la Kakonko pia tumeshazindua, mkandarasi ameshawasha umeme katika Kijiji cha Katale na ataendelea Nyamtukuza. Niwape taarifa wananchi wa Kigoma kwamba mara baada ya taratibu za kimahakama kukamilika vijiji vyote 120 vilivybaki vitapelekewa umeme.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Bobali swali la nyongeza.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru.

Kumekuwa na tabia ya umeme kukatika katika Mkoa wa Lindi hususan maeneo ya Mchinga, Mvuleni na Kilolambwani kadri mvua inaponyesha, lakini siku mvua haikunyesha umeme huwa haukatiki.

Nataka kujua, kuna changamoto gani kwamba siku za mvua lazima umeme ukatike hata kama hatuoni nguzo iliyodondoka?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nishati, majibu.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali moja zuri sana la Mheshimiwa Mbunge wa Lindi. Ni kweli, kwanza kabisa nitumie nafasi hii kuipongeza sana Serikali yetu, kulikuwa na matatizo makubwa sana ya umeme katika Mkoa wa Mtwara na Lindi

miaka na miezi michache iliyopita. Lakini tangu mwezi Desemba, Serikali yetu imetenga fedha na imelipa fedha na tumekarabati mitambo yote iliyokuwa haifanyi kazi katika Jimbo la Mheshimiwa Mbunge na Mikoa ya Mtwara na Lindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika ni kweli mvua na umeme ni vitu viwili tofauti sana, mara zote kunapokuwa na mvua hasa ya muungurumo wa radi huwa inaingilia sana miundombinu ya umeme, hata inapokuwa mvua ya upепo mara nyingi nguzo zetu zinaanguka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa amesema mara zote kunapokuwa hakuna mvua umeme hauna shida, ili kuondokana na tatizo hilo sasa hivi tunaanza utaratibu wa kuleta nguzo za zege ambazo zitakuwa imara, wakati wa mvua zitakuwa hazidondoki. Kwa hiyo, tatizo hilo litakwisha mara moja, siyo kwa Lindi tu ni kwa nchi nzima.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Juma Ali Juma, Mbunge wa Dimani, sasa aulize swali lake.

Na. 106

Mgogoro wa Ardhi kati ya Jeshi na Wananchi wa Kisakasaka

MHE. JUMA ALI JUMA aliuliza:-

Kuna mgogoro wa ardhi kati ya Jeshi na wananchi wa Kisakasaka hali inayoleta wasiwasi kwa wananchi.

(a) Je, ni lini Serikali itaupatia ufumbuzi mgogoro huo?

(b) Je, kwa nini Serikali isiwaruhusu wananchi hao kuendelea na shughuli za kilimo na mifugo wakati wakisubiri ufumbuzi wa tatizo hilo?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Juma Ali Juma, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, inatambua uwepo wa mgogoro wa ardhi kati ya Jeshi na Wananchi katika eneo la Kisakasaka. Katika kupata ufumbuzi wa kudumu wa mgogoro huu, Makao Makuu ya Jeshi iliridhia kurekebisha mpaka wa Kambi ya Kisakasaka ili kuwaachia wananchi eneo lenye mgogoro na hivyo kuleta suluhisho la kudumu kwenye mgogoro huo. Zoezi hilo halijafanyika kutokana na ufinyu wa bajeti, hata hivyo katika mwaka huu wa fedha wa 2017/2018 tunategemea kutekeleza zoezi hili.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa napenda kuwasihii wananchi wawe wastahimilivu wakati Serikali inachukua hatua stahiki ili kuzuia madhara yoyote yanayoweza kutokea kwa wananchi endapo wataendelea na shughuli za kilimo na mifugo katika eneo hilo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Juma Ali Juma swalii la nyongeza.

MHE. JUMA ALI JUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru. Naomba kuuliza swalii dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgogoro huu ni wa muda mrefu toka mwaka 1979, viongozi mbalimbali wametembelea katika eneo lile lakini hadi leo halijapatiwa ufumbuzi. Je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari mimi na yeye pamoja na viongozi wanaolizunguka lile eneo tukae pamoja ili tuupatie ufumbuzi mgogoro huu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, majibu.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba mgogoro huu ni wa muda mrefu na nataka nimfahamishe Mheshimiwa Juma

kwamba mimi binafsi nimefika eneo hilo, nilifanya mazungumzo na uongozi wa kikosi pamoja na uongozi wa eneo na wananchi wa pale tulizungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyo sema katika jibu langu la msingi, kinachokwamisha kutatua sasa hivi ni suala la fedha za kupima kwa sababu Jeshi lilisharidhia kufanya mabadiliko ya mipaka yake ili wananchi ambao sasa hivi wanaonekana wapo ndani ya eneo la kambi waweze kutolewa. Hata hivyo, nitakuwa tayari kuzungumza na Mheshimiwa Mbunge ili kumueleza zaidi ni hatua gani ambazo zinastahili kuchukuliwa kwa mujibu wa ziara niliyofanya pale na fedha zikipatikana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hassan Masala swalii la nyongeza.

MHE. HASSAN E. MASALA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kunipa nafasi niweze kuuliza swalii la nyongeza.

Moja ya matatizo makubwa makubwa ambayo tumekabiliana nayo kwa wananchi wanaozunguka Kambi ya Maji Maji kikosi Namba 41 na kikosi cha JKT katika Kata ya Mchonda ni tatizo ya migogoro ya ardhi, na tatizo hili tayari tumesharipoti kwa watu wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kufahamu msimamo wa Serikali au Wizara juu ya fidia ambazo wameahidi kuwalipa wananchi wale ili waweze kuachia yale maeneo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, majibu.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kuna Kambi nyingi ambazo zina migogoro ya ardhi. Kama ninavyosema mara kwa mara hapa migogoro hii iko ya aina nyingi, kuna migogoro ambayo Jeshi limechukua ardhi lakini wananchi

bado hawajalipwa fidia, yapo maeneo ambayo wananchi wamevamia Kambi za Jeshi na na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachowenza kusema hapa ni kwamba tumeweka fedha kwenye bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ili kwa yale maeneo ambayo fidia zinahitajika tuweze kulipa ili kumaliza migogoro hii, mwaka wa bajeti haujaisha na nimategemeo yetu kwamba fedha hizo zikipatikana tutatoa fidia kwa wale ambao wanastahili kupewa fidia maana wako wengine ambao wao wamevamia kambi za Jeshi hao hawatalipwa fidia. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Lathifah Hassan Chande, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 107

Mradi wa Umwagiliaji Kata ya Mtawango Liwale

MHE. LATHIFAH H. CHANDE aliuliza:-

Halmashauri ya Mji wa Liwale imetumia takribani shilingi milioni 540 katika ujenzi wa mradi wa umwagiliaji katika Kata ya Mtawango, lakini mradi huo umejengwa chini ya kiwango na hakuna thamani ya matumizi ya fedha (*value for money*).

Je, Serikali ipo tayari kwenda kukagua mradi huo na kufanya uchunguzi ili kubaini kasoro za mradi huo na kuwawajibisha wote watakaobainika kuuhujumu mradi huo?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lathifah Chande, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa umwagiliaji wa Mtwango upo katika kijiji cha Mtawango, Kata ya Mbaya, Tarafa ya Liwale, Halmashauri ya Wilaya ya Liwale. Mradi huu uliibuliwa nawananchi mwaka 2008 na una jumla ya eneo la hekta 230.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua za uboreshaji zilianza mwaka 2009 kwa kufanya upimaji na usanifu wa awali. Katika mwaka 2011/2012 mradi huo ilitengewa fedha kiasi cha shilingi milioni 220 kupitia Mfuko wa Wilaya wa Kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji kwa ajili ya ujenzi wa banio, uchimbaji wa mfereji mkuu mita 1,000, ujenzi wa vigawa maji vinne. Kazi hizo zilifanyika na kukamilika kulingana na matakwa ya mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014 mradi ilitengewa fedha kiasi cha shillingi milioni 184 kwa ajili ya kusakafia mfereji uliochimbwa na mita 1,000 kujenga vigawa maji nane, kujenga ukuta wenyewe urefu wa mita 250 kwa ajili ya kukinga mafuriko, kujenga kivusha maji na kivuko kwa ajili ya watembea kwa miguu na mitambo. Kazi hizo zilifanyika na kukamilika kulingana na matakwa ya mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kasoro alizobainisha Mheshimiwa Mbunge, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, itaunda timu ya wataalam kwa ajili ya uchunguzi na endapo itabainika kweli kuna hujuma katika mradi huo, hatua stahiki zitachukuliwa kwa wahusika.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lathifah Chande swali la nyongeza.

MHE. LATHIFAH H. CHANDE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba Serikali imesema kwamba itaunda timu maalum kwa ajili ya kushughulikia suala hili la Mtawango, lakini Kamati ya LAAC

ilituletea taarifa yake hapa Bungeni ambayo ilionesha kwamba kuna ujisadi mkubwa unaoendelea katika miradi mbalimbali ya maji hapa nchini. (*Makof!*)

Je, Serikali ipo tayari kuunda Tume ya Kitaifa itakayoweza kuchunguza miradi mbalimbali ya maji hapa nchini na kutuletea taarifa ya ripoti yake hapa Bungeni kama ambavyo Kamati ya *LAAC* ilipendekeza?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Ng'apa wa maji safi na salama ambaao uko Lindi uliopelekea hadi Rais akamtumbua na kumfukuza nchini yule mhindi mpaka leo hii haujakamilika na kusababisha wananchi wa Lindi kukosa maji salama na safi.

Je, ni kwa nini mradi huu mpaka leo hii haujakamilika pamoja na kuwepo na maagizo ya Rais? (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji majibu.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza ni maelekezo ya Kamati ya *LAAC* ambayo yaliweka maazimio ya kuunda mpaka Tume kuhusu kuchunguza miradi ya maji, kwa sababu tayari maazimio hayo yalikubalika na Bunge nafikiri hebu tuyaache sasa, hayo maazimio yaweze kufanyiwa kazi badala ya kuunda tume nyingine ya pili.

Swali la pili, ameulizia kuhusu Mradi wa Ng'apa nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mradi wa Ng'apa umekamilika na sasa hivi unatoa maji Mjini Lindi, kama una ndugu zako wako Lindi kule naomba uwapigie simu, tayari mradi umekamilika na nimetoa tena fedha shilingi milioni 500 ili tuweze kuweka miundombinu ya kusambaza maji Mjini Lindi ili maeneo mengi yaweze kufaidika na mradi wa Ng'apa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Juma Nkamia swali la nyongeza.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nipate kuuliza swali moja dogo tu la nyongeza.

Nheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaipongeza Serikali kwa kutoa shilingi bilioni mbili kwa ajili ya mradi wa maji wa Ntomoko kule Kondoa na Chemba.

Swali langu ni kwamba pamoja na Serikali kutoa fedha hizi mradi ule umehujumiwa Serikali inajua na wananchi wa Kondoa na Chemba wanajua na waliohujumu mradi huu wamehamishwa kutoka Halmashauri ya Kondoa kwenda Halmashauri nyingine. Nilitaka kujua ni nini kauli ya Serikali kuhusu hali hii? (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji majibu.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli zipo dalili za ule mradi kuhujumiwa kutokana na utekelezaji kuchukua muda mrefu, lakini tumeamua kuchukua hatua mbili kwa sababu wananchi wa Kondoa/wananchi wa lile eneo wanahitaji maji tumechukua hatua mbili. Sasa hivi utekelezaji wa ule mradi tumeukabidhi kwa Mamlaka ya Maji Dodoma (*DUWASA*) wakati wowote tunatangaza *tender*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuhakikisha kwamba sasa hawa wananchi wanapata huduma ya maji, ndio tunarudi nyuma kuangalia ni watu gani waliotufikisha hapa, kwa hiyo, stahiki zao zitachukuliwa kwa mujibu wa sheria na Mheshimiwa Nkamia hata kama wamehamishwa hawajapelekwa nje ya nchi wako Tanzania hapa, kama mtu atabainika kwamba alihujumu atafuatwa, atakwenda kuchomolewa aliko ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Yosepher Komba swali la nyongeza.

MHE. YOSEPHER F. KOMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Muheza kuna mradi wa maji kutoka kwenye Kata ya Pongwe kuja Muheza Mjini, mradi ambao umeanza tangu mwaka 2016, lakini wananchi wa Muheza wamekuwa na wasiwasi juu ya ukamilishwaji wa mradi ule.

Mheshimiwa Waziri anaweza kutuambia ni lini wananchi wa Muheza tutapata maji kutokana na mradi ule ili kupunguza adha ya maji katika Wilaya ya Muheza?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji majibu.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa Muheza ni kweli tumesaini mkataba mwaka jana na kazi inaendelea vizuri na juzi tumelipa fedha, tunatoa bomba la maji kutoka tenki la Pongwe kupeleka katika Mji wa Muheza. Sasa hivi mkataba bado unaendelea siyo kwamba mkataba umekamilika, kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge nikuhakikishie kwamba ule mradi ukisha kamiliaka maji yatapatikana Muheza.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete swali la nyongeza.

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Waziri nafikiri leo unatambua kwamba leo ndio tarehe ya mwisho ya ule mradi maji Chalinze, ninachotaka hapa ni kusikia kauli ya Serikali juu ya nini sasa kinafuata baada ya leo kuwa *deadline* ya ule mkataba wetu wa ujenzi wa Mradi wa Maji Chalinze?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji majibu.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kauli hiyo unayoizungumza iko katika taratibu za kimikataba, nikishauri tu Mheshimiwa Mbunge sisi

wanasiasa watunga sera si vyema tuingilie mikataba, tusubiri kwanza utekelezaji wa mikataba ufanyike hatua zitakazochukuliwa basi tutazitolea taarifa.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza maswali tuliyokuwa nayo leo, kwa hiyo tutaanza na matangazo ambayo yametufikia.

Tangazo la kwanza ni tangazo la wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, tutaanza na wageni wa Waheshimiwa Wabunge.

Kundi la kwanza ni wageni 11 wa Mheshimiwa Jenista Mhagama ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu na Mnadhimu Mkuu wa Serikali. Wageni 11 wa Mheshimiwa Jenista, karibuni sana hawajasema wanatokea wapi, lakini mnakaribishwa sana Bungeni. (*Makofii*)

Pili, ni wageni 41 wa Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum ambao ni viongozi wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi kutoka Wilaya Saba za Mkoa wa Dodoma wakiongozwa na Mwenyekiti wa Jukwaa hilo Ndugu Faustine Sabugo, karibuni sana.

Pia tunao Wageni Wawili wa Mheshimiwa Yosepher Komba ambao ni Mwenyekiti wa Kijiji cha Kwalubuye ambaye Ndugu Mwanahamisi Shabani na Katibu wa Kata ya Kicheba Ndugu Musa Kopwe kutoka Muheza, Mkoani Tanga, karibuni sana. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni 32 wa Mheshimiwa Antony Mavunde ambaye ni Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira ambao ni Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM – Tawi la Reli kutoka Mkoani Dodoma, karibuni sana. Pia tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Alex Raphael Gashaza ambao ni viongozi wa *Rusumo Faus Hydroelectric Power Project* kutoka Ngara, Mkoa wa Kagera, wakiongozwa na Meneja Biashara, Ndugu Huang Liang, karibuni sana. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, tunae pia mgeni wa Mheshimiwa Venance Mwamoto ambaye ni Mwenyekiti wa Wazazi Wilaya ya Kilolo, Mchungaji Johanis Salufu, karibu sana. Tunao pia wageni sita wa Mheshimiwa Pauline Gekul ambao ni viongozi wa Halmashauri ya Mji wa Babati na wazee kutoka Wilaya ya Babati, Mkoa wa Manyara, wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Mheshimiwa Mohamed Kibiki, karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni walio tembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ambao ni wanafunzi 75 na Walimu 15 wa shule ya sekondari ya wasichana ya St. Monica ya Jijini Arusha, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wanafunzi 95 na walimu watatu kutoka shule ya sekondari Kigwe ya Mkoani Dodoma, karibuni sana. Pia tunao wanafunzi 54 kutoka Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijiji Mkoani Dodoma, karibuni sana wageni wetu Bungeni. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge ninayo pia matangazo mengine mawili, tangazo la kwanza linatoka kwa Mheshimiwa Dkt. Suleiman Ally Yussuf, anawatangazia Wabunge wote waislamu kwamba mkutane katika Ukumbi wa *Annex Dispensary* saa 7.00 mchana leo, mara baada ya kuahirisha shughuli za Bunge, kwa hiyo mnaombwa mkutane ukumbi wa *dispensary*.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwa Mheshimiwa Maftaha Nachuma anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba *caucus* ya CUFimefanya uchaguzi na wamemchagua Mheshimiwa Kiza Hussein Mayeye kuchukua nafasi aliye kuwa Mheshimiwa Maulid Mtulia ambaye alikuwa ni Mnadhimu ya Kambi hiyo, kwa hiyo anawatangazia kwamba Mheshimiwa Kiza Mayeye ndiye atakuwa Mnadhimu sasa. (*Makofi*).

Waheshimiwa Wabunge, yako mambo yanayozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge na

ninalazimika kuyatolea ufanuzi hasa kuhusu maswali humu Bungeni. Kanuni zetu zinazohusu maswali zipo nyngi katika hizi Kanuni zetu na yule ambaye anaafuatiilia akiwa na Kanuni zetu anaweza kuanza Kanuni ya 38 mpaka Kanuni ya 46.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni hizi sitaziizungumzia zote nitazungumzia moja inayohusu maswali ya nyongeza maana Wabunge mnaandika hapa mbele mambo mengi mkilalamika kuhusu utaratibu unaotumika. Kwa hiyo, nitaisoma Kanuni ya 44 inayohusu maswali ya nyongeza ili wote tuwe na uelewa wa pamoja.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 44(1)inasema maswali ya nyongeza yanaweza kuulizwa na Mbunge ye yeyote kwa madhumuni ya kupata ufanuzi zaidi juu ya jambo lolote lilitotajwa katika jibu lilitotolewa. Mbunge anayeuliza swali la msingi ataruhusiwa kuuliza maswali ya nyongeza yasiyo zidii mawili na Mbunge mwengine yeyote atakayepewa nafasi ataruhusiwa kuuliza swali moja tu la nyongeza.

Kanuni ya 44(3) kwa madhumuni ya Kanuni hii swali ambalo litawekwa katika vifungu vya (a) na (b) litahesabiwa kuwa ni maswali mawili. Fasili ya 4 isipokuwa kama Spika ataaelekeza vinginevyo Wabunge watakaouliza maswali ya nyongeza hawatazidi watatu kwa swali moja la msingi na Mbunge hataruhusiwa kusoma swali lake.

Waheshimiwa Wabunge, tunakumbushana siku zote kuzisoma hizi Kanuni, ziko nyakati Waheshimiwa Wabunge mnapouliza maswali yenu mnasoma na ziko nyakati mnapouliza maswali ya nyongeza yanakuwa ni marefu kupita muda ule ambao tumejiwekea kwenye Kanuni zetu kwa maana ya Kanuni ya 43 na kwa hiyo, muda ambao Kanuni 43 inasema muda wetu wa maswali ni saa moja na nusu kwa kipindi ambacho si cha Bunge la Bajeti na wakati wa Bunge la Bajeti muda wa maswali ni saa moja, idadi ya maswali anayepanga ni Mheshimiwa Spika kwamba maswali yawe mangapi.

Waheshimiwa Wabunge, sasa yapo maswali ambayo

huulizwa na aliyekalia Kiti hatoi swali la nyongeza kwa Mbunge ambaye si mwenye swali.

Kwa hiyo, kwa mujibu wa Kanuni ya 44 siyo kosa la Kiti kuto kutoa swali kwa mtu ambaye si mwenye swali, hiyo ni kwa sababu Kanuni hii inasema Mbunge mwingine yejote atakayepewa nafasi, kwa hiyo kama hukupewa nafasi si haki yako kuuliza swali la msingi. Kwa maana hiyo, wakati mwingine muda ukiwa umebanda Kiti kina uwezo wa kufanya kinavyoona kinafaa kwa maana ya kwamba muuliza swali la msingi ndiye ambaye apewe maswali ya msingi, watu wengine wote maswali yanatolewa kwa mujibu wa muda uliopo na Kiti kinavyoona inafaa. Hivyo yale malalamiko tuliyonayo tupitie vizuri Kanuni zetu ziko vizuri na ninaamini kwamba wote tutakuwa tumelewana kwenye jambo hilo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo ninamkaribisha sasa Mheshimiwa Chenge ili aweze kuendelea na ratiba inayoendelea.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya dharura.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwanza nikiwa nimesimama hamruhusiwi kuzungumza, wale wanaozungumzia hoja la dharura ama mwongozo, wote mnapaswa kunyamaza, atakapokaa anayekuja unaweza kuzungumza kama anataka kukusikiliza.

Sasa kwa sababu mtu akisimama hapa mnaendelea kuzungumza huko ndiyo maana mnadhani ni utaratibu, Kanuni zinakataza nikiwa nazungumza mtu mwingine kusimama na kuzungumza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Chenge karibu.

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Katibu.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya dharura, jambo la dharura.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, hata kama ni dharura nasema hivi asome hatua inayofuata.

NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA KAMATI

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo na Kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2017

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria Kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2017

na

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa Kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2017

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bashe.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, natumia Kanuni ya 47 sitaisoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo la dharura, *on top of it* ni jambo la masikitiko. Jana nilisimama ndani ya Bunge hili baada ya maswali, nikaeleza tatizo linaloendelea katika Halmashauri nyingi lakini tatizo *specifically* la maji lilioko Nzega. Mwenyekiti wa Bunge akaagiza Mawaziri wanaohusika wakutane na mimi tuweze kujadiliana juu ya jambo hili na litafutiwe *solution*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *as I speak* Halmashauri ya Mji wa Nzega leo ni siku ya 13 haina maji. Hospitali ya Wilaya ya Nzega leo ninavyoongea imekosa maji imebidi nikodi maboza kwa ajili ya kupeleka maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili limekosa majibu toka mwezi wa Julai mwaka jana. Siyo tu la Halmashauri ya Nzega bali la Halmashauri nyingi katika nchi hii. Wizara ya Nishati, Wizara ya Maji, Wizara ya Fedha na Wizara ya TAMISEMI hailichukulii jambo hili kuwa ni jambo la dharura. Wananchi wa Halmashauri ya Mji wa Nzega wanaadhibiwa kwa uzembe uliofanywa na Serikali *for the last 10 years*. Wananchi wa Nzega hawadaiwi hata shilingi moja ya maji. Narejea, hawadaiwi hata senti moja ya maji, lakini leo wanaoadhibiwa ni wananchi wa Nzega.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *this is unfair to my people* na *I am ready to take any risk for this!* Ninasema hili jambo lijadiliwe ndani ya Bunge hili tupate *solution today*. Bunge hili linadharauliwa sana na *Executive*, bila kupata majibu juu ya masuala ya msingi *we can not continue like this! (Makofi)*

Ninaomba jambo hili lijadiliwe ndani ya Bunge, na ninataka niwaambie Wabunge wa chama changu *we can not allow wananchi waliotupigia kura na kumpa kura Rais wa nchi hii na Serikali ya chama chetu kuendelea kuwa - punished kwa arrogance ya Mawaziri*. Hawapeleki fedha za OC, hawafuati maagizo ya Bunge halafu wananchi wangu wanaumizwa, *we can not allow like this!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali leo tulijadili tupate *solution*, naweka *on record* kwamba jambo hili la wananchi wa Nzega kama Wabunge wengine wa majimbo ya CCM watakuwa tayari kuendelea na dharau hii, mimi siko tayari. Lolote litakalotokea Nzega, lolote litakalotokea Nzega dhambi hiyo ataibeba Waziri wa Fedha Dkt. Mpango, ataibeba Waziri wa Nishati Kalemani, ataibeba Waziri wa TAMISEMI Mheshimiwa Selemani Jafo, ataibeba Waziri wa Maji Mheshimiwa Isack Kamwele, *we cannot continue*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi wa Novemba nimekuja na Mkurugenzi wangu, nimeenda TAMISEMI, nimekutana na Waziri wa Maji, tumefanya *all necessary effort*, Serikali haijapeleka fedha za *utility for the last 10 years!* Why

are you suffering? Kwa nini mnawatesa wananchi wa Nzega, why? Ninaomba solution in a serious note. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru naomba natoa hoja Wabunge waniunge mkono. (*Makofi*)

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tuelewane basi.

Mheshimiwa Hussein Bashe ametumia Kanuni ya 47 na alisema hataisoma kwa sababu ya muda, ameelezea changamoto ambayo inawakumba wananchi wa Mji wa Nzega Jimboni kwake, hoja hii jana aliitoa tena lakini Kiti kilitoa mwongozo na kwa mujibu wa Kanuni zetu hii 47 ambayo lazima uisome pamoja na 48(4) ndiyo inayoniambia iwapo Spika ataridhika kwamba jambo hilo ni la dharura halisi.

Waheshimiwa Wabunge, changamoto ya maji ni kubwa nchini na ndiyo maana Mbunge anapouliza suala la maji unaangalia wale wanaosimama kuuliza maswali ya nyongeza wengi, ni kama ilivyo kwa umeme na ndio maana Mwenyekiti jana alitumia busara sana na mimi nataka niende huko huko kwamba hali ya Nzega ambayo anaifahamu sana Mheshimiwa Mbunge wa pale na Serikali, kwa sababu wana taarifa za ndani, sisi wengi tutakuwa ni kama wasindikizaji kwa sababu kama huna kitu hukifahamu utakuwa unachangia yale ya juu juu lakini hamuendi kwenye kiini cha changamoto hiyo.

Kwa hiyo, mimi narudi kwa yale aliyoelekeza Mwenyekiti jana kwamba upande wa Serikali uje kwa haraka sana katika kutoa majibu kwa suala hili. Kwa vile suala hili tumekwenda nalo tangu jana mnawezwa mkajua jinsi ambavyo mmejipanga lakini tutendee wananchi wetu haki. (*Makofi*)

Nashindwa mimi kuelewa kama kweli anayoyasema

Mheshimiwa Mbunge kwamba hatuna majawabu! Mimi naamini Serikali ingeweza ikajibu, ikatoa taarifa hali ilivyo kwa Nzega tukajua. Kwa hiyo, ninarejesha huko kwa Mheshimiwa *Chief Whip* yupo, kama una la kusema tusaidieni. Ahsante sana. (*Makofii*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuelewa sana kwa maamuzi yako ya Kiti ambayo umeyatoa hivi punde na hasa kwa kuzingatia unyeti wa jambo hilo, maelekezo yako uliyoyatoa ya kubainisha wazi kwamba tatizo hili ni lazima Serikali na Mbunge husika watakuwa wanalfahamu kwa undani na kwa jinsi vile ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupokea agizo hilo na mimi niwaombe Waziri wa Maji, Waziri wa Nishati, Waziri wa Fedha na Mbunge husika itakapofika 7.00 mchana leo tukutane ofisini kwangu ili angalau tulitizame hilo jambo na tuweze kupeana mwelekeo unaotakiwa wa kuona ni kwa kiasi gani tunaweza kutatua tatizo hilo. (*Makofii*)

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

MWENYEKITI: Tunaenda kwenye Mwongozo; Mheshimiwa Joseph Musukuma, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Mheshimiwa Mwita Waitara. Naongelea Mwongozo, msinifanye mimi kama mnansaidia kuongoza Bunge. Tunaongelea Mwongozo, Mheshimiwa Waitara, Mheshimiwa Mbarouk ni Mwongozo, Mheshimiwa Pascal na Mheshimiwa Flatei, samahani sana.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hukuniona mimi huku labda kwa sababu ni mfupi Mheshimiwa Nkamia Mwongozo.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kumbukeni

tuna shughuli mbele yetu hatuwezi kuishi kwa miongozo tu humu.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Mwongozo ni sehemu ya shughuli. Mimi naitwa Nkamia.

MWENYEKITI: Nani anamsemea Halima Mdee? Mimi ndio naweza kuamua. (*Kicheko*)

Tunaanza na Mheshimiwa Nkamia.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7) na kwa kuwa tuko wengi sina sababu ya kuisoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi hapa nilipata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kuhusu mradi wa maji wa Ntomoko ambao Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilitoa shilingi bilioni mbili kwenda Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Maji wa Ntomoko ambao ungehudumia Wilaya ya Kondoa na Wilaya ya Chemba. Leo tunavyozungumza hapa wananchi wa vijiji 17 ambao walikuwa wahudumiwe na mradi huu hawapati hata tone la maji. Lakini fedha ilikwenda kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa na imetafunwa yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Waziri amesimama hapa amesema wamegundua kwamba kweli kuna figisu figisu za ulaji wa fedha zile na wamezuia shilingi milioni 800 ziende *DUWASA* ili zikafanye kazi za mradi huu. Mheshimiwa Waziri amenijibu hapa, Mzee wangu namheshimu sana kwamba kwanza watashughulikia tatizo la maji baadae ndiyo washughulike na watu waliokula fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wangu naomba kujua hivi wale wananchi wa vijiji 17 watakuwa wanasubiri mpaka lini kupata maji, wakati Serikali inahangaika hangaika kwamba *DUWASA* waende wakafanye kazi wakati hapa hapa Dodoma Mjini yenyewe *DUWASA* inapata matatizo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilikuwa naomba halafu waliokula hela wanaachwa leo wanaendelea kupata mishahara ya Serikali hii iliyotoa fedha na huko walikohamishwa wanaenda kuharibu tena. Kwa hiyo, wakiharibu na kule watahamishwa tena wakati Serikali inafanya uchunguzi kule waliko wahamishwe tena sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako, kwa nini watu hawa kwanza wasitafutwe sasa, Serikali iwachukulie hatua wakati ikiendelea kushughulikia tatizo hili, kuliko kuwaacha wanafaidi matunda ya Serikali, halafu wakati huo huo wananchi wanapata matatizo huku chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Flatei.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nasimama kwa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nilikuwa na swali langu hapa namba 99. Swali hili nimelileta kwa mara ya nne leo hapa, swali hili linahusu sana Mji Mdogo wa Haydom ambao kimsingi una hospitali kubwa pale, majibu ya Serikali siyakatai lakini kila siku imebaki asilimia 10 ili mradi ukamilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko yangu pale taarifa Serikali inayo kwamba Mji wa Haydom umekumbwa na kipindupindu mara nyingi na huu mradi tumekuwa tukiulilia mara nyingi na mimi nimesumbuka sana nimekuja Wizarani hapa na Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi na timu yote ya Wilaya. Lakini nasikitika sana ahadi zimekuwa nyingi na nimezisema kwenye swali langu la msingi. Mheshimiwa Waziri amefika anajua na alipewa ahadi na mkandarasi pale akiwepo. Leo ni mwaka ule mradi haujakamilika, sasa tutakuwa tunaleta maswali huku na kupata majibu namna hii mpaka lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako

ili wananchi wangu wa Haydom na Hospitali kubwa iko pale ambayo inategemewa na Mikoa mitano hali ya pale ni mbaya mno. Haitofautiani kabisa..

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Halima Mdee.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako kwa kuzingatia mambo yafuatayo:-

Mosi, wakati Taarifa ya *LAAC* imetoa ripoti yao ya mwaka ilionesa kwamba kuna ujisadi mkubwa sana wa miradi ya maji; pili, wakati Mheshimiwa Bashe anatoa ripoti yake ya kuomba jambo la dharura lijadiliwe amebainisha kwamba kuna ujisadi mkubwa wa maji na utendaji mbovu wa Mawaziri; tatu, wakati Mheshimiwa Flatei anajenga hoja yake ameonesha kwamba kuna shida kubwa sana kwenye sekta hii ya maji, hali kadhalika Mheshimiwa Nkamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako, kwa kuzingatia kwamba Mheshimiwa Bashe amekidhi vigezo vya Kanuni 47 amekidhi, vigezo vya Kanuni 48(1) na (2) na zaidi amekidhi vigezo vya Kanuni ya Bunge 48(3) ambayo naomba ninukuu...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima Mdee kaa chini nakuomba. Uliomba Mwongozo wangu, hapana usiende kwenye dharura usinirudishe kwenye dharura. Usitumie Kanuni ya 47 *stick* kwenye 68(7).

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, uko sahihi kabisa kwamba ninaomba Mwongozo wako na kuomba Mwongozo hakuzuii kufanya marejea ya maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hivyo kwa sababu tunavyozungumza tatizo la maji linahusu maeneo yote na siyo Nzega peke yake. (*Makof*)

Kwa maelezo hayo jana Kiti kilielekeza Mawaziri wakutane na Mheshimiwa Hussein Bashe hawakukutana naye; na kwa kuzingatia sasa, kwamba kwa maelezo ya Wabunge wa CCM waliyotoa asubuhi hii kwa miongozo na kwa maelezo ambayo yamejibowi na Waziri asubuhi kwenye maswali, ninadhani naomba Mwongozo wako ni kwa nini hili jambo usilione ni la muhimu kujadiliwa kwa udharura kwa sababu linahusu maeneo mbalimbali ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako ambao vilevile utaelekeza Mawaziri hawa, kama unadhani kwamba haiwezi kujadiliwa kwa dharura kwa sababu ya muda ikutane leo na Wabunge wote ambao wana kero hii kama hatujajikuta Bunge linatoa hapa kujadili haya mambo. Naomba Mwongozo wako kwa hilo na ninajua una busara sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante . Mheshimiwa Musukuma.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nnakushukuru sana na mimi natumia Kanuni hiyo ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi wakati nachangia kwenye mchango wangu kuhusiana na suala la uvuvi yalitolewa majibu mepesi na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Luhaga Mpina, lakini hivi sasa tunavyozungumza kwenye majimbo yetu tuna wapiga kura wanaoishi katikati ya maji yaani visiwani na nchi kavu. Wale watu wanaoishi Visiwani hawana mashamba hawana kitu kingine kazi yao ni uvuvi. Leo ni karibu siku ya saba *operation* ile inaendelea na tunavyozungumza kwenye Jimbo langu Kisiwa cha Izumacheri mtu mmoja amekufa kwa njaa jana. Majibu yaliyotolewa na Waziri ni kwamba sasa hairuhusiwi mtu yejote kukanyaga kwenye ziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile inaendelea *operation* ya kukamata pipipiki zina samaki mbili, tatu ili hali niliona jana kantini kumejaa sato na Wabunge mnakula. Pia tumeona kwenye *Bombadier* na *Air Tanzania* wanashushwa samaki kule kupelekea watu wengine huko Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako ni nini kauli ya Serikali inayomuelekeza Waziri Mpina kuendelea na *operation* ya uvuvi haramu na kuacha wavuvi halali waendelee kufanya kazi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete.

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Nasimama kwa Kanuni ya 68(7) nikiomba Mwongozo wako mapema leo niliposimama kuuliza swali la nyongeza kufuatia swali lilitoulizwa na dada Lathifah, majibu niliyopewa na Mheshimiwa Waziri wa Maji kwa kweli binafsi yangu hayakunifurahisha kabisa, nataka niliweke wazi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimetumwa na watu wa Chalinze, kwa maana Jimbo la Chalinze, Halmashauri ya Chalinze kuja kuuliza juu ya shida zao, sifanyi siasa katika jambo hili. Ninatambua kwamba mkataba wa maji baina ya Mamlaka yetu pale kwa maana ya *CHALIWASA, DAWASCO* na Wizara kwa maana ya Serikali na yule mkandarasi inakwisha leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninajua hilo, nauliza Serikali inipe juu ya nini kinafuatia baada ya mkataba huo kuisha, majibu ninayopewa na Waziri yanaonekana kama mimi nafanya siasa katika jambo la kitaalam. Nataka nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kwanza mimi ni mwanasheria, ninaelewa ninachokifanya na nimetumwa na watu walio na akili timamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia hapo hapo nataka nimkumbushe Mheshimiwa Waziri, ninaposimama leo hii hapa, huu ni mwezi wa pili sasa unakwenda wa tatu wananchi wanaoishi katika Halmashauri ya Chalinze hawapati maji kabisa. Sasa leo hii nasimama hapa unanijibu kwamba mimi nataka nifanye siasa, Mheshimiwa Waziri hata kama tulichaguliwa kwa siasa, lakini mimi sifanyi siasa, naomba nikupe taarifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu hii inafanya juhudini kubwa kuendeleza viwanda na Chalinze inafahamika kwamba ndio sehemu yenye chemchem ya viwanda kwa sasa, lakini cha kushangaza kukosekana kwa maji kumepelekea Kiwanda cha Sayona kufungwa, natoa taarifa hiyo hapa, kiwanda kimefungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi ninaposimama na ninapouliza nini kauli ya Serikali juu ya *way forward* baada ya mkataba huu kuisha siku ya leo, najibwa majibu ambayo yanakatisha tamaa sio kwangu mimi tu, lakini hata Rais wangu Mheshimiwa John Pombe Magufuli naye pia hayapendi majibu hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba, naomba Mwongozo wako juu ya kauli ya Serikali, juu ya nini kinafuatia baada ya mkataba huu kufa leo lakini nini ambachoo kinatakiwa kifanyike ili kuhakikisha kwamba sera iliyowekwa na CCM, sera iliyosimamiwa na Serikali yetu, inayosimamiwa na mimi Mbunge na maendeleo ya Chalinze na wananchi wangu wa Chalinze wanaohangaika kutafuta maji wakati maji tunayo, mradi upo lakini hatuelewi kinachofanyika...

MWENYEKITI: Umeelewaka Mheshimiwa Kikwete.

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

MWENYEKITI: Tunaendelea, Mheshimiwa Susan Kiwanga.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nasimama kwa Kanuni ya 68(7), nikiomba Mwongozo wako jambo ambalo kwa namna moja au nyingine limetokea hapa Bungeni lakini linafanana kabisa na ninachoombua mwongozo kuhusu majibu na ufuatiliaji wa Wabunge kuhusu masuala yanayotokea ndani ya majimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninapozungumza, Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Tizeba na Mkurugenzi wa

Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero amefuatilia karibuni wiki mbili zilizopita, kuna hatari kubwa kwa wakulima karibuni Jimbo la Mlimba hasa nasikia Wilaya 20 kimbunga cha panya kinakula mahindi na mpunga wote wanafukua, mpaka mahindi yaliyokuwa juu wanapanda wanakula yote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyosema sumu ya panya haipatikani na Wizara ya Kilimo ndiyo yenye haki ya kutuambia hiyo sumu inapelekwa huko na msimu wa kilimo unaisha tarehe 15 Februari na hakuna jitihada zozote za Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba Mwongozo wako na Bunge hili sasa tunaahirisha hivi kesho, ni nini sasa Serikali itoe kauli itapeleka sumu ya panya hasa Mlimba ili wakulima wale na Mlimba na Wilaya nydingine zipone kwa njaa na Rais anasema hakuna kutangaza njaa nchini. Naomba Mwongozo wako kuhusu kauli ya Serikali. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Mbarouk.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, asante, nimesimama kwa Kanuni ya 68(7) na hoja yangu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako, wakati nikijibowi swali namba 105 hapa, lilizungumzia suala la *transformerna* najua kwamba Serikali inaendelea na mradi wa *REA Phase III* lakini wakati kamati yetu ilipokwenda kutembelea huko, tulikuta kwamba wananchi wanalamika *transformerza 50KV*haziendeshi hata mashine tano za kusaga wala mashine za *welding* kumi haziwezi kuendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako, Waziri atueleze je, mpango ule tulioshauri kwamba *transformerzibadilishwe*, zimebadilishwa? Na nina amini hiso *transformer* kuwa hazina nguvu ndizo zinapelekea miradi ya maji ikawa ina matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile pia Mheshimiwa Bashe jana alizungumza hapa akitaka akutane na Mawaziri, leo ametueleza tena lakini tunaambiwa kwamba eti baada ya shughuli za Bunge watakutana na Mawaziri kwenye Ofisi ya...

MWENYEKITI: Mheshimiwa nimekuelewa.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaomba jambo la dharura kama hili kwa nini lisijadiliwe hapa, likajadiliwe ofisini wakati ni la kero la Wabunge wote wanaohusiana na masuala ya maji. Ahsante. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbarouk, Waheshimiwa Wabunge, kama mnataka kuchangia maana sasa hivi sasa mnaenda kusivyo. Mheshimiwa Waitara.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naomba Mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge liliopita, niliuliza swalii nyongeza na Mheshimiwa Naibu Waziri akaniahidi kwamba ataenda Ukonga na nilimuahidi kwamba aje Ukonga nimuitie wakina mama wa Ukonga ambao hawana maji na hasa wakati wa mvua kwamba wanachota maji yale machafu ndio wanakunywa, Naibu Waziri Mheshimiwa Aweso hakuja. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeypata taarifa ya miradi ya maji kwenye Kamati yetu ya TAMISEMI, taarifa ambayo walitupa ni kwamba mpaka sasa umepokea asilimia 25 ya bajeti ya miradi ya maji yote katika nchi nzima. Hii maana yake na hapa ukiangalia kila Mbunge aliyesimama na sijui Wabunge wa Tanzania wamerogwa na nani na hasa Wabunge wa CCM wamerogwa zaidi, tumeombwa hoja ya maji hapa hawakusimama. Naomba nikuhakikishie kwamba Wabunge wamesimama sio kwamba wanafurahia mambo haya, jambo hili ni jambo kubwa kweli kweli. Kitendo cha

kusema Mheshimiwa Bashe aende na Waziri ofisini kwake sio sawasawa. Kama bajeti haitoshi ilitakiwa Bunge lijadili ili tujue tunafanyaje kuondoa kero ya maji katika nchi hii... (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa...

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo jambo hili, ni kwa nini busara yako isitumike tulijadili wote kwa pamoja tupate majibu katika Taifa hili. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Pascal Haonga.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7) kuhusu jambo lilitotokea leo mapema Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na kaugonjwa ka baadhi ya Naibu Mawaziri wakati wanajibu maswali ya Wabunge wa Chama cha Mapinduzi wanawasifia sana kwamba wewe ni tingatinga, Mbunge makini, jembe; lakini wanapokuwa wanajibu maswali ya Wabunge kutoka upinzani wanajibu utafikiri wanasukumwa yaani kama vile hataki, yaani utafikiri Mbunge kama vile anambeza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali namba 100 lilipokuwa linajibowi na Kangi Lugola, alimuita Mheshimiwa Boniface Getere kwamba wananchi wanakuita tingatinga la maendeleo na hata jana pia limejirudia kuna Mbunge mwingine pia Naibu Waziri wa Maliasili akamwambia kijana mmoja anasema wewe ni Mbunge makini, lakini wanapojibu maswali ya upande wa pili inaonekana kwamba hayo maneno hayapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tuelewe, nataka Mwongozo wako hawa Mawaziri na Naibu Mawaziri wanalipwa kodi za Watanzania lakini inaonekana wanafanya kazi ya siasa hapa Bungeni. Sasa jambo hili linaruhusiwa au haliruhusiwi? (*Makofii/Kicheko*)

MBUNGE FULANI: Wewe huna umakini!

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, mmeomba miongozo lakini mengi naona mlitaka kuchangia tu na kutoa yale mliyonayo moyoni.

Nianze na Mheshimiwa Nkamia, maana nilikua naangalia hapa orodha ya maswali, Mheshimiwa Nkamia wewe uliuliza swali la nyongeza na mwenye swali la msingi alijibowiye yeye hajasimama kulalamika, wewe umejaribu kutoa ushauri kwa Serikali.

Mwongozo wangu kwa upande wa kwako ni ule ule ambaao nimekuwa nikisema tuzingatia mwongozo alioutoa huko nyuma Mheshimiwa Spika wetu kwamba wewe kama hukuridhika na swali la nyongeza ambalo halikutokana na swali la msingi la Mbunge mwingine andaa swali lingine tu lakini huwezi ukalalamika kwamba hukupewa majibu ya kutosheleza.

Kwa hali ile uliyoeleza kuhusia na vijiji 17 kwa Mradi wa Ntomoko mimi nadhani Wizara ya Maji wapo, waendelee kulishughulikia hilo.

Mheshimiwa Flatei swali namba 99, hoja yako ni kwamba hiyo asilimia 10 iliyobaki kukamilisha kazi hii, wananchi wa Haydom wapate maji itakamilika lini. Nilimsikia Waziri akijibu katika majibu ya Serikali kwa swali lako la msingi.

Sasa kama unadhani majibu ya Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI hayatoshelezi, itabidi Sekretarieti tuangalie jinsi swali lako liliyyoulizwa na majibu ya Serikali kama kuna upungufu wowote. Kama itaonekana kwamba kuna upungufu kwamba kuna maeneo hayajibowi basi tutasema lirejeshwe ili lijibowi tena.

Kwa maelezo yako wewe mwenyewe nilivyokusikia sasa hivi, unasema yamekuwa ni majibu yale yale ya Serikali, ahadi zile zile lakini hukusema kwamba majibu yaliyotolewa na Serikali kwamba hayajitoshelezi. Mimi nasema acha

tuangalie tuone kama kweli ulichokiuliza kimejibiwa kikamilifu kwa mujibu wa Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Halima Mdee, hata mimi nilisema tatizo la maji nchini ni kubwa ndio maana nikasema tukichukua *specific issue* ya Mheshimiwa Bashe ambaye alikuwa anaomba dharura, nikasema tutaanza kuongea haya haya, mimi nitaanza kuongelea ya Bariadi, huyu ataongea ya huku, tutatoka kwenye hoja ya Nzega.

Sasa ndio maana niliishukuru sana Serikali iliposema saa 7.00 mchana tutakapositisha shughuli za Bunge, Mawaziri ambao Mnadhimu Mkuu wa Serikali humu Bungeni amesema wakutane ofisini kwake, mimi ningeenda zaidi ya hapo sasa kwamba wakutane hiyo saa saba au muda watakaoona baadae, lakini saa 11 jioni Bunge litakaporudia tungependa angalau majibu yoyote yatakayopatikana yaweze kutolewa humu. Nadhani ndio tutakuwa tunaenda vizuri na eneo hili. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, mzunguko wa bajeti ya Serikali ni keshokutwa tu, tutakaporejea mwezi ujao shughuli kubwa itakuwa ni hiyo. Kwa hiyo, mengi haya kwa upande wa sekta ya maji, uchambuzi ambao umeonekana iwe ni kwa kupitia Kamati ya LAAC, kama kuna ubadhirifu, mapungufu ambayo yapo na *way forward* mtayasema na mmekuwa mnayasema vizuri tu. Sasa mimi nadhani mengine sio lazima tuyaseme wote, tuweke na akiba pia.

Changamoto ya maji ndugu zangu ni kubwa, Mheshimiwa Nkamia, Mheshimiwa Flatei, Mheshimiwa Bashe na Mheshimiwa Waitara ni maji na wengine ni maji. Kwa hiyo, mimi nasema ni changamoto ambayo lazima tujue lakini sio kwamba eti na Serikali inajifanya kwamba haitaki kuleta huduma ya maji kwa wananchi, hapana kuna sababu.

Mheshimiwa Musukuma mambo ya juzi hayo leo hatuwezi kuyarejesha humu. Kanuni ya 68(7) uliyoiombea Mwongozo ni jambo ambalo limetokea mapema leo. Sasa

juzi ilikuwa juzi, lakini hoja yako mimi nadhani Serikali wameisikia, hatuwezi kujifanya tu maana Serikali si ni wananchi, Serikali hii inatokana na wananchi, matatizo ya wananchi ni ya Serikali. Kwa hiyo, unataka sasa wewe uyasilizile, kama sheria hajakaa vizuri waambieni wananchi kwamba sheria hajakaa vizuri tunataka kuinyoosha kwa utaratibu huu. (*Makof*)

Mimi nadhani hilo endeleeni kulichukua, lakini ipo changamoto, Wabunge hawa ni wawakilishi wa wananchi hao, tusipuuze puuze haya walijonayo. Mimi nasema sasa *operation* inayoendelea ni *operation* ya Serikali, jinsi wanavyoitekeleza mimi nisingependa kuingia ndani huku, lakini mimi ninaamini watakuwa na maelezo ya kutosha. Kwa Mwongozo wangu nasema hajaingia kwenye dira ya mimi kulipatia Mwongozo kwa sababu halikutokea mapema leo. (*Makof*)

Mheshimiwa Ridhiwani, ni mambo ya maji, swali liliulizwa na Mheshimiwa Lathifah Chande ninavyokumbuka mimi, Mheshimiwa Ridhiwani ukapewa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza ukauliza vizuri, ukajibiwa.

Narudia palepale, endapo hukuridhika na majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji au Naibu wake, wewe huwezi ukaja kwa kulilalamikia namna hiyo. Lakini una haki sasa baadae ya kuja kuwasilisha swali *specific* kuhusiana na mkataba unaokwisha leo, *way forward* yake inakuwa nini. Huo ndio Mwongozo wangu kwa eneo hilo.

Mheshimiwa Susan Kiwanga, Mlimba kule panya kama ilivyo maeneo mengine, wadudu wale wanaoharibu mahindi na pamba na nini, kwako nadhani ni panya. Sasa hawa panya waharibifu na viwavi jeshi, Serikali jana niliwasikia kwa mbali, lakini ni tatizo hili. Mimi nadhani wanaweza wakalitolea majibu, lakini na lenyewe kwa taratibu zetu halijatokea mapema leo humu Bungeni, sijaona panya humu akija kutafuta..., kwa hiyo, nielewe namna hiyo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mbarouk nimekuelewa, lakini haya malalamiko ya majumuisho mimi nilikuwa nakuomba tu Mheshimiwa Mbarouk sijakupatia Mwongozo lakini tusifanye majumuisho kwa hali ya Tanga Mjini au viunga vyake kwamba *transfomer* kama imekuwa na upungufu unataka kusema nchi nzima *transfomer* ambazo zimeletwa zinakuwa na upungufu kama uliouona mahali fulani, nadhani itakuwa sio sahihi. Lakini ukiongelea *specific* na mtu akifuatilia wataenda kusema kitaalam kwamba kuna upungufu hapa na nini na nini kifanyike.

Lakini mimi nadhani nitapenda kusikia upande wa Serikali kwenye eneo hili la umeme kwa sababu limegusiwa sana na nilivyokuwa naangalia leo waliokuwa wanasmama maswali ya nyongeza walikuwa wengi. Kwa hiyo, nitaipatia Serikali waseme kidogo kwa upande wa umeme.

Mheshimiwa Waitara, ni maji, ahadi ya Naibu Waziri alikuahidi kwenda jimboni kwako, mkumbushie tu, Mwongozo wangu ni kwamba hili suala halijatokea leo humu, Mheshimiwa Waitara, halijatokea humu na wewe unajua. Nioneshe wapi ambapo nimefungua maji ya Ukonga hapa, sikuyaona. Lakini mimi nakuelewa vizuri sana, unataka ahadi ya Serikali itekelezwe. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Pascal Haonga, ndiyo Kanuni, wewe unasema kwamba Mawaziri hawa wanaposimama kujibu maswali yanayoulizwa na Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi wanapambwa sana kuliko Upinzani. Sasa nianze na hatua moja, Mwongozo wangu, je, inakatazwa au inaruhusiwa?

Kanuni inasema kujibu maswali yanayoulizwa na Waheshimiwa Wabunge kikamilifu, lakini unajua pia ni siasa, tuko Bungeni, wananchi wasikie, hakuna ubaya kusifu kazi inayofanywa na kiongozi mwenzako na hiyo ndiyo inakuwa chachu na kwa wengine ambao tunaona hatufanyi vizuri kujitahidi tufanye vizuri. Huo ndiyo mwongozo wangu kwa hayo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, angalieni muda tuliochukua. Ndiyo, mimi ndio Mwenyekiti, sasa msije mkalalamika mbona muda wa kuchangia umekuwa kidogo finyu, tumekula sana muda. Lakini ni kazi yetu Waheshimiwa Wabunge. Niite Serikali iseme kidogo, Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeyapokea maelekezo yako vizuri sana lakini ili kuweka rekodi za kikao hiki vizuri, nadhani ni lazima pamoja na Serikali kukutana saa saba kama nilivyokuwa nimeahidi hapa, ni lazima tutoe taarifa ya Serikali ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maagizo yako, tumefanya *consultation* ndani ya Serikali na tumegundua kwamba yale maagizo ya Serikali ya jana si kweli kwamba Serikali haikutana na Mheshimiwa Bashe, Waziri wa Nishati alipata nafasi ya kuzungumza na Mheshimiwa Bashe na yako mambo ya msingi ambayo walikubaliana na kuagizana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa sababu Serikali hii inafanya kazi kwa kuzingatia heshima ya Kiti chako, tutakuwa tayari kukutana saa saba kama tulivyoahidi ndani ya Bunge, lakini tunaomba kurekebisha rekodi zetu kwamba Serikali imeshakutana na Mheshimiwa Bashe...

TAARIFA

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Jana na Waziri wa Nishati na Madini alifanya hivyo jana.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa msemaji, nimekutana na Waziri wa Nishati jana kabla ya agizo la mimi kuinuka kutoa taarifa juu ya tatizo la Nzega, *that is number one*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, hatujakubaliana, na ndicho kilichosababisha kuleta hili jambo ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, tofauti ya msimamo kati ya Halmashauri ya Nzega na Wizara ya Nishati, Wizara ya Fedha, Wizara ya TAMISEMI, Wizara ya Maji, ni jambo ambalo tumetofautiana kwa zaidi ya miezi sita. Jukumu la deni hili sio la Halmashauri ya Nzega, madeni haya ni ya *central government* ambayo yalitakiwa yalipwe, na *central government* haijapeleka fedha za *utilities*, naomba nieleweke, fedha za *utility* kwa ajili ya umeme na maji katika Wilaya ya Nzega kwa miaka tisa, kwa hiyo, hatuwezi kubebesha wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa hiyo hatujadiliana jambo hili, ...kwenye *corridor*.

MWENYEKITI: Endelea Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Bashe awe mtulivu katika jambo hili...

WABUNGE FULANI: Aaaah!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa na maana ifuatayo...

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, hebu muacheni Mheshimiwa Waziri ajibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hapa ya msingi ni Serikali kuhakikisha kwamba inakutana na kushughulikia suala hilo, hiyo ni ya kwanza, hiyo ndio hoja ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hoja inayoambatana na hiyo hoja ya msingi ni utayari wa Serikali kukutana na Mbunge, jambo ambalo hata Mbunge yeye anakiri kwamba Mawaziri tayari walishaanza kukutana naye toka jana. Kwa hiyo, ninaomba Bunge hili lielewe kwamba hakuna tabia yoyote ya Mawaziri hawa ambayo inataka kuonekana ndani ya Bunge lako kwamba hawako tayari kutii maagizo ya Kiti na kufanya kazi na Wabunge kama inavyotaka kujitokeza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka niliweke hilo sawa, kama kweli Mheshimiwa Waziri alithubutu kukutana na Mbunge na kumfuata kwenye kiti chake, ni dalili ya kwamba Mawaziri walikuwa wasikivu na walitekeleza wajibu wao wa kufanya hivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naendelea kusisitiza kwamba sisi Mawaziri tutakutana na tutakutana na Mbunge, na hizo hoja zote mbili, ikiongozwa na hoja ya msingi ya kukutana na kumaliza tatizo hilo tutaifanya, lakini Bunge hili liondoke likiwa linaelewa kwamba Mawaziri tumekuwa tukitii Kiti na tumekuwa tukikutana na Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti na wewe ni shahidi, hata Wabunge wengine wamekuwa wakitutembelea kwenye viti vyetu kwa ajili ya kuomba tuwasaidie katika matatizo mbalimbali yanayowakabili. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Kalemani.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Bashe kusema ukweli kwa niaba ya Wabunge wote ambako kuna shida ya maji nchini,

nampongeza sana kwa sababu ameshuhudia sana kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme, pamoja na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Jenista, niongeze tu kwamba tumekuwa tukikutana sana na Mheshimiwa Bashe. Tumekutana jana mara nne, jana; mara mbili kabla na mara mbili baada ya hoja yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata leo tumekutana mara mbili, leo, kwa jambo hilihili.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Nataka nimpe majibu.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitambue umuhimu wa maji kwa wananchi wote, kero ya maji nchini ni kubwa na sisi kama Serikali tungependa kuona wananchi wote wanapata maji. Sisi kupitia Bunge lako tukufu nitumie nafasi hii kuwapongeza sana Mheshimiwa Bashe, Mheshimiwa Ngeleja na Mheshimiwa Bulaya, wamekuwa wakija. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Bulaya wananchi wake wamefunguliwa maji, Mheshimiwa Ngeleja wananchi wake wamefunguliwa maji. Jana Mheshimiwa Bashe nimemuomba Mkurugenzi wake akakutane na Meneja wangu aji-*commit afunguliwe* maji, Mkurugenzi wake inavyoonekana amegoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe, tutakaa na Mheshimiwa Bashe, wananchi wake wataji-*commit* na wataendelea kupata maji, tutazungumza pamoja. Lakini niseme Halmashauri ya Nzega inadaisha milioni 320; ni kweli ni za zamani kama ambavyo Mheshimiwa Bashe anasema, lakini la msingi wananchi wapate maji. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Bashe, tutakutana tena hata kama ni mara kumi wananchi wa Nzega waendelee kupata maji. (*Makofii*)

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niweke kumbukumbu sawa...

MWENYEKITI: Nakushukuru sana...

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, hapania, nakuomba...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bashe, tafadhali, unajua kanuni, huwezi kuanza kuongea tu kama unavyotaka. Naelewa changamoto ya maji ya wananchi wako, lakini tusikilize na yanayosemwa na Serikali. Mabishano hayatusaidii, tunataka tutanzue changamoto iliyo mbele yetu.

Suala hili kama alivyosema Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, waende wakakutane na kukutana tunapokutana kujadiliana sio lazima tuafikiane kila kitu, ni ukweli tu huo tusilazimishe kwamba mambo yake lazima yakubalike. Mimi nadhani wakakutane lakini sasa Serikali itatoa taarifa na kuelezea mahali penye tatizo ni wapi ili wote tujue.

Mheshimiwa Bulaya, usicheze ngoma usiyoifahamu, nakuomba, nakutolea mfano tu. (*Kicheko*)

Namuita Makamu wa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo na Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club*, Mheshimiwa Ngeleja. (*Makofii*)

MHE. WILLIAM M. NGELEJA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa niaba yako binafsi kama Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo na kwa niaba ya Kamati yetu, sasa niwasilishe Taarifa ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2017 hadi Januari, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuturuzuku uhaki na kutuwezesha kuendelea na utekelezaji wa majukumu yetu kikamilifu. Nitumie fursa hii kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo kumkumbuka aliyejewa Mjumbe wa Kamati hii, Mheshimiwa Leonidas Tutubert Gama, aliyejewa Mbunge

wa Songea Mjini ambaye alifariki mwezi Novemba, 2017. Tutaendelea kukumbuka na kuenzi mchango muhimu alioutoa kwa Kamati hii pamoja na Bunge kwa ujumla wakati wote alipokuwa Mbunge kwa kuiga mfano wake wa uwajibikaji. Tukumbuke kwamba wote tu wa Mwenyezi Mungu na kwake tutarejea, Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya ya utangulizi, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu matokeo ya uchambuzi wa sheria ndogo ili Bunge liweze kuipokea na kujadili taarifa hii pamoja na maoni na mapendekezo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu nne, sehemu ya kwanza inahusu maelezo ya jumla, sehemu ya pili inatoa matokeo ya uchambuzi wa sheria ndogo, sehemu ya tatu inahusu maoni na mapendekezo na sehemu ya nne na ya mwisho ni hitimisho na uwasilishaji wa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Kamati ya Sheria Ndogo yameelezwa katika kifungu cha 11 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kwa mujibu wa kifungu hicho, Kamati inalo jukumu la kuchambua sheria ndogo zilizotungwa na mamlaka mbalimbali ili kujiridhisha iwapo zimekidhi matakwa na masharti ya Katiba, sheria mama na sheria nyingine za nchi. Madhumuni ya kanuni hiyo ni kuliwezesha Bunge kutekeleza mamlaka yake ya udhibiti ya utungaji wa sheria ndogo (*Parliamentary control over subsidiary legislation*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwa makusudi kabisa kuchukua fursa hii kukumbusha kuwa sheria ndogo ni sehemu ya sheria za nchi kama ambavyo umekuwa ukieleza. Maelezo ambayo yanakubaliana pia na kauli ya wataalam katika kitabu chao cha *How Parliaments Works*. Naomba kunukuu maneno hayo kama ifuatavyo, ni sehemu tu ya maneno mengi yaliyoelezwa katika nini maana hasa ya sheria

ndogo; “*The delegated legislation is law made by Ministers or certain public bodies under powers given to them by Acts of Parliament but it is just as much part of the law of the land as are those Acts*” mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza kutafsiri maneno hayo kwa kusema kuwa sheria ndogo zilizotungwa na Mawaziri ama mamlaka fulani za umma chini ya madaraka yaliyokasimiwa kwao na sheria ya Bunge lakini sheria hizo ni sehemu ya sheria za nchi kama ilivyo kwa sheria zinazotungwa na Bunge moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Ibara ya 64 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, moja ya marekebisho yake, Bunge ndicho chombo chenye mamlaka ya kutunga sheria. Aidha, Ibara ya 97 ya Katiba imeliruhusu Bunge lako tukufu kukasimu madaraka ya kutunga sheria kwa mtu ye yeyote au kwa idara yoyote ya Serikali. Hata hivyo, ruhusa hii haiondoi wajibu wa msingi wa Bunge wa udhibiti wa kundi hili la sheria za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Tafsiri ya Sheria za Nchi, Sura ya Kwanza imeweka masharti maalum yanayolipa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mamlaka ya udhibiti wa sheria ndogo zinazotungwa na Serikali pamoja na vyombo vyake. Msingi huo unaipa Kamati uwezo wa kufanya uchambuzi wa sheria ndogo kwa niaba ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna njia ambazo zinatumika kutekeleza majukumu ya Kamati yetu, na ninaomba niseme kama ifuatavyo; kwamba baada ya sheria ndogo kutungwa na mamlaka husika na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali, sheria ndogo hizo zinatakiwa kwa mujibu wa kifungu cha 38(1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kuwasilishwa Bungeni ndani ya siku sita ya vikao vya Bunge katika Mkutano husika. Masharti haya pia yanapewa nguvu na Kanuni ya 37(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 inayosomeka kama ifuatavyo, nanukuu; “Nakala za matoleo yote ya Gazeti pamoja na Nyongeza zake zilizochapishwa tangu kikao cha mwisho cha Mkutano

wa Bunge uliopita, zitawasilishwa Bungeni na Waziri na kugawiwa kwa Wabunge."

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hiyo inatoa fursa kwa Bunge kufanya uchambuzi wa sheria ndogo iliyowasilishwa Bungeni kwa mujibu wa kifungu cha 38(1) cha Sheria ya Tafsirri ya Sheria kikisomwa kwa pamoja na kifungu cha 11 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ndogo ambazo hutungwa na vyombo mbalimbali nya Serikali ambavyo Bunge limekasimu kwake madaraka ya kutunga sheria ni nyngi. Hivyo basi, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati imejiwekea utaratibu wa kutekeleza wajibu wake kwa kufanya yafuatayo:-

- (i) Kuandaa orodha ya sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Bunge.
- (ii) Kufanya uchambuzi wa awali wa sheria ndogo zote zilizowasilishwa.
- (iii) Kuandaa jedwali la uchambuzi wa Kamati (*matrix*) linalobainisha matokeo ya uchambuzi wa Kamati na kuliwasilisha Serikalini kuititia Ofisi ya Waziri Mkuu ili kupata majibu ya hoja mbalimbali zilizoibuliwa kuhusu sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni.
- (iv) Kukutana na Wizara husika ili kupokea majibu ya Serikali kutokana na uchambuzi wa Kamati.
- (v) Kuwasilisha Bungeni taarifa kuhusu uchambuzi wa sheria ndogo uliofanywa na Kamati kutoa maoni na mapendekezo ili Bunge liridhie kwa azimio la Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa Serikali.
- (vi) Kupokea taarifa ya utekelezaji wa Serikali itokanayo na maoni na mapendekezo ya taarifa ya Kamati kuhusu uchambuzi wa sheria ndogo kama ilivyoazimiwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hizo za utekelezaji wa majukumu ya Kamati zimeelezwa katika kielelezo chetu ambacho kimeambatanishwa kwenye taarifa rasmi na ninaomba kwa sababu ya *interest*ya muda hatuwezi kusoma taarifa yote kwa urefu wake, lakini naomba *Hansard* liingize taarifa yote kwa mapana yake kama ilivyo.

Kwa hiyo, nasema kielelezo namba moja cha taarifa yetu kina maelezo yanayotoa muhtasari wa mchakato wa udhibiti wa Kibunge wa sheria ndogo zilizowasilishwa Mezani baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nielezee kazi zilizotekeliza kwa kipindi cha Januari, 2017 hadi Januari, 2018. Katika kipindi cha Januari, 2017 hadi Januari, 2018, Kamati ilitekeleza kazi ya uchambuzi wa sheria ndogo mbalimbali 404 zilizowasilishwa Bungeni na Serikali. Sheria hizo ziliwekwa mezani katika Mkutano wa Sita, Mkutano wa Saba, Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa uchambuzi, Kamati, pamoja na mambo mengine muhimu, ilitaka kujiridisha sheria ndogo hizo kama:-

- (i) Zinakiuka misingi ya Katiba pamoja na haki za binadamu;
- (ii) Zimewekwa masharti yasiyoendana na uhalisia, yasiyotekelzeka;
- (iii) Zina kasoro za kiuhariri na kiuandishi; au
- (iv) Zinakinzana na Sheria Mama au sheria nyingine za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutimiza dhana ya udhibiti wa Kibunge kwa mamlaka zilizokasimiwa kutunga sheria ndogo katika kipindi hicho Kamati pia ilipokea taarifa ya sheria kuhusu utekelezaji wa mapendekezo yaliyotokana na uchambuzi wa Kamati kuhusu jumla ya sheria ndogo 173 zilizowasilishwa katika Mkutano wa Sita na wa Saba wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya uchambuzi wa sheria ndogo zilizowekwa Mezani katika Mkutano wa Sita na Mkutano wa Saba wa Bunge; tarehe 14 Septemba, 2017 Kamati iliwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu taarifa ya uchambuzi wa sheria ndogo 173 zilizowasilishwa katika Mkutano wa Sita na Mkutano wa Saba wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hiyo ya uchambuzi iliainisha kuwa katika Mkutano wa Sita wa Bunge, Serikali iliwasilisha sheria ndogo 48 ambapo kati ya hizo, sheria ndogo nane zilibainika kuwa na dosari mbalimbali au kuhitaji ufanuzi kutoka katika mamlaka zilizohusika. Matokeo ya uchambuzi yalidhihirisha kuwa kati ya sheria ndogo 125 zilizowasilishwa katika Mkutano wa Saba wa Bunge, sheria 70 zilikuwa na dosari mbalimbali au kuhitaji ufanuzi kutoka mamlaka zilizohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kulikumbusha Bunge lako tukufu dosari mbalimbali zilizobainishwa katika baadhi ya sheria ndogo, na dosari hizo ni kama ifuatavyo kwa ujumla wake.

- (i) Baadhi ya sheria hizo ndogo ambazo ziliwasilishwa kwenye Kamati yetu zilibainika kuwa zinakiuka misingi ya Katiba pamoja na haki za binadamu;
- (ii) Zimeweka masharti yasiyoendana na uhalisia na yasiyoteklezeka;
- (iii) Lakini pia ziko baadhi zinaonesha kwamba kuna kasoro za kiuandishi ikiwemo kukosea rejea kifungu cha sheria mama kinachotoa madaraka ya kutungwa kwake; kukokesea rejea ya kifungu ndani ya sheria ndogo kinachotoa mamlaka ya kutungwa jedwali ndani ya sheria ndogo hiyo; dosari za kiuandishi wa majedwali pamoja na makosa mengine ya kiuchapaji na kiuandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na taarifa ya kamati iliyowasilishwa Bungeni, Bunge lilipitisha maazimio kwa kila dosari iliyohainishwa hapo juu na kuitaka Serikali

iwasilishe taarifa na kuitaka Serikali iwasilishe taarifa kuhusu utekelezaji na mapendekezo ya Kamati. Ikiwemo marekebisho yaliyofanyika katika sheria ndogo hizo Bunge lilitoa muda wa Serikali ili iwasilishe taarifa kwenye Kamati ya Sheria Ndogo kabla ya Mkutano wa Tisa wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati yaliyotokana na uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Sita na Mkutano wa Saba wa Bunge. Katika eneo hili ili kuliwezesha Bunge kufuatilia ipasavyo na kudhibiti utungaji wa sheria ndogo, Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya Bunge kuhusu baadhi ya sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Sita na wa Saba wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hiyo ya Serikali ilijuisha sheria ndogo 77 zenye jumla za hoja 201 zilizojitokeza wakati wa uchambuzi. Aidha, kamati ilijulishwa hatua za utekelezaji wa marekebisho ya sheria ndogo 75.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kulihalifu Bunge lako tukufu kuwa Kamati ilibaini kwamba mapendekezo muhimu ya kurekebisha sheria ndogo mbili ambazo ni The Tanganyika *Law Society Election and Regulations* za mwaka 2016 zilizochapishwa katika *Government Notes No. 332* chini ya Wizara ya Katiba na Sheria na sheria ndogo za ushuru za Halmashauri ya Mji wa Nanyamba zilizochapishwa katika Gazeti la Serikali Na. 125 chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI mwaka 2017 hayajazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yako inaipongeza Serikali kwa kutekeleza maazimio ya Bunge lako tukufu. Taarifa ya Serikali imeonesha kuwa hoja zote za uchambuzi wa sheria ndogo 77 ziliwasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Sita na Saba wa Bunge zimejibowi ipasavyo kwa zaidi ya asilimia 97. Pamoja na pongezi hizo Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutekeleza maazimio ya Bunge kuhusu marekebisho ya sheria ndogo mbili nilizo zitaja katika taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Nane wa Bunge. Katika Mkutano wa Nane wa Bunge Serikali iliyasilisha mezani jumla ya sheria ndogo 141 na kati ya hizo sheria ndogo zenye hoja ni sheria ndogo 56 kwa uwiano kwamba sheria ndogo 21 ni marekebisho mbalimbali yalitokana na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati katika mukutano wa pili wa Bunge na sheria ndogo 35 zina hoja mbalimbali au kuhitaji maelezo kutoka kwa Waziri mwenye dhamana na sheria ndogo hizo. Hoja zilizobainika katika uchambuzi ni:-

- (i) Sheria ndogo kukiuka misingi ya Katiba pamoja na haki za binadamu;
- (ii) Sheria ndogo kuwa na kinyume na masharti ya sheria nyingine za nchi;
- (iii) Sheria ndogo kuwa na vifungu na majedwali ambayo hayaendani na maudhui ya sheria ndogo husika; na
- (iv) Sheria ndogo kunakili vifungu vya sheria ndogo za maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sheria ndogo husika kwenda kinyume na masharti ya sheria nyingine za nchi, tulichokibaini nikili kwamba katika uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Nane wa Bunge Kamati ilibaini baadhi ya sheria ndogo kwenda kinyume na masharti ya sheria zingine za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano ni kanuni ya 18 ya sheria ndogo za *The Surface and Marine Transport Regulatory Authority Act* ya mwaka 2017 iliyotungwa chini ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano inampa wajibu wa lazima Wakala wa *Clearing and Forwarding* kuwajibika kwa kosa linalofanywa na mwajiriwa ambalo linapelekea kuvunja masharti ya sheria ndogo. Masharti ya kanuni hii hayazingatii misingi ya sheria ya madhara yaani *vicarious liability* ambapo mwajiri hapaswi kuwajibika kwa makosa yanayofanywa na mwajiriwa ambayo yametendwa pasipo

ridhaa ya mwajiri, wake au wakati akiwa anatekeleza kazi za mwajiri wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri kuwa kanuni hii ifanyiwe marekebisho kwa kuondoa wajibu wa lazima kama inavyosomeka sasa na kuweka masharti ambayo yatazingatia vigezo vilivywewekwa kwa mujibu wa misingi ya sheria ya madhara ili kuamua iwapo mwajiri anahusika na kosa lilitendwa na mwajiriwa au la!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sheria ndogo kuwa na vifungu na majedwali hayaendani na maudhui sheria ndogo husika, katika eneo hili Kamati imebaini kuwa baadhi ya sheria ndogo hazizingatii masharti bora ya uandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kifungu cha (16) cha sheria ndogo za usafi wa hifadhi za mazingira za Halmashauri ya Mji wa Nzega za mwaka 2017 iliyotungwa chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kina maudhui ambayo hayaendani na sheria ndogo hii kwa kuwa kifungu kinazungumzia kuhusu usafi na hifadhi ya Ziwa Tanganyika. Ziwa ambalo kimsingi halipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Nzega badala yake linapatikana katika Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huu wa kunakili sheria ndogo umeendelea kuleta changamoto kwa kuwa makosa ambayo yanapatikana katika sheria ndogo moja yanahamishiwa katika sheria ndogo ya Halmashauri nyingine. Kamati inashauri dosari zilizobainika katika sheria ndogo hii zilekebishwe ili kukidhi masharti ya uandishi mzuri wa sheria ndogo. Mfano wa sheria ndogo ambayo ina maudhui yasiyo endana na sheria ndogo yenye we ni kanuni ya *The Petroleum Refinery Operations Rules* za mwaka 2017 iytungwa chini ya Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majedwali ya kwanza na ya pili ya kanuni hizi yamerejea kanuni ambazo si za kanuni hizi na pia hazijakamilika. Kamati inashauri kuwa majedwali yote yaliyobainika kuwa na dosari yafanyiwe marekebisho na kuainisha vifungu sahihi vinavyo yahanzisha. Halikadhalika

marebisho yafanywe ili kuweka majedwali ambayo yanatokana na sheria ndogo husika ili kukidhi matakwa ya kifungu cha 25(2) cha sheria ndogo cha sheria ya tafsiri sura ya kwanza inayolekeza kuwa majedwali yote yanapokuwa ni sehemu ya sheria ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sheria ndogo kuwa na makosa ya uchapaji, uandishi na kurejea vifungu visivyo sahihi. Mfano wa sheria ndogo zenye dosari hii ni kanuni za kudumu za Halmashauri ya Wilaya ya Nzega za mwaka 2017 zilizotungwa chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Uchambuzi umeonesha kuwa jedwali la kanuni hizi limerejea kuanzishwa chini ya kanuni ya 42(3) ambayo haijo katika sheria hizo. Kamati ilibaini kuwa kanuni sahihi ilipaswa kurejewa kwa ajili ya kuanzisha jedwali hili ni kanuni ya 44(3). Dosari nyingine iliyobainika katika sheria hiyo ndogo ni kuweka masuala ya alna tofauti katika jedwali moja illyoanzishwa chini ya kanuni ya 42(3).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa masuala hayo ni kuhusu hadidu za rejea za Kamati za Kudumu za Halmashauri zinazoanzishwa chini ya kanuni ya 42(3) ya kanuni hizi. Kimsingi hadidu za rejea ni suala linalo jitegemea na linazungumziwa chini ya kanuni ya 44(3). Hivyo kanuni hizi zinapaswa kuwa na jedwali lingine linalozungumzia hadidu za rejea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Tisa wa Bunge, katika eneo hili katika Mkutano wa Tisa wa Bunge Serikali iliwasilisha Bungeni kwa kuweka mezani jumla ya sheria ndogo 90. Uchambuzi umeonyesha kuwa sheria ndogo ya 46 kati ya 90 zilizowasilishwa zimebainika kuwa na hoja mbalimbali au kuhitaji maelezo kutoka kwa Mawaziri wenye dhamana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ndogo zenyе dosari zimebainishwa katika jedwali ambalo ni kiambatanisho namba mbili na dosari hizo kwa ujumla wake zinaonyesha kwamba kama nilivyokwisha kuelezea kwamba baadhi yake zinakiuka misingi ya katiba pamoja na haki za binadamu,

kuwa na makosa ya kiuandishi, ya kiuchapaji, kutoainisha kifungu cha sheria mama kinachotoa mamlaka ya kuanzishwa kwa sheria hizo, kutofanya rejea sahihi ya vifungu vinavyoanzisha majedwali au majedwali kutoendana na maudhui ya sheria ndogo husika, kuwa na baadhi ya vifungu visivyokuwa maelezo ya pemberi yaani *marginal notes* au kuwa na maelezo ya pemberi hizo *marginal notes* yasiyohusu maudhui ya kifungu husika na kwa kweli nyingine zinatoa tafsiri za maneno ambayo hayajitoshelezi au haziendani na tafsiri zilizokwisha kutolewa na sheria mama. Dosari hizo zimeainishwa kuanzia Ibara 2(4)(3) hadi Ibara ya 2(4)(4) ya taarifa hii inayohusu sheria ndogo kukiuka misingi ya Katiba na haki za binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini maelezo yetu yameendelea pia kuhusu sheria ndogo kuwa na makosa ya kiuandishi na ya kiuchapaji taarifa yetu inaelezea kwa kina na haya makosa yamejitekeza katika halmashauri zippi na mamlaka zippi. Pia suala la sheria ndogo kutofanya rejea sahihi ya vifungu vilivyoanzishwa na majedwali kutoendana na maudhui ya sheria ndogo pia kimelezwa kwa kina katika taarifa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia sheria ndogo kuwa na baadhi ya vifungu visivyo kuwa na *marginal notes* au kuwa na *marginal notes* zenye maudhui yasiyoendana na maudhui ya kifungu husika pia taarifa yetu kwa pamoja kabisa imezamia kwa undani na Waheshimiwa Wabunge wanayo fursa ya kusoma na kupata undani wake. Hata hili la sheria ndogo kwa kutoa tafsiri ya maneno ambayo hayajitoshelezi au haiendani na tafsiri zilizokwisha kutolewa na sheria mama na yenye pia ni maeneo ambayo kimsingi tu yana maelezo ya kina ya kutosha kwenye taarifa yetu ambayo yapo kwenye kitabu ambacho naamini Ofisi ya Katibu wa Bunge inaendelea kuigawa kwa ajili ya mjadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maoni na mapendekezo ya Kamati yetu na nianze na utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya Kamati.

Kwa kuwa majibu baadhi ya Mawaziri kuhusu hoja na dosari zilizobainika katika baadhi ya sheria ndogo yamejaa ahadi za utekelezaji unaochukua muda mrefu, wakati sheria ndogo zenye dosari zikiendelea kutumika kinyume na matarajio ya Bunge linapokasimu badala yake ya kutunga sheria kwa mamlaka hizo.

Na kwa kuwa kuendelea kutumika kwa baadhi ya sheria hizo zenye dosari kuna sababisha madhara makubwa kwa wananchi kiuchumi na katika haki zao za msingi jambo ambalo linaweza kusababisha Bunge kufanya marekebisho ya sheria ndogo hizo likiona ulazima wa kufanya hivyo kwa mujibu wa kifungu cha 38 cha Sheria Tafsiri ya Sheria, Sura ya Kwanza.

Kwa hiyo basi, tunaliomba Bunge, mamlaka za Serikali zillizokasimliwa madaraka ya kutunga sheria ndogo ambazo Kamati imebaini kuwa zina dosari zifanye marekebisho yaliyopendekezwa haraka na kutangaza katika gazeti la Serikali kabla ya Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yako pia inaendelea kuhusu uwasilishaji wa sheria Bungeni kwamba kwa kuwa kifungu cha 38 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya Kwanza kimeweka sharti la kuweka mezani Bungeni sheria ndogo zilizotangwaza katika Gazeti Rasmi la Serikali ndani ya siku sita ya vikao vya Bunge baada ya kutangazwa.

Kwa hiyo basi, Serikali tunaomba ihakikishe kwamba inawaslisha kwa wakati katika Mkutano wa Bunge sheria ndogo zote zilizochapishwa tangu kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita ili kuliwezesha Bunge kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kuepusha mgogoro wa kiutendaji wa sheria ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uhariri wa sheria ndogo, tunashauri kwamba:-

Kwa kuwa imebainika kwamba sheria ndogo nyingi zilizowasilishwa mezani zina makosa mengi ambayo

yanaashilia kukosekana kwa umakini na uhariri wa kutosha kuondoa makosa hayo.

Na kwa kuwa makosa hayo yanaweza kuleta changamoto ya kimaudhui na kiutekelezaji wa sheria ndogo au baadhi ya vifungu vyta sheria ndogo husika.

Kwa hiyo basi, Bunge tuliomba liazimie kwamba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na hasa kitengo cha Mwandishi Mkuu wa Sheria *CPD* pamoja na Idara za Serikali kwa maana ya Wizara mbalimbali husika kuendelea kufanya uhariri wa kutosha katika sheria ndogo zote zilizotungwa na mamlaka zilizokasimiwa jukumu la utungaji wa sheria ndogo, ili kuondoa dosari mbalimbali za kiuandishi na za kimaudhui zilizojitokeza kabla ya sheria ndogo hizo kuchabishwa katika gazeti la Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kuhusu vifungu vinavyoikiuka masharti ya katiba ya sheria mama na sheria nyingine za nchi. Tuna shauri kwamba:-

Kwa kuwa baadhi ya sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa wa Bunge zilibainika kuwa na vifungu vinavyoikiuka masharti ya katiba, sheria mama na sheria nyingine za nchi kinyume na masharti ya kifungu cha 36(1) cha Sheria Tafsri ya Sheria, Sura ya Kwanza.

Hivyo basi, sisi kama kamati tuliomba Bunge liazimie kwamba kwanza sheria ndogo zote zilizobainika kuwa dosari hizo kama zilivyoorodheshwa katika jedwali la uchambuzi iliyoambatishwa katika taarifa hii zirekebishwe kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili Serikali iwasilishe taarifa kuhusu utekelezaji wa maoni mapendekezo ya kamati pamoja na marekebisho yaliyofanywa katika sheria ndogo hizo kabla ya Vikao vyta Kamati kuelekea Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge.

Kuhusu dosari za uandishi na uchapaji katika baadhi ya majedwali fomu na vifungu vinanyoanzisha, Kamati yetu inashauri kwamba kwa kuwa wakati wa uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa wa Bunge Kamati ilibaini baadhi ya sheria ndogo zina dosari za uandishi na uchapaji katika baadhi ya majedwali, fomu na vifungu vinavyo yaanzisha majedwali hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi sisi kama Kamati tunaliomba Bunge liazimie kwamba sheria ndogo zote zilizobainika kuwa na dosari za kiuandishi na kiuchapaji katika majedwali na fomu kama zilivyo orodheshwa katika taarifa ya Kamati na zile zilizoainishwa katika jedwali la uchambuzi lilloambatishwa katika taarifa hii zirekebishwe kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

Pili Serikali iwasilishe taarifa kuhusu utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya Kamati pamoja na marekebisho yaliyofanywa katika sheria ndogo hizo kabla ya Vikao vyta Kamati kuelekea Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhushu dosari ya kunakili vifungu vyta sheria ndogo za maeneo mengine, tunashauri kwamba kwa vile Kamati ilibaini kwamba baadhi ya sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa wa Bunge zina dosari ya kunakili vifungu vyta sheria ndogo za maeneo mengine ambayo hayaendani na maudhui ya sheria ndogo za maeneo yao. Basi tunaliomba Bunge kwa mara nyingine tena liazimie kwamba kwanza Serikali ifanye marekebisho katika sheria ndogo zote zenye vifungu vilivyonakiliwa katika sheria ndogo za maeneo mengine na ambavyo haviendani na maeneo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Bunge liazimie kwamba Serikali iwasilishe taarifa kuhusu utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya Kamati pamoja na marekebisho yaliyofanywa katika sheria ndogo hizo kabla ya Vikao vyta Kamati kuelekea Mkutano wa Kumi na Moja. Na kuhusu dosari ya kutoa tafsiri za baadhi ya maneno bila kufanya rejea,

Kamati yetu inashauri kwamba kwa Kamati ilibaini kwamba baadhi ya sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa wa Bunge zina dosari za kutoa tafsiri za baadhi ya maneno bila kufanya rejea ya maneno hayo yaliyokwisha kutafsiria katika sheria mama husika basi tunaliomba Bunge lako laizimie kwamba Serikali ifanye marekebisho katika sheria ndogo zote zenye tafsiri ambazo hazijafanya rejea ya tafsiri inayotolewa katika sheria mama husika kama ziliivo hainishwa katika taarifa na jedwali la uchambuzi liiloambatanishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali iwasilishe taarifa kuhusu utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya Kamati pamoja na marekebisho yaliyofanywa katika sheria ndogo hizo kabla ya Vikao vya Kamati kuelekea Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii ikiwa ni sehemu ya hitimisho kwa niaba yako kutoa shukrani kabisa kwa Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, ninyi Wenyeviti wa Bunge letu Tukufu kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza wajibu wake kwa ufanisi katika kipindi cha Januari 2017 hadi Januari 2018. Hii ni pamoja na kuweka utaratibu wa kuchambua na kuwasilisha taarifa za Kamati ya Sheria Ndogo katika Bunge lako Tukufu ni matumaini yangu kwamba utaratibu huu utakuwa endelevu kwa kuzingatia ukweli kwamba sheria ndogo ni sehemu ya sheria za nchi yetu na zinagusa maisha ya siku hadi siku ya wananchi wengi kwani sheria ndogo zenye dosari zinapoendelea kutumika zina madhara makubwa kwa walengwa wa sheria hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kabisa kwa niaba yako tena kwa mara nyingine tunajua kwamba unawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kwa kazi kubwa na nzuri ya kuchambua bila kuchoka sheria ndogo zilizowaslishwa katika Mkutano wa Sita, Mkutano wa Saba, Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa wa Bunge na hatimaye kufanikisha maandalizi ya taarifa hii ya mwaka. Kwa kuwa Kamati za Bunge zinamaliza muda wake najua unatumia fursa hii kutushukuru kwa dhati

kwa ushirikiano sisi Wajumbe wenzako kwenye kipindi chote cha uhai wa Kamati yetu, lakini pia unatutakia heri na uwajibikaji mwema katika Kamati tutakazopangiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme tu kwa namna ambavyo sisi Wajumbe wa Kamati tumependezeshwa na kumependa kufanyia kazi eneo hili tunaouomba uongozi wa Bunge uendelee kutafakari ombi letu la Wajumbe wa Kamati wa Sheria Ndogo wakati Kamati zinaundwa tubaki kama tulivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa naomba majina ya Wajumbe wa Kamati hii na watumishi waendelee kutambua kama ambavyo tunawasikia kwenye taarifa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikimalizia kwa dakika moja naomba kwa moyo ya dhati kabisa kama ambavyo nawasilisha kwa niaba yako kuwashukuru Mheshimiwa Jenista, Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenyewe Ulemavu kwa uratibu ambao umeiwezesha Kamati kwa kipindi cha Januari, 2017 hadi sasa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Hii ni pamoja na kuwasilishwa Bungeni kwa wakati Magazeti ya Serikali pamoja na viambatisho vyake na hovyo kurahisisha utekelezaji wa Kamati hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, niwashukuru Mawaziri na Naibu Mawaziri wote ambao walipata nafasi ya kufika kwenye Kamati yetu na kutoa ufanuzi wa hoja mbalimbali. Vilevile tunashukukuru na tunatoa salam zetu za dhati kabisa za kwa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi mahili wa Ndugu Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake, aidha, pia tunawashukuru Mkurugenzi wa kamati Ndugu Athuman Hussein akisaidiwa na Ndugu Angelina Sanga, Mkurugenzi Msaidizi kwa usimamizi wa shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini si kwa umuhimu, tunawashukuru Makatibu wetu Ndugu Yona

Kirumbi, Ndugu Angela Shekifu, Ndugu Mkuta Masoli, Ndugu Stanslaus Kagisa na Ndugu Chacha Nyakega wakisaidiwa na Ndugu Paul Chima kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati hadi kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo tunashukuru sana kwa muda wote ambao tumeshirikiana Wabunge wengine wote kwa ujumla wake wakitusaidia wakitushauri na tukishirikiana nao kuboresha sheria ndogo ambazo sehemu ya sheria mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kwa mara nyingine tena nasema ahsante sana kwa kunipa fursa hii kwa niaba yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**TAARIFA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE
YA SHERIA NDOGO KWA KIPINDI CHA JANUARI 2017 HADI
JANUARI 2018 - KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

1.1 MAELEZO YA AWALI

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwangi wa rehema kwa kuturuzuku uhai na kutuwezesha kuendelea na utekelezaji wa majukumu yetu kikamilifu. Nitumie fursa hii kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo, kumkumbuka aliyejewa Mjumbe wa Kamati hii Mhe. Leonidas Tutubert Gama (Mb), aliyejewa Mbunge wa Songea Mjini, ambaye alifariki mwezi Novemba, 2017.

Tutaendelea kukumbuka na kuenzi mchango muhimu alioutoa kwa Kamati hii pamoja na Bunge kwa ujumla wakati wote alipokuwa Mbunge, kwa kuiga mfano wake wa uwajibikaji. Tukumbuke kwamba, wote tu wa Mwenyezi Mungu na kwake tutarejea, Amina!

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo. Taarifa hii inaelezea kwa muhtasari majukumu mbalimbali yaliyoteklezwa na Kamati katika kipindi cha Mwaka mmoja kuanzia Januari, 2017 hadi Januari, 2018.

Aidha, Taarifa hii imeainisha matokeo ya Uchambuzi wa Sheria Ndogo mbalimbali zilizowasilishwa katika Mkutano wa Nane na Tisa wa Bunge, pamoja na maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusu Sheria Ndogo hizo.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii vilevile inafafanua kuhusu njia mbalimbali zilizotumika katika kutekeleza majukumu ya Kamati sanjari na mapendekezo ya Kamati kuhusu namna bora ambayo Bunge linaweza kuismamia Serikali katika mchakato wa utungaji wa Sheria Ndogo.

1.2 **MAJUKUMU YA KAMATI NA MSINGI WA UTEKELEZAJI WAKE**

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 11 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo ni kuchambua Sheria Ndogo zilizotungwa na mamlaka mbalimbali ili kujiridhisha iwapo zimekidhi matakwa na masharti ya Katiba, Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi. Malengo ya masharti haya ya kikanuni ni kulipatia Bunge mamlaka ya udhibiti wa utungaji wa Sheria Ndogo kwa vyombo vingine (*Parliamentary Control Over Subsidiary Legislation*) ambavyo Bunge limekasimu kwake mamlaka ya kutunga Sheria kwa mujibu wa Ibara ya 97 (5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 (*The Interpretation of Laws Act, Cap 1 R.E. 2002*) imeweka masharti maalum yanayolipa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nguvu ya udhibiti wa Sheria Ndogo zinazotungwa na Serikali pamoja na vyombo vyake. Msingi huu unaipa

Kamati uwezo wa kufanya uchambuzi wa Sheria Ndogo kwa niaba ya Bunge ambalo ndicho chombo kikuu cha uwakilishi kinachoshauri na kuisimamia Serikali. Hii pia ni kwa sababu Sheria Ndogo zinagusa moja kwa moja maisha ya kila siku ya mwananchi wa kawaida na shughuli za kiuchumi zinazofanywa na jamii kubwa ya Watanzania.

1.3 **NJIA ZINAZOTUMIKA KUTEKELEZA MAJUKUMU YA KAMATI**

Mheshimiwa Spika, baada ya Sheria Ndogo kutungwa na mamlaka husika na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali, Sheria hiyo inatakiwa, kwa mujibu wa Kifungu cha 38 (1), kuwasilishwa Bungeni (*laid before the National Assembly*) ndani ya siku sita (6) za Vikao vya Bunge (six sitting days) katika Mkutano husika. Matakwa haya ya Sheria yanapewa pia nguvu na Kanuni ya 37 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inayosomeka kama ifuatavyo:-

"37.- (2) Nakala za matoleo yote ya Gazeti pamoja na Nyongeza zake zilizochapishwa tangu kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita, zitawasilishwa Bungeni na Waziri ... "

Baada ya hatua hiyo, Bunge linakuwa na fursa ya kufanya uchambuzi wa Sheria Ndogo iliyowasilishwa kwa mamlaka inayopatikana katika Kifungu cha 11 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 4 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sheria Ndogo ambazo hutangazwa katika Gazeti la Serikali na kuwasilishwa Bungeni ni kama zifuatazo:-


- a) *Orders (Amri);*
- b) *Proclamations (Matamko);*
- c) *Rules (Kanuni);*
- d) *Rules of Court (Kanuni za Mahakama);*
- e) *Regulations (Kanuni);*
- f) *Notices (Taarifa);*
- g) *By - Laws (Sheria Ndogo za Halmashauri); na*
- h) *Instruments (Hati Idhini).*

Mheshimiwa Spika, Sheria Ndogo ambazo hutungwa na vyombo mbalimbali nya Serikali ambavyo Bunge limekasimu kwake madaraka ya kutunga Sheria ni nyingi. Hivyo basi, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati imejiwekea utaratibu wa kutekeleza wajibu wake kwa kufanya yafuatayo:-

- a) Kuandaa Orodha ya Sheria Ndogo zote zilizowasilishwa katika kila Mkutano wa Bunge;
- b) Kufanya uchambuzi wa awali wa Sheria Ndogo zote zilizowasilishwa;
- c) Kuandaa Jedwali la Uchambuzi wa Kamati (*Matrix*) linalobainisha matokeo ya Uchambuzi wa Kamati na kuliwasilisha Serikalini ili iandae majibu ya hoja zilizoibuliwa kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni;
- d) Kukutana na Wizara husika (*relevant Ministries*) ili kupokea majibu ya Serikali kutohana na Uchambuzi wa Kamati;
- e) Kuwasilisha Bungeni Taarifa Kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo uliofanywa na Kamati na kutoa maoni na mapendekezo ili Bunge liridhie kwa Azimio la Bunge (*Parliamentary Resolution*) kwa ajili ya utekelezaji wa Serikali; na
- f) Kupokea Taarifa ya Utekelezaji wa Serikali itokanayo na Maoni na Mapendekezo ya Taarifa ya Kamati Kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo kama yalivyoazimiwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, kielelezo kinachofuata kinaonyesha kwa muhtsari na katika lugha ya picha hatua za utekelezaji wa majukumu ya Kamati katika mchakato wa udhibiti wa kibunge wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Kielelezo Na. 1 MCHAKATO WA UDHIBITI WA KIBUNGE WA SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA BUNGENI (*THE PROCESS OF PARLIAMENTARY CONTROL OVER SUBSIDIARY LEGISLATION*)



SEHEMU YA PILI

- 2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWANA KAMATI KATI YA JANUARI, 2017 NA JANUARI, 2018
- 2.1 UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA KATIKA MKUTANO WA SITA, MKUTANO WA SABA, MKUTANO WA NANE NA MKUTANO WA TISA WA BUNGE

Mheshimiwa Spika, katika Mikutano ya Bunge iliyotajwa hapo juu, ambayo ni kwa kipindi cha Januari, 2017 hadi Januari, 2018, Serikali iliwasilisha Bungeni Sheria Ndogo mbalimbali zipatazo **Mia Nne na Nne (404)** ambazo zimechambuliwa na Kamati. Aidha, Kamati ilipokea kutoka Serikalini Taarifa ya utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya uchambuzi wa Kamati **kuhusu Sheria Ndogo 173** zilizowekwa mezani katika Mkutano wa Sita na Saba wa Bunge.

- 2.2 MATOKEO YA UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA KATIKA MKUTANO WA SITA NA MKUTANO WA SABA WA BUNGE

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa Nane wa Bunge, tarehe 14 Septemba, 2017 Kamati iliwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu, taarifa ya Uchambuzi wa **Sheria Ndogo 173** zilizowasilishwa katika Mkutano wa Sita na Mkutano wa Saba wa Bunge.

Taarifa hiyo ya Uchambuzi iliainisha kuwa, katika Mkutano wa Sita wa Bunge, Serikali iliwasilisha Sheria Ndogo **Arobaini na Nane (48)** ambapo kati ya hizo, **Sheria Ndogo Nane (8)** zilibainika kuwa na dosari mbalimbali au kuhitaji ufanuzi kutoka kwa Mawaziri wenye dhamana.

Aidha, taarifa hiyo ya Kamati iliainisha kuwa, katika Mkutano wa Saba wa Bunge, Serikali iliwasilisha **Sheria Ndogo Mia Moja na Ishirini na Tano (125)** ambapo kati ya hizo, **Sheria Ndogo Sabini (70)** zilibainika kuwa na dosari mbalimbali au kuhitaji ufanuzi kutoka kwa Mawaziri wenye dhamana.

Kutokana na matokeo ya Uchambuzi yaliyoainishwa na taarifa hiyo Kamati ilibaini baadhi ya Sheria Ndogo kuwa na dosari zifuatazo:-

- a) Sheria Ndogo kukiuka Misingi ya Katiba pamoja na Haki za binadamu;
- b) Sheria Ndogo kuweka masharti yasiyoendana na uhalsia na yasiyotekelvezek (*unreasonable provisions*);
- c) Sheria Ndogo kuwa na dosari za kiuandishi. Hii ni pamoja na kukosea rejea ya kifungu cha Sheria Mama kinachotoa madaraka ya kutungwa kwake (*wrong citation of enabling provision*), kukosea rejea ya kifungu ndani ya Sheria Ndogo kinachotoa mamlaka ya kutungwa kifungu kingine ndani ya Sheria Ndogo hiyo, dosari za uandishi wa majedwali pamoja na makosa mengine ya kiuchapaji na kiuandishi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa hiyo ya uchambuzi wa Kamati, Bunge lako Tukufu lilipitisha Maazimio kwa kila dosari iliyoainishwa hapo juu na kuitaka Serikali iwasilishe taarifa kuhusu utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya Kamati pamoja na marekebisho yaliyofanyika katika Sheria Ndogo hizo, kabla ya Vikao vya Kamati za Bunge kuelekea Mkutano wa Tisa wa Bunge.

2.3 UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA BUNGE KUTOKANA NA UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA KATIKA MKUTANO WA SITA (6) NA MKUTANO WA SABA (7) WA BUNGE

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, katika kutekeleza majukumu yake wakati wa Mkutano wa Tisa wa Bunge, Kamati ilipokea kutoka Serikalini Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni na Mapendekezo ya Kamati kwa baadhi ya Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Sita na Saba wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, taarifa hiyo ya utekelezaji inahusisha jumla ya **Sheria Ndogo 77** ambazo zina **jumla ya hoja 201** zilizotokana na uchambuzi uliofanywa na Kamati. Katika taarifa hiyo Serikali imetolea maelezo ya hatua za utekelezaji wa **Sheria Ndogo 75**.

Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwepo kwa **Sheria Ndodo 2** kati ya **77** ambazo bado maoni na mapendekezo ya Kamati yalikuwa hayajatekelezwa kama yalivoazimiwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza Maazimio ya Bunge lako Tukufu kwa kuwa hoja zote za Uchambuzi wa Sheria Ndodo 77 zilizowasilishwa Serikalini katika Mkutano wa Sita na Mkutano wa Saba wa Bunge, zimejibiwa na Serikali kwa zaidi ya **asilimia 97%**. Aidha, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuendelea kutekeleza ushauri wa Kamati katika kurekebisha dosari mbalimbali zilizopo katika Sheria Ndodo chini ya Wizara na Taasisi husika za Serikali.

2.4 UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA KATIKA MKUTANO WA NANE WA BUNGE.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa Nane wa Bunge, Serikali iliwasilisha Mezani **jumla ya Sheria Ndodo 141**. Kati ya hizo, **Sheria Ndodo** zilizobainika kuwa na hoja ni **56** kwa uwiano kwamba **Sheria Ndodo 21** ni marekebisho mbalimbali kutokana na Uchambuzi uliotekelawa na Kamati katika Mkutano wa Pili wa Bunge na **Sheria Ndodo 35** zilibainika kuwa na hoja mbalimbali au kuhitaji maelezo kutoka kwa Mawaziri wenye dhamana na Sheria Ndodo husika.

2.5 MATOKEO YA UCHAMBUZI

- a) Sheria Ndodo husika kwenda kinyume na masharti ya Sheria nyingine za nchi.**

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wa Sheria Ndodo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Nane wa Bunge Kamati ilibaini baadhi ya Sheria Ndodo kwenda kinyume na masharti ya Sheria nyingine za nchi. Mfano ni **Kanuni ya 18** ya SHERIA NDOGO ZA THE SURFACE AND MARINE TRANSPORT REGULATORY AUTHORITY ACT, REGULATIONS, 2017 iliyotungwa chini ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, ambayo inampa wajibu wa lazima Wakala wa *Clearing and Forwarding* kuwajibika kwa kosa linalofanywa na mwajiriwa ambalo litapelekea kuvunja masharti ya Sheria Ndodo.

Mheshimiwa Spika, masharti ya Kanuni hii hayazingatii Misingi ya Sheria ya Madhara (*Vicarious Liability*) ambapo mwajiri hapaswi kuwajibika kwa makosa yanayofanywa na mwajiriwa ambayo yametendwa pasipo ridhaa (*Dully authorized*) na mwajiri wake au wakati akiwa anatekeleza kazi za mwajiri wake (*in the course of employment*).

Kamati inashauri kuwa, Kanuni hii ifanyiwe marekebisho kwa kuondoa wajibu wa lazima kama inavyosomeka sasa na kuweka masharti ambayo yatazingatia vigezo vilivyowekwa kwa mujibu wa misingi ya Sheria ya Madhara ili kuamua iwapo Mwajiri anahusika na kosa lilitotendwa na Mwajiriwa au la.

- b) *Sheria Ndogo kuwa na vifungu na majedwali ambayo hayaendani na maudhui ya Sheria Ndogo husika.*

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa baadhi ya Sheria Ndogo hazizingatii masharti bora ya uandishi. Kwa mfano, **Kifungu cha 16** cha *SHERIA NDOGO ZA (USAIFI WA HIFADHI YA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA MJI WA NZEGA, 2017* iliyotungwa chini ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI), kina maudhui ambayo hayaendani na Sheria Ndogo hii kwa kuwa kinazungumzia kuhusu usafi na hifadhi ya Ziwa Tanganyika, ambalo kimsingi ziwa hilo halipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Nzega badala yake linapatikana Mkoani Kigoma.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu wa kunakili Sheria Ndogo umeendelea kuleta changamoto kwakuwa makosa ambayo yanapatikana katika Sheria Ndogo moja yanahamishiwa katika Sheria Ndogo ya Halmashauri nyingine. Kamati inashauri dosari zilizobainika katika Sheria Ndogo hii zirekebishwe ili kukidhi masharti ya uandishi mzuri wa Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Spika, mfano wa Sheria Ndogo ambayo ina maudhui yasiyoendana na Sheria Ndogo yenyewe ni Kanuni ya *THE PETROLEUM (REFINERY OPERATIONS) RULES, 2017* iliyotungwa chini ya Wizara ya Nishati. Jedwali la Kwanza na la Pili katika Kanuni hizi yamerejea vifungu ambavyo si vya Kanuni hizi na pia havijakamilika.

Mheshimiwa Spika, Jedwali la Pili la Kanuni hizi linaweka faini kwa masuala ambayo Kanuni hajijayaonyesha kama ni masharti yanayopaswa kutekelezwa na mwenye leseni. Mfano, sehemu ya 22 inaweka faini kwa mwenye leseni iwapo atashindwa kuweka *paving* katika eneo linalozunguka mtambo wa kusafishia mafuta.

Kamati inashauri kuwa, majedwali yote yaliyobainika kuwa na dosari yafanyiwe marekebisho kwa kuainisha vifungu sahihi vinavyoyaanzisha. Halikadhalika, marekebisho yafanyiwe ili kuweka majedwali ambayo yanatokana na Sheria Ndogo husika ili kukidhi matakwa ya Kifungu cha 25 (2) cha Sheria ya Tafsiri, Sura ya 1, inayoelekeza kuwa majedwali yote yawe sehemu ya Sheria Ndogo.

**c) Sheria Ndogo kuwa na Makosa ya Uchapaji,
Uandishi na kurejea vifungu visivyo sahihi;**

Mheshimiwa Spika, wakati Kamati ikifanya uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Nane wa Bunge, ilibaini baadhi ya Sheria Ndogo kuwa na makosa ya kiuchapaji na kiuandishi.

Mfano wa sheria hizo ni, Sheria Ndogo hiyo ni *KANUNI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA NZEGA, 2017* iliyotungwa chini ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI). Katika Sheria Ndogo hii kuna dosari katika rejea ya majedwali ambapo Jedwali la Kanuni hizi limefanya rejea ya **Kanuni ya 42(3)**. Kimsingi Kanuni hii haipo katika Sheria Ndogo hizi na badala yake Kanuni sahihi iliyopaswa kurejewa kuanzisha Jedwali hili ni **Kanuni ya 44(3)** ya Sheria Ndogo hizi.

Mheshimiwa Spika, halikadhalika dosari nyingine iliyobainika katika Sheria Ndogo hii ni masuala yote ya aina tofauti katika Jedwali yamewekwa kuwa yanaanzishwa na **Kanuni ya 42(3)**, mfano wa masuala hayo ni kuhusu hadidu za rejea za Kamati za Kudumu za Halmashauri na kuonyesha kuwa nazo zinatokana na **Kanuni ya 42(3)** ya Kanuni hizi. Kimsingi suala la Hadidu za rejea linajitegemea na linazungumziwa chini ya **Kanuni ya 44(3)**, hivyo ilipaswa kuwepo kwa Jedwali lingine ambalo litazungumzia Jedwali la Hadidu za rejea.

Mheshimiwa Spika, mfano wa Sheria Ndogo nyingine ni *SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MASOKO NA UVUVI) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA LINDI, 2017* iliyotungwa chini ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI). Katika Sheria Ndogo hii Jedwali la tatu lina dosari ya kurejea kifungu kinacholianzisha ambapo limerejea Kifungu cha 18(1) kinachohusu wajibu wa kutumia soko kuwa ni Kifungu kinachoanzisha Jedwali hilo. Hata hivyo rejea sahihi ya Kifungu kinachoanzisha Jedwali hilo ni Kifungu cha 17(1).

Kamati inashauri kuwa, dosari zote zilizobainika katika Sheria Ndogo zilizoainishwa na kuwa na dosari zifanyiwe marekebisho ili kuondoa dosari za kurejea vifungu vya Sheria visivyo sahihi pamoja na makosa ya uchapaji.

2.6 **UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA KATIKA MKUTANO WA TISA WA BUNGE.**

Mheshimiwa Spika, Katika Mkutano wa Tisa wa Bunge, Serikali iliwasilisha Mezani **jumla ya Sheria Ndogo 90**. Kati ya hizo, **Sheria Ndogo 50** zina hoja mbalimbali au kuhitaji maelezo kutoka kwa Mawaziri Wenye Dhamana na Sheria Ndogo husika. Aidha, **Sheria Ndogo 26** hazikuwa na hoja za kiuchambuzi na **14 ni Sheria Ndogo** zenyenye marekebisho mbalimbali.

2.7 **MATOKEO YA UCHAMBUZI**

- a) **Sheria Ndogo kukiuka Misingi ya Katiba pamoja na Haki za Binadamu;**

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Mezani katika Mkutano wa Tisa wa Bunge na kubaini kuwa, Kanuni **ya 31** ya Kanuni za *THE NATIONAL YOUTH REGULATIONS, 2017* zilizotungwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, inakiuka misingi ya Katiba ya Nchi na Haki za Binadamu.

Kanuni hiyo inatoa sharti kwamba, maamuzi ya Waziri ya Shauri la Rufaa iliyotoka kwa Katibu Mkuu yatakuwa ni ya mwisho na hayatahojiwa na chombo chochote. Masharti

ya Kanuni hii ni Kinyume na **Ibara ya 13 (6) (a)** ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayotamka kama ifuatavyo;

Kwa madhumuni ya kuhakikisha usawa mbele ya Sheria, Mamlaka ya Nchi itaweka taratibu zinazofaa a kuzingatia misingi kwamba:-wakati haki na wajibu wa mtu yoyote inapohitajika kufanyiwa uamuzi na mahakama au chombo kingine chochote kinachohusika, basi mtu huyo atakuwa na haki ya kupewa fursa ya kusikilizwa kwa ukamilifu, na pia haki yakukata rufani au kupata nafuu nyingine ya kisheria kutokana na maamuzi ya mahakama au chombo kinginecho kinachohusika.

Kamati inashauri kuwa, **Kanuni ya 31** ya Kanuni hizo ifanyiwe marekebisho kwa kuzingatia masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

b) **Sheria Ndogo kuwa na Makosa ya Kiuandishi na Kiuchapaji;**

Mheshimiwa Spika, wakati wa Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Tisa wa Bunge, Kamati ilibaini kuwa, **jumla ya Sheria Ndogo 44** kati ya 50 zenye hoja zilikuwa na jumla ya **dosari zipatazo 90** za kiuandishi (*Legal Drafting Errors*). Baadhi ya Dosari hizo ni pamoja na;-

(i) **Sheria Ndogo kutoainisha Kifungu cha Sheria Mama (*Enabling Provision*) kinachotoa Mamlaka ya kuanzishwa kwa Sheria Ndogo hiyo;**

Mfano wa Sheria ndogo hizo, ni *THE NATIONAL YOUTH REGULATIONS, 2017*, iliyotungwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambapo Kanuni imerejea **Kifungu cha 27** cha Sheria Mama kuwa ndicho kinaanzisha Sheria hii ambacho kimsingi si sahihi kwakuwa Kifungu hiki kinahusu mahesabu na ukaguzi wa mahesabu.

Sheria nyingine iliyobainika kuwa na Dosari kama hiyo ni Kanuni za *THE ELECTRICITY (DEVELOPMENT OF SMALL POWER PROJECTS)*

RULES, 2017 zilizotungwa chini ya Wizara ya Nishati ambapo hakuna **kifungu cha 46** cha Sheria ya *THE ELECTRICITY ACT, SURA YA 131* (Sheria Mama) kinachotoa Mamlaka ya kutangaza Kanuni hizi katika Gazeti la Serikali.

Kamati inashauri kuwa, Kanuni hizo zifanyiwe marekebisho kwa kuainisha vifungu sahihi vya Sheria Mama vinavyozianzisha (*Enabling Provisions*) ili kukidhi matakwa ya Kifungu cha 36(1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 (*The Interpretation of Laws Act, Cap 1 R.E. 2002*).

- (ii) **Sheria Ndogo kutofanya rejea sahihi ya Vifungu vinavyoanzisha Majedwali na Majedwali kutokwenda na maudhui ya Sheria Ndogo husika.**

Mfano wa Sheria ndogo hizo, ni *SHERIA NDOGO ZA (AFYA NA USAFI WA MAZING'IRA) ZA HALMASHAURI YA MJI WA MBINGA, 2017* zilizotungwa chini ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) ambapo **Kifungu cha 28** cha Sheria ndogo hizi kinafanya rejea ya Jedwali la Tatu badala ya kurejea Jedwali la Nne linalohusu hati ya kufifilisha kosa.

Aidha, **Kanuni ya 6 (3) (f)** ya Kanuni za *THE TRANSPORT LICENCING (PUBLIC SERVICE VEHICLES) REGULATIONS, 2017* zilizotungwa chini ya Wizara Ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, inayohusu *payment of Application Fees* ambayo inafanya rejea ya Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi. Hata hivyo, maudhui ya **Kanuni ya 6(3) (f)** yameainishwa chini ya Jedwali la Pili na siyo Jedwali la kwanza.

Kamati inashauri kuwa, Majedwali yote yaliyobainika kuwa na dosari yafanyiwe marekebisho kwa kuainisha vifungu sahihi vinavyoyaanzisha, halikadhalika kuweka Majedwali ambayo yanaendana na Sheria Ndogo husika ili kukidhi matakwa cha Sheria ya Tafsiri, Sura ya 1.

- (iii) **Sheria Ndogo kuwa na baadhi ya Vifungu visivyo kuwa na *Marginal Notes* au kuwa na *Marginal Notes* zenye maudhui yasiyoendana na Maudhui ya Kifungu husika,**

Mfano wa Sheria ndogo hizo, ni *SHERIA NDOGO ZA (HIFADHI YA MAZINGIRA) ZAHALMASHAURI YA WILAYA YA TABORA, 2017*, zilizotungwa chini ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) ambapo, **Kifungu cha 28** cha Sheria Ndogo hizi hakina *Marginal Notes* yenye kuainisha maudhui ya Kifungu husika.

Aidha, **kifungu cha 4** cha *SHERIA NDOGO ZA (UHIFADHI WA VYANZO VYA MAJI) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MASASI, 2017*, zilizotungwa chini ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI), kilibainika kuwa na namba za Simu ya Mkononi ambazo haziendani na maudhui ya Kifungu husika.

Kamati inashauri kuwa, Serikali ifanye marekebisho kwa Sheria Ndogo zote zilizobainika kuwa na kasoro za kiuandishi katika *marginal Notes* zake ili kukidhi masharti ya uandishi bora wa sheria kwa mujibu wa Kifungu cha 25(1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 (*The Interpretation of Laws Act, Cap 1 R.E. 2002*).

- (iv) **Sheria Ndogo kutoa tafsiri za maneno ambazo hazijitoshelezi au haziendani na tafsiri zilizokwisha tolewa na Sheria Mama;**

Mfano wa Sheria ndogo hizo, ni *SHERIA NDOGO ZA (KODI YA MAJENGO) (MAREKEBISHO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MAGU, 2017* zilizotungwa chini ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI), ambapo **Kifungu cha 3** kinatafsiri neno 'Benki' kuwa ni jengo maalum ambalo linatumwiwa kuhifadhi fedha au vito vya thamani, jengo hilo lazima liwe maalum kwa shughuli za Benki. Kimsingi, tafsiri hii ina mapungufu kwani inatofautiana na tafsiri kwa mujibu wa Sheria ya *The Banking and Financial Institutions Act*, ya Mwaka 1991 inayotoa tafsiri ya neno benki kama ifuatavyo:-

“bank” means a financial institution authorised to receive money on current account subject to withdrawal by cheque’.

Aidha, **kifungu cha 4** cha *SHERIA NDOGO ZA (USAIFI NA HIFADHI YA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KONGWA, 2017* chini ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI), ambacho kinatoa tafsiri ya maneno ‘mazingira’, ‘taka’, ‘taka gesi’, ‘taka ngumu’, ‘taka yenye madhara’, taka vimiminika na maneno mengine yanayohusiana na mazingira ambayo tayari yametafsiriwa na sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sheria Na. 20 ya mwaka 2004 (*The Environment Management Act, 2004*), pasipo kufanya rejea ya Sheria hiyo.

Kamati inashauri kuwa, ni vyema tafsiri hizi za baadhi ya maneno katika Sheria Ndogo zikafanya rejea ya tafsiri illyokwishatolewa chini ya Sheria Mama illyotungwa na Bunge kuhusu suala husika. Hatua hiyo itaondoa uwezekano wa kuwa na tafsiri zaidi ya moja kwa suala moja ambalo tayari limefanyiwa kazi na sheria nyingne (*To maintain Uniformity of Law*), na hivyo kukidhi matakwa ya kifungu cha 39 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 (*The Interpretation of Laws Act, Cap 1 R.E. 2002*).

SEHEMU YA TATU

- 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**
- 3.1 MAONI NA MAPENDEKEZO YA JUMLA KUHUSU SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA KATIKA MKUTANO WA NANE NA MKUTANO WA TISA WA BUNGE**

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi uliofanyika kwa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa wa Bunge, Kamati inashauri Serikali kufanya marekebisho katika Sheria Ndogo zote zilizobainika kuwa na dosari mbalimbali, kwa kuzingatia maoni na mapendekezo kama yalivyoelekezwa katika taarifa hii pamoja na Jedwali la Uchambuzi.

3.2 HOJA

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, baadhi ya Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa wa Bunge zilibainika kuwa na vifungu vinavyoonekana kukiuka masharti ya Katiba, Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi kinyume na masharti ya Kifungu cha 36(1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 ambayo inazitaka sheria ndogo kutokiuka masharti ya Sheria Mama.

Na kwa kuwa, Sheria Ndogo zinazokinzana na Kifungu cha 36(1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 zinahesabika kuwa ni batili kwa kiwango cha masharti hayo yaliyokiukwa

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba:-

- a) Sheria Ndogo zote zillizobainika kuwa na dosari hizo kama zilivyoorodheshwa katika Taarifa ya Kamati pamoja na zile zilizoainishwa katika **Jedwali la Uchambuzi** lilioambatishwa katika taarifa hii, zirekebishwe kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.
- b) Serikali iwasilishe Taarifa kuhusu utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya Kamati pamoja na marekebisho yaliyofanywa katika Sheria Ndogo hizo kabla ya vikao vya Kamati kuelekea Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, wakati wa Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Nane na Mkutano Tisa wa Bunge, Kamati ilibaini baadhi ya Sheria Ndogo zina dosari za uandishi na uchapaji katika baadhi ya Majedwali, Fomu na Vifungu vinavyoyaanzisha.

Na kwa kuwa, Majedwali na Fomu ni sehemu ya Sheria husika, hivyo maudhui yake lazima yaendane na vifungu vinavyoyaanzisha kwa mujibu wa **kifungu cha 25** cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1.

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba:-

- a) Sheria Ndodo zote zilizobainika kuwa na dosari za kiuandishi na kiuchapaji katika Majedwali na Fomu kama zilivyoorodheshwa katika Taarifa ya Kamati na zile zillizoainishwa katika **Jedwali la Uchambuzi** lilioambatishwa katika taarifa hii, zirekebishwe kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Kamati.
- b) Serikali iwasilishe Taarifa kuhusu utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya Kamati pamoja na marekebisco yaliyofanywa katika Sheria Ndodo hizo kabla ya vikao vya Kamati kuelekea Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Kamati ilibaini kwamba baadhi ya Sheria Ndodo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa wa Bunge zina Dosari ya kunakili vifungu ya Sheria Ndodo za maeneo mengine ambayo hayaendani na maudhui ya Sheria Ndodo za maeneo yao.

Na kwa kuwa, makosa hayo ya kunakili Sheria za maeneo mengine yanaweza kusababisha utekelezaji mgumu wa Sheria hiyo kwa wananchi wa maeneo hayo ambayo Sheria hiyo imetungwa kutumika.

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba:-

- a) Serikali ifanye marekebisco katika Sheria Ndodo zote zenye vifungu vilivyonakiliwa katika Sheria Ndodo za maeneo mengine na ambavyo haviendani na maeneo yao.
- b) Serikali iwasilishe Taarifa kuhusu utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya Kamati pamoja na marekebisco yaliyofanywa katika Sheria Ndodo hizo kabla ya vikao vya Kamati kuelekea Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Kamati ilibaini kwamba baadhi ya Sheria Ndodo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa wa Bunge zina dosari ya kutoa tafsiri za baadhi maneno bila kufanya rejea ya maneno hayo yaliyokwisha tafsiriwa na Sheria Mama husika.

Na kwa kuwa, dosari hiyo yakufanya tafsiri mbadala kinyume cha tafsiri iliyokwishatolewa na Sheria mama ni kinyume na masharti yaliyoainishwa katika **kifungu cha 39(1)** cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1, ambacho kinataka tafsiri za Maneno ya Sheria Ndogo ziwe ni zile zilizotafsiriwa katika Sheria Mama husika,

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba:-

- a) Serikali ifanye marekebisho katika Sheria Ndogo zote zenyetafsiri ambazo hazijafanya rejea ya tafsiri iliyotolewa katika Sheria Mama husika kama zilivyoainishwa katika taarifa hii na **Jedwali la Uchambuzi** liliomboambatishwa.
- b) Serikali iwasilishe Taarifa kuhusu utekelezaji wa maoni na mapendelekezo ya Kamati pamoja na marekebisho yaliyofanywa katika Sheria Ndogo hizo kabla ya vikao vya Kamati kuelekea Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge.

3.3 MAONI YA JUMLA

3.3.1 Utekelezaji wa Maoni na Mapendelekezo ya Kamati

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba mamlaka ya kutunga Sheria Ndogo yaliyokasimiwa kwa Mawaziri na vyombo vingine vya Serikali kwa Sheria zilizotungwa na Bunge, si mamlaka Kamili (*it is only delegated*). Muda wowote Bunge linaweza kufanya mabadiliko ya Sheria Ndogo yoyote ambayo Bunge litaona ulazima wa kuifanyia marekebisho kwa mujibu wa masharti yaliyoainishwa katika **Kifungu cha 38** cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1. Kwa sababu hiyo, Kamati inashauri Mawaziri na vyombo vyote vilivyoakasimiwa madaraka ya kutunga Sheria Ndogo ambazo Kamati imebaini kuwa na dosari wafanye marekebisho yaliyopendekezwa haraka na kutangaza katika Gazeti la Serikali kabla ya Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, mapendelekezo haya yanatokana na Kamati kubaini kuwa majibu ambayo baadhi ya Mawaziri wamekuwa wakiwasilisha mbele ya Kamati, yamejaa ahadi za utekelezaji unaochukua muda mrefu wakati Sheria Ndogo

zilizobainika kuwa na dosari bado zinaendelea kutumika na baadhi kuwa na madhara makubwa kwa wananchi kiuchumi na katika haki zao za msingi.

3.3.2 Uwasilishaji wa Sheria Ndogo Bungeni

Mheshimiwa Spika, Kwa kuzingatia masharti ya **Kifungu cha 38** cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1, Kamati inaendelea kusisitiza na kuishauri Serikali kuhakikisha inawasilisha kwa wakati katika kila Mkutano wa Bunge, Sheria Ndogo zote zilizochapishwa tangu Kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita. Hatua hii italiwezesha Bunge kutekeleza majukumu yake kikamilifu lakini pia litaepusha mgogoro wa kiutendaji wa Sheria Ndogo yoyote ambayo Bunge linaweza kuazimia isitumike kwa kutowasilishwa Bungeni kwa wakati.

3.3.3 Uharii wa Sheria Ndogo

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kitengo cha Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Bunge (CPD) pamoja na Idara za Sheria za Wizara, kuendelea kufanya uhariri katika Sheria Ndogo zote zilizotungwa na Mamlaka zilizokasimiwa jukumu la utungaji wa sheria Ndogo ili kuondoa dosari mbalimbali za kiuandishi na kimaudhui zinazojitokeza kabla ya Sheria Ndogo hizo kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Spika, ni vyema ikakumbukwa kwamba, Bunge kupitia Kamati hii siyo chombo cha uhariri wa sheria ndogo zinazotungwa na mamlaka mbalimbali, bali lina jukumu la kupitia kwa lengo la kujiridhisha iwapo Sheria Ndogo hizo zimekidhi matakwa ya Kikatiba na Sheria nyingine za nchi.

SEHEMU YA NNE

- 4.0 **HITIMISHO**
- 4.1 **SHUKRANI**

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na Uongozi wa Bunge lako tukufu kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza wajibu wake kwa ufanisi katika kipindi cha Januari, 2017 hadi Januari, 2018.

Hii ni pamoja na kuweka utaratibu wa kuchambua na Kuwasilisha taarifa za Kamati ya Sheria Ndogo katika Bunge lako tukufu. Ni matumaini yangu kwamba, utaratibu huu utakuwa endelevu kwa kuzingatia umuhimu wa Kamati hii katika maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo kwa kazi kubwa na nzuri ya kuchambua Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Sita, Mkutano Saba, Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa wa Bunge na hatimaye kufanikisha taarifa hii ya mwaka. Kwa kuwa Kamati za Bunge zinamaliza muda wake nitumie fursa hii kuwashukuru kwa ushirikiano wao kwangu katika kipindi chote cha uhai wa Kamati. Niwatakie heri na kuwajibika kwema katika Kamati watakazopangiwaa. Kwa heshima kubwa naomba majina yao kama yalivyoanishwa katika Taarifa hii yaingizwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard). Majina hayo ni haya yafuatayo:-

1. Mhe. Andrew John Chenge (Mb)
2. Mhe. William Mganga Ngeleja (Mb)
3. Mhe. Abdallah Ally Mtolea (Mb)
4. Mhe. Halima James Mdee (Mb)
5. Mhe. Daniel Edward Mtuka (Mb)
6. Mhe. Rashid Ali Abdallah (Mb)
7. Mhe. Aida Joseph Khenani (Mb)
8. Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete (Mb)
9. Mhe. Esther Michael Mmasi (Mb)
10. Mhe. Salome Wycliffe Makamba (Mb)
11. Mhe. Hassani Selement Kaunje (Mb)
12. Mhe. Sadifa Juma Khamis (Mb)
13. Mhe. Khamis Mtumwa Ali (Mb)
14. Mhe. Hassan Elias Massala (Mb)
15. Mhe. Almas Athuman Maige (Mb)
16. Mhe. Goodluck Asaph Mlinga (Mb)
17. Mhe. Kiteto Zawadi Koshuma (Mb)
18. Mhe. Elibariki Emmanuel Kingu (Mb)
19. Mhe. Tundu Antipas Mughway Lissu (Mb)

Mheshimiwa Spika, Kwa moyo wa dhati kabisa nimshukuru Mhe. Jenista J. Mhagama (MB) – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemaevu) kwa uratibu ambao umeiwezesha Kamati kwa kipindi cha Januari, 2017 hadi Januari, 2018 kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Hii ni pamoja na kuwasilisha kwa wakati Magazeti ya Serikali pamoja na Viambatisho vyake na hivyo kurahisisha utekelezaji wa kazi za Kamati hii. Aidha, niwashukuru Mawaziri na Naibu Mawaziri wa sekta mbalimbali kwa kufika mbele ya Kamati na kujibu hoja zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati. Kwa heshima na taadhima naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Selemani Saidi Jafo (Mb)
Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI)
2. Mhe. Jenista Joakim Mhagama (Mb)
Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge)
3. Mhe. William Vangimembe Lukuvi (Mb)
Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi
4. Mhe. Dkt. Medard Matogolo Kalemani (Mb)
Waziri wa Nishati
5. Mhe. Prof. Palamagamba, J.A.M. Kabudi (Mb)
Waziri wa Katiba na Sheria
6. Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (Mb)
Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano
7. Mhe. Subira Mgalo (Mb)
Naibu Waziri wa Nishati
8. Mhe. Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji (Mb)
Naibu Waziri wa Fedha na Mipango
9. Mhe. Eng. Atashasta Nditiye (Mb)
Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano

10. Mhe. Joseph Kakunda (Mb)

Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI)

11. Mhe. Anthony Peter Mavunde(Mb)

Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Bunge)

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi mahiri wa Ndg. Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge kwa ushirikiano wanaoipatia Kamati iliweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, nimshukuru Mkurugenzi wa Kamati Ndg. Athuman Hussein akisaidiwa na Bi. Angelina Sanga, Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati kwa usimamizi mzuri wa shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu, niwashukuru Makatibu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, Ndg. Yona Kirumbi, Ndg. Angela Shekifu, Ndg. Mkuta Masoli, Ndg. Stanslaus Kagisa na Ndg. Chacha Nyakega wakisaidiwa na Ndg. Paul Chima kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

4.2 HOJA

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza shughuli zilizotekelizwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo na kufafanua matokeo ya uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu utekelezaji wa shughuli zake katika kipindi cha kuanzia Mwezi Januari, 2017 hadi Januari, 2018 pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo kwenye Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Andrew John Chenge (Mb)

MWENYEKITI

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo

8 Februari, 2018

MHE. PROF. NORMAN A. S. KING: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nakushukuru sana Mheshimiwa Makamu wa Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo. Tunaendelea Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Mwenyekiti mwenyewe, Mheshimiwa Mchengerwa. (*Makofi*)

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGESA YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa taarifa yangu itasomwa na miaka 100 ijayo na vizazi vijavyo, ninaomba kuondoa maneno ambayo siyo maagizo ya Kamati yangu. Ukurasa wa nne yako maneno yanayozungumza kwamba Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa Wizara ya Katiba na Sheria, Kamati yangu hajawahi kwenda kutembelea mradi wowote ulio chini ya Wizara ya Katiba na Sheria, lakini pia hajawahi kushiriki kwenye shughuli yoyote iliyo chini ya Mahakama ya Tanzania. Kwa hiyo, naomba eneo hili liondolewe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda nimshukuru sana Mwenyezi Mungu mwinge wa rehema aliyenjaalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako hili tukufu kwa ajili ya kuwasilisha taarifa ya mwaka ya Kamati hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni taarifa yangu ya mwisho ya Kamati kwa kipindi cha miaka mwili na nusu ya kuanza kwa uhai wa Bunge hili. Kwa kuzingatia hilo, naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa kujitoa kwao na kufanya kazi kwa weledi na ufanisi katika kuhakikisha kwamba Kamati inatekeleza majukumu yake kwa wakati na ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kusoma taarifa hii napenda kumpongeza sana Dkt. Adelardus Kilangi kwa

kuteuliwa kuwa Mwanasheria Mkoo wa Serikali na Ndugu Paul Ngwembe kwa kuteuliwa kuwa Naibu Mwanasheria Mkoo wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwanasheria Mkoo wa Serikali ni kiungo muhimu sana kati ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria na Serikali kwa ujumla na hivyo tunawatakia utumishi uliotukuka katika dhamana kubwa waliyopewa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ina wajibu wa kuwasilisha taarifa ya mwaka ya shughuli zake kwa madhumuni ya kujadiliwa katika mukutano wa mwisho kabla ya mukutano wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii inaelezea shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha Januari 2017 hadi Januari 2018 na imegawanyika katika sehemu kuu nne kama zifuatazo:-

Sehemu ya Kwanza, inatoa maelezo ya Jumla kuhusu majukumu ya Kamati na shughuli zilizotekelezwa;

Sehemu ya Pili, inahusu uchambuzi na matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati;

Sehemu ya Tatu, inabainisha maoni na mapendekezo ya Kamati; na

Sehemu ya Nne, ni hitimisho la taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Kamati, Kamati hii inasimamia Wizara Tatu ambazo ni, Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano, Ofisi ya Waziri Mkoo, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu na Wizara ya Katiba na Sheria. Majukumu ya Kamati hii katika kusimamia na kuishauri Serikali ni majukumu ya kikatiba, kisheria na kikanuni na yanajumusisha kushughulikia bajeti za Wizara

inayosimamia, miswada na mikataba ya Kimataifa na kujadili taarifa za utekeezaji wa majukumu ya Wizara na Taasisi inayoisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia na mbinu zilizotumika kutekeleza majukumu yake; ili kutekeleza majukumu yake kwa weledi na ufanisi, Kamati ilitumia njia na mbinu mbalimbali kama vile kupokea, kujadili na kuchambua taarifa za utekelezaji wa Wizara na Taasisi inayoisimamia, kupokea maoni ya wadau, kufanya ziara na ukaguzi wa miradi ya maendeleo, kualika na kupokea maoni ya wadau na kupokea mafunzo mbalimbali kuwajengea uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Januari, 2017 hadi Januari, 2018 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria imetekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kutembelea na kukagua utekekelezaji wa miradi ya maendeleo. Ili kukidhi matakwa ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, kuhusu Kamati za kisekta kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha unaoisha, Kamati hii ilitembelea na kukagua miradi ya maendeleo iliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais iliyo Unguja, Pemba na Dar es Salaam. Kamati pia ilitembelea Miradi wa Ukuzaji Masoko na Mitaji Vijijini (*MIVARF*) ulioko Dakawa-Morogoro na mradi wa kiwanda cha sukari cha Mkulazi uliopo Wilayani Mvomero-Morogoro tarehe 18 Novemba, 2017.

(ii) Kuchambua Miswada ya Sheria na mikataba ya Kimataifa inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1) ikisomwa pamoja na Nyongeza ya 7(1)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, katika kipindi kinachotolewa Taarifa, Kamati yangu ilishughulikia Miswada ya Sheria tisa na Maazimio mawili ya Kimataifa kama ifuatavyo:-

(i) Miswada sita ya Sheria za Marekebisho ya Sheria Mbalimbali yaani *Miscellaneous Amendments*.

(ii) Sheria ya Utoaji wa Huduma za Msaada wa Kisheria ya mwaka 2017 yaani *The Legal Aid Act, 2017*.

(iii) Maazimio mawili ya Bunge kuhusu Mkataba wa Vitambulisho vya Mabaharia namba 185 wa Mwaka 2003 yaani *Seafarer's Identity Documents Convention (Revised) of 2003* na Mkataba wa Kimataifa wa kazi za Ubaharia wa Shirika la Kazi Duniani wa mwaka 2006 yaani *Maritime Labour Convention of 2006*.

(iv) Kamati kwa kushirikiana na Kamati zingine nne za Kisekta ilichambua na kujadili Miswada miwili ya sheria kuhusu Sheria ya mapitio na majadiliano kuhusu masharti hasi katika mikataba ya maliasili na nchi ya nchi wa mwaka 2017 yaani *The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-Negotiation of Unconcessionable Terms, Bill of 2017* na Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusiana na Umiliki wa Maliasili wa mwaka 2017 yaani *The Natural Wealth and Resources Permanent Sovereignty Bill, 2017*.

Kamati ilichambua kwa weledi na umakini miswada na maazimio hayo kwa kuwasilisha maoni na ushauri wake katika Bunge lako tukufu ambapo yote yaliridhiwa na kupidishwa na Bunge lako tukufu kuwa sheria za nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipokea na kujadili taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Wizara inayosimamia pamoja na taasisi zake. Taarifa hizo ni:-

(i) Taarifa ya Wizara ya Katiba na Mambo ya Sheria kuhusu utekelezaji wa majukumu yake na taasisi zilizochini yake kama ilivoorodheshwa katika taarifa ya Kamati.

(ii) Taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu kuhusu utekelezaji wa majukumu ya ofisi pamoja na taasisi zilizo chini kama zilivyotajwa katika taarifa yangu.

(iii) Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais kuhusu utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo pamoja na taasisi zilizo chini yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji wa Wizara na Taasisi zake ilikuwa ni kutekeleza jukumu lililo chini ya Ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Baada ya kujadili taarifa hizo, Kamati ilibaini masuala mbalimbali ambayo yanafafanuliwa katika sehemu ya pili ya taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuchambua taarifa za Wizara kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98(2) ikisomwa pamoja na Nyongeza ya Nane, kifungu 7(1)(a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ilichambua taarifa za utekelezaji wa bajeti za Wizara inayozisimamia kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na kufanya ulinganisho wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hizo kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Matokeo ya uchambuzi uliofanywa na Kamati yanaelezewa kwa kina katika sehemu ya pili ya taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili ni uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya kamati. maelezo ya jumla, baada ya kuainisha majukumu ya kamati na shughuli zilizoteklezwa na Kamati kwa kipindi cha Januari 2017 hadi Januari 2018, naomba sasa nitoe taarifa kuhusu masuala mbalimbali ambayo Kamati imeyabaini wakati ikitekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala yanayoelezewa taarifa kwamba Kamati imebaini kuwa ni changamoto ambazo zinahitaji kupewa umuhimu wa kipekee ili kuziwezesha Kamati, Wizara na Taasisi zake kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, hivyo kuleta tija kwa Taifa. Masuala hayo ni pamoja na:-

(i) Ushiriki wa wadau katika utungwaji wa sheria;

- (ii) Upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo;
- (iii) Ufinyu na ukomo wa bajeti kwa Taasisi zote ambazo Kamati inazisimamia;
- (iv) Ufinyu wa muda kwa Kamati kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo;
- (v) Usimamizi sahihi wa matumizi ya fedha za umma;
- (vi) Semina na mafunzo;
- (vii) Usimamizi na utoaji wa haki nchini;
- (viii) Changamoto za ukosefu wa ajira kwa vijana; na
- (ix) Ujenzi wa mazingira wezeshi kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kutoa maelezo kuhusu matokeo ya uchambuzi wa Kamati kwenye masuala yaliyoainishwa hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ushiriki wa wadau katika utungwaji wa sheria, katika kipindi kinachotolewa taarifa, Kamati ilichambua na kujadili Miswada mitatu ya kisekta, Maazimio mawili na Miswada sita ya Sheria za Marekebisho ya Sheria Mbalimbali. Jumla ya Sheria zote zilizochambuliwa na kujadiliwa na Kamati zikiwemo Sheria zilizomo katika Miswada ya marekebisho ya Sheria Mbalimbali ni sheria 41.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa uchambuzi Kamati ilibaini changamoto ya Wizara au Taasisi husika kutowashirikisha wadau wa marekebisho yanayofanyika. Kwa mfano katika Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba 4 wa mwaka 2016 ambao ulisomwa Bungeni kwa mara ya pili na tatu mwezi Februari,

2017 Kamati ilibaini kuwa wadau wa sekta ya usafirishaji wa mafuta hawakushirikishwa vya kutosha katika marekebisho yaliyokusudiwa kufanywa katika sheria ya tozo za barabara na mafuta, Sura ya 220.

Katika Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba 3 wa mwaka 2017 ambao ulisomwa kwa mara ya pili na mara ya tatu Bungeni mwezi Septemba, 2017, Kamati ilibaini kwamba wadau wa Sekta ya usafirishaji hawakushirikishwa vya kutosha katika marekebisho yaliyokusudiwa kufanywa katika Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini yaani *SUMATRA*, Sura ya 413.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Julai, mwaka 2017 Kamati ilijadili na kuchambua Muswada wa Sheria ya Marekebisho Mbalimbali Namba 4 wa mwaka 2017. Muswada huu ulifanya marekebisho makubwa katika Sheria ya madini, Sura ya 123 yaani *The Mining Act, CAP123*pamoja na nyingine zilizoguswa na marekebisho hayo.

Katika uchambuzi wa muswada huu, kwa kutumia Kanuni ya 84(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, Kamati iliwaalika wadau mbalimbali zaidi ya 40 kutoka Taasisi za Serikali, Asasi za Kiraia, Taasisi za Kidini na wawakilishi kutoka Sekta Binafsi na hasa makampuni ya mafuta na gesi ambao walifika kwenye Kamati kutoa maoni yao kuhusu muswada huu. Ushiriki wa wadau wengi katika muswada huu uliku ni mfano mzuri wa namna ambayo wadau wanatakiwa kushirikishwa kwa wingi na vya kutosha katika uchambuzi wa muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika muswada huu, pamoja na mambo mengine, Kamati ilipitisha marekebisho mbalimbali yanayoleta tija katika sekta ya madini kama vile kuundwa kwa Tume ya Madini na kuongeza wigo wa ushiriki wa wananchi katika utoaji wa huduma mbalimbali kutoka migodi yaani *local content*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wajibu wa kuwashirikisha wadau katika mchakato wa kutunga au kurekebisha sheria

yoyote ni wajibu wa Kikatiba kwa mujibu wa Ibara ya 8(d) na Ibara ya 21(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Jukumu hili pia ni jukumu la kikanuni kwa mujibu wa Kanuni ya 84(2) na 117(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016. Hivyo ni jukumu la kila Wizara au Taasisi ya Serikali inayokusudia kuwa na muswada au kufanya marekebisho ya sheria yoyote kuwashirikisha wadau wakuu katika muswada huo au marekebisho yanayokusudiwa kabla ya muswada au sheria husika kusomwa Bungeni kwa mara ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo; Kamati ilizingatia masharti ya kanuni ya 98(1) na kufanya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kwa Wizara na Taasisi inazozisimamila, Kamati ilitembelea Mradi Namba 4944 wa *MIVARF* uliopo huko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu huko Unguja, Pemba, jengo la Ofisi ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora lilokoko Pemba na miradi iliyo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais iliopo Pemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara hiyo, Kamati ilibaini kuwa miradi mingi iliyotengewa fedha haikutekelezwa ipasavyo kutokana na fedha ndogo kutolewa. Kwa mfano ukarabati wa Ofisi ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora - Pemba ulichukua zaldi ya miaka mitano tangu mwaka wa fedha 2011/2012 kukamilika kutokana na kutengewa fedha kidogo kwa ajili ya ukarabati. Hata hivyo katika mwaka wa fedha 2016/2017 Tume ilitenga fedha ya kutosha kukamilisha ukarabati wa ofisi hii ambao umegharimu shilingi milioni 40 mpaka kukamilika kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo miradi ya maendeleo ambayo haikupokea fedha kabisa mpaka mwezi Machi, 2017 wakati Kamati inafanya uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa bajeti za Wizara. Kwa mfano, mradi Namba 4945 (Mfuko wa Maendeleo ya Vijana) na mradi Namba 6577 (Mradi wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi) ambayo ipo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya *MIVARF* iliyoko Pemba na Unguja imekua ikitekelezeka kwa ufanisi mkubwa kwa sababu ufadhili kutoka Benki ya Maendeleo Afrika (*African Development Bank*) pamoja na Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Kilimo

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Miradi ya *MIVARF* iliyoko Pemba, Unguja na sehemu mbalimbali hapa nchini, Kamati iliishauri Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika na Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Kilimo kukamilisha mchakato wa makubaliano ya awamu ya pili ya uendelezaji na utekelezaji wa miradi hii katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufinyu na ukomo wa bajeti kwa taasisi ambazo Kamati inazisimamia; Kamati ilifanya uchambuzi wa kina wa taarifa za bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kwa mafungu 14 ya Wizara na Taasisi inayozisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya uchambuzi wa bajeti ya Wizara na Taasisi hizi na kulishauri Bunge lako tukufu kuzipitisha bajeti zake pamoja na changamoto zilizoonekana katika kila Taasisi. Kwa mfano, katika uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Fungu namba 55, kwa mwaka wa fedha 2015/2016 na makadirio ya mapato na matumizi ya Tume kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Kamati ilibaini kwamba Tume imekua ikitengewa fedha kidogo sana katika kila bajeti kwa miaka zaidi ya miaka mitatu mfululizo hivyo kuathiri utekelezaji wa majukumu yake. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 Tume iliidhinishiwa na Bunge lako tukufu kiasi cha shilingi 5,578,338,000 lakini ilipokea kiasi cha shilingi 2,571,887,401 ambayo ni sawa na asilimia 46.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya jitihada za kutosha ili bajeti ya Tume iongezwe kwa kupeleka ombi katika Kamati ya Bunge ya Bajeti kwa lengo la kuishawishi Serikali kuongeza bajeti ya Tume. Hata hivyo, jitihada hizi hazikufanikiwa katika mwaka wa fedha 2016/2017 kutoptera

na ukomo wa bajeti. Hivyo Serikali iliahidi kulifanyia kazi suala hili katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutimiza ahadi yake katika mwaka wa fedha 2016/2017 kwa kuongeza bajeti ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa fedha ya matumizi mengineyo (*OC*) ambayo ni shilingi 995,514,000. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 shilingi 1,566,080,000 katika mwaka wa fedha 2016/2017, ongezeko hili ni sawa na asilimia 57.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufinyu wa muda wa Kamati kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo, kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inazitaka Kamati za Kisekta kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha. Jukumu hili siyo hisani, ni jukumu la kikanuni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufinyu wa muda unakwamisha utekelezaji wa kanuni hii. Kamati ya Katiba na Sheria inasimamia Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano ambayo ina miradi Unguja na Pemba. Siku za kikanuni za Kukagua miradi ya maendeleo ni siku saba tu ambazo kiuhalisia hazitoshii kukagua miradi ya maendeleo kwa ufanisi Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ufinyu wa muda wa ukaguzi wa miradi ya maendeleo Kamati ilifanikiwa kutembelea miradi ya maendeleo michache sana katika kipindi cha Januari 2017 na 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi sahihi wa matumizi ya fedha za umma, Kamati ya Katiba na Sheria inasimamia pia sekta ya kazi na ajira ambayo ndani yake kuna baadhi ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kama Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (*WCF*). Katika taarifa za Kamati kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2015/2016 na mwaka wa fedha 2016/2017 pamoja na

Makadirio ya mapato na matumizi kwa Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na 2017/2018 ambazo zilisomwa mwezi Aprili, 2016 na 2017. Kamati iliishauri Serikali kufuatilia kwa karibu na kuchukua hatua kali za kinidhamu kwa watendaji wote wa *NSSF* waliohusika na tuhuma mbalimbali za ubadhirifu wa fedha za umma katika miradi yake mbalimbali ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa ya Kamati iliyosomwa mwezi Aprili, 2017 Kamati illieleza Bunge lako tukufu kwamba Serikali ilikua inaendelea na uchunguzi wa tuhuma hizi na hasa kwa kutumia Mamlaka ya Kupambana na Kudhibiti Rushwa, Benki Kuu ya Tanzania, Mamlaka ya Usimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii yaani *SSRA* pamoja na mamlaka nyingine za kichunguzi wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Tano imejipambanua katika kubana matumizi na kuziba mianya yote ya rushwa na ubadhirifu wa fedha za umma. Ni muhimu kwa Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii kutumia na kuwekeza fedha za wananchi zilizowekwa katika mifuko hiyo kwa namna ilio na tija kwa wananchama wake na katika uendelevu na uimara wa kifedha wa mifuko husika yaani *financial sustainability and liquidity of the funds*. Kwa namna ya kipekee Kamati inaipongeza Serikali kwanza kwa kuunda bodi mpya ya *NSSF* na pili inaipongeza Bodii mpya ya *NSSF* kwa kuchukua hatua stahiki ya kuwasimamisha kazi wafanyakazi wote wa *NSSF* ambao wametajwa katika tuhuma hizo tarehe 30 Juni, 2017 katika kikao chake cha kawaida cha 72 cha Bodii ya *NSSF*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema Watumishi wa sekta ya Hifadhi ya Jamii kutambua kwamba wamepewa dhamana kubwa ya kusimamia vizuri fedha za Wanachama na wanapaswa kuibeba dhamana hii kwa uangalifu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hii kwa miaka Miwili mfululizo iliishauri Serikali kutazama uwezekano wa kuunganisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili kuwa na sekta ya

Hifadhi ya Jamii iliyo na mifuko michache na inayoweza kuwafikia wafanyakazi wengi kwa usahihi na ufanisi zaidi. Tunapenda kwa mara nyingine tena kuipongeza Serikali hii sikivu ya Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuufanya kazi ushauri huu wa Kamati na kuunganisha mifuko hii kuititia Muswada wa Kuanzisha Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Sekta ya umma wa mwaka 2017 yaani *The Public Service Social Security Fund Bill, of 2017* ambao tayari umesomwa kwa mara ya pili na ya tatu na kuitishwa na Bunge hili kuwa sheria ya nchi yetu hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Januari 2017 mpaka Januari 2018 Kamati ilipatiwa semina ya mafunzo kutoka taasisi na asasi mbalimbali za kiraia kwa ajili ya kujenga uelewa wa masuala mbalimbali ya kisheria. Kamati inazishukuru sana taasisi zote ambazo zimetoa mafunzo kwa Kamati katika kipindi hiki na naomba majina yote yaingie kwenye *Hansard* kama yalivyo kwenye taarifa ya Kamati. Kutokana na mafunzo yaliyotolewa, Wajumbe wamejengewa uwezo kuhusu mafunzo mbalimbali ya kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utatuzi wa kero za Muungano, moja kati ya maeneo muhimu ambayo Kamati hii inashughulika nayo ni kuhakikisha kwamba kero za Muungano zinatatuliwa kwa wakati. Kamati ilikutana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia masuala ya Muungano tarehe 2 Novemba, 2017 hapa Dodoma na kupokea taarifa ya utekelezaji kutoka Kamati Maalum ya Kutatua Kero za Muungano iliyoundwa na Wataalamu mbalimbali kutoka sekta ya Muungano - Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kamati hii maalum iliundwa toka mwaka 2006 kwa lengo la kuhakikisha kwamba kero za Muungano zinapunguzwa na kutatuliwa kabisa ili wananchi wa pande zote mbili waendelee kufurahia matunda ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo kero ambazo Ofisi ya Makamu wa Rais inatakiwa kuendelea kuzitatau kuititia Kamati hii Maalum ili kuendelea kudumisha Muungano. Kwa

mfano ajira kwa watumishi wa Zanzibar na katika Taasisi za Muungano, ushirikiano wa Zanzibar na Taasisi za nje, uwezo wa Serikali ya Zanzibar kukopa ndani na nje ya nchi, ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, mgawanyo wa mapato ya kodi na misaada ya Wafanyakazi wa Zanzibar kuendelea kutozwa kodi mara mbili, utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia na usajili wa vyombo nya moto. Kero hizi zote zinaendelea kutatuliwa na Serikali zote mbili na jitihada kubwa zimefanyika na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhakikisha kwamba kero hizi zinapungua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usimamizi na utoaji wa haki nchini, moja kati ya jukumu majukumu ya Wizara ya Katiba na Mambo ya Sheria ni kusimamia haki na mfumo wa utoaji haki eneo hili bado limekuwa na changamoto nyingi hapa Tanzania kama vile ufinyu wa bajeti na mlundikano wa kesi mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutohana na ufinyu wa bajeti kumekuwa na uhaba mkubwa wa Mahakimu na Majaji na Rasilimaliwatu katika kusimamia utoaji haki Tanzania kwamfano mwaka 2016 pekee Mahakama ya Tanzania ulikuwa na jumla ya mashauri 335,624 kama hakuna ubunifu wa mipango mikakati ya kupunguza wingi wa mashauri kitaalam haki za watu wengi zitaathirika. Pamoja na mrundikano wa kesi kuanzia katika Mahakama za Mwanzo hadi Mahakama ya Rufaa ya Tanzania bado ni kubwa sana kwa mfano katika Mahakama ya Rufaa ya Tanzania kwa muda wa miaka sita mfululizo idadi ya majaji imebakia kuwa ni 15 tu, lakini idadi ya mashauri ya mwaka imekuwa ikiongezeka siku hadi siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapongeza sana uamuza wa Mahakama ya Rufaa ya Tanzania wa tarehe 2 Februari, 2018 kwa kumuondolea Mkurugenzi wa Mashtaka yaani *DPP* mamlaka ya kuzuia dhamana ya mshtakiwa bila kulazimika kutoa sababu chini ya kifungu cha 148(4) cha Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai katika hukumu hiyo katika kesi ya rufaa ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

dhidi ya mwanaharakati wa haki za binadamu Jeremia Mtobesya, Mahakama ya Rufaa imesema kwamba kifungu hiki ni kinyume na Ibara ya 13(6) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ni batili. Kifungu hiki kimekuwa ni kikwazo kikubwa katika kusimamia haki za watuhumiwa wengi na uamuzi huu wa Mahakama ya Rufaa ni wa kupongezwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto za ukosefu wa ajira kwa vijana, mapendekezo ya Kamati ushiriki wa wadau katika utungwaji wa sheria, haki ya wananchi kushiriki katika shughuli za Serikali ni haki ya kikatiba. Ushiriki huo ni matakwa ya kikanuni na matakwa pia ya Kanuni za Kudumu za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutowashirikisha wananchi katika utungwaji wa sheria kunaondoa uhalali wa sheria hizo.

Hivyo basi, Kamati inashauri Wizara na taasisi zote za Serikali zinazotunga zinazokusudia kurekebisha sheria zao kuwashilikisha kwa kina wadau wote wanaoguswa na sheria zote kabla na baada ya kusomwa Bungeni kwa mara ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, miradi ya maendeleo ni muhimu kwa maendeleo uchumi wa nchi yetu;

Na kwa kuwa utekelezwaji wa miradi hii unategemea upatikanaji wa fedha kutoka Hazina.

Na kwa kuwa ukutolewa kwa fedha miradi ya maendeleo ni wa kati kunaathiri utekelezaji wa miradi husika.

Hivyo basi, Kamati inatoa ushauri zifuatazo; Serikali itoe fedha kwa wakati ili kutekeleza miradi ya maendeleo iliyo chini ya ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na Wizara ya Katiba na Sheria. Lakini Serikali pia itoe kipaumbele kwa miradi ya maendeleo ambayo imekuwa ikipokea fedha chache siku zote hususani Mfuko wa

Maendeleo wa Vijana na Mfuko wa Taifa wa Uwezeshaji Kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufinyu wa ukomo wa bajeti na taasisi ambazo Kamati inaisimamia, ufanisi wa taasisi yoyote unategemea kiwango cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge;

Kwa kuwa kiwango cha utekelezaji wa majukumu ya taasisi zote unategemea sana kiasi cha fedha kilichotolewa;

Na kwa kuwa uhaba wa fedha unaathiri utekelezaji wa majukumu ya taasisi hizo;

Hivyo basi, Kamati inashauri Serikali kutenga fedha ya kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya taasisi inayosimamia na Kamati katika mwaka wa fedha 2018/2019 na kutoa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa taasisi hizo katika nusu ya pili ya utekelezaji wa bajeti wa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ufinyu wa muda kwa Kamati kutembelea na ukaguzi wa miradi wa maendeleo; ukaguzi wa miradi ya maendeleo ni jukumu la msingi kwa Kamati zote za kisekta;

Kwa kuwa muda uliopo wa ukaguzi wa miradi ya maendeleo hautoshi kwa Kamati za kisekta kufanya ukaguzi wa miradi hii kwa ufanisi unaotakiwa;

Hivyo basi, Kamati inashauri Kamati za Kisekta zote zipewe muda wa kutosha wa ukaguzi wa miradi ya maendeleo katika kalenda ya shughuli za Bunge ili kujiridhisha na utekelezaji wa bajeti ya Serikali katika mradi wa maendeleo ultiotengewa fedha katika mwaka wa fedha husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, semina na mafunzo ya Kamati, Kamati hii ina jukumu la kuchambua na kujadili

miswada yote ya kisheria na marekebisho ya sheria mbalimbali ambazo zinagusa karibu Wizara zote mtambuka. Mafunzo ni muhimu kwa Waheshimiwa Wabunge ili kupanua wigo wa uwelewa katika mambo mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu yao, elimu haina mwisho.

Kamati inashauri kwamba Wizara ofisi na taasisi zote zinazosimamiwa na Kamati hii kuendelea kutoa mafunzo mbalimbali ya kisekta ili kujenga uwezo wa Kamati. Ofisi ya Bunge iendelee kuratibu kuwajengea uwezo wajumbe wa Kamati kwa kuandaa mafunzo maalum ya Kamati ndani na nje ya nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utatuzi wa kero za muungano kumekuwepo pia kero mbalimbali za Muungano toka kuanzishwa kwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar mwaka 1964. Jithada mbalimbali zimechukuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kutatua kero mbalimbali za Muungano, hivyo Kamati inashauri ofisi ya Makamu wa Rais Muungano kuititia tume ya pamoja ya kutatua kero za Muungano kuendelea kutatua kero mbalimbali za Muungano na kuhakikisha kwamba wananchi wa pande zote mbili wanatumia na kufaidi na fursa mbalimbali zilizotokana na Muungano huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria napenda kukushukuru wewe, napenda kumshukuru Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa ushirikiano mkubwa walioutoa kwa kamati yangu katika kutekeleza majukumu kwa kipindi cha mwaka mmoja uliopita. Nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri wote na Watendaji wote wakuu wa Wizara na taasisi ambazo kamati inaisimamia kwa ushirikiano wao katika kutekeleza majukumu ya Kamati kwa kipindi cha mwaka mmoja uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani za pekee zimwendee Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Mheshimiwa

Jenista Mhagama (Mbunge), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Mheshimiwa January Makamba (Mbunge) na Waziri wa Katiba na Sheria Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (Mbunge), Naibu Mawaziri wote, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu Mheshimiwa Antony Mavunde, Mheshimiwa Ikupa Alex pamoja na Mheshimiwa Kangi Lugola Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na makatibu Wakuu wote wa Wizara hizi.

Kamati pia inamshukuru kwa namna ya kipekee aliyekuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu aliyeshughulikia masuala ya watu wenye ulemavu Mheshimiwa Dkt. Abdallah Possi ambaye kwa sasa ni Balozi wa Tanzania nchini Ujerumanı ambaye alifanya kazi nzuri sana na Kamati wakati wa utumishi akiwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kuwashukuru sana aliyekuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa George Masaju na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa Gerson Mdemu ambaao walitoa ushirikiano mkubwa sana katika Kamati kipindi chote cha utumishi wao katika ofisi hiyo. Kamati inawapongeza sana kwa kuteuliwa kwao kuwa Majaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania na inawatakiwa utumishi uliotukuka katika muhimili wa Mahakama. Kamati inawashukuru sana wanasheria wote, waandishi wa sheria chini ya Ofisi Mwandishi Mkuu wa Sheria yaani *CPD* ambaao wametoa ushirikiano mkubwa kwa Kamati wakati wa uchambuzi wa miswada mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mshauri Mkuu wa Mambo ya Sheria Ofisi ya Bunge pamoja na Wanasheria wote wa Ofisi hiyo walioshiriki katika shughuli za uchambuzi wa miswada kwenye Kamati ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nitumie nafasi hii kutambua mchango wa wadau mbalimbali waliofika mbele ya Kamati yao kutokana na muda sitowataja, lakini nitaomba orodha yao iingie katika *Hansard* ya Bunge lako Tukufu.

Kwa heshima kwa mara nyingine nichukue fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu wa Bunge ya Katiba na Sheria kwa kufanya kazi nzuri na kwa umakini na uzalendo wa hali ya juu katika kutekeleza, kufanikisha majukumu ya Kamati kuisimamia na kuishauri Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba majina yao yote yaingie katika Kumbukumbu Rasmi za Taarifa za Bunge yaani *Hansard* kama ambavyo nimeziorodhesha.

Mwisho kabisa lakini sio kwa umuhimu wake napenda kuishukuru Sekretarieti yote ya Bunge chini ya uongozi thabiti wa Katibu wetu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai kwa ushirikiano wao kwa kufanikisha shughuli za Kamati. Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge, Mkurugenzi wa Idara ya Taarifa Rasmi, Mkurugenzi wa Kamati za Bunge Ndugu Athumani Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Angelina Sanga, Katibu wa Kamati Ndugu Dunford Mpelumbe ambaye amekuwa kiungo mkubwa wa Kamati hii, Masaidizi wa Kamati Ndugu Rahel Masima kwa umakini na weledi wao katika kufanikisha kazi za Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza kwa kina shughuli zilizotekewa na Kamati yangu uchambuzi wa matokeo wa shughuli hizo maoni na mapendekezo ya Kamati naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa Tukufu lipokee na kuikubali Taarifa ya Kudumu ya Bunge ya katiba na sheria pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo katika taaarifa hii.

Naomba kuwasilisha lakini pia naomba yale yote ambayo sijayasoma yaingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge lako tukufu. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Toa hoja.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:
Mheshimia Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**TAARIFA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE
YA KATIBA NA SHERIA KWA KIPINDI CHA JANUARI, 2017
HADI JANUARI 2018 -KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

SEHEMU YA KWANZA

MAELEZO YA JUMLA

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mungu kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Kamati. Hii ni taarifa ya mwisho ya Kamati kwa kipindi cha Miaka Miwili na Nusu ya kwanza ya uhai wa Bunge hili. Kwa kuzingatia hilo, naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa kujitoa kwao na kufanya kazi kwa weledi na ufanisi katika kuhakikisha kwamba Kamati inatekeleza majukumu yake kwa wakati na ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kusoma Taarifa hii, napenda kumpongeza sana Dr. Adelardus Kilangi kwa kuteuliwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ndgg Paul Ngwembe kwa kuteuliwa kuwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni Kiungo muhimu sana kati ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria na Serikali kwa ujumla na hivyo tunawatakia utumishi uliotukuka katika dhamana kubwa waliyopewa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ina wajibu wa kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya shughuli zake kwa madhumuni ya kujadiliwa katika Mkutano wa mwisho kabla ya Mkutano wa Bajeti.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii inaelezea shughuli zilizotekelizwa na Kamati kwa kipindi cha Januari 2017 hadi Januari 2018 na imegawanyika katika Sehemu Kuu Nne zifuatazo:-

- i. Sehemu ya Kwanza inatoa Maelezo ya Jumla kuhusu majukumu ya Kamati na shughuli zilizotekelzwa;
- ii. Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi na matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati;
- iii. Sehemu ya Tatu inabainisha maoni na mapendekezo ya Kamati;na
- iv. Sehemu ya Nne ni hitimisho la taarifa.

1.1 Majukumu ya Kamati

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane, Fasili ya 6, Kifungu cha 2 na Fasili ya 7 Kifungu cha 1 cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ni moja kati ya Kamati Tisa za Kudumu za Bunge za Kisekta. Kamati hii inasimamia Wizara Tatu ambazo ni, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu na Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, Majukumu ya Kamati hii ni:-

- i. Kushughulikia Bajeti za Wizara inazozisimamia;
- ii. Kushughulikia Miswada na Mikataba ya Kimataifa inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;
- iii. Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila Mwaka za Wizara hizo; na
- iv. Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

1.2 Njia na Mbinu zilizotumika kutekeleza

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza majukumu yake kwa weledi na ufanisi, Kamati ilitumia njia na mbinu mbalimbali

zilizoendana na matakwa ya Kanuni ya 84(2), 117 (3) (5) (8), na (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016 kuhusu kukutana, Ushirikishaji wa Wadau kuhudhuria na kushiriki shughuli za Kamati na uzingatiaji wa Bajeti ya Kamati iliyoidhinishwa kwa Mwaka 2016/2017 na 2017/2018. Njia zilizotumika ni:-

i. Vikao na Wizara kwa ajili ya kupokea na kujadili Taarifa za utekelezaji wa Wizara na Taasisi inazosimamia;

ii. Kuwataka Mawaziri kutoa maelezo na ufanuzi wa masuala mbalimbali yaliyohitaji ufanuzi. Kwa mfano katika Mkutano wa Tisa wa Bunge la 11, Kamati ilipokea Taarifa Maalumu kutoka Tume ya Pamoja ya Utatuvi wa Kero za Muungano ambayo ipo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano);

iii. Ziara za kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016 ili kujiridhisha na ufanisi wa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ilio chini ya Wizara zinazosimamiwa na Kamati;

iv. Kuwaalika Wadau mbalimbali kwa ajili ya kutoa maoni yao kwenye Miswada ya Sheria ilyoletwa kwenye Kamati kwa mujibu wa Kanuni ya 84 (2) na 117(8) (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016;

v. Kuwasilisha mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti hoja mahsusizi zilizotokana na Bajeti za Wizara zinazosimamiwa na Kamati za Mwaka wa Fedha 2017/2018; na

vi. Kupata mafunzo mbalimbali kwa lengo la kujifunza na kubadilishana uzoefu na Taasisi mbalimbalmali za Serikali na Asasi za Kiraia.

1.3 Shughuli zilizofanyika

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Januari, 2017 hadi Januari, 2018 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria imetekeleza shughuli zifuatazo:-

1.3.1 Kutembelea na kukagua utekekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, ili kukidhi matakwa ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, kuhusu Kamati za Kisekta kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha unaoishia, Kamati hii ilitembelea na kukagua Miradi mbalimbali ya maendeleo iliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, *Wizara ya Katiba na Sheria... [Maneno Haya Yalifutwa na Mwenyekiti wa Kamati]*

na Ofisi ya Makamu wa Rais iliyopo Unguja, Pemba na Dar es Salaam. Kamati pia ilitembelea Mradi wa Ukuzaji Masoko na Mitaji Vijijini (MIVARF) ulioko Dakawa, Morogoro na Mradi wa Kiwanda cha Sukari cha Mkulazi uliopo Wilayani Mvomero Morogoro tarehe 18 Novemba, 2017.

1.3.2 Kuchambua Miswada ya Sheria na Mikataba ya Kimataifa inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1), ikisomwa pamoja na Nyongeza ya Nane 7(1) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, katika kipindi kinachotolewa Taarifa, Kamati yangu ilishughulikia Miswada ya Sheria 9, na Maazimio Mawili ya Kimataifa kama ifuatavyo:-

i. Miswada 6 ya Sheria za Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Miscellaneous Ammendments Bills),

ii. Sheria ya Utoaji wa Huduma za Msaada wa Kisheria ya Mwaka 2017 (*The Legal Aid Act, 2017*),

- iii. Maazimio Mawili ya Bunge kuhusu Mkataba wa Vitambulisho vya Mabaharia (Na.185) wa Mwaka 2003 (*Seafarer's Identity Documents Convention (Revised) of 2003*) na Mkataba wa Kimataifa wa Kazi za Ubaharia wa Shirika la Kazi Duniani wa Mwaka 2006 (Maritime Labour Convention of 2006);
- iv. Kamati kwa kushirikiana na Kamati zingine Nne za Kisekta ilichambua na kujadili Miswada Miwili ya Sheria kuhusu Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Maliasili za Nchi wa Mwaka 2017 (*The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re - Negotiation of Unconscionable Terms) Bill of 2017*) na Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Maliasili wa Mwaka 2017(*The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Bill, 2017*).

Mhesimiwa Spika, Kamati ilichambua kwa weledi na umakini Miswada na Maazimio hayo na kuwasilisha Maoni na Ushauri wake katika Bunge lako ambapo yote yaliridhiwa na kupitishwa na Bunge lako Tukufu kuwa Sheria za nchi.

1.3.3 **Kupokea na kujadili Taarifa za Utekelezaji za Wizara**

Mhesimiwa Spika, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Wizara inazozisimamia pamoja na Taasisi zake. Taarifa hizo ni :-

- i. Taarifa ya Wizara ya Mambo ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa majukumu ya:-

- Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;
- Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka;
- Shule ya Sheria Tanzania;
- Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini;
- Tume ya Marekebisho ya Sheria;
- Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora
- Tume ya Utumishi wa Mahakama na;
- Chuo cha Utumishi wa Mahakama Lushoto

ii. Taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, kuhusu Utekelezaji wa majukumu ya Taasisi zifuatazo:-

- Tume ya Taifa ya Uchaguzi;
- Ofisi ya Msajili Mkuu wa Vyama vya Siasa;
- Wakala wa Afya na Usalama Mahali pa Kazi;
- Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi;
- Shirika la Tija la Taifa;
- Tume ya Usuluhishi na Utatuzi; na
- Kazi na Ajira.

Mheshimiwa Spika, lengo la kupokea na kujadili Taarifa za utekelezaji wa Wizara na Taasisi zake ilikuwa ni kutekeleza jukumu la Kibunge la kuisimamia Serikali kama inavyoainishwa katika Ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Baada ya kujadili Taarifa hizo, Kamati ilibaini masuala mbalimbali ambayo yanafafanuliwa katika Sehemu ya Pili ya Taarifa hii.

1.3.4 **Kuchambua Taarifa za Wizara kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017; na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.**

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98(2) ikisomwa pamoja na Nyongeza ya Nane Kifungu 7(1)(a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ilichambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na kufanya ulinganisho wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hizo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchambuzi uliofanywa na Kamati yanaelezewa kwa kina katika Sehemu ya Pili ya Taarifa hii.

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

2.1 Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, baada ya kuainisha majukumu ya Kamati na shughuli zilizotekelzeza na Kamati kwa kipindi cha Januari 2017 hadi Januari 2018, naomba sasa nitoe Taarifa kuhusu masuala mbalimbali ambayo Kamati imeyabaini wakati ikitekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, masuala yatakayotolewa Taarifa ni yale ambayo Kamati imebaini kuwa ni changamoto ambazo zinahitaji kupewa umuhimu wa kipekee ili kuziwezesha Kamati, Wizara na Taasisi zake kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, hivyo kuleta tija kwa Taifa. Masuala hayo ni :-

- i. Ushiriki wa Wadau katika Utungwaji wa Sheria;
- ii. Upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo;
- iii. Ufinyu na ukomo wa Bajeti kwa Taasisi zote ambazo Kamati inazisimamia;
- iv. Ufinyu wa muda kwa Kamati kutembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo;
- v. Usimamizi Sahihi wa Matumizi ya Fedha za Umma;
- vi. Semina na Mafunzo;
- vii. Usimamizi na Utoaji wa Haki Nchini;
- viii. Changamoto za Ukosefu wa Ajira kwa Vijana
- ix. Ujenzi wa Mazingira Wezeshi kwa Watu wenye Ulemavu

2.2 Matokeo ya Uchambuzi wa Kamati

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kutoa maelezo kuhusu matokeo ya uchambuzi wa Kamati kwenye masuala yaliyoainishwa hapo juu.

2.2.1 Ushiriki wa Wadau katika Utungwaji wa Sheria

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kinachotolewa taarifa, Kamati ilichambua na kujadili Miswada Mitatu ya Kisekta (3), Maazimio Mawili (2) na Miswada Sita (6) ya Sheria za Marekebisho ya Sheria Mbalimbali. Jumla ya Sheria zote zilizochambuliwa na kujadiliwa na Kamati zikiwemo Sheria zilizomo katika Miswada ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ni Sheria 41.

Mheshimiwa Spika, wakati wa uchambuzi Kamati ilibaini changamoto ya Wizara au Taasisi husika kutowashirikisha Wadau wanaoguswa na Marekebisho ya Sheria husika katika mchakato wa Marekebisho yanayofanyika. Kwa mfano katika Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, Na. 4 wa Mwaka 2016 ambao ulisomwa Bungeni kwa mara ya Pili na Tatu Mwezi Februari, 2017, Kamati ilibaini kuwa Wadau wa Sekta ya usafirishaji na mafuta hawakushirikishwa vya kutosha katika Marekebisho yaliyokusudiwa kufanywa katika Sheria ya Tozo za Barabara na Mafuta, Sura ya 220.

Katika Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, Na. 3 wa Mwaka 2017 ambao ulisomwa kwa mara ya Pili na Tatu Bungeni Mwezi Septemba, 2017, Kamati ilibaini kwamba Wadau wa Sekta ya Usafirishaji hawakushirikishwa vya kutosha katika Marekebisho yaliyokusudiwa kufanywa katika Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA) Sura ya 413.

Mheshimiwa Spika, mwezi Julai Mwaka 2017 Kamati ilijadili na kuchambua Muswada wa Sheria ya Marekebisho mbalimbali, Na. 4 wa Mwaka 2017. Muswada huu ulifanya marekebisho makubwa katika Sheria ya Madini, Sura ya 123 (The Mining Act, CAP 123), Sheria ya Petroli, Sura ya 392 (The

Petroleum Act, Cap 392), Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332 (The Income Tax Act, Cap 332), Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148 (The Value Added Tax Act, Cap 148, Sheria ya Bima, Sura ya 394 (The Insurance Act, Cap 394 na Sheria ya Usimamizi wa Kodi, Sura ya 438 (The Tax Administration Act, Cap 438). Katika Uchambuzi wa Muswada huu, kwa kutumia Kanuni ya 84(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, Kamati iliwaalika Wadau, mbalimbali zaidi ya 40 kutoka taasisi za Serikali, asasi za kiraia, Taasisi za Dini na wawakilishi kutoka Sekta Binafsi na hasa Makampuni ya Mafuta na Gesi ambaao walifika kwenye Kamati kutoa maoni yao kuhusu Muswada huu. Ushiriki wa Wadau wengi katika Muswada huu ulikua ni mfano mzuri wa namna ambayo Wadau wanatakiwa kushirikishwa kwa kiwango cha kutosha katika uchambuzi wa Miswada.

Mheshimiwa Spika, katika Muswada huu, pamoja na mambo mengine, Kamati ilipitisha marekebisho mbalimbali yanayoleta tija katika Sekta ya Madini kama vile kuundwa kwa Tume ya Madini na kuongeza wigo wa ushiriki wa Wananchi katika utoaji wa huduma mbalimbali katika migodi. (Local content).

Mheshimiwa Spika, wajibu wa kuwashirikisha Wadau katika mchakato wa kutunga au kurekebisha Sheria ye yeyote ile ni wajibu wa Kikatiba kwa mujibu wa Ibara ya 8(d) na 21(2) ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Jukumu hili pia ni Jukumu la Kikanuni kwa mujibu wa Kanuni ya 84(2) na 117(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016. Hivyo ni jukumu la Kila Wizara au Taasisi ya Serikali inayokusudia kuwa na Muswada au kufanya Marekebisho ya Sheria ye yeyote kuwashirikisha wadau wakuu katika Muswada huo au Marekebisho yanayokusudiwa kabla ya Muswada wa Sheria husika kusomwa Bungeni kwa mara ya kwanza.

2.2.2 **Upatikanaji wa Fedha kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.**

Mheshimiwa Spika, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya

98 (1) na kufanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 kwa Wizara na Taasisi inazozisimamia kama ifuatavyo:-

i. Ofisi ya Waziri Mkuu - Fungu 37

- Mradi Na. 4494 - Ujenzi wa Soko na Barabara Pemba ; na
- Mradi Na. 4494 - Ujenzi wa Soko na Barabara Unguja

ii. Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) Fungu 31

Mradi wa Ujenzi wa Barabara kwa kiwango cha changarawe kwa kushirikiana na Mradi wa MIVARF huko Pemba.

iii. Wizara ya Mambo ya Katiba na Sheria (Fungu 41)

Mradi wa Ujenzi wa Ofisi ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora iliyoko Pemba (**Fungu 55**).

Mheshimiwa Spika, katika ziara hizo, Kamati ilibaini kuwa Miradi mingi iliyotengewa fedha haikutekelezwa ipasavyo kutokana na fedha ndogo kutolewa. Kwa Mfano Ukarabati wa Ofisi ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Pemba ulichukua zaidi ya Miaka Mitano tangu Mwaka wa Fedha 2011/2012 kukamilika kutokana na kutengewa fedha kidogo kwa ajili ya Ukarabati. Hata hivyo katika Mwaka wa fedha 2016/2017 Tume ilitenga fedha ya kutosha kukamilisha Ukarabati wa Ofisi hii ambao umegharimu **Shilingi Milioni Arobaini (40,000,000/=)** mpaka kukamilika kwake.

Mheshimiwa Spika, ipo Miradi ya Maendeleo ambayo haikupokea fedha kabisa mpaka Mwezi Machi, 2017 wakati Kamati inafanya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti za Wizara. Kwa Mfano Mradi Na. 4945 - Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na Mradi Na. 6577 - Mradi wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambayo ipo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Miradi ya MIVARF iliyoko Pemba na Unguja Mradi Na.4494 unaohusu ujenzi wa Masoko na Barabara Unguja na Pemba imekua ikitekelezeka kwa ufanisi mkubwa kwa sababu ya ufadhilli kutoka Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB) pamoja na Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Kilimo (IFAD).

Mheshimiwa Spika, kuhusu Miradi ya MIVARF iliyoko Pemba, Unguja na sehemu mbalimbali hapa Tanzania Bara, Kamati ilishauri Serikali kwa kushirkiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika na Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Kilimo kukamilisha mchakato wa makubaliano ya awamu ya pili ya uendelezaji na utekelezaji wa miradi hii katika Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

2.2.3 Ufinyu na ukomo wa Bajeti kwa Taasisi ambazo Kamati inazisimamia

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina wa Taarifa za Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 kwa Mafungu 14 ya Wizara na Taasisi inazozisimamia kama ifuatavyo:-

• Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais (Fungu 26);

- Ofisi ya Makamu wa Rais (Fungu 31);
- Ofisi Binafsi ya Waziri ya Waziri Mkuu (Fungu 25);
- Ofisi ya Waziri Mkuu (Fungu 37);
- Tume ya Usuluhishi na Utatuzi(Fungu 15);
- Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa (Fungu 27);
- Tume ya Taifa ya Uchaguzi (Fungu 61);
- Kazi na Ajira (Fungu 65);
- Wizara ya Sheria na Katiba (Fungu 41);
- Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Fungu 16);
- Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka (Fungu 35);
- Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (Fungu 55);
- Tume ya Maboresho ya Sheria (Fungu 59) na
- Tume ya Utumishi wa Mahakama (Fungu 12).

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa bajeti ya Wizara na Taasisi hizi na kulishauri Bunge lako Tukufu kuzipitisha bajeti zake pamoja na changamoto zilizoonekana katika kila Taasisi. Kwa mfano katika uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (Fungu 55) kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume kwa Mwaka wa fedha 2016/2017, Kamati ilibaini kwamba, Tume imekua

ikitengewa fedha kidogo sana katika kila bajeti kwa Miaka zaidi ya Mitatu (3) mfululizo hivyo, kuathiri utekelezaji wa majukumu yake. Kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 Tume iliidhinishiwa na Bunge kiasi cha **Shilingi 5,578,338,000/=** lakini ilipokea kiasi cha **Shilingi 2,571,887,401/= tu.** Sawa na asilimia 46.1.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya jitihada za kutosha ili bajeti ya Tume iongezwe kwa kupeleka ombi katika Kamati ya Bunge ya Bajeti kwa lengo la kuishawishi Serikali kuongeza bajeti ya Tume. Hata hivyo jitihada hizi hazikufanikiwa katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 kutokana na ukomo wa bajeti. Hivyo Serikali iliahidi kulifanya kazi suala hili katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutimiza ahadi yake katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwa kuongeza bajeti ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa Fedha ya Matumizi Mengineyo (OC) kutoka **Shilingi Milioni Mia Tisa Tisini na Nne, Laki Tano Kumi na Nne Elfu (994,514,000.00)** katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 mpaka **Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tano Sitini na Sita, na Themanini Elfu (1,566,080,000.00)** katika Mwaka wa Fedha 2017/2018. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 57.

2.2.4 Ufinyu wa Muda wa Kamati Kutembelea na Kukagua Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inazitaka Kamati za Kisekta kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa fedha unaoisha. Ufinyu wa muda unakwamisha utekelezaji wa Kanuni hii. Kamati ya Katiba na Sheria inasimamia Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) ambayo ina Miradi Unguja na Pemba. Siku za Kikanuni za Kukagua Miradi ya Maendeleo ni siku saba ambazo kiuhalisia hazitoshi kukagua Miradi ya Maendeleo kwa ufanisi Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa muda wa Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo Kamati ilifanikiwa kutembelea Miradi ya Maendeleo michache sana katika kipindi cha Januari 2017 hadi Januari 2018.

2.2.5 **Usimamizi Sahihi wa Matumizi ya Fedha za Umma**

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Katiba na Sheria inasimamia pia Sekta ya Kazi na Ajira ambayo ndani yake kuna baadhi ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kama Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF). Katika Taarifa za Kamati kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 na 2016/2017 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na 2017/2018 ambazo zilisomwa Mwezi Aprili, 2016 na 2017, Kamati iliishauri Serikali kufuatilia kwa karibu na kuchukua hatua kali za kinidhamu kwa watendaji wote wa NSSF waliohusika na tuhuma mbalimbali za ubadhirifu wa fedha za Umma katika Miradi yake mbalimbali ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, Katika taarifa ya Kamati iliyosomwa Mwezi Aprili, 2017 Kamati illieleza Bunge lako Tukufu kwamba Serikali ilikua inaendelea na uchunguzi wa tuhuma hizi na hasa kwa kutumia Mamlaka ya Kupambana na kudhibiti Rushwa, Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Mamlaka ya Usimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii (SSRA) pamoja na Mamlaka nyingine za kichunguzi za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano imejipambanua katika kubana matumizi na kuziba mianya yote ya rushwa na ubadhirifu wa fedha za Umma. Ni muhimu kwa Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii kutumia na kuwekeza fedha za Wananchi zilizowekwa katika Mifuko hiyo kwa namna ilio na tija kwa Wananchama wake na katika uendelevu na uimara wa kifedha wa Mifuko husika (Financial sustainability and liquidity of the funds).

Kwa namna ya pekee Kamati inaipongeza Serikali kwanza kwa kuunda Bodi mpya ya NSSF na pili inaipongeza Bodi mpya

ya NSSF kwa kuchukua hatua stahiki ya kuwasimamisha kazi Wafanyakazi wote wa NSSF ambao wametajwa katika tuhuma hizo tarehe 30 Juni, 2017 katika kikao cha kawaida cha 72 cha Bodi ya NSSF.

Mheshimiwa Spika, ni vema Watumishi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii kutambua kwamba wamepewa dhamana kubwa ya kusimamia vizuri fedha za Wanachama na inawapasa kuibeba dhamana hii kwa uangalifu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii kwa Miaka Miwili mfululizo iliishauri Serikali kutazama uwezekano wa kuunganisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili kuwa na Sekta ya Hifadhi ya Jamii ilio na Mifuko michache na inayoweza kuwafikia wafanyakazi wengi kwa urahisi na kwa ufanisi zaidi. Tunapenda kwa mara nyingine tena kuipongeza Serikali hii sikivu ya Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuufanya kazi ushauri huu wa Kamati na kuunganisha Mifuko hii kupitia Muswada wa kuanzisha Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Sekta ya Umma wa Mwaka 2017 (The Public Service Social Security Fund Bill, of 2017) ambao tayari umesomwa kwa mara ya pili na ya tatu na kupitishwa na Bunge hili kuwa Sheria ya nchi.

2.2.6 Semina na Mafunzo

Mheshimiwa Spika, katika Kipindi cha Januari 2017 mpaka Januari 2018 Kamati ilipatiwa Semina/mafunzo kutoka Taasisi na Asasi mbalimbali za Kiraia kwa ajili ya kujenga uelewa wa masuala mbalimbali ya kisheria. Taasisi ambazo zimetoa mafunzo kwa Kamati katika Kipindi hiki ni kama ifuatavyo:-

- Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa chini ya Mradi wake wa Legislative Support Program (UNDP - LSP);
- Shirika la Umoja wa Mataifa la Wanawake (UN - Women) kwa kushirikiana na Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania (TWPG);
- Umoja wa Mabunge Duniani (IPU);

- Jukwaa la Uchambuzi wa Sera Tanzania (Policy Forum);
- Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA);
- Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC);
- Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS);
- Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA); na
- Mamlaka ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi (OSHA).

Mheshimiwa Spika, kutohana na mafunzo yaliyotolewa, Wajumbe wamejengewa uwezo kuhusu mambo ya Sheria.

2.2.7 Utatuzi wa Kero za Muungano

Mheshimiwa Spika, moja kati ya maeneo muhimu ambayo Kamati hii inashughulika nayo ni kuhakikisha kwamba kero za Muungano zinatatuliwa kwa wakati. Kamati ilikutana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia masuala ya Muungano tarehe 02 Novemba, 2017 hapa Dodoma na kupokea Taarifa ya Utekelezaji kutoka Kamati Maalum ya pamoja ya Kutatua Kero za Muungano iliyoundwa na Wataalamu mbalimbali kutoka Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kamati hii Maalum iliundwa toka Mwaka 2006 kwa lengo la kuhakikisha kwamba Kero za Muungano zinapunguzwa na kutatuliwa kabisa ili Wananchi wa pande zote mbili waendelee kufurahia matunda ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, zipo kero ambazo Ofisi ya Makamu wa Rais inatakiwa kuendelea kuzitatua kuititia Kamati hii Maalum ili kuendelea kudumisha Muungano. Kwa mfano Ajira kwa Watumishi wa Zanzibar katika Taasisi za Muungano, Ushirikiano wa Zanzibar na Taasisi za Nje, Uwezo wa Serikali

ya Zanzibar kukopa ndani na nje ya nchi, Ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mgawanyo wa Mapato ya Kodi na Misaada, Wafanyabiashara wa Zanzibar kuendelea kutozwa kodi mara mbili, utafutaji na uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia na Usajili wa vyombo vya moto. Kero hizi zote zinaendelea kutatuliwa na Serikali zote mbili na jitihada kubwa zimefanyika na Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kuhakikisha kwamba kero hizi zinapungua.

2.2.8 Usimamizi na Utoaji wa Haki Nchini

Mheshimiwa Spika, moja kati ya majukumu ya Wizara ya Mambo ya Katiba na Sheria ni kusimamia Haki na Mfumo wa Utoaji Haki. Eneo hili bado limekua na changamoto nyingi hapa Tanzania kama vile ufinyu wa Bajeti na mrundikano wa Kesi Mahakamani. Kutokana na Ufinyu wa Bajeti kumekua na uhaba mkubwa wa Mahakamu na Rasilimali Watu katika kusimamia utoaji Haki Tanzania. Kwa mfano kwa Mwaka 2016 pekee, Mahakama ya Tanzania ilikua na jumla ya mashauri **335,624¹**. Kama hakuna ubunifu na Mipango Mikakati ya kupunguza wingi wa mashauri haya Kitaalam, haki za Watu wengi zitaathirika.

Mheshimiwa Spika, tatizo la mrundikano wa kesi kuanzia katika Mahakama za Mwanzo hadi Mahakama ya Rufaa ya Tanzania bado ni kubwa sana. Kwa mfano katika Mahakama ya Rufaa ya Tanzania kwa muda wa Miaka 6 mfululizo idadi ya Majaji imebakia kuwa ni 15 lakini idadi ya mashauri kwa Mwaka imekua inaongezeka kila Mwaka; Kwa mfano, 2,466 (2012), 2,629 (2013), 2,916 (2014), 3,244 (2015), 3,975 (2016) na 4,439 (2017)².

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza sana uamuzi wa Mahakama ya Rufaa wa Tarehe 2 Februari 2018 kwa kumwondolea Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) Mamlaka ya

¹Taarifa ya Utekelezaji ya Mahakama ya Tanzania kwa Mwaka 2016/2017

²Hotuba ya Jiji Mkuu wa Tanzania katika Maadhimisho ya Siku ya Sheria Nchini, Tarehe 01 Februari, 2018. uk. 2

kuzuia dhamana ya mshtakiwa bila kulazimika kutoa sababu chini ya Kifungu cha 148 (4) cha Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai. Katika hukumu hiyo katika kesi ya rufaa ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali dhidi ya Mwanaharakati wa Haki za Binadamu, Jeremia Mtobesya, Mahakama ya Rufaa imesema kwamba Kifungu hiki ni Kinyume na Ibara ya 13(6) ya Katiba na ni batili. Kifungu hiki kimekua ni kikwazo kikubwa katika kusimamia Haki za Watuhumiwa wengi na uamuvi huu wa Mahakama ya Rufaa ni wa kupongezwa sana.

Changamoto za Ukosefu wa Ajira kwa Vijana na Uwekaji wa Mazingira Wezeshi kwa Watu Wenye Ulemavu

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu inaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kukabiliana na changamoto mbalimbali za ukosefu wa Ajira kwa Vijana na uwekaji wa mazingira wezeshi kwa Watu wenye Ulemavu. Hata hivyo maeneo haya ya Maendeleo ya Vijana na Watu wenye Ulemavu hayana mafungu ya moja kwa moja ya Kibajeti katika Ofisi ya Waziri Mkuu. Kukosekana kwa Mafungu ya Kibajeti "mahususi" kwa ajili ya Vijana na Watu wenye Ulemavu kunaleta changamoto kubwa katika usimamizi na utekelezaji wa Sera, Sheria, Uratibu na Mipango Kazi ya kusimamia maslahi na maendeleo ya Vijana na Watu wenye Ulemavu.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAPENDEKEZO YA KAMATI

USHIRIKI WA WADAU KATIKA UTUNGWAJI WA SHERIA

Mheshimiwa Spika, KWA KUWA, haki ya Wananchi kushiriki katika shughuli za Serikali ni haki ya Kikatiba,

NA KWA KUWA ushiriki huo ni matakwa ya kikanuni ya Kanuni za Kudumu za Bunge;

NA KWA KUWA, kutokuwashirikisha Wananchi katika utungwaji wa Sheria kunaondoa uhalali wa Sheria hizo;

HIVYO BASI; Kamati inashauri Wizara na Taasisi zote za Serikali zinazotunga au zinazokusudia kurekebisha Sheria zao kuwashirikisha kwa kina Wadau wote wanaoguswa na Sheria hizo kabla na baada ya kusomwa Bungeni kwa mara ya kwanza;

3.1 UPATIKANAJI WA FEDHA KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

Mheshimiwa Spika, KWA KUWA, Miradi ya Maendeleo ni muhimu kwa maendeleo ya uchumi wa nchi yetu,

NA KWA KUWA, utekelezaji wa Miradi hii unategemea upatikanaji wa fedha kutoka Hazina,

NA KWA KUWA; kutotolewa kwa fedha za Miradi ya Maendeleo kwa wakati kunaathiri utekelezaji wa Miradi husika;

HIVYO BASI; Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

i) Serikali itoe fedha kwa wakati ili kutekeleza Miradi ya Maendeleo ilio chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na Wizara ya Katiba na Sheria kwa nusu ya Pili ili yobakia katika Mwaka huu wa Fedha 2017/2018.

ii) Serikali itoe kipaumbele kwa Miradi ya Maendeleo ambayo imekua ikipokea fedha chache siku za nyuma hususani Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na Mfuko wa Taifa wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

3.2 UFINYU NA UKOMO WA BAJETI KWA TAASISI AMBAZO KAMATI INAZISIMAMIA

Mheshimiwa Spika, KWA KUWA, ufanisi wa Taasisi ye yeyote unategemea kiwango cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge;

NA KWA KUWA; kiwango cha utekelezaji wa majukumu ya Taasisi hizo unategemea sana kiasi cha fedha kilichopokelewa ;

NA KWA KUWA; Uhaba wa Fedha unaathiri utekelezaji wa majukumu ya Taasisi hizo;

HIVYO BASI; Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha ya kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Taasisi zinazosimamiwa na Kamati katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 na kutoa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa Taasisi hizo katika nusu hii ya pili ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

3.3 UFINYU WA MUDA WA KAMATI KUTEMBELEA NA KUKAGUA MIRADI YA MAENDELEO

Mheshimiwa Spika, KWA KUWA; ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo ni jukumu la Msingi kwa Kamati zote za Kisekta;

NA KWA KUWA; muda uliopo wa Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo hautoshi kwa Kamati za Kisekta kufanya ukaguzi wa miradi hii kwa ufanisi unaotakiwa;

HIVYO BASI; Kamati inaishauri Kamati za Kisekta zipewe muda zaidi wa ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo katika kalenda ya shughuli za Bunge ili kujiridhisha na utekelezaji wa Bajeti ya Serikali katika Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha husika;

3.4 USIMAMIZI SAHIHI WA MATUMIZI YA FEDHA ZA UMMA

Mheshimiwa Spika, KWA KUWA, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii imepewa dhamana ya kupokea michango ya Wanachama wa Mifuko hiyo;

NA KWA KUWA; Menejimenti na Bodi za Mifuko hiyo zinawajibika moja kwa moja na usimamizi wa Mifuko hiyo;

NA KWA KUWA; ni wajibu wa Watumishi katika Mifuko hii kuwa waadilifu na waaminifu katika kutunza fedha za Wanachama wa Mifuko husika;

HIVYO BASI; Kamati inashauri hatua kali za Kisheria zichukuliwe dhidi ya Watumishi wote wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ambao wanatumia fedha za Mifuko kwa ubadhirifu na kwa kutokufuata Kanuni bora za fedha na hesabu katika matumizi na uwekezaji wa fedha hizo za Wanachama.

3.5 SEMINA NA MAFUNZO KWA KAMATI

Mheshimiwa Spika, KWA KUWA, Kamati hii ina jukumu la Kuchambua na kujadili Miswada yote ya Sheria za Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ambazo zinagusa karibu Wizara zote (Mtambuka);

NA KWA KUWA; mafunzo ni muhimu kwa Waheshimiwa Wabunge ili kupanua wigo wa uelewa katika mambo mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu yao;

NA KWA KUWA; Elimu haina mwisho;

HIVYO BASI; Kamati inashauri kwamba:-

- i) Wizara, Ofisi na Taasisi zote zinazosimamiwa na Kamati hii kuendelea kutoa mafunzo mbalimbali ya kisekta ili kujenga uwezo kwa Kamati;
- ii) Ofisi ya Bunge iendelee na utaratibu wa kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati kwa kuandaa mafunzo Maalumu ya Kamati ndani na nje ya nchi;
- iii) Wizara na Taasisi za Serikali zenyе maeneo yanayofanyiwa marekebisho ya Sheria kuendelea kutoa mafunzo kwa Kamati ili kuendelea kujenga uwezo na uelewa wa Kamati katika maeneo husika.

3.6 UTATUZI WA KERO ZA MUUNGANO

Mheshimiwa Spika; KWA KUWA, kumekuwepo Kero mbalimbali za Muungano toka kuasiwiwa kwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar Mwaka 1964;

NA KWA KUWA, Jitihada mbalimbali zimechukuliwa na Serikali ya Jamuhuri Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kutatua Kero mbalimbali za Muungano;

HIVYO BASI; Kamati inashauri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kuititia Tume ya Pamoja ya Kutatua Kero za Muungano kuendelea kutatua Kero mbalimbali za Muungano na kuhakikisha kwamba Wananchi wa pande zote mbili wanatumia na kufaidika na fursa mbalimbali zinazotokana na Muungano huu.

3.7 USIMAMIZI NA UTOAJI WA HAKI NCHINI

Mheshimiwa Spika; KWA KUWA, usimamizi na utoaji haki ni suala la msingi la Kikatiba na Haki za Binadamu;

NA KWA KUWA, kumekuwepo na kero mbalimbali katika Mahakama na vyombo vingine vinavyohusika na usimamizi na utoaji wa haki nchini kama vile mrundikano wa kesi, uhaba wa Mahakimu na ufinyu wa Bajeti;

HIVYO BASI; Kamati inaishauri Serikali kuititia Wizara ya Katiba na Sheria, Mahakama ya Tanzania, Tume ya Utumishi wa Mahakama, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ziendelee kufanya kazi kwa weledi, ubunifu na kwa kuzingatia misingi ya Ibara 13 ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 katika kutoa na kusimamia Haki Nchini. Pia Serikali iendelee kuajiri Watumishi zaidi wa Mahakama pamoja na Mahakimu, Majaji wa Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa ili kuboresha mazingira ya Utoaji Haki nchini.

3.8 CHANGAMOTO ZA UKOSEFU WA AJIRA KWA VIJANA

Mheshimiwa Spika; KWA KUWA ukosefu wa ajira bado ni tatizo kubwa kwa Vijana wengi hapa nchini;

NA KWA KUWA Vijana ni nguvu kazi kubwa katika Taifa lolote;

HIVYO BASI Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za kutosha na stahiki katika kuendelea kujenga Mifumo endelevu ya kukuza Ajira kwa Vijana katika Sekta rasmi na zisizo rasmi. Kamati inaishauri Serikali kutekeleza yafuatayo;

i) Serikali iboreshe Sera ya Taifa ya Ajira ya Mwaka 2008 ili iendane na mahitaji ya nyakati zilizopo na kutoa fursa zaidi za ajira kwa vijana

ii) Serikali ianzishe kwa haraka Baraza la Taifa la Vijana ambalo lillianzishwa na Sheria ya Baraza la Taifa la Vijana toka Mwaka 2015. Baraza hili mpaka leo bado halijaanzishwa.

iii) Serikali itoe Mwongozo kwa Halmashauri zote kuhusu utoaji wa fedha za mikopo kwa Vijana cha asilimia 5 na kiasi cha riba ambazo Vijana wanatakiwa kulipa kuliko kuacha utaratibu wa sasa ambapo kila Halmashauri inajipangia utaratibu wake

3.8.1 **UWEKAJI WA MAZINGIRA WEZESHI WA WATU WENYE ULEMAVU**

Mheshimiwa Spika; KWA KUWA Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasimamia usawa kati ya Watu wote;

NA KWA KUWA Watu wenye Ulemavu ni sehemu muhimu ya Jamii ya watu wa Tanzania;

HIVYO BASI Kamati inaishauri Serikali kufanya yafuatayo ili kuboresha maslahi ya Watu wenye Ulemavu;

i) Serikali iendelee kutenga bajeti ya kutosha na kutekeleza misingi iliyotajwa katika Sera ya Huduma na Maendeleo kwa Watu wenye Ulemavu ya Mwaka 2004 na Sheria ya Watu wenye Ulemavu ya Mwaka 2010 ambavyo vinataka ushiriki mkamilifu (Inclusion) wa watu wenye Ulemavu katika mambo yote ya Kijamii.

ii) Serikali itenge bajeti ya kutosha kwa ajili ya Baraza la ushauri la Watu wenye Ulemavu ambalo lipo kwa mujibu wa Sheria ili liweze kufanya Shughuli zake kwa ukamilifu.

3.8.2 UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA KAMATI

Mheshimiwa Spika; KWA KUWA, Bunge lina dhamana kubwa ya kuisimamia na kuishauri Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 63 ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977;

NA KWA KUWA, katika kutimiza jukumu hili Kamati imekua ikitoa Ushauri, Mapendekezo na maelekezo mbalimbali kwa Serikali kupitia Wizara na Taasisi zake;

HIVYO BASI; Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara na Taasisi zake kuendelea kupokea na kutekeleza ushauri na mapendekezo mbalimbali ya Kamati na kutoa Taarifa ya Utekelezaji wa ushauri na mapendekezo hayo kila inapotakiwa kufanya hivyo.

SEHEMU YA NNE

4.0 HITIMISHO

4.1 Shukrani

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa ushirikiano mlioutoa kwa Kamati katika kutekeleza majukumu yake kwa kipindi cha Mwaka Mmoja uliopita.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Mawaziri wote na Watendaji Wakuu wote wa Wizara na Taasisi ambazo Kamati inazisimamia kwa ushirikiano wao katika kutekeleza majukumu ya Kamati kwa kipindi cha Mwaka Mmoja Uliopita. Shukrani za Pekee ziwaendee Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Mhe. Jenista Mhagama (Mb), Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Mhe. January Makamba (Mb), na Waziri wa Katiba na Sheria Prof. Palamagamba John Aidan

Mwaluko Kabudi (Mb), Manaibu Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu Mhe. Antony Mavunde (Mb) na Mhe. Ikupa Alex (Mb), Mhe. Kangi Lugola (Mb), Naibu waziri Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na Makatibu Wakuu wote wa Wizara hizi. Kamati pia inamshukuru kwa namna ya pekee aliyekua Naibu waziri Ofisi ya Waziri Mkuu aliyeshughulikia masuala ya Watu wenye Ulemavu, Dr. Abdallah Possi ambaye kwa sasa ni Balozi wa Tanzania nchini Ujerumani ambaye alifanya kazi vizuri sana na Kamati wakati wa utumishi wake katika Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuwashukuru sana aliyekua Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. George Masaju na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Gerson Mdemu ambao walitoa ushirikiano mkubwa sana katika Kamati kipindi chote cha utumishi wao katika Ofisi hiyo. Kamati inawapongeza sana kwa kuteuliwa kuwa Majaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania na inawatakitia Utumishi uliotukuka katika Mhimili wa Mahakama. Kamati inawashukuru sana Wanasheria wote Waandishi wa Sheria chini ya Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria wa Serikali (CPD) ambao wametoa ushirikiano mkubwa kwa Kamati wakati wa uchambuzi wa Miswada mbalimbali. Vilevile, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Mshauri Mkuu wa Mambo ya Sheria Ofisi ya Bunge (CPLC) pamoja na Wanasheria wote wa Ofisi hiyo walioshiriki katika shughuli za uchambuzi wa Miswada kwenye Kamati ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nitumie nafasi hii kutambua mchango wa Wadau na Taasisi ambazo zimeshirikiana na Kamati wakati wa kutekeleza Majukumu katika kipindi cha Januari 2017 hadi Januari 2018. Kwa uchache naomba kuwataja Wadau wafuatao:-

- Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP);
- Shirika la Umoja wa Mataifa la Wanawake (UN-WOMEN);
- Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania (TWPG)
- Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC),
- Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS),
- Umoja wa Mabunge Duniani (IPU),

- Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA),
- Chuo Kikuu cha Dodoma,
- Chuo cha Mipango Dodoma;
- Chuo cha CBE Tawi la Dodoma;
- Taasisi ya Uwezeshaji wa Watoa Huduma ya Msaada wa Kisheria LSF) ;
- Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF);
- Shirika la OXFAM; na
- Baraza la Maendeleo ya Kijamii Tanzania (TACOSODE)

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kwa mara nyingine nichukue fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa kufanya kazi nzuri na kwa umakini na uzalendo wa hali ya juu katika kutekeleza na kufanikisha majukumu ya Kamati ya kuisimamia na kuishauri Serikali. Naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu ya Taarifa Rasmi za Bunge (HANSARD) kama ifuatavyo:

1. Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Najma Murtaza Giga, Mb- M/Mwenyekiti
3. Mhe Ally Saleh Ally, Mb –Mjumbe
4. Mhe. Mboni Mohamed Mhita, Mb –Mjumbe
5. Mhe Taska Restituta Mbogo, Mb –Mjumbe
6. Mhe. Makame Mashaka Foum, Mb –Mjumbe
7. Mhe. Seif Ungando Ally, Mb- Mjumbe
8. Mhe. Nassor Suleiman Omar, Mb- Mjumbe
9. Mhe. George Simbachawene, Mb –Mjumbe
10. Mhe. Twahir Awesu Mohamed, Mb-Mjumbe
11. Mhe. Ussi Pondeza, Mb- Mjumbe
12. Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb –Mjumbe
13. Mhe. Ajali Rashid Akbar, Mb- Mjumbe
14. Mhe. Omary Ahmad Badwel, Mb- Mjumbe
15. Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb –Mjumbe
16. Mhe. Prof. Jumanne Abdallah Maghembe, Mb- Mjumbe
17. Mhe. Joram Ismail Hongoli, Mb- Mjumbe
18. Mhe. Anna Joram Gidarya, Mb –Mjumb
19. Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb –Mjumbe
20. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb –Mjumbe
21. Mhe. Selemani Zedi, Mb –Mjumbe
22. Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb –Mjumbe

23. Mhe. Selemani Nchambi, Mb –Mjumbe
24. Mhe. Juma Kombo Hamad, Mb –Mjumbe
25. Mhe. Dkt. Mathayo David Mathayo, Mb – Mjumbe
26. Mhe. Zainab Mndolwa, Mb-Mjumbe

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu, napenda kuishukuru Sekretariati yote ya Bunge chini ya Uongozi thabitii wa Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai kwa ushirikiano wao katika kufanikisha shughuli za Kamati, Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Angelina Sanga, Katibu wa Kamati Ndg. Dunford Mpelumbe, Msaidizi wa Kamati Ndg. Raheli Masima kwa umakini na weledi wao katika kufanikisha kazi za Kamati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza kwa kina Shughuli zilizotekelezwa na Kamati, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli hizo, maoni na mapendekezo ya Kamati, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii .

Mheshimiwa Spika, Naomba kutoa Hoja.

Mohamed Omary Mchengerwa, Mb
MWENYEKITI
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE
YA KATIBA NA SHERIA

8 Februari 2018

MHE. PROF. NORMAN A. S. KING: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante hoja imetolewa na imeungwa mkono tunakushukuru sana Mheshimiwa Mchengerwa,

Mwenyekiti wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Katiba na sheria. Tunaendelea lakini kabla sijamuita Mwenyekiti niongeze kwa mamlaka niliyonayo niongeze muda usiozidi dakika 30 ili tuweze kutendea haki haya yaliyo mbele yetu. Sasa namuita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa Mheshimiwa Jasson Rweikiza.

MHE. JASSON S. RWEIKIZA – MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGЕ YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ifuatayo ni taarifa ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kwa kipindi cha kuanzia Januari 2017 hadi Januari 2018. Kwa mujibu wa Kanuni 117(15) ya Kanuni ya Kudumu za Bunge za mwaka 2016 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu taarifa ya mwaka ya shughuli ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2017 hadi Januari 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba taarifa nzima liingie kwenye kumbukumbu za *Hansard* kwa sababu sitasoma yote. Shughuli zilizotekelawa ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2016/17 miradi iliyotembelewa ni ambayo ilitengewa fedha katika mwaka wa fedha 2016/2017 na ilitekelezwa katika Mikoa ya Tanga, Morogoro, Njombe, Iringa na Mbeya na ni ile iliyopo katika Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuchambua taarifa kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2016/2018; Kamati ilichambua taarifa ya utekelezaji wa ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais; katika kipindi cha Januari, 2017 hadi Januari, 2018 Kamati ilipokea na akujadili taarifa mblimbali za utekelezaji wa majukumu ya

Ofisi ya Rais na kushiriki semina mbalimbali. Wajumbe wa Kamati walipata fursa ya kushiriki katika semina mbalimbali zilizoandalowi na Ofisi ya Bunge Wizara na taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais na *TARURA* na taasisi binafsi ya MVIWATA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya uchaguzi, ukaguzi wa miradi ya maendeleo:-

(a) MKURABITA – Mpango huu unaandaa na kusimia mfuko wa kitaifa wa umiliki na urasimishaji wa biashara unaotambulika na kukubalika kisheria nchini na hivyo kuwawezesha wanyonge kurasimisha mali zao, ardhi na biashara ili kuwawezesha kujikwamua kiuchumi. Aidha, mpango huu umekuwa ukihamasisha na kuchangia ujenzi wa masijala za ardhi katika vijiji na mitaa na kuwawezesha uhifadhi madhubuti wa na usalama wa nyaraka, hati za hakimiliki za kimila na nyaraka nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati iltembelea jumla ya maeneo 11 katika Mikoa ya Dodoma, Morogoro, Tanga, Njombe na Mbeya. Baadhi ya maeneo hayo ni mitaa ya Tuelewane na Kihonda B katika Mkoa wa Morogogo ambapo MKURABITA imewezesha kupimwa kwa jumla ya viwanja 822 na ramani zake kuidhinishwa na Mkurugenzi wa Upimaji wa Rasilimali na Ramani wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Hadi wakati huo jumla ya hakimiliki 132 sawa na asilimia 16 zilikuwa zimetolewa kwa wananchi na nyingine zilikuwa zinaendela kuandaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika Mkoa wa Njombe mpango huo umewawezesha kupimwa kwa jumla ya viwanja 1635 kati ya na hati 730 sawa na asilimia 45 ziliandalowi na kukabidhiwa kwa wananchi na vijiji vya Joshoni, Melinze, Mpechi, Nazareti, Idundilaga na Mtaa wa Kambarage. Kijiji cha Pwaga kilichopo kwenye Wilaya ya Mpwapwa, Mkoani Dodoma kimefanikiwa kwa kiwango kikubwa kutokana na urasimishaji wa ardhi uliotekelawa na MKURABITA. Katika kijiji hicho jumla ya mashamba 1277 yamepimwa na hati 131 sawa na asilimia 81 zimeandalowi na kukabidhiwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mpango huu umegharamia ujenzi wa masijala ya ardhi katika kijiji hicho kwa kutoa shilingi milioni 32.

Katika maeneo ambayo Kamati ilifanikiwa kukagua utekelezaji wa MKURABITA ilibainika kwamba baadhi ya wananchi wameweza kutumia urasimishwaji wa maeneo ya bishara kujikwamua kiuchumi. Wananchi hao wametumia hati za hakimiliki za kimila kama dhamana katika benki na taasisi za fedha na hivyo kupata mikopo. Mfano wanufalka wanne katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe wamefanikiwa kukopa kati ya shilingi milioni 50 hadi 500 kwa kutumia hati hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inaweza mpango huu kutekelezwa nchi nzima kwani unaweza kusaidla kuondoa mligororo ya ardhi nchini pamoja na kuwainua wananchi kiuchumi kwa haraka kutokana na kutumia hati za hakimiliki za kimila kama dhamana katika benki za taasisi za fedha. Aidha, Serikali ifanyie kazi changamoto ya baadhi ya benki na taasisi za fedha kukataa kupokea hati za hakimiliki za kimila kama dhamana ya mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Rais wakujitegemea (*PTF*) majukumu ya msingi ya mfuko huu ni kutoa mikopo ushauri na mafunzo ya kibiashara kwa wajasiilamali wadogo wadogo na wa kati nchini. Kamati ilikagua utendaji wa mfuko huu kwa kutembela vikundi sita katika Mikoa ya Njombe na Morogoro ambavyo vinajishughulisha na ufundi wa magari na uchomeleaji vyuma ukamuaji wa mafuta, ufugaji, ususi na ufumaji, uzoaji taka na uokwaji wa mikate. Kwa ujumla vikundi hivyo ambavyo vinaundwa na wanachama wasiopungua watano kila kimoja vimepewa jumla ya shilingi milioni 32.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfuko huu umekuwa ni mkombozi kwa baadhi ya vijana na wanawake kwani umewawezesha kupata mitaji na kujajiri, mfano mzuri ni kikundi cha Mwale *Cleaners* ambacho ni kati vikundi sita

ambao ni wahitimu wa chuo kikuu waliamua kutosubiria ajira za maofisini wakaamua kujingiza katika ujasiriamali. Kikundi hicho kilanza kwa kuchukua mkopo wa shilingi milioni 2.5 na hadi kimefikia hatua ya kuchukua mkopo wa shilingi milioni kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *TASAF*, mfuko huu upo katika Awamu ya *Tatu ambayo* imejikita katika kuzisaidia kaya maskini na kuzipatia ruzuku ya fedha ili ziweze kuboresha maisha kwa kupata chakula, kulisha watoto kuhuduria shulen na pamoja na kliniki kwa wale walio chini ya umri wamiaka mitano. Taarifa ya utekelezaji imeonesha kuwa hadi sasa takribani Watanzania milioni 5.9 wameandikishwa ili wanufaika na utaratibu huu na kumekuwa na mafanikio makubwa ya watoto wanaotoka katika kaya masikini kuhuduria shulen na kliniki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo sita ambayo Kamati ilitembelea kwenye Mikoa ya Morogoro, Tanga, Mbeya, Njombe na Iringa imebainika kwamba jumla ya kaya 753 zimenufaika katika awamu ya malipo 11 kwa kupokea jumla ya shilingi milioni 216.8. Utaratibu wa ruzuku wa kaya masikini umekuwa na mafanikio makubwa kutokana na kuwawezesha walengwa kuboresha maisha kwa kupata milo miwili kwa siku na kuwawezesha watoto kuhuduria shulen na kliniki. Vilevile baadhi ya wanufaika wametumia sehemu ya ruzuku kuanzisha miradi mbalimbali ya kiuchumi kama vile kilimo, ufugaji na biashara na hivyo kujiongezea uwezo wa kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Utumishi wa Umma kilianzishwa kwa lengo la kutoa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu katika fani za uongozi menejimenti ya utawala, kutoa ushauri wakitaalam, kufanya utafiti na kutoa machapisho ya kitaalamu katika utumishi wa umma. Chuo hiki ambacho ni nguzo muhimu ya mafunzo ya kiutumishi kwa watumishi wa umma hasa kwa kuzingatia kwamba hakuna taasisi nyingine inayotoa mafunzo ya aina hiyo ina jumla ya *campus* sita katika maeneo mbalimbali nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa miji ya mkakati, mradi huu unatekelezwa katika mikoa saba ambayo ni Arusha, Mwanza, Mbeya, Tanga, Dodoma, Mtwara, Mikindani na Kigoma Ujiji. Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa miradi hii katika maeneo sita kwenye Halmashauri za Majiji ya Tanga na Mbeya ambako kwa ujumla wake yalitengewa jumla ya shilingi bilioni 8.04.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Mfuko wa Barabara (*Road Fund Board*), bodi hii ilianzishwa mwaka 1992 kwa lengo la kukarabati, kuboresha na kutengeneza barabara muhimu za Mikoa, Wilaya, za Miji na kutumia vyanzo vya ndani vya mapato kama vile tozo na ushuru katika matumizi ya barabara ya mafuta leseni na usajili wa magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa miradi ya barabara kwa gharama za *Road Fund* katika maeneo sita ya Mkoa wa Tanga, Morogoro na Iringa. Miradi katika mikoa hiyo ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 12.4 kupitia akaunti maalum ya Bodi ya Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukarabati na uendelezaji wa hospitali za mikoa; mradi huu umekuwa ukilenga kukarabati na kuendeleza majengo ya hospitali za mikoa ili kuziwezesha hospitali hizo kutoa huduma ya rufaa katika mikoa hiyo. Katika mikoa ya Tanga na Mbeya ambayo Kamati ilitembelea ilibaini kwamba mradi huu ultengewa shilingi bilioni 1.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mfuko wa Uendelezaji wa Vijana na Wanawake kamati ilitembelea kwa lengo la kukagua utekelezaji wa mfuko wa maendeleo ya vijana wanawake ambao walitokana na *Local Government Own Source Projects*. Mradi huu ultengewa jumla ya shilingi milioni 460.6; mradi unalenga kusaidia vikundi vya wanawake na vijana kupitia Halmashauri kwa kutenga asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya mfuko wa maendeleo ya vijana na wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukamilisha ukaguzi wa miradi ya maendeleo Kamati ilijiekeleza katika uchambuzi wa bajeti ya ofisi ya Rais.

Kuhusu maduhuli uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa wafungwa 56 ofisi ya Rais, TAMISEMI haukuwa wakuridhisha kwani hadi kufikia mwezi Februari 2017 ni shilingi bilioni 4.8 tu kati ya bilioni 16.9 zilizokadiliwa ndio zilikuwa zimekusanya; kiwango hiki kikiwa na asilimia 24 ya malengo liliokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha katoka Hazina katika uchambuzi Kamati ilibaini kwamba mtiririko kutoka hazina haukuwa mzuri kutokana na kukosa ulinganifu kati ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa mwaka huo na kiasi kilichotolewa na hazina.

Kwa mfano, hadi kufikia mwezi Februari, 2017 kiasi cha fedha kilichotolewa kwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Taasisi zake kwa ajili ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo kilikuwa ni shilingi bilioni 202.2 kati ya shilingi bilioni 354 zilizoidhinishwa. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 57 ya fedha yote iliyo idhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maoni ya Kamati, uchambuzi ulibaini kwamba Ofisi ya Rais, TAMISEMI ilizingatia maoni ya Kamati kwa kiwango cha kuridhisha kutokana na kutekeleza kwa kikamilifu baadhi ya maoni na kuendelea na utekelezaji wa maoni mengine, kati ya 15 yaliyotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018; ili kutekeleza malengo yaliyopangwa kwa mwaka huo wa fedha, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa na Halmashauri, ziliomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi trillioni 6.6. Kati ya fedha hizo, shilingi trillioni 4.5 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi trillioni 1.8 kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kwa kwa upande wa Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Kamati ilifanya uchambuzi wa mafungu husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa fedha kutoka Hazina; uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ulibaini kwamba, hakuna ulinganifu kati ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge lako tukufu kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na kiasi kilichotolewa. Kamati ilibaini kwamba fedha zilizoidhinishwa zilikuwa zinatolewa kidogo kuliko ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio ya mapato kwa mwaka wa fedha 2017/2018; ili kutekeleza malengo yake, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, illomba kuidhinishwa shilingi billioni 821.32; kati ya fedha hizo shilingi billioni 430.35 zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi billioni 390.97 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji, uamuzi wa Serikali kutekeleza mpango wa kuhamia Dodoma ambao ulikuwepo kwa miaka mingi ultolewa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, tarehe 25 Julai, 2016. Utekelezaji wake ambao umegawanyika katika awamu nne, ulianza kutekelezwa Januari, 2017 na uko katika awamu ya tatu hadi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mpango wa usambazaji maji safi na salama vijiji unaotekeliza chini Ofisi ya Rais, TAMISEMI unalenga kuboresha huduma ya maji safi na salama vijiji na kuboresha mazingira. Malengo ya mpango huu ni kuboresha huduma ya upatikanaji wa maji safi na salama kwa asilimia 85 kwa maeneo ya vijiji na asilimia 90 kwa maeneo ya mijini ifikapo mwaka 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa mipango miji katika Halmashauri za miji nchini. Katika kipindi cha mwaka

wa 2016/2017, Ofisi ya Rais, TAMISEMI iliweza kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali pamoja na uandaaji wa mipango ya jumla ya uendeshaji ambayo inahusu uandaaji wa mipango kabambe na mipango ya matumizi ya ardhi ya muda wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha kuna usimamizi wa utekelezaji wa mpango wa anwani za makazi na *post code* katika mwaka wa fedha 2016/2017 Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ilizindua miongozo ya mpango wa anwani za makazi na *post code* pamoja na sheria ndogo za mfano za kusimamia utekelezaji wa mpango huo. Mpango huu utahusisha maeneo yaliyopangwa na yasiyopangwa isipokuwa maeneo hatarishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi la kuondoa watumishi hewa na uhakiki wa vyeti katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, za wilaya, vituo vya afya na zahanati za umma. Ili kuhakikisha Watumishi walioajiriwa wana sifa stahiki za kuwa katika utumishi wa umma, Serikali ya Awamu ya Tano iliamua kufanya uhakiki mkubwa ambao ulianza na hatua ya kubainisha mishahara hewa, kuondoa watumishi waliokuwa na vyeti vya kughushi kujipatia ajira na walioajiriwa kwa vyeti vya darasa la saba baada ya mwaka 2004 ambao hawakuijendeze na kupata elimu ya kidato cha nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhakiki huo umeathiri sekta mbalimbali kutokana na kupoteza watumishi wengi kwa kuondolewa kazini. Mionganoni mwa sekta hizo ni afya kwenye Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri mbalimbali. Sekta hiyo ilipoteza jumla ya watumishi 3310 wa kada mbalimbali za afya kutokana na uhakiki wa vyeti hewa, na hivyo kuongeza upungufu kutoka asilimia 51 iliyokuwepo kabla ya uhakiki hadi asilimia 54.4 mara baada ya uhakiki. Upungufu huo wa wataalam katika sekta hiyo ulifikia watumishi 57,788.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa, chombo kilianzishwa mwaka 1986 chini ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, ili kutekeleza mionganoni

mwa mambo mengine, jukumu la kutoa mikopo kwa Halmashauri nchini ili kuziwezesha kutekeleza miradi ya maendeleo na shughuli za kiuchumi kwa lengo la kuongeza mapato ya Halmashauri. Hadi tarehe 30 Juni, 2017 Bodi ilikuwa imefanikiwa kutoa jumla ya mikopo 68 yenye thamani ya shilingi bilioni 9.7 tu kwa Halmashauri 54 katи ya Halmashauri 185 kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Barabara za Viijjini na Mijini (*TARURA*) itasaidia kukabiliana na changamoto zinazokabili miundombinu ya barabara katika maeneo ya vijiji ni na mijini. Pamoja na kwamba Wakala hii itaendesha shughuli zake kwa kuzingatia sheria, lakini pia itakuwa inazingatia biashara, hata hivyo, itazingatia ufanisi wa ghamama na masuala mengine mtambuka ya kijamii kwa ajili ya maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wakala huu unatakiwa kisheria kupokea fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina, Kamati inashauri fedha hizo zipelekwe kwa wakati ili kutoathiri miradi ya wakala huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miradi ya sekta ya afya katika mwaka wa fedha 2017/2018 (ujenzi wa hospitali za mikoa na wilaya na upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi); Halmashauri 64 nchini hazina hospitali za wilaya, jambo ambalo linawanyima wananchi wa halmashauri hizo fursa za kupata huduma za afya za hospitali za Wilaya na hivyo kulazimika kwenda Wilaya jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya walimu na miundombinu ya kielimu, sekta ya elimu ya msingi na sekondari ndiko watoto wa nchi hii wanapopata msingi wa elimu na kujengewa uwezo wa kuendelea na taaluma nyingine. Sekta hiyo imekuwa ikikabiliwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na upungufu wa walimu na miundombinu ya kielimu, kama vile vyumba vya madarasa, nyumba za walimu na matundu ya vyoo. Kwa mantiki hiyo, ni lazima jamii itambue kwamba hatua ya Serikali kuongeza uwekezaji katika elimu, kutekeleza mipango wa elimu msingi

bure na kufanya ukarabati wa shule kongwe za sekondari za Serikali nchini ni jambo lenye ghamama kubwa sana.

Hata hivyo, tutakubaliana wote kwamba manufaa yatokanayo na elimu ni sawa na tunda tamu kutoka katika mti wenye mizizi michungu. Tukubali kama Taifa kukabili upungufu wa matundu ya vyoo ambaao unatutia aibu, upungufu wa vyumba vya madarasa, nyumba za walimu na hata upungufu wa walimu wenyewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua na kupongeza hatua ya Serikali kutoa fedha kiasi cha shilingi milioni 750 ikiwa ni sehemu ya mchango wake wa shilingi bilioni tatu zilizoidhinishwa katika Bajeti ya mwaka 2017/2018. Hii ni ishara nzuri na ambayo itawapa moyo wafadhili wengine katika *TASAF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufanikisha utekelezaji wa shughuli za urasimishaji nchini, MKURABITA inazijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa Tanzania bara na visiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mapendekezo, mpango wa usambazaji maji safi na salama vijijini, Kamati inashauri Bunge iitake Serikali kuhakikisha fedha zinazopangwa kwa ajili ya utekelezaji wa mpango huu ipatikane kikamilifu na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa mipango miji katika mijini, Kamati inashauri Bunge iitake Serikali izipatie halmashauri wataalam wa ardhi na fedha za kutosha ili iweze kutekeleza kikamilifu mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu zoezi la kuondoa Watumishi hewa, Kamati inalishauri Bunge iitake Serikali kukabiliana na upungufu huo kwa kujirisha watumishi wa afya wa kada mbalimbali katika hospitali za rufaa za mikoa, wilaya na vituo vingine vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuipatia *TARURA* ofisi na watumishi wa

kutosha. Mgao wa fedha kutoka Bodi ya Mfuko wa Barabara (*Road Fund*) Kamati inaishauri Serikali kuharakisha mchakato wa kupitia kanuni (*formula*) ya mgao wa fedha za bodi ya Mfuko wa Barabara ili kuongeza mgao wa *TARURA* kutoka asilimia 30 na kupanda kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali isimamie kikamilifu Halmashauri ziweze kutoa michango yake katika mfuko huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya miundombinu na sekta ya elimu, Kamati inaishauri Bunge Llitake Serikali kuongeza bajeti kwa ajili ya kujenga miundombinu hiyo ya kielimu ii kuondoa changamoto iliyopo katika kuruhusu utoaji wa elimu bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali za wilaya, Kamati inaishauri liitake Serikali kujenga hospitali katika wilaya 64 ambazo hazina hospitali za wilaya.

Mheshimiwa MWenyekiti, watendaji wa Serikali kukaimu muda mrefu, Kamati inaishauri Bunge kuitaka Serikali ama kuwathibitisha watumishi ambao wamekaimu muda mrefu ama kuwaondoa wale ambao hawana uwezo na kuajiri wale wenye uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *TASAF*, upungufu wa fedha kwa baadhi ya maeneo kutofikiwa. Kamati inalishauri Bunge kutoka Serikali itoe fedha za kutosha na kuhakikisha mpango huu wa kunusuru kaya maskini unafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watendaji wa halmashauri kusaidia kaya maskini, Kamati inashauri Serikali kupitia Maafisa Mipango na Maafisa Maendeleo ya Jamii katika halmashauri nchini kuwasaidia wananchi kutumia hela za *TASAF* vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Kujitegemea wa Rais (*PTF*), Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kutenga

bajeti ya kutosha kwa mfuko wa kujitegemea ili kuuwezesha kuongeza kiwango cha ufanisi cha mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa kurasimisha wa MKURABITA, Kamati inashauri Bunge kuitaka Serikali kuongeza bajeti ya MKURABITA ili kufanikisha malengo yалиyowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, nitoe shukrani za dhati kabisa kwa Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri. Vilevile niwashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Rais. (*Makoff*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano wallonipatia katika kipindi chote cha uhai wa Kamati hii. Weledi na ushirikiano wao umenisaidia sana katika kutimiza majukumu yetu kwa ufanisi mkubwa shughuli zake katika kipindi chote cha uhai wake. Kwa heshima kubwa naomba majina yao na makatibu wao yaingine kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge (*Hansard*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna pekee nimshukuru sana Katibu wa Bunge ndugu Stephen Kagaigai kwa ushirikiano wake aliouzezesha Kamati kutekeleza majukumu yake. Vilevile nimshukuru ndugu Athumani Hussein, Mkurugenzi na wasaidizi wake wote kwa kusimamia na kusaidia shughuli za Kamati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza hayo kwa kina shughuli zilizoletwa na Kamati, uchambuzi na matokeo ya utekelezaji wa shughuli hizo, maoni na mapendekezo ya Kamati, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu sasa liipokee na kuikubali taarifa hii ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo katika taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**TAARIFA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE
YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA KWA KIPINDI CHA
JANUARI 2017 HADI 2018**

*[Inatolewa Chini ya Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za
Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016]*

SEHEMU YA KWANZA

MAELEZO YA JUMLA

1.0 Utangulizi

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu,Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kwa kipindi cha kuanzia Januari,2017 hadi Januari,2018.

Taarifa hii inalenga kuelezea shughuli zilizotekelozwa na Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa kwa kipindi cha mwaka mmoja na jinsi ilivyoweza kuisimamia na kuishauri Serikali katika utekelezaji wa majukumu yake.

1.1 Majukumu

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 6(4) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, inasimamia shughuli za Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Aidha, Kanuni ya 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, inaanisha majukumu ya Kamati hii kuwa ni:-

- a) Kushughulikia Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora, na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;
- b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Ofisi ya Rais;

c) Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila mwaka za Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na TAMISEMI ;na

d) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais.

1.2 Njia zilizotumika kutekeleza Majukumu

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake Kamati ilitumia njia mbalimbali kama ifuatavyo:-

a) Vikao na Wizara, Taasisi na Idara zilizo chini ya Ofisi ya Rais ili kufahamu muundo,majukumu na shughuli zinazotekelzwa;

b) Uchambuzi wa Taarifa mbalimbali za kiutendaji kutoka Ofisi ya Rais;

c) Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016; na

d) Mafunzo na Semina za kuwajengea uwezo (*capacity building*) Wajumbe wa Kamati.

Mantiki ya kutumia mbinu hizo tofauti ni kuhakikisha kwamba, Wajumbe wa Kamati wanajielimisha vya kutosha kuhusiana na nyanja mbalimbali ambazo wanapaswa kuisimamia na kuishauri Serikali.

1.3 Shughuli zilizotekelzwa na Kamati

Mheshimiwa Spika, ili kukidhi matakwa ya Kanuni ya 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, katika kipindi cha Januari, 2017 hadi Januari, 2018 Kamati ilipanga na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

1.3.1 Ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo 2016 /2017

Mheshimiwa Spika, ili kuzingatia Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari ,2016 Kamati ilifanya ziara za ukaguzi katika Miradi ya Maendeleo inayotekelzwa

na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Miradi iliyotembelewa ni ambayo ilitengewa fedha katika mwaka wa fedha 2016/2017 na inatekelezwa katika mikoa ya Tanga, Morogoro, Njombe, Iringa na Mbeya kama ifuatavyo:-

i) **Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**

- Mpango wa Miji Mkakati Tanzania (Tanzania Strategic Cities Project – TSCP);
- Bodi ya Mfuko wa Barabara (Road Fund Board);
- Mfuko wa Maendeleo wa Vijana na Wanawake (Asilimia 10 ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri); na
- Ukarabati na Uendelezaji wa Hospitali za Mikoa.

ii) **Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora**

- Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF);
- Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA);
- Mfuko wa Rais wa Kujitengemea (PTF); na
- Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC).

1.3.2 Kuchambua Taarifa kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitekeleza jukumu hili kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2), ambapo ilichambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais; Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Uchambuzi huo ulikuwa na lengo la kuiwezesha Kamati kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

1.3.3 Kupokea na kujadili Taarifa za Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais,

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Januari, 2017 hadi Januari 2018 Kamati ilipokea na kujadili Taarifa mbalimbali za utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais. Lengo la kujadili taarifa hizo za utekelezaji ni kuzingatia jukumu la kikanuni la kuisimamia na kuishauri Serikali ambalo msingi wake ni Ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Tanzania ya Mwaka, 1977. Kutokana na kujadili taarifa hizo masuala mbalimbali yalibainika na ufanuzi wake unapatikana katika sehemu ya pili ya Taarifa hii.

1.3.4 Kushiriki katika Semina za Ndani

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Kamati walipata fursa ya kushiriki katika Semina mbalimbali zilizoandalowi na Ofisi ya Bunge (Legislative Support Programme), Wizara na Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais (TARURA), na Taasisi binafsi ya MVIWATA.

Semina hizo zililenga kuwaongeza ujuzi Wajumbe katika maeneo mbalimbali pamoja na kuwakumbushia kuhusu majukumu na wajibu wa Kibunge katika kuisimamia na kuishauri Serikali.

1.3.5 Ziara za Ukaguzi wa shughuli za Ofisi ya Rais

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea na kukagua shughuli mbalimbali zinazotekelvezwa na Ofisi ya Rais, kuititia Taasisi na Idara zake. Ziara hizi zilitoa fursa kwa Wajumbe kujiridhisha kuhusiana na utekelezaji ikilinganishwa na Taatifa za utekelezaji ambazo ziliwasilishwa na Serikali mbele ya Kamati.

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

2.1 Maelezo ya Jumla;

Mheshimiwa Spika, sehemu hii ya Taarifa inaelezea kwa ufasaha, majukumu yaliyotekelvezwa na Kamati kwa kipindi chote cha mwaka mmoja. Uchambuzi wa kina wa matokeo ya shughuli hizo umefanyika, ukianisha Wizara, Taasisi au Idara

iliyohusika na kuonesha changamoto na mafanikio. Aidha, ili kufafanua zaidi na kuongeza uelewa katika baadhi ya maeneo ya uchambuzi wa matokeo, sehemu hii itatumia takwimu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Januari, 2017 hadi Januari, 2018 Kamati ilikutana na kutembelea Ofisi ya Rais kama ifuatavyo:-

2.1.1 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora;

- a) Tume ya Utumishi wa Umma;
- b) Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa(TAKUKURU);
- c) Mpango wa Kurasimisha Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA);
- d) Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF);
- e) Wakala wa Serikali Mtandao,(eGA);
- f) Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC);
- g) Mfuko wa Kujitegemea wa Rais (PTF); na
- h) Wakala wa Mafunzo kwa njia ya Mtandao (TaGLA).

2.1.2 Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI)

- a) Tume ya Utumishi wa Waalimu (TSC);
- b) Wakala wa Mabasi yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART);
- c) Mikoa Ishirini na Sita (26) ya Tanzania Bara;
- d) Wakala wa Barabara Mijini na Vijiji (TARURA);
- e) Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB);
- f) Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa; na
- g) Mfuko wa Pensheni wa LAPF.

Mheshimiwa Spika, masuala ambayo yatachambuliwa katika sehemu kuhusu Wizara/Taasisi/I dara zilizoanishwa hapo juu yamegawanyika katika maeneo yafuatayo:-

- a) Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo;
- b) Uchambuzi wa Bajeti;
- c) Taarifa za Utekelezaji; na
- d) Ziara za ukaguzi wa shughuli za kiutendaji.

2.2 Matokeo ya Uchambuzi wa Kamati

2.2.1 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa miradi ya maendeleo ni sehemu ya majukumu ya Kamati kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Kamati ilitembelea na kukagua miradi iliyotengewa na kuidhinishiwa fedha katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 ambayo inatekelezwa na Ofisi ya Rais, katika mikoa ya Dodoma, Tanga, Morogoro, Iringa, Njombe na Mbeya.

Mantiki ya ukaguzi huo ni kuwawezesha Wajumbe wa Kamati kujiridhisha iwapo utekelezaji wa miradi hiyo unaendana na thamani halisi ya fedha “**value for money**” iliyotolewa. Hali halisi ya utekelezaji wa miradi, itawafanya Wajumbe wa Kamati kuwa na uelewa wa kutosha na hivyo kuweza kuishauri vyema Serikali katika Bajeti ya Mwaka unaofuata. Ifuatayo ni baadhi ya miradi iliyotembelewa na Kamati:-

(a) Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) Dodoma, Morogoro, Tanga, Njombe na Mbeya

Mheshimiwa Spika, MKURABITA unatekelezwa chini ya Kifungu 1003 “Policy and Planning” cha Fungu 30 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri. Mpango huu unaandaa na kusimamia Mfuko wa Kitifa wa Umiliki wa Raslimali na Uendeshaji wa Biashara unaotambulika na kukubalika kisheria nchini, na hivyo kuwawezesha Wanyonge kurasimisha mali zao (ardhi na biashara) ili ziwawezeshe kujkwamua kiuchumi.

Aidha, mpango huu umekuwa ukihamasisha na kuchangia ujenzi wa Masijala za Ardhi katika Vijiji/Mitaa, ili kuweshera uhifadhi madhubuti na salama wa Nyaraka (Hati za Hakimiliki za Kimila na Nyaraka nyingine).

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea jumla ya maeneo Kumi na Moja (11) katika Mikoa ya Dodoma, Morogoro, Tanga, Njombe na Mbeya kwa lengo la kujiridhisha kuhusu hali ya utekelezaji wa mpango huu.

Baadhi ya maeneo hayo ni Mitaa ya Tuelewane na Kihonda 'B' katika Mkoa wa Morogoro, ambapo MKURABITA imewezesha kupimwa kwa jumla ya viwanja 822 na ramani zake kuidhinishwa na Mkurugenzi wa Upimaji wa Ramani wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Hadi wakati huo jumla ya Hatimiliki 132 (sawa na asilimia 16) zilikuwa zimetolewa kwa Wananchi na nyingine zilikuwa zinaendelea kuandaliwa.

Vilevile, katika Mkoa wa Njombe, mpango huu umewezesha kupimwa kwa jumla ya viwanja 1,635 na Hati 730 (sawa na asilimia 45) zimeandalila na kukabidhiwa kwa Wananchi wa Vijiji vya Joshoni, Melinze, Mpechi, Nazareti, Idundilaga na Mtaa wa Kambarage.

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Pwaga kilichopo Wilaya ya Mpwapwa, Mkoani Dodoma, kimefanikiwa kwa kiwango kikubwa kutokana na urasimishaji wa ardhi uliotekelizwa na MKURABITA. Katika kijiji hicho jumla ya mashamba 1,277 yamepimwa na Hati 1,031 (sawa na asilimia 81) zimeandalila na kukabidhiwa kwa Wananchi. Aidha, mpango huo umegharamia ujenzi wa Masijala ya Ardhi katika kijiji hicho kwa kutoa Shilingi Milioni 32.

Katika maeneo ambayo Kamati ilifanikiwa kukagua utekelezaji wa MKURABITA, ilibaini kwamba, baadhi ya Wananchi wake wameweza kutumia urasimishwaji wa maeneo na biashara kujikwamua kiuchumi. Wananchi hao wametumia Hati za Hakimiliki za Kimila kama dhamana katika Benki na Taasisi za Fedha na hivyo kupata mikopo. Mfano; wanufaika wanne (4) katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, wamefanikiwa kukopa kati ya Shilingi Milioni 50 hadi 500 kwa kutumia hati hizo.

Vilevile, utaratibu huo umesaidia kuepusha migogoro ya ardhi, kwani unawezesha mpango mzuri wa matumizi ya ardhi na kutoa fursa kwa Wanawake kumilikishwa ardhi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inawezesha mpango huu kutekelezwa nchi nzima kwani

unaweza kusaidia kuondoa migogoro ya ardhi nchini, pamoja na kuwainua Wananchi kiuchumi kwa haraka kutokana na kutumia Hati za Hakimiliki za Kimila kama dhamana katika Benki na Taasisi za Fedha. Aidha, Serikali ifanyie kazi changamoto ya baadhi ya Benki na Taasisi za fedha kukataa kupokea Hati za Hakimiliki za Kimila kama dhamana ya mikopo.

b) Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF)

Mheshimwa Spika, Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF) unatekelezwa chini ya Kifungu 1003 *"Policy and Planning"*, Fungu 30 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri. Majukumu ya msingi ya mfuko huu ni kutoa mikopo, ushauri na mafunzo ya kibiashara kwa Wajasiriamali wadogo na wa kati nchini.

Kamati ilikagua utekelezaji wa mfuko huu kwa kutembelea Vikundi Sita (6) katika Mikoa ya Njombe na Morogoro, ambavyo vinajishughulisha na ufundi wa magari na uchomeleaji vyuma (welding), ukamuaji wa mafuta, ufugaji, ususi na ufumaji, uzoaji taka na uokaji wa mikate. Kwa ujumla Vikundi hivyo ambavyo vinaundwa na wanachama wasiopungua watano (5) kila kimoja, vimepewa jumla ya **Shilingi 32,400,000/=**

Wastani wa mkopo kwa kikundi ulianzia **shilingi 2,400,000/=** hadi **10,000,000/=** na fedha hizo zilitakiwa kurejeshwa ndani ya kipindi cha miezi sita.

Mheshimwa Spika, mfuko huu umekuwa ni mkombozi kwa baadhi ya Vijana na Wanawake kwani umewawezesha kupata mitaji na kujajiri. Mfano mzuri ni kikundi cha Mwale Cleaners, ambacho ni kati ya vikundi sita viliviyotembelewa na Kamati. Kikundi hicho kilichopo mkoani Morogoro, kinaundwa na vijana Sita (6) ambao ni wahitimu wa chuo kikuu walioamua kutosubiria ajira za maofisini wakaamua kuijingiza katika ujasiriamali.

Kikundi hicho kilianza kwa kuchukua mkopo wa **shilingi milioni 2.5**, na sasa kimefikia hatua ya kukopeshwa **shilingi milioni 10**.

Aidha, Mfuko huu umekuwa msaada kwa watu wa makundi maalum kama vile walemovu, na wanaoishi na VVU kwa kuwapatia mikopo ili waweze kuendesha shughuli za kiuchumi kwa lengo la kujikwamua kiuchumi. Mfano watu 16 kutoka makundi ya walemovu na wanaoishi na VVU wamekopeshwa jumla ya shilingi Milioni Saba (7) Mkoani Morogoro.

Mheshimiwa Spika, malengo ya mfuko huu ni mazuri sana, hata hivyo utekelezaji wake umeshindwa kuwafikia vijana na wanawake katika maeneo mengi nchini kutohana na uwezo mdogo wa kifedha. Ni maoni ya Kamati kwamba, Serikali longeze bajeti ya mfuko huu illi uweze kuendana na hadhi ya Ofisi ya Rais, pamoja na kuongeza wigo wa shughuli zake nchini na hivyo kutoa fursa ya mikopo kwa Vijana na Wanawake wengi ambao hawana mitaji ya kuwawezesha kujikwamua kiuchumi.

c) Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)

Mheshimiwa Spika, mradi huu ambao unatekelezwa chini ya kifungu 1003 cha Fungu 30 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, unalenga kuzisaidia kaya maskini nchini kukuza uchumi na kupunguza umasikini wa kipato; kuinua ubora wa maisha na ustawi wa jamii, pamoja na kuhamasisha utawala bora na uwajibikaji.

Utekelezaji wa mradi huu uko katika awamu ya tatu ambayo imejikita katika kuzisaidia Kaya maskini kwa kuzipatia ruzuku ya fedha ili ziweze kuboresha maisha kwa kupata chakula, kuwezesha Watoto kuhudhuria shulenii pamoja na kliniki kwa wale walio chini ya umri wa miaka mitano.

Taarifa ya utekelezaji inaonesha kuwa, hadi sasa takribani Watanzania **milioni 5.9** wamendikishwa ili kunufaika na utaratibu huu, na kumekuwa na mafanikio makubwa ya watoto wanaotoka kaya maskini kuhudhuria shulenii na kliniki.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo Sita ambayo Kamati ilitembelea kwenye Mikoa ya Morogoro, Tanga, Mbeya, Njombe na Iringa, ilibainika jkwamba, jumla ya kaya 753 zimenufaika katika awamu za malipo kumi na moja (11) kwa kupokea jumla ya **shilingi milioni 216.8**

Aidha, ili kuhakikisha Kaya zisizo na sifa hazinufaiki na mpango huu, katika maeneo hayo yaliyotembelewa na Kamati, ilibainika kuwa jumla ya kaya 71 ziliondolewa katika utaratibu huo kutokana na kubainika kukosa sifa. Idadi hiyo ni sawa na asilimia 9.4 ya kaya zinazonufaika na mpango wa ruzuku katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo yaliyotembelewa, Kata ya Isakalilo iliyopo, Halmashauri ya Wilaya ya Iringa ilibainika kuwa na idadi kubwa kwa upande wa Kaya zinazonufaika na utaratibu huu, pamoja na Kaya zilizoondolewa katika utaratibu huu kwa kukosa sifa. Kata hiyo ilikuwa na jumla ya Kaya 236 zinazonufaika na utaratibu huu ambazo ni sawa na asilimia 31.3 ya Kaya zinazonufaika katika maeneo yote yaliyotembelewa na Kamati.

Aidha, Kata hiyo ilibainika kuwa na jumla ya Kaya 55 zilizoondolewa katika utaratibu huu, idadi ambayo ni sawa na asilimia 77.4 ya kaya zote zilizoondolewa kwa kukosa sifa.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa ruzuku kwa Kaya maskini umekuwa na mafanikio makubwa kutokana na kuwawezesha walengwa kuboresha maisha kwa kumudu kupata angalau milo miwili kwa siku, na kuwzesha watoto kuhudhuria shulen na kliniki. Vilevile, baadhi ya wanufaika wametumia sehemu ya ruzuku kuanzisha miradi ya kiuchumi kama vile, kilimo, ufugaji na biashara na hivyo kujiongezea uwezo wa kipato.

Aidha, Kamati inatambua kwamba, utoaji wa fedha za ruzuku kwa Kaya maskini umekuwa ukiambatana na kuelimisha Wanufaika juu ya umuhimu wa kuijunga na Mfuko wa Hifadhi wa Jamii (CHF). Hata hivyo, mwitikio wa wanufaika hao umekuwa ni mdogo kutokana na madai kwamba, wale waliojiunga na CHF hawapati huduma nzuri

ya afya. Ni maoni ya Kamati kwamba, Serikali iangalie namna ya kuboresha huduma za afya kwa watu wenyе bima ya CHF ili kuvutia wananchi wengi wa maeneo ya vijijini kujunga na utaratibu huo.

d) Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC)

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC) kilianzishwa kwa lengo la kutoa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu katika fani za uongozi, menejimenti na utawala, kutoa ushauri wa kitaalam, kufanya utafiti na kutoa machapisho ya kitaalam katika utumishi wa umma.

Chuo hiki ambacho ni nguzo muhimu ya mafunzo ya kiutumishi kwa Watumishi wa Umma, hasa kwa kuzingatia kwamba, hakuna Taasisi nyingine inayotoa mafunzo ya aina hiyo, kina jumla ya Kampasi Sita (6), katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea kwa lengo la kukagua utekelezaji wa shughuli za chuo hiki katika Kampasi mbili zilizopo Mbeya na Tanga, na kubaini kwamba, licha ya kuwa na majukumu ya kutoa mafunzo ya kiutumishi, kimekuwa kimbilio kwa wananchi wengi amba si watumishi hasa vijana wanaojiunga kwa kozi za muda mfupi na muda mrefu.

Vilevile, Kamati ilibaini kwamba chuo kinatumia fedha nyingi kwa ajili ya kukodisha majengo kwani hakina majengo yake katika kampasi hizo. Mfano, majengo ya Kampasi ya Mbeya yamekodiwa kutoka Halmashauri ya Jiji la Mbeya kwa gharama ya Shillingi Milioni 22 kwa Mwezi, sawa na Shillingi Milioni 264 kwa mwaka. Kiasi hicho cha fedha ni kikubwa sana na kingeweza kutekeleza majukumu mengine, iwapo chuo kingekuwa na majengo yake. Aidha, bado chuo kinatumia Wakufunzi wa Mkataba, jambo ambalo linakiingiza katika gharama zaidi.

Mheshimiwa Spika, ni mtazamo wa Kamati kwamba, kwa kuwa hii ndiyo taasisi pekee ambayo Serikali inaitegemea kwa ajili ya kutoa mafunzo ya kiutumishi kwa Watumishi wa

Serikali na wa maeneo mengine, ni vyema Serikali ikakiwezesha chuo hiki kupata majengo yake na kupata kibali cha kuajiri Watumishi kwa masharti ya kudumu ili kiweze kutimiza malengo yake kwa ufanisi zaidi.

e) **Mradi wa Tanzania Strategic Cities Project (TSCP)**

Mheshimiwa Spika, mradi huu unatekeleza kuititia Kifungu 8071 cha Mafungu ya Bajeti katika mikoa Saba nchini ambayo ni Arusha, Mwanza, Mbeya, Tanga, Dodoma, Mtwara Mikindani, na Kigoma (Ujiji). Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa mradi huu katika maeneo Sita (6) kwenye Halmashauri za Majiji ya Tanga na Mbeya, ambayo kwa ujumla wake yalitengewa ya Shilingi **8,042,405,000**.

Utekelezaji wa mradi huo katika maeneo hayo ulikuwa umefikia asilimia 55 na ullilenga kuboresha miundombinu ya barabara kwa kujenga kwa kiwango cha lami ngumu, kuweka taa za barabarani, kujenga vituo vya mabasi na mifereji ya majitaka. Hatua ya ujenzi iliyosalia inahusisha ujenzi wa maabara ya kupimia malighafi na vifaa vya ujenzi katika Jiji la Tanga na Dampo la kisasa la kukusanya taka ngumu katika Jiji la Mbeya.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huu umekuwa na manufaa makubwa sana kwa maeneo husika, kwani umeboresha miundombinu ya barabara; umeongeza thamani ya viwanja na majengo yaliyo jirani na miradi ya TSCP; umepunguza kero ya usafiri na msongamano kwa wananchi kutokana na vituo vya mabasi vilivyojengwa, pamoja na kutoa fursa za biashara kwa wananchi wa maeneo yaliyo kando na miradi ya TSCP.

Mheshimiwa Spika, ziara ya Kamati katika maeneo hayo ilibaini kwamba, licha ya mafanikio yaliyopatikana zipo changamoto kadhaa ambazo zisipodhibitiwa manufaa yaliyotarajiwa kutokana na mradi huu yanaweza yasifikasiwe kikamilifu. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na kukosekana kwa mifereji ya kuondoa maji ya mvua kwenye barabara zilizojengwa na mradi, jambo linalosababisha maji kuntuama kwa muda mrefu na hivyo kuharibu barabara.

Aidha, baadhi ya madereva wamekuwa wakipitisha magari yenyе uzito zaidi ya unaotakiwa kwenye barabara zilizojengwa. Mfano; ni barabara za Kabwe – Block T, Kisanji na Sae – Ituha za Jijini Mbeya ambazo zimejengwa kwa ajili ya magari yasiyozidi uzito wa Tani 10. Hata hivyo, baadhi ya madereva wamekuwa wakipitisha magari yenyе uzito zaidi ya huo.

f) **Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB)**

Mhesimiwa Spika, Bodi hii ilianzishwa mwaka 1992 kwa lengo la kukarabati, kuboresha na kutengeneza barabara muhimu za mikoa, wilaya na miji kwa kutumia vyanzo vya ndani vya mapato kama vile tozo na ushuru katika matumizi ya barabara na mafuta, leseni na usajili wa magari.

Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa miradi ya barabara kwa gharama ya RFB katika maeneo Sita (6) ya mikoa ya Tanga, Morogoro na Iringa. Miradi ya katika mikoa hiyo ilitengewa jumla ya **shilingi 12,395,296,399** kuititia Akaunti maalum ya Bodi ya Mfuko wa Barabara katika mikoa hiyo.

Kamati ilibaini kuwa, RFB imechangia kuongezeka kwa mtandao wa barabara za lami na changarawe katika mikoa husika. Mfano, katika Jiji la Tanga, Bodi ya Mfuko wa Barabara imetengeneza kilomita tisa (9) za barabara kwa kiwango cha changarawe. Aidha, katika mkoa wa Iringa, madaraja 11 yamejengwa katika mwaka wa fedha 2016/17 pekee kwa lengo la kuhakikisha barabara za maeneo korofii zinapitika katika muda wote wa mwaka

Mhesimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo Kamati imebaini baadhi ya changamoto zikiwemo ucheleweshaji kwa fedha za RFB katika baadhi ya miradi iliyokusudiwa, urasimu wa kuhamisha miundombinu ya majisafi na majitaka, na nguzo za umeme, na uchache wa mitambo ya kutengenezea barabara katika halmashauri nydingi.

Changamoto hizo zimekuwa zikichangia kukwamisha utekelezaji wa miradi ya ya Bodi ya Mfuko wa Barabara, hivyo ni vyema Serikali ikaangalia namna bora ya kuzitatua ili

miradi iliyokusudiwa iweze kutekelezwa kikamilifu na kwa wakati.

g) Ukarabati na Uendelezaji wa Hospitali za Mikoa (Regional Hospitals Rehabilitation)

Mheshimiwa Spika, mradi huu umekuwa ukilenga kukarabati na kuendeleza majengo ya Hospitali za Mikoa ili kuziwezesha hospitali hizo kutoa huduma ya rufaa katika mikoa hiyo. Katika mikoa ya Tanga na Mbeya, ambayo Kamati ilitembelea mradi huu ilitengewa **shilingi 1, 342, 700, 000/=** chini ya kifungu cha 3001 cha mafungu ya mikoa hiyo. Katika ukaguzi huo Kamati ilibaini kuwa mradi huo umeweza kwa gari la wagonjwa na kujengwa kwa maeneo muhimu kama vile **Sadaruki** (ICU) na jengo la grade one katika Hospitali ya Mkoa wa Tanga; na nija za kupitia wagonjwa (walk ways) zenyet urefu wa mita 429 katika Hospitali ya Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Spika, ni jambo lililo wazi kuwa pamoja na jitihada za Serikali za kuboresha huduma katika hospitali hizi za mikoa bado kuna changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na bajeti finyu na isiyopatikana kikamilifu, msongamano mkubwa wa wagonjwa, ukosefu wa majengo muhimu kama vile jengo la huduma ya dharura (*casualties*) na upasauji (theatre) katika Hospitali ya Mkoa wa Mbeya. Aidha, hospitali hizo zote zinakabiliwa na ukosefu wa vifaa kama Ct Scan, Echo na vitendanishi vya maabara na bajeti finyu kwa ajili ya dawa.

h) Mfuko wa Maendeleo kwa Vijana na Wanawake

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea kwa lengo la kukagua utekelezaji wa Mfuko wa Maendeleo kwa Vijana na Wanawake ambao unatokana na Local Government Own Source Projects. Utekelezaji wa mradi huu ilitengewa jumla ya **shilingi 460,589,216** kupitia na Fungu 78:-Mkoa wa Mbeya; Fungu 54: Mkoa wa Njombe na Fungu 86: Mkoa wa Tanga. Mradi unalenga kusaidia Vikundi vya Wanawake na Vijana kupitia Halmashauri kwa kutenga asilimia kumi (10%) ya mapato ya ndani ya Halmashauri, kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo wa Vijana na Wanawake.

Kwa upande wa mradi huu, katika maeneo matano (5) ambayo Kamati iliyatembelea kwenye Mikoa ya Tanga, Mbeya na Njombe, mambo kadhaa yalibainika yakijumuisha mafanikio na changamoto

a) **Mafanikio**

- i. Baadhi ya Wanawake na Vijana wamewezeshwa kupata elimu ya ujasirimali na mikopo ya kuanzisha miradi ya kiuchumi;
- ii. Wanufaika wameweza kuongeza kipato na hivyo kuboresha hali ya maisha;na
- iii. Kupungua kwa uhalifu kwani Vijana wanapata mitaji inayowawezesha kuanzia shughuli za kiuchumi.

b) **Changamoto**

- i. Kukosekana kwa Sheria inayosimamia utekelezaji wa Agizo la Serikali la kuzitaka Halmashauri kutenga kikamilifu asilimia kumi (10%) ya mapato ya ndani kwa ajili ya Mfuko wa Vijana na Wanawake;
- ii. Baadhi yan Vijana na Wanawake kukosa elimu ya ujasilimali na hivyo kushindwa kuendesha miradi wanayoianzisha;
- iii. Baadhi ya Vikundi vya Wanawake na Vijana kutorejesha fedha kikamilifu ili kutoa fursa kwa wengine kukopeshwa;na
- iv. Vijana na Wanawake kukosa maeneo rasmi ya kuendeshea shughuli wanazoanzisha kutohana na mikopo wanayopewa na mpango huu.

2.2.2 Uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Rais

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilisha ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati ilijielekeza katika uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, hii ikiwa ni kwa mujibu wa Kanuni ya 98(2), ikisomwa pamoja na Kanuni ya 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Bajeti ya Ofisi ya Rais, inahusisha Mafungu 28 kutoka Tawala za Mikoa

na Serikali za Mitaa, na Mafungu 9 kutoka Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Uchambuzi huo ulijikita katika kuititia Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali, kwa mwaka wa Fedha 2017/18. Vikao vya uchambuzi wa bajeti vilifanyika kuanzia tarehe 19 Machi, 2017 na kuendelea hadi tarehe 03 Aprili, 2017 kama ifuatavyo:-

2.2.3 Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa bajeti katika Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ulihusisha mafungu yafuatayo:-

1. Fungu 56 - Ofisi ya Rais –TAMISEMI
2. Fungu 2 - Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC)
3. Fungu 70 - Mkoa wa Arusha
4. Fungu 88 - Mkoa wa Dar Es Salaam
5. Fungu 78 - Mkoa wa Mbeya
6. Fungu 63 - Mkoa wa Geita
7. Fungu 90 - Mkoa wa Songwe
8. Fungu 89 - Mkoa wa Rukwa
9. Fungu 80 - Mkoa wa Mtwara
10. Fungu 85 - Mkoa wa Tabora
11. Fungu 84 - Mkoa wa Singida
12. Fungu 75 - Mkoa wa Kilimanjaro
13. Fungu 71 - Mkoa wa Pwani
14. Fungu 36 - Mkoa wa Katavi
15. Fungu 81 - Mkoa wa Mwanza
16. Fungu 73 - Mkoa wa Iringa
17. Fungu 87 - Mkoa wa Kagera
18. Fungu 54 - Mkoa wa Njombe
19. Fungu 74 - Mkoa wa Kigoma
20. Fungu 76 - Mkoa wa Lindi
21. Fungu 95 - Mkoa wa Manyara
22. Fungu 77 - Mkoa wa Mara
23. Fungu 47 - Mkoa wa Simiyu
24. Fungu 86 - Mkoa wa Tanga
25. Fungu 72 - Mkoa wa Dodoma

26. Fungu 82 - Mkoa wa Ruvuma
27. Fungu 83 - Mkoa wa Shinyanga
28. Fungu 79 - Mkoa wa Morogoro

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi wa mafungu hayo, Kamati ilibaini kwamba, utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ulizingatia makusanyo ya maduhuli kwa kulinganisha na malengo na mwenendo wa upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa.

i) **Ukusanyaji wa Maduhuli**

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba, mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa Fungu 56 (Ofisi ya Rais, TAMISEMI) haukuwa wa kuridhisha kwani kwani hadi kufikla mwezi Februari, 2017 (katikati ya robo ya tatu) ni **shilingi bilioni 4.8** tu katи ya **bilioni 16.9** zilizokadiriwa ndiyo zilikuwa zimekusanya. Kiwango hicho kilikuwa sawa na asilimia 28 tu ya lengo lilllokusudiwa.

Kamati ilibaini kwamba, pamoja na kiwango cha ukusanyaji wa maduhuli kuwa chini, bado kiasi kilichopatikana katika kipindi hicho kiliongezeka kwa zaidi ya asilimia 16 ikilinganishwa na kiwango cha asilimia 12 kilichokusanya katika kipindi kama hicho katika mwaka fedha 2015/16.

Uchambuzi ulibaini kwamba, miongoni mwa sababu za kutokufikiwa kwa malengo ya ukusanyaji wa maduhuli ni kutokana na kuweka malengo makubwa bila kuzingatia vyanzo vilivyopo. Ni mtazamo wa Kamati kwamba, malengo ya ukusanyaji wa maduhuli yazingatie vyanzo halisi vya mapato vilivyopo, ili kuondoa dhana ya kutowajibika kwa mamlaka zinazohusika na ukusanyaji wa mapato.

ii) **Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina**

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi Kamati ilibaini kwamba, mtiririko wa fedha kutoka Hazina haukuwa mzuri kutokana na kukosa ulinganifu katи ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa mwaka wa fedha

2016/17 na kiasi kilichotolewa na Hazina. Kwa mfano; hadi kufikia mwezi Februari, 2017 kiasi cha fedha kilichotolewa kwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Taasisi zake kwa ajili ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo kilikuwa ni **shilingi bilioni 202.2** katи ya **shilingi bilioni 354** zilizoidhinishwa. Kiasi hiki ni sawa na **asilimia 57** ya fedha yote iliyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa wastani, upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida na maendeleo ulikuwa ni asilimia 60, kiwango ambacho ni kizuri ikilinganishwa na asilimia 47 katika mwaka wa fedha 2015/16. Hata hivyo, ukweli unabaki palepale kwamba, bado lengo husika halikufikiwa kikamilifu kwani ilitakiwa katika kipindi hicho angalau zaidi ya asilimia 70 ya fedha ziwe zimepokelewa (wastani wa asilimia 25 kwa kila robo).

iii) Utekelezaji wa Maoni ya Kamati

Mheshimiwa Spika, uchambuzi ulibaini kwamba, Ofisi ya Rais TAMISEMI ilizingatia maoni ya Kamati kwa kiwango cha kuridhisha kutokana na kutekeleza kikamilifu baadhi ya maoni na kuendelea na utekelezaji wa mengine, katи ya 15 yaliyotolewa na Kamati. Miogoni mwa maoni yaliyotekeliza kikamilifu na kuanza kuonesha mafanikio ni pamoja na:-

(a) Kuhakikisha Halmashauri na Mikoa inatumia mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato (*Local Government Revenue Collection Information System - LGRCIS* na *Got – HOMIS*). Hadi kufikia Februari, 2017 jumla ya Halmashauri 175 (sawa na asilimia 94.6) katи ya 185 zilikuwa zimeanza kutumia mfumo wa LGRCIS, na zilizosalia zilikuwa katika utaratibu wa kufunga mfumo huo.

Aidha, Hospitali za Rufaa za Mikoa 19, Hospitali 43 za Wilaya na Vituo vya Afya 38 vilikuwa vimeanza kutumia mfumo wa Got – HOMIS.

(b) Ukahiki wa Watumishi hewa na kuwaondoa katika mfumo wa malipo ya mishahara (pay roll) ili kuepusha

upotevu wa fedha za umma. Hadi mwishoni mwa Februari, 2017 jumla ya Watumishi 13,369 walibainika na kuondolewa katika orodha ya malipo ya mishahara ya Serikali kutokana na sababu mbalimbali huku kati ya hao 4,968 (sawa na asilimia 37) wakiwa ni watumishi hewa. Idadi hiyo ya watumishi hewa ilikuwa imeisababishia Serikali hasara ya **shilingi bilioni 25.** 3. Aidha, Kamati inatambua juhudzi za Ofisi ya Rais – TAMISEMI katika kurejesha fedha hizo, kwani hadi wakati huo zilikuwa zimesaidia kurejeshwa kwa shilingi bilioni 2.7 huku juhudzi zaidi zikiendelea.

Mheshimiwa Spika, katika maoni ambayo utekelezaji wake ulikuwa unaendelea, Kamati ilishauri mkazo zaidi uwekwe kwenye kuhakikisha Halmashauri zinatenga kikamilifu asilimia kumi (10%) ya mapato ya ndani kwa lengo la kuwawezesha Vijana na Wanawake. Kamati ilishauri suala hilo kuingizwa katika mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa (Sura 290) ili kuupa nguvu ya kisheria Mfuko ya Maendeleo Vijana na Wanawake.

iv) Makadirio ya mapato kwa mwaka wa Fedha 2017/2018

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza malengo yaliyopangwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Tume ya Utumishi wa Waalimu, Mikoa na Halmashauri, ziliomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi **6,568,841,586,637**. Kati ya fedha hizo, Shilingi **4,535,390,860,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **1,779,128,523,846** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Uchambuzi ulibaini kwamba, bajeti hiyo imeongezeka kwa **shilingi bilioni 516.2** (sawa na asilimia 8.5) ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2016/17. Hata hivyo, kiwango hicho cha ongezeko ni kidogo ikilinganishwa na kile kilichoongekeza katika mwaka wa fedha 2016/17 ambacho kilikuwa ni asilimia 12. Sura hiyo ya ongezeko kwa kiwango cha kupungua (*increasing at decreasing rate*) ilishuhudiwa pia katika fedha za maendeleo, ambazo zilliongezeka kwa asilimia 9.1 ikilinganishwa na asilimia 74.8 katika mwaka wa fedha 2016/17. Ongezeko hilo limepungua kwa zaidi ya mara saba katika kipindi cha mwaka mmoja wa bajeti, jambo

linaloleta mashaka katika utekelezwaji wa miradi ya maendeleo iliyoanzishwa katika mwaka wa fedha uliotangulia.

Mheshimiwa Spika, ni wazi Ofisi ya Rais - TAMISEMI ndiyo inayochukua sehemu kubwa ya bajeti ya Taifa ikilinganishwa na Wizara nyingine za Serikali. Katika mwaka wa fedha 2017/18 bajeti ya TAMISEMI ni asilimia 20.7 ya bajeti ya Taifa, ambayo ni shilingi triliioni 31.69. Hata hivyo, uchambuzi unaonesha kwamba, uwiano wa bajeti ya TAMISEMI dhidi ya bajeti ya taifa umeendelea kuwa chini ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2015/16 ambapo bajeti ya TAMISEMI ilikuwa ni asilimia 24 ya bajeti ya taifa.

Ni mtazamo wa Kamati kwamba, kwa kuwa Serikali inaendelea kuongeza na kuboresha utoaji wa huduma za kijamii (elimu bure na afya) kwa Wananchi, na huduma hizo ziko chini ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, ni wazi kwamba bajeti ya ofisi hiyo ingepaswa kuongezeka kwa kiwango kikubwa.

2.2.4 Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Kamati ilifanya uchambuzi wa Mafungu yafuatayo:-

1. Fungu 20 – Ikulu;
2. Fungu 3 - Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri;
3. Fungu 32 - Menejimenti ya Utumishi wa Umma;
4. Fungu 33 - Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;
5. Fungu 67 - Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;
6. Fungu 94 - Tume ya Utumishi wa Umma;
7. Fungu 09 – Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma;
8. Fungu 4- Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa; na
9. Fungu 11- Ofisi ya Ushauri wa Mafuta na Gesi.

a) Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ulibaini kwamba, hakuna ulinganifu kati ya

kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge lako tukufu kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na kiasi kilichotolewa. Kamati ilibaini kwamba, fedha zilizoidhinishwa ziliikuwa zinatolewa kidogo kuliko ilivyokusudiwa katika Mpango wa upatikanaji fedha (cash flow plan).

Hadi kufikia mwezi Februari, 2017 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, pamoja na taasisi zilizo chini yake, ilikuwa imepokea **shilingi bilioni 527** kutoka Hazina ikiwa ni sawa na asilimia 59.75 ya bajeti yote iliyoidhinishwa kwa ofisi hiyo.

Kiasi hicho cha fedha kilipungua kwa asilimia 23.11 ikilinganishwa na kiasi kilichopokelewa katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ambacho kilikuwa ni asilimia 82.86 ya fedha iliyoidhinishwa kwa mwaka huo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa fedha za maendeleo uchambuzi umebaini kwamba, hadi kufikia Mwezi Februari, 2017 Ofisi hii ilikuwa imepokea jumla ya **shilingi bilioni 246.8** kutoka Hazina. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 52.93 ya fedha yote iliyoidhinishwa kwa ajili ya maendeleo. Hata hivyo, fedha hizo zilipungua kwa asilimia 21.28 ikilinganishwa na fedha zilizopokelewa kwa kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2015/2016, ambazo ziliikuwa ni sawa na asilimia 74.21.

Mheshimiwa Spika, katika ofisi hii pia Kamati imebaini kwamba, mwenendo wa upatikanaji wa fedha (matumizi ya kawaida na maendeleo) haukuwa mzuri kwani fedha zilizopatikana ziliikuwa ni wastani wa asilimia 59.75 ya fedha zote zilizoidhinishwa, kiasi ambacho ni chini ya matarajio ya angalau asilimia 70 ya fedha iliyoidhinishwa.

Hata hivyo, Kamati ilibaini kwamba, fedha za matumizi ya kawaida zilipatikana kwa kiwango cha juu zaidi (asilimia 67.41) ikilinganishwa na fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, taswira ilijoitokeza katika uchambuzi huo ni kwamba, bado kasumba ya kuelekeza fedha nyingi katika matumizi ya kawaida ikilinganishwa na fedha za maendeleo imeendelea kutamalaki

b) Makadirio ya Mapato kwa mwaka wa Fedha 2017/2018
Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza malengo yake, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ilionba kuidhinishiwa **shilingi bilioni 821.32**. Kati ya Fedha hizo **shilingi bilioni 430.35** zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi bilioni 390.97** ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

Uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba, bajeti hiyo ilikuwa imepungua kwa **shilingi bilioni 60.79** (sawa na asilimia 6.89) ikilinganishwa bajeti ya **shilingi bilioni 882.11** iliyoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2016/2017.

Vilevile, bajeti ya maendeleo ilibainika kupungua kwa **shilingi bilioni 75.25** (sawa na asilimia 16.13) ikilinganishwa na **shilingi bilioni 466.22** zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2016/17.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba, Bajeti ya shilingi bilioni 821 iliyombwa kuidhinishwa kwa ajili ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora katika mwaka wa fedha 2017/18, ilikuwa ni sawa na asilimia 2.59 ya Bajeti ya Taifa ambayo ni shilingi trilioni 31.699

Aidha, wakati uchambuzi ukionesha ongezeko la Bajeti ya Taifa kwa asilimia 7.31 katika mwaka wa fedha 2017/18, bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ilipungua kwa asilimia 6.89.

Ni mtazamo wa Kamati kwamba, ongezeko la Bajeti ya Taifa lingeweza kusababisha kuongezeka kwa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, hasa kutokana na ukweli kwamba, ndiyo yenye dhamana ya kusimamia ajira na ustawi wa Watumishi nichini, sekta ambayo inakua kila kukicha.

2.2.5 Kupokea na kujadili taarifa za Utekelezaji

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitekeleza jukumu hili ikiwa ni uzingatiaji wa Kanuni ya 7(1) (c) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

a) Utekelezaji wa Agizo la Serikali kuhamia Dodoma

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa Serikali kutekeleza mpango wa kuhamishia shughuli zake Mkoani Dodoma, ambao ulikuwepo kwa miaka mingi, ultolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, tarehe 25 Julai, 2016. Utekelezaji wake ambao umegawanywa katika awamu nne, ulanza kutekelezwa Januari, 2017 na uko katika awamu ya tatu hadi sasa.

Kamati inaipongeza Serikali kwa namna ambavyo imekuwa ikitekeleza kwa kasi uamuzi huo wa Rais, hasa kwa kuzingatia ukweli kwamba, mpango wa kuhamia Dodoma ulikuwepo kwa zaidi ya miongo mine (miaka 40), hata hivyo dhamira ya utekelezaji wake ilikuwa ikisuasua. Hatua ya Serikali ya Awamu ya Tano kuamua kuutekeleza mpango huu, inaifanya nchi yetu kuingia katika orodha ya nchi chache duniani ambazo zilliamua kuhamisha makao makuu ya shughuli za Serikali na kutekeleza kikamilifu maamuzi hayo.

b) Mpango wa Usambazaji Maji Safi na Salama Vijijini.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Usambazaji Maji Safi na Salama Vijijini unaotekeliza chini Ofisi ya Rais TAMISEMI unalenga kuboresha huduma ya maji na usafi wa mazingira. Malengo ya mpango huu ni kuboresha huduma ya upatikanaji wa maji safi na salama kwa asilimia 85 kwa maeneo ya vijijini na asilimia 90 kwa maeneo ya mijini ifikapo mwaka 2020; kuwa na vyombo huru na madhubuti vya watumiaji maji kwa ajili ya usimamizi na uendeshaji wa miradi na huduma ya maji na usafi wa mazingira vijijini; na kuimarisha mifumo madhubuti na endelevu na yenye ufanisi ya matumizi ya rasillimali za maji.

Kwa kuwa, Ofisi ya Rais – TAMISEMI ina jukumu la kusimamia na kuratibu Sera ya Ugatuaji wa Madaraka kutoka Serikali Kuu kwenda Mamlaka za Serikali za Mitaa, utekelezaji wa programu za maji vijijini unafanyika kwa kiwango kikubwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kushiiikiana na wananchi. Hata hivyo, Ofisi ya Rais – TAMISEMI inashirikiana na Wizara ya Maji na Umwagiliaji kusimamia na kuratibu utekelezaji wa miradi hiyo kupitia mikoa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua na kupongeza juhudzi za Serikali katika kutenga fedha nydingi kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi iliyo chini ya Mpango wa Usambazaji Maji Safi na Salama Vijijini. Kwa mfano; katika mwaka wa fedha 2016/2017 **shilingi bilioni 296.64** ziliidhinishwa kwa ajili ya ujenzi na ufuatiliaji wa miradi ya maji na usafi wa mazingira vijijini.

Ni mtazamo wa Kamati kwamba, juhudzi hizo zisiishie katika kutenga fedha tu, bali pia zielekezwe katika kupeleka fedha zilizotengwa ili miradi iliyokusudiwa iweze kutekelezwa kikamilifu na Wananchi waweze kunufaika na huduma hii muhimu katika maisha yao ya kila siku.

c) Usimamizi wa Mipango Miji katika Halmashauri za Majiini nchini

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017, Ofisi ya Rais, TAMISEMI iliweza kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali pamoja na uandaaji wa mipango ya jumla ya uendelezaji ambayo inahusu uandaaji wa mipango kabambe na mipango ya matumizi ya ardhi ya muda wa kati (*interim land use plans*).

Halmashauri za Miji 37 ziko kwenye hatua mbalimbali za kuandaa mipango kabambe ya muda mrefu (miaka 20) na mipango ya muda wa kati (miaka 10). Mipango hii inaanadaliwa kwa ufadhili wa Benki ya Dunia kupitia Mpango wa Uimarishaji wa Halmashauri za Miji (ULGSP) na fedha kutoka vyanzo vya mapato ya ndani.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha matumizi ya mfumo wa taarifa za kijiografia na ili kurahisiahua upangaji, upimaji na usimamizi wa utawala wa ardhi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017 ilikamilisha mapitio ya mkakati wa matumizi ya mfumo wa taarifa za kijiografia (*Geografia Information System – GIS*) katika shughuli za uendelezaji wa miji.

Mfumo huu utawezesha kuwepo kwa uwazi katika kupanga, kupima na kugawa ardhi ikiwemo utoaji wa Hatimiliki za ardhi katika miji na utunzaji wa kumbukumbu za Ardhi, Nyumba na Anwani za Makazi. Lengo ni kuziwezesha Halmashauri zote nchini kujimarisha katika kutumia mfumo huo kwenye uendelezaji wa miji na hivyo kupunguza gharama za kuandaa mipango kabambe, kutatua migogoro ya ardhi na kupanga na kudhibiti uendelezaji wa miji.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuna usimamizi wa utekelezaji wa mpango wa anwani za makazi na postikodi katika mwaka wa fedha 2016/2017, Ofisi ya Rais -TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ilizindua miongozo ya Mpango wa Anwani za Makazi na Postikodi pamoja na Sheria Ndogo za mfano za kusimamia utekelezaji wa mpango huo. Mpango huu utahusisha maeneo yallyopangwa na yasiyopangwa isipokuwa maeneo hatarishi.

Ni matumaini ya Kamati kwamba, Serikali itaongeza nguvu katika kusimamia utekelezaji wa mpango huu kwani utakuwa na faida nydingi kwa jamii ikiwa ni pamoja na kuwezesha kila mtu, biashara au huduma iliyosajiliwa kutambulika kwa kuwa na anwani halisi ya makazi. Vilevile, mamlaka za mapato zitawenza kuwabaini na kuwafikia walipa kodi kwa urahisi. Aidha, Mamlaka za Serikali za Mitaa zitawenza kutoa majina kwa barabara, njia na mitaa pamoja na kuweka namba kwenye nyumba za makazi na majengo ya matumizi mbalimbali vijijini na mijini.

d) Zoezi la kuondoa Watumishi hewa na uhakiki wa Vyeti katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, Hospitali za Wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati za Umma

Mheshimiwa Spika, ni jukumu la Serikali yoyote duniani kutoa kwa huduma zote muhimu kwa Wananchi wake kwa kuhakikisha inaanjiri Watumishi wenye weledi na sifa stahiki sambamba na kuweka mazingira wezeshi yatakayoleta matokeo yenye tija katika utoaji wa huduma hizo.

Ili kuhakikisha Watumishi walioajiriwa wana sifa stahiki za kuwa katika Utumishi wa Umma, Serikali ya Awamu ya Tano iliamua kufanya uhakiki mkubwa ambao uliana na hatua ya kubainisha mishahara hewa, kuondoa watumishi waliotumia vyeti vya kughushi kujipatia ajira na walioajiriwa kwa vyeti vya darasa la saba baada ya mwaka 2004 ambao hawakujidoleza na kupata elimu ya kidato cha nne.

Mheshimiwa Spika, uhakiki huo umeathiri sekta mbalimbali kutokana na kupoteza Watumishi wengi kwa kuondolewa kazini. Miongoni mwa sekta hizo ni Afya kwenye Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Sekta hiyo ilipoteza jumla ya **Watumishi 3310** wa kada mbalimbali za afya kutokana na uhakiki wa vyeti pekee, na hivyo kuongeza upungufu kutoka asilimia 51 iliyokuwepo kabla ya uhakiki hadi asilimia 54.4 Mara baada ya uhakiki. Upungufu huo wa wataalam katika sekta hiyo uliflikia Watumishi 57,788.

Kamati imetambua na kupongeza juhudzi za Serikali katika kukabiliana na upungufu huo ikiwa ni pamoja na kutoa kibali na kuajiri Madaktari 206 waliotakiwa kwenda nchini Kenya na kuwatawanya katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa mwezi Mei, 2017. Hata hivyo, kwa kuzingatia upungufu uliopo ni wazi kwamba, Wananchi bado wanapata shida katika kupata huduma ya afya. Ni mtazamo wa Kamati kwamba, juhudzi zaidi za makusudi zinahitajika ili kuongeza idadi ya wataalam wa afya katika ngazi hizo.

e) **Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa**

Mheshimiwa Spika, chombo hiki kilianzishwa mwaka 1986 chini ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa (Sura 290), ili kutekeleza miongoni mwa mambo mengine, jukumu la kutoa mikopo kwa Halmashauri nchini ili kuziwezesha kutekeleza miradi ya maendeleo na shughuli za kiuchumi kwa lengo la kuongeza mapato ya halmashauri.

Hadi tarehe 30 Juni, 2017 Bodi ilikuwa imefanikiwa kutoajumla ya mikopo 68 yenye thamani ya **Shilingi bilioni 9.7** kwa Halmashauri 54 kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo.

Miradi iliyopewa fedha ni pamoja na ujenzi wa masoko katika Halmashauri 8, ujenzi wa vituo vya mabasi katika Halmashauri 8, ujenzi wa kumbi za mikutano katika Halmashauri 2, ununuzi wa Kangavuke kwa ajili ya kuzalisha umeme katika Halmashauri 1, na kilimo cha mazao ya tumbaku na zabibu katika Halmashauri 1.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kwamba, dhamira ya kuanzishwa kwa Bodi hii ni nzuri kwani inazisaidia Halmashauri kupata mikopo yenyenye masharti nafuu. Hata hivyo, uwezo wa chombo hiki kifedha umekuwa hauongezeki kwa kiwango cha kuridhisha kutokana na Halmashauri nyingi kushindwa kuchangia Michango ya Akiba (*Minimum Compulsory Reserve – MCR*) na Nyongeza ya Mtaji. Mfano; kati ya mwaka 1986 hadi mwaka 2017, halmashauri zipatazo 152 zilikuwa zinadaifa jumla ya **shilingi bilioni 5.6** sawa na asilimia 43.1 ya **shilingi bilioni 12.9** zillizopaswa kuwa zimechangiwa na halmashauri zote katika kipindi hicho.

Hali hii duni ya kifedha inakikwamisha chombo hiki, kwanza kutoa mikopo mikubwa kwa halmashauri zinazohitaji, na pili ni kushindwa kutoa mikopo kwa halmashauri nyingi. Kwa mfano; hadi sasa ni Halmashauri 54 tu kati ya Halmashauri 185 zilizopo nchini ndiyo zimenufaika na mikopo ya Bodi. Idadi hiyo ya halmashauri ni sawa na asilimia 29.1 ya halmashauri zote nchini.

Ni mtazamo wa Kamati kwamba, Serikali izilazimishe Halmashauri zinazodaiwa na chombo hiki kutoa michango inayotakiwa pamoja na kurejesha mikopo stahiki ili chombo hiki kiweze kutoa mikopo mingi yenyenye masharti nafuu kwa Halmashauri na hivyo kuziwezesha kugharamia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo, hasa yenyenye kuhitaji fedha nyingi.

f) Wakala wa Barabara za Vijiji na Mijini (TARURA)

Mheshimiwa spika, kuanzishwa kwa Wakala huu ni muendelezo wa utekelezaji wa maboresho kwenye sekta ya

ujenzi na barabara yaliyoanza mwaka 1998. Maboresho hayo yalihusu kurekebisha Sheria ya Tozo za Barabara (Road Tolls Act), kuanzishwa kwa Bodi ya Mfuko wa Barabara (Road Fund Board), kuanzishwa kwa Wakala wa Barabara (TANROADS) na sasa Wakala wa Barabara za Vijiji na Mijini (TARURA).

TARURA itasaidia kukabiliana na changamoto zinazokabili miundombinu ya barabara katika maeneo ya Vijiji na Mijini. Pamoja na kwamba, Wakala hii itaendesha shughuli zake kwa kuzingatia misingi ya kibashara, hata hivyo, itazingatia ufanisi wa gharama na masuala mengine mtambuka na ya Kijamii kwa ajili ya maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi.

Tangua kuanzishwa kwake, chombo hiki kimebainika kukabiliwa na changamoto kadhaa zikiwemo ukosefu wa ofisi katika mikoa na wilaya nyingi nchini pamoja na uhaba wa Watumishi hasa katika fani za uhandisi, uhasibu na ununuizi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua na kupongeza juhudini zinazofanywa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili kukabili changamoto zilizopo ili Wakala hii iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Aidha, Kamati inatambua kwamba, Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB) imeanza mchakato wa kupitia kanuni (to revise formula) ya mgawo wa fedha za Mfuko huo ili kuongeza fedha zinazokwenda TARURA kutoka asilimia 30 ya sasa.

Kwa kuwa, Wakala huu unatakiwa kisheria kupokea fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina (*Consolidated Fund*), Kamati inashauri fedha hizo zipelekwe kwa wakati ili kutoathiri utekelezaji wa majukumu ya wakala. Aidha, ni maoni ya Kamati kwamba, wakala ianzishiwe kifungu (sub vote) cha maendeleo katika bajeti ijayo ili iweze kutengewa fedha za maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya barabara.

- g) **Utekelezaji wa Miradi ya Sekta ya Afya katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 (Ujenzi wa Hospitali za Mikoa na Wilaya na Upatikanaji wa Dawa, Vifaa Tiba na Vitendanishi).**

Mheshimiwa Spika, uendelezaji wa miundombinu ya sekta ya Afya na utoaji wa huduma za Afya katika ngazi za Hospitali za Wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati vinatekelezwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kwa upande wake Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, inahusika na kuandaa Sera, miongozo ya kuandaa viwango, kusimamia ubora wa huduma na kusimamia Hospitali za Rufaa za Mikoa.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri 64 nchini hazina Hospitali za Wilaya, jambo ambalo linawanyima Wananchi wa Halmashauri hizo fursa za kupata huduma za afya za hospitali teule za Wilaya na hivyo kulazimika kwenda kupata huduma hizo katika Halmashauri za Wilaya zilizopo jirani. Idadi hiyo ya Halmashauri ni sawa na asilimia 34.78 ya lengo la kuwa na Hospitali za Wilaya 184.

Ni mtazamo wa Kamati kwamba, Serikali iweke juhudini za makusudi katika kuhakikisha inaweka mpango utakaowezesha kuanza kujengwa kwa Hospitali za wilaya katika halmashauri hizo ambazo hazina huduma za hospitali teule za Wilaya.

h) Changamoto ya Walimu na Miundombinu ya Kielimu

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Elimu ya Msingi na Sekondari ndiko watoto wa nchi yetu wanapopata msingi wa elimu na kujengewa uwezo wa kuendelea na taaluma nyingine. Sekta hiyo imekuwa ikitabiliwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na upungufu wa Walimu na miundombinu ya kielimu, kama vile Vyumba vya Madarasa, Nyumba za Walimu na Matundu ya Vyoo.

Upungufu katika maeneo hayo umebainika kuongezeka zaidi baada ya Serikali kuanza utekelezaji wa Mpango wa Elimu Msingi bila malipo. Takwimu zinaonesha kuwa, shule za msingi nchini zinakabiliwa na upungufu wa vyumba vya madarasa kwa **asilimia 47.96**, nyumba za Walimu kwa

asilimia 80.54 na matundu ya vyoo kwa asilimia **59.34**. Kwa upande wa Shule za Sekondari takwimu zinaonesha kwamba, kuna upungufu mkubwa wa nyumba za Walimu unaofikia **asilimia 84.54** pamoja na upungufu wa matundu ya vyoo kwa **asilimia 27.14**.

Mheshimiwa Spika, hali hiyo inabainisha kwamba, pamoja na juhudini kubwa za Serikali katika kuboresha mazingira ya elimu nchini, bado kuna changamoto kadhaa zinazohitaji kutatuliwa ikiwa ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya kielimu. Mwanafalsafa wa Kifaransa Arisotle aliwahi kusema "*The roots of education are bitter, but the fruit is sweet.*" Kwa tafsiri ya Kiswahili isiyo rasmi anachokisema Mwanafalsafa huyu ni kwamba, "*Mizizi ya elimu ni michungu, lakini tunda lake ni tamu*".

Ni kwa mantiki hiyo hiyo, ni lazima jamii itambue kwamba hatua ya Serikali kuongeza uwekezaji katika elimu, kutekeleza mpango wa Elimumsingi bure na kufanya ukarabati wa shule kongwe za Sekondari za Serikali nchini ni jambo lenye gharama kubwa sana. Hata hivyo, tutakubaliana wote kwamba manufaa yatokanayo na elimu ni sawa na tunda tamu kutoka katika mti wenye mizizi michungu. Tukubali kama Taifa kukabili upungufu wa matundu ya vyoo ambaou unatutia aibu, upungufu wa vyumba vyaa madarasa, nyumba za Walimu na hata upungufu wa Walimu wenyewe.

h) Utekelezaji wa Shughuli za Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kuititia mpango wa ruzuku ya fedha kwa kaya masikini nchini umekuwa mkombozi wa kiuchumi kwa wananchi maskini. Utaratibu huu ambaou ni awamu ya tatu ya utekelezaji wa TASAF umewezesha familia maskini kumudu mahitaji ya chakula, kuboresha mahudhurio ya watoto shulenii na klikini (watoto wa chini ya miaka mitano) kwa wastani wa asilimia 96.65 na kuwekeza katika miradi ya ujasiriamali. Hadi sasa mpango huu wa ruzuku ambaou unatekelezwa kwa zaidi ya miaka mitano sasa, umenafaisha zaidi ya Kaya milioni moja (1,000,000) kwa kiasi cha zaidi ya **shilingi bilioni 555**.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua na kupongeza hatua ya Serikali kutoa fedha kiasi cha **shilingi milioni mia saba na hamsini (750,000,000/=)** ikiwa ni sehemu ya mchango wake wa **shilingi bilioni tatu (3,000,000,000/=)** zilizoidhinishwa katika bajeti ya mwaka 2017/2018. Hii ni ishara nzuri na ambayo itawapa moyo wafadhili wengine katika mfuko huu hasa ikizingatiwa kwamba, Serikali haikutoa kiasi chochote katika mchango wake wa 1/3 katika mwaka wa fedha 2015/16 na 2016/17. Katika kipindi hicho cha miaka miwili mchango wa Serikali ulipaswa kuwa **Shilingi bilioni 28**.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri juhudzi zaidi zifanyike ili mpango huu wa ruzuku uweze kuyafikia maeneo ambayo hayajafikiwa na kutoa fursa kwa Kaya maskini katika maeneo hayo kunufaika. Aidha, halmashauri kupitia Wataalam wa Maendeleo ziwasaidie wanufaika ambao wameanzisha miradi ya kiuchumi kutokana na ruzuku ili miradi hiyo iweze kukua na kuwasaidia kiuchumi.

i) **Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)**

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha utekelezaji wa shughuli za urasimishaji nchini, MKURABITA inazijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa Tanzania Bara na Wizara za Kisikta kwa upande wa Zanzibar, kwa kutoa mafunzo kwa watendaji wa Halmashauri za Wilaya, Manispaa na Miji, Kata, na Shehia ili kuendeleza urasimishaji katika maeneo yao.

Katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Disemba, 2017 mpango huu umefanya mapitio ya mkakati wa mawasiliano na kuandaa mkakati mpya kwa kuwashirikisha wataalamu kutoka Wizara za Kisikta na Ofisi ya Rais TAMISEMI, Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania, Tume ya Mipango Zanzibar, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Spika, mbali na mpango huu kulenga kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kutumia rasilimali walizonazo, pia ni njia nzuri ya kuepusha migogoro ya ardhi baina ya makundi mbalimbali katika jamii. Katika maeneo

ambayo MKURABITA imeratibu na kusimamia urasimishaji wa shughuli za wananchi, kumekuwa na matumizi mazuri ya ardhi, pamoja na ongezeko la shughuli za kiuchumi kwa wananchi hao.

Hata hivyo, changamoto ya upungufu wa fedha zinazotengwa na Serikali kwa ajili ya MKURABITA na Halmashauri kukosa fedha za kuendeleza kazi za urasimishaji baada ya kujengewa uwezo na mpango huu, vinaathiri kwa kiasi kikubwa kuenea kwa shughuli za urasimishaji wa ardhi na biashara katika maeneo mengi ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ni mtazamo wa Kamati kwamba, Serikali iongeze fedha zinazotengwa kwa ajili ya MKURABITA ili kuwezesha utekelezwaji wa shughuli zake katika maeneo mengi nchini. Aidha, halmashauri zitenge bajeti itakayoziwesha kuendeleza shughuli za urasimishaji baada ya kujengewa uwezo na mpango huo.

2.2.6 Semina kwa Wajumbe wa Kamati

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka mmoja cha utekelezaji wa majukumu ya Kamati, Wajumbe walipata fursa ya kushirika katika semina ambazo zililenga kuwajengea uwezo. Baadhi ya Semina hizo ni pamoja na:

a) Semina ya uchambuzi wa Bajeti

Mheshimiwa Spika, Semina hii iliandaliwa na kuendeshwa na Mradi wa *Legislative Support Program* (LSP) ambao unatekelezwa na Ofisi ya Bunge chini ya ufadhili wa Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDP). Kupitia semina hiyo Wajumbe walielimishwa kuhusu uchambuzi wa Bajeti ya Serikali, mambo ya kuzingatia na upangaji wa vipaumbele vyta Taifa.

b) Wajibu wa Mbunge katika Mapambano dhidi ya Rushwa

Mheshimiwa Spika, Semina hii iliandaliwa na kuendeshwa na Chama cha Mtando wa Wabunge Wanaopambana na Rushwa (APNAC) kwa kushirikiana na Mradi wa *Legislative Support Program* (LSP) ambao unatekelezwa na Ofisi ya

Bunge chini ya ufadhili wa Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDP).

Kupitia semina hiyo ambayo iliwahusisha pia Wabunge wengine, Wajumbe waliweza kuelewa kwamba wao ni wawakilishi wa Wananchi katika chombo ambacho kinatunga sheria, kinaisimamia na kuishauri Serikali pamoja na kupitisha bajeti ya Serikali. Kutokana na fursa hiyo muhimu ya Bunge katika kusimamia maendeleo ya nchi, ni wazi kwamba Wabunge wanapaswa kuwa makini sana katika mienendo yao, la sivyo ipo hatari ya kutumiwa na vikundi maslahi (interest groups) ili kufanikisha mambo yao kupitia majukumu ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, kupitia semina hiyo Wajumbe waliweza kupata visa mbalimbali kuhusu Wabunge au Wajumbe wa Vyombo vyta Wawakilishi kutoka baadhi ya nchi duniani ambaao walijikuta wameingia katika kashfa ya rushwa kutokana na kukosa mienendo mizuri ya kimaadili.

Mfano; ni kashifa ya “*cash for Questions*” iliyotokea nchini Uingereza mwaka 1994 ambapo ilibainika kwamba, baadhi ya Wabunge nchini humo walikuwa wakilipwa fedha na Wafanyabiashara ili waulize maswali Bungeni.

c) Semina ya Mtando wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA)

Mheshimiwa Spika, Mtando huu ulianzishwa kwa lengo la kuwaunganisha wakulima wadogo ili waweze kuwa na nguvu na sauti moja katika kujitetea kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na katika manufaa ya kisasa. Lengo la Semina hii lilikuwa namna Wabunge ambaao ni wawakilishi wa Wananchi wakiwemo Wakulima Wadogo, wanavyoweza kuunga mkono juhudzi za MVIWATA na kusaidia kumkwamua Mkulima Mdogo.

Mtando huu umeweza kuhamasisha na kutafuta ufadhili kwa ajili ya ujenzi wa masoko ya kisasa na kuhamasisha Wakulima kuyatumia kuuza mazao yao, ambapo mazao huuzwa kwa kupimwa kwenye mizani badala ya kutumia

magunia au kukadiria. Kupitia njia hii wakulima wengi wadogo wameweza kukuza kipato chao kutokana na mazao wanayozalisha.

Mheshimiwa Spika, kupitia semina hii Wabunge walipata fursa ya kutambua namna ambavyo uhamasishaji wao kupitia mawazo ya MVIWATA ulivyowezesha Serikali katika bajeti ya mwaka wa fedha 2017/18, kupunguza pamoja na kuondoa baadhi ya kodi, tozo na ushuru ambavyo vilikuwa ni kero kubwa kwa Wakulima.

Vilevile, Serikali iliweza kuondoa vizuizi vya barabarani ambavyo vilikuwa ni kero kubwa kwa Wakulima pale wanaposafirisha mazao yao kutoka mashambani.

Katika michango ya kwenye Semina hii Wajumbe waliahidi kuendelea kushirikiana na MVIWATA katika kumpigania mkulima hasa kuondoa kero zilizosalia ambazo ni ukosefu wa masoko, migogoro ya ardhi, pembejeo duni na ukosefu wa mitaji ya kuwawezesha kuongeza wigo wa shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Wajumbe kukiri mafanikio kwa yale maeneo ambayo wameshuhudia MVIWATA ikitekeleza shughuli zake, ipo changamoto ya baadhi ya Watendaji hasa katika ngazi za Serikali za Mitaa kushindwa kutoa ushirikiano wa kutosha katika uendeshaji wa masoko yaliyojengwa kwa msaada na hamasa ya MVIWATA. Hali hiyo imesababisha miundombinu ya masoko hayo kukosa ukarabati na hivyo kuanza kuchakaa, jambo linalotishia masoko hayo kusitisha utoaji wa huduma zake kwa wakulima. Mfano wa masoko hayo ni Soko la Kimataifa la Mahindi la Kibaigwa.

2.2.7 Ziara za Ukaguzi wa Miradi

i. Mpango wa Ukarabati wa Shule Kongwe za Sekondari

Mheshimiwa Spika, Serikali ilianza kutekeleza Mpango wa Ukarabati wa Shule Kongwe za Sekondari za Serikali nchini katika mwaka wa fedha 2016/17. Mpango huu ambaao utatekelezwa kwa Awamu Tatu unalenga kujenga na kukarabati 88 ambazo zimechakaa kwa kiwango kikubwa.

Kwa kuanzia kila shule imetengewa takribani shilingi bilioni moja (1,000,000,000/=) kwa ajili ya ukarabati au ujenzi huo.

Kamati ilitembelea Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Msalato ambayo ni mionganini mwa shule zinazonufaika na ukarabati huo ili kujionea namna unavyotekelawa.

Mheshimiwa Spika, ukarabati wa shule hiyo ultengewa **shilingi milioni 939. 19** na hadi wakati Kamati inatembelea shulenii hapo ukarabati ambao unatekelezwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) ulikuwa umefikia asilimia 90. Kamati iliridhishwa na kazi nzuri ili ofanyika katika ukarabati huo kwani, inaonesha thamani halisi ya fedha (*value for money*)

Kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza mpango huu wa ujenzi na ukarabati wa Shule Kongwe za Sekondari za Sekondari nchini kwani shule hizo zilikuwa katika halli mbaya sana kutokana na kiwango kikubwa cha uchakavu. Ni wazi kuwa hatua hiyo itarejesha heshima ya shule hizo pamoja na kuinua morali ya Walimu na Wanafunzi katika shule hizo.

ii. Mradi wa Jengo la Kitega Uchumi la Rock City Mall

Mheshimiwa Spika, mradi huu unatekelezwa kwa ubia baina ya Halmashauri ya Manispaa ya Jiji la Mwanza na Halmashauri ya Manispaa ya Illemela (zilizotoa ardhi) na Mfuko wa Pensheni wa LAPF uliota shilingi bilioni 73.36 kwa ajili ya kugharamia ulipaji fidia, ushauri wa kitaalam, ujenzi, na shughuli za utawala. Mradi huu unahusisha eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 60,000 ulikamilika tangu mwishoni mwa mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipotembelea mradi huu ilibaini kwamba, takribani asilimia 70 ya maeneo ya jengo hilo yameishapata wapangaji na shughuli za biashara zilikuwa zikiendelea. Hata hivyo, jambo ambalo liliishangaza Kamati ni kwamba, licha ya mradi huu kukamilika ikiwa ni zaidi ya miaka miwili iliyopita, mbali na kutozinduliwa, haukuwahi kuwekewa jiwe la msingi kuashiria uzinduzi wa ujenzi wa mradi huo.

Kamati inafikiri ni vyema Serikali ikatoa ufanuzi ni kwanini mradi mkubwa wa aina hii ambao umegharimu pesa nyingi (*zaidi ya shilingi bilioni 73*) haukuwekewa jiwe la msingi hadi ujenzi wake unakamilika, na miaka miwili hata baada ya kukamilika kwake imeshindikana kuuzindua.

iii. Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Kilolo

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata fursa ya kutembelea na kukagua ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Kilolo, Mkoani Iringa. Kukamilika kwa Hospitali hiyo kutasaidia kutoa huduma ya matibabu kwa takribani wakazi 229,146 wa Wilaya hiyo.

Vilevile, kukamilika kwa hospitali hii kutawezesha Wilaya ya Kilolo kukabiliana na kiwango kikubwa cha maambukizi ya VVU/UKIMWI ambacho kinakadiriwa kuwa asilimia 11. Aidha, huduma za hospitali hiyo zitasaidia kupunguza kiwango cha magonjwa na vifo kwa watoto chini ya umri miaka mitano na vifo vya akina mama wajawazito.

Mheshimiwa Spika, katika ziara hiyo Kamati ilibaini kwamba, utekelezaji wa mradi unasuasua kutohana na Serikali kuchelewesa malipo ya Wakandarasi baada ya kuwasilisha hati (*certificates*) za kazi zilizokamilika. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha malipo ya hati hizo yanatoka kwa wakati ili kutoathiri utekelezaji wa mradi huo ambao kukamilika kwake kutawezesha Wananchi wa Kilolo kuondokana na shida ya kukosa huduma za afya, ambazo hulazimika kuzifuata Iringa Mjini.

Aidha, Kamati inashauri maandalizi ya ikama ya Watumishi kwa ajili ya Hospitali hiyo yaanze mapema ili ujenzi wake utakapokamilika Wananchi wa Kilolo waanza kupata huduma ya matibabu mara moja.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

3.1 Maoni

Mheshimiwa Spika, yafuatayo ni maoni ya Kamati kuhusiana na shughuli zilizoteklezwa katika kipindi chote cha mwaka

mmoja, ambayo yanabainisha mtazamo wa kile kilichojiri wakati Kamati ikitimiza majukumu yake. Maoni hayo ni haya yafuatayo:-

a) Ofisi ya Rais ,Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;

i. Utekelezaji wa miradi ya Programu ya Maji Vijijini umekuwa ukiathiriwa na ufinyu wa bajeti inayotengwa na Serikali;

ii. Uhaba wa Wataalam wa ardhi na mipango miji pamoja na ufinyu wa bajeti vinakwamisha dhamira ya halmashauri kuendeleza programu za mipango miji;

iii. Zoezi la kuhakiki na kuwaondoa kazini Watumishi hewa na wenye Vyetti feki limesababisha athari ya upungufu wa Wataalam mbalimbali wa afya katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

iv. Ukosefu wa ofisi na uhaba wa Watumishi kwa Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) katika ngazi za Mkoa na Wilaya, unaathiri utekelezaji wa majukumu wa chombo hicho;

v. Asilimia 30 ya Mgawo wa fedha ambao TARURA inapata kutoka Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB) ni ndogo ikilinganishwa na idadi ya miradi ya barabara inayopaswa kutekelezwa chini ya wakala hii;

vi. Hatua ya Halmashauri nyingi kushindwa kutoa michango ya akiba na nyongeza ya mtaji, na zilizokopa kushindwa kurejesha mikopo kwa wakati, viinaathiri uwezo wa kifedha wa Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa na hivyo kushindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu;

vii. Kukosekana kwa Hospitali za Wilaya katika Halmashauri 64 nchini, kunawanyima Wananchi wa halmashauri hizo fursa ya kupata huduma za afya za Hospitali Teule za Wilaya na hivyo kulazimika kuzifuata katika Halmashauri za jirani:

viii. Upungufu wa miundombinu muhimu ya kielimu; kama vyumba vyaya madarasa, nyumba za Walimu na matundu ya vyoo, vinaathiri jitihada za Serikali kutoa elimu bila malipo;

- ix. Kukosekana kwa mifereji ya kuondoa maji ya mvua kwenye miundombinu ya barabara iliyojengwa na Mradi wa Miji ya Kimkakati (TSCP) kunasababisha maji kutuama katika barabara hizo na hivyo kutishia uharibifu wa mapema wa barabara hizo;
- x. Urasimu wa kuhamisha miundombinu ya maji safi na maji taka, pamoja na nguzo za umeme, kunachelewa kuanza kwa utekelezaji wa miradi ya Bodi ya Mfuko wa Barabara;
- xi. Uchache wa matundu ya vyoo ikilinganishwa na idadi ya watumiaji katika shule za msingi za Serikali nchini, kunahatarisha afya ya Walimu na Wanafunzi pamoja na kuathiri utoaji wa elimu katika shule hizo. Aidha, jambo hilo linaitia aibu Serikali pamoja na kushusha utu wa Walimu na Wanafunzi katika shule husika;
- xii. Kukosekana kwa mgawanyo mzuri wa Walimu katika shule za mijini na vijijini kunasababisha mrundikano wa Walimu katika shule za mijini na uhaba katika shule za Vijijini;
- xiii. Kukosekana kwa ushiriki mzuri wa Serikali za Mitaa katika masoko ya mazao ambayo yamejengwa na kuendeshwa kwa msaada wa Mungano wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA) kunasababisha miundombinu ya masoko hayo kukosa ukarabati na hivyo kuanza kuharibika. Aidha, hali hiyo inaathiri juhudhi za kumsaidia mkulima aweze kuuza mazao yake kwa kutumia vipimo sahihi;
- xiv. Kukosekana kwa sheria ya kusimamia utekelezaji wa Agizo la Serikali kwa Halmashauri kutenga kikamilifu asilimia kumi (10%) ya mapato ya ndani kwa ajili ya Mfuko wa Vijana na Wanawake.

b) Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora;

- i. Kutatuliwa kwa changamoto za kisera, kisheria na ukosefu wa raslimali watu na fedha, zinazoikabili Wakala wa Serikali Mtandao (e - GA) kutaiwezesha wakala hiyo kusambaza huduma zake katika taasisi nyingi za Umma na hivyo

kuiwezesha Serikali kuongeza uwajibikaji na uwazi katika kuhudumia Wananchi;

ii. Upungufu wa raslimali fedha umekwamisha TASAF kuvififikia Viji, Mitaa na Shehia nyingi zenyne kaya maskini na hivyo kuibua malalamiko mengi kutoka mionganoni mwa wananchi wa maeneo hayo;

iii. Hatua ya baadhi ya Wananchi kukosa uwazi imesababisha Kaya zisizo na sifa za umaskini kuingizwa katika mpango wa kuzinusu Kaya maskini;

iv. Hatua ya baadhi ya Wakuu wa Idara na Vitengo kukaimu kwa muda mrefu katika Wizara, Taasisi na Idara za Umma kunaathiri ufanisi wa kazi kwa kukosekana kwa maamuzi ya kiutendaji katika ofisi hizo. Aidha, hali hiyo inawakatisha tamaa Watumishi wanaokaimu kwa muda mrefu kwa kuwafanya wadhani hawana sifa stahiki.

v. Hatua ya shughuli za Mfuko wa Rais kujikita katika maeneo ya mijini kunawanyima fursa Vijana na Wanawake katika maeneo ya vijiji kunufaika na huduma za mfuko huo;

vi. Ufinyu wa bajeti inayotengwa kwa ajili ya Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) unaathiri uwezo wa mpango huo katika kuongeza wigo wa utekelezaji wa shughuli zake.

3.2 Mapendekezo

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza maoni ya Kamati, naomba kutoa mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo:-

3.3 Mpango wa Usambazaji Maji Safi na Salama Vijiji:

KWA KUWA, utekelezaji wa Mpango wa Usambazaji Maji Safi na Salama Vijiji umekuwa ukikabiliwa na ucheleweshaji wa fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya mpango huo;

NA KWA KUWA, hali hiyo inakwamisha kukamilika kwa miradi mingi chini ya mpango huu na hivyo kuwafanya Wananchi waendelee kukabiliwa na adha ya kukosa maji;

KWA HIYO BASI, Kamati inashauri Bunge liitake Serikali kuhakikisha fedha zilizopangwa kwa ajili ya utekelezaji wa mpango huu zinapatikana kikamilifu na kwa wakati ili miradi ilioanza kutekelezwa ikamilike kwa wakati na hivyo kuwawezesha wananchi kupata huduma ya maji na kuondokana na aza iliyopo.

3.3.1 Usimamizi wa Mipango Miji nchini

KWA KUWA, uhaba wa Wataalam wa Ardhi na Mipango Miji pamoja na ufinyu wa bajeti, vinaathiri uwezo wa Halmashauri nchini kuendeleza programu za mipango miji;

NA KWA KUWA, hali hiyo inasababisha miji mingi kuendelezwa bila kuzingatia taratibu za mipango jambo linalosababisha uwepo wa makazi holela na miji isiyopangwa;

KWA HIYO BASI, Kamati inalishauri Bunge liitake Serikali izipatie Halmashauri Wataalam wa ardhi na fedha za kutosha ili ziweze kutekeleza kikamilifu programu za mipango miji. Aidha, hali hiyo itawezesha miji kuendelezwa kwa taratibu zinazotakiwa na hivyo kupunguza kasi ya ukuaji wa makazi holela.

3.3.2 Zoezi la kuondoa watumishi hewa na uhakiki wa vyeti katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, Hospitali za Wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati za Umma,

KWA KUWA, zoezi la kuondoa Watumishi hewa na Watumishi wenye vyeti feki limeongeza upungufu wa Wataalam wa kada mbalimbali za afya katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, Hospitali za Wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati za Umma;

NA KWA KUWA, upungufu huo wa Wataalam umeathiri kwa kiasi kikubwa utoaji wa huduma za tiba kwa Wagonjwa katika hospitali hizo;

KWA HIYO BASI, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kukabiliana na upungufu huo kwa kuajiri Watumishi wa Afya wa kada mbalimbali katika Hospitali za Rufaa za Mikoa,

Hospitali za Wilaya, Vituo vya Afya na Zahanati. Aidha, Kamati inatambua na kupongeza hatua ya Serikali ya kuajiri Madaktari 206 kati ya 500 waliotakiwa kwenda nchini Kenya, na kuwasambaza katika mikoa mbalimbali. Hatua hii inaonesha dhamira ya Serikali ya kukabiliana na upungufu uliopo.

3.3.3 Wakala wa Barabara za Vijiji ni na Mijini (TARURA)

(a) Ukosefu wa ofisi na uhaba wa Watumishi

KWA KUWA, Wakala huu umebainika kukabiliwa na changamoto ya ukosefu wa ofisi na uhaba wa Wataalam wa kada za uhandisi, uhasibu na ununuzi;

NA KWA KUWA, hali hiyo inaathiri utekelezaji wa majukumu wa wakala huo na hivyo kusababisha hali ya miundombinu ya barabara inayopaswa kusimamiwa na wakala huu kuendelea kuwa katika hali mbaya;

KWA HIYO BASI, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali kuipatia TARURA ofisi na Watumishi wa kada zinazohitajika ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu na hivyo kuboresha hali ya miundombinu ya barabara za mijini na vijiji ambazo ziko chini ya wakala.

(b) Mgawo wa fedha kutoka Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB)

KWA KUWA, mgawo wa fedha wa asilimia thelathini (30%) ambao TARURA inaupata kutoka Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB) ni mdogo ikilinganishwa na majukumu ya wakala huo;

KWA KUWA, kiasi cha fedha kutokana na mgawo huo ni hakiwezi kuiwezesha TARURA kutekeleza miradi mingi ya barabara za mijini na vijiji ambazo zinapaswa kuhudumiwa na wakala huo;

HIVYO BASI, Kamati inashauri Serikali kuharakisha mchakato wa kupitia kanuni (formula) ya mgawo wa fedha za Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB) ili kuongeza mgawo wa TARURA kutoka asilimia 30 ya sasa. Aidha, Serikali ianzishe kifungu (sub

vote) cha maendeleo katika bajeti ya TARURA ili kuwezesha wakala hii kupata fedha za maendeleo kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina (Consolidated Fund).

3.3.4 Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa

KWA KUWA, Kamati imebaini kwamba, halmashauri nyingi hazitoi michango ya akiba na nyongeza ya mtaji husika katika Bodi ya Mikopo ya Halmashauri, pamoja na zile zilizokopa katika chombo hicho kushindwa kurejesha mikopo kwa ukamilifu;

NA KWA KUWA, hali hiyo inaathiri uwezo wa Bodi hiyo kutekeleza majukumu ya kutoa mikopo ya masharti nafuu kwa Halmashauri nchini kwa lengo la kutekeleza miradi ya maendeleo;

KWA HIYO BASI, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali isimamie kikamilifu Halmashauri ziweze kutoa michango ya akiba na nyongeza, na zile zilizokopa kurejesha mikopo husika kikamilifu ili kutoathiri uwezo wa Bodi hiyo katika kutekeleza majukumu yaliyokusudiwa.

3.3.5 Changamoto ya Miundombinu katika Sekta ya Elimu

KWA KUWA, utoaji wa elimu ya msingi na sekondari bila malipo umesababisha changamoto ya upungufu wa miundombinu ya kielimu kama vile, vyumba vyaya madarasa, nyumba za Walimu na matundu ya vyoo;

NA KWA KUWA, upungufu huo unaathiri utoaji wa elimu ya msingi na sekondari kutokana na kusababisha mrundikano wa wanafunzi darasani, Walimu kukosa nyumba za kuishi na Walimu na wanafunzi kuchangia matundu machache ya choo;

KWA HIYO BASI, Kamati inalishauri Bunge liitake Serikali kuongeza bajeti kwa ajili ya kujenga miundombinu hiyo ya kielimu ili kuondoa changamoto iliyopo na hivyo kuruhusu utoaji wa elimu bora.

3.3.6 Upungufu wa Hospitali za Wilaya

KWA KUWA, kukosekana kwa Hospitali za Wilaya katika Halmashauri za Wilaya 64 nchini kunawanyima Wananchi wa halmashauri hizo fursa ya kupata huduma za afya za Hospitali teule za Wilaya;

NA KWA KUWA, hali hiyo inawalazimu Wananchi hao kusafiri umbali mrefu kufuata huduma za Afya katika Halmashauri zilizopo jirani;

KWA HIYO BASI, Kamati inalishauri Bunge kuitaka Serikali iongeze kasi ya ujenzi wa Hospitali za Wilaya ili kuwaondolea adha ya kukosa huduma za afya za Hospitali Teule za Wilaya katika halmashauri zao.

3.3.7 Miradi ya Miji ya Kimkakati (*Tanzania Strategic Cities Project*)

KWA KUWA, baadhi ya miundombinu ya barabara iliyojengwa chini ya Mradi wa Miji ya Kimkakati (*Tanzania Strategic Cities Project*) haina mifereji ya kuondoa maji ya mvua;

NA KWA KUWA, hali hiyo inasababisha maji ya mvua kutuama katika barabara hizo na hivyo kutishia uharibifu wa mapema wa miundombinu hiyo;

KWA HIYO BASI, Kamati inashauri Bunge liitake Serikali kuchukua hatua za haraka kuhakikisha mifereji ya kuondolea maji inajengwa katika barabara hizo ambazo zimegharimu fedha nyingi na hivyo kuepusha hasara inayoweza kujitokeza kutokana na uharibifu.

3.3.8 Ushirikiano wa Serikali za Mitaa na Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA)

KWA KUWA, imebainika kwamba baadhi ya Watendaji wa Serikali za Mitaa hawatoi ushirikiano wa kutosha katika kuhudumia na kuendesha masoko ya mazao ya Wakulima yaliyojengwa na kuendeshwa kwa hamasa na msaada wa MVIWATA;

NA KWA KUWA, hali hiyo inasababisha usimamizi mbovu wa masoko hayo kiasi cha kusababisha miundombinu ya masoko hayo kukosa ukarabati muhimu na hivyo kuanza kuharibika;

HIVYO BASI, Kamati inashauri Bunge liitake Serikali kuchukua hatua za haraka ili kurekebisha hali hiyo na hivyo kuwezesha masoko hayo kuijendesha kwa ufanisi na hivyo kuendelea kumkomboa mkulima kwa kumuwezesha kuuza mazao kwa vipimo sahihi.

3.3.9 Watendaji wa Serikali Kukaimu muda mrefu

KWA KUWA, imebainika kwamba, baadhi ya Wakuu wa Idara na Vitengo katika ofisi za Umma wanakaimu kwa muda mrefu bila kuthibitishwa;

NA KWA KUWA, hali hiyo inaathiri ufanisi wa kiutendaji kwa kukosekana kwa uamuzi kwa baadhi ya masuala katika ofisi hizo, pamoja na kuwaathiri watusika kwa kuwafanya wadhani hawana vigezo vinavyotakiwa;

HIVYO BASI, Kamati inashauri Bunge kuitaka Serikali ama kuwathibitisha Watumishi ambao wamekaimu kwa muda mrefu na wamebainika kuwa na sifa stahiki, au kutafuta watu wenye sifa zinazotakiwa katika nafasi hizo iwapo wanaokaimu watabainika kukosa stahiki.

3.3.10 Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)

(a) Upungufu wa Fedha na baadhi ya maeneo kutofikiwa

KWA KUWA, upungufu wa raslimali fedha umesababisha utekelezaji wa TASAF Awamu ya Tatu kutoyafikia baadhi ya maeneo;

NA KWA KUWA, hali hiyo inasababisha Kaya maskini katika maeneo ambayo hayajafikiwa kukosa fursa ya kuingizwa katika utaratibu wa kunufaika na ruzuku hizo ambazo zingewawezesha kujikwamua na umaskini uliokithiri;

NA HIVYO BASI, Kamati inashauri Bunge kuitaka Serikali itoe fedha za kutosha na kuhakikisha mpango wa kunusuru kaya maskini unayaifikia maeneo yote ambayo haya jafikiwa ili kutoa nafasi kwa Kaya maskini kunufaika na utaratibu huu.

(b) Watendaji wa Halmashauri kusaidia Kaya maskini kuendeleza miradi ya kiuchumi

KWA KUWA, baadhi ya wanufaika wa ruzuku kwa Kaya maskini wametumia sehemu ya fedha wanazozipata kuanzisha miradi midogo midogo ya kiujasiriamali;

NA KWA KUWA, miradi hiyo inashindwa kuendelea vizuri kutokana na walengwa hao kukosa elimu ya ujasiriamali, uendeshaji na usimamizi wa miradi, jambo linalotishia miradi hiyo kufilisika;

HIVYO BASI, Kamati inashauri Serikali kupitia Maafisa Mipango na Maafisa Maendeleo ya Jamii katika halmashauri nchini kuwasaidia wanufaika hao wa TASAF katika juhudii zao za kuendeleza na kukuza miradi yao ili kujikwamua kiuchumi.

3.3.11 Mfuko wa Kujitegemea wa Rais (PTF)

KWA KUWA, ufinyu wa bajeti umesababisha shughuli za Mfuko wa Kujitegemea wa Rais kujikita katika kusaidia vikundi vichache vyta Vijana na Wanawake katika maeneo ya mijini tu;

NA KWA KUWA, hali hiyo inawanyima Vijana na Wanawake wengi katika maeneo ya mijini na vijijiini fursa ya kunufaika na mikopo inayotolewa na Mfuko huo;

HIVYO BASI, Kamati inashauri Bunge kuitaka Serikali kutenga bajeti ya kutosha kwa Mfuko huu ili kuuwezesha kuongeza wigo wa huduma za mikopo kwa Vijana na Wanawake katika maeneo mbalimbali nchini.

3.3.12 Mpango wa Kurasimisha Raslimali za Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)

KWA KUWA, ufinyu wa bajeti unakwamisha MKURABITA kuongeza wigo wa utekelezaji wa shughuli za urasimishaji katika maeneo mengi nchini;

NA KWA KUWA, hali hiyo inawanyima Wananchi wa maeneo mengi ambayo hayajafikiwa na MKURABITA fursa ya kurasimishiwa ardhi na biashara zao, na hivyo kuweza kuzitumia kama dhamana ya mikopo;

HIVYO BASI, Kamati inashauri Bunge kuitaka Serikali kuongeza bajeti ya MKURABITA ili kuwezesha mpango huu kuongeza wigo wa shughuli zake na hivyo kuwafikia Wananchi wengi wanaohitaji kurasimisha ardhi na biashara zao ili waweze kuzitumia kama dhamana ya mikopo katika benki na taasisi za fedha.

SEHEMU YA NNE

4.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, ninapohitimisha napenda kunukuu maneno ya Waziri Mkuu wa India, Narendra Modi, kwamba *“Good governance can not remain merely a philosophy. Concrete steps have to be taken for realizing its goals”*

Tafsiri ya Kiswahili isiyo rasmi ya nukuu hiyo ni kwamba, *“utawala bora hauwezi ukasalia kuwa falsafa tu. Hatua madhubuti zinapaswa kuchukuliwa ili kufikia malengo yake (utawala bora)”*

Malengo ya dhana ya utawala bora ni kuhakikisha kunakuwa na ustawi mzuri wa kijamii na kiuchumi kwa Wananchi. Hilo linawezekana pale panapokuwa na ushirikishwaji wa wananchi katika maamuzi. Bunge ambalo ni chombo cha uwakilishi wa Wananchi linalo jukumu la kushirikiana na Serikali katika kuhakikisha dhana ya utawala bora inazingatiwa.

Nitumie fursa hii kulithibitishia Bunge lako Tukufu, kwamba Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, itaendelea kutekeleza kikamilifu jukumu la kuisimamia na kuishauri Serikali, kupitia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ili kuhakikisha, Serikali inatimiza kikamilifu na kwa tija, mipango ya kuwaletea maendeleo Wananchi na Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nitoe shukrani za dhati kabisa kwa Mhe. George Huruma Mkuchika, (Mb) – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Selemani Said Jafo (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Naibu Mawaziri wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mhe. Josephat Sinkamba Kandege (Mb) na Mhe. George Joseph Kakunda (Mb) kwa ushirikiano wao kwa Kamati.

Vilevile, niwashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Rais, wakiongozwa na Dkt. Laurean Ndumbaro - Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, na Mhandisi Mussa Iyombe - Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, kwa namna walivyoshirikiana na Kamati katika utekelezaji wa shughuli zake. Nikiri kwamba, ushirikiano wao umesaidia sana Kamati katika kutekeleza shughuli zake.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kwa ushirikiano walionipatia katika kipindi chote cha uhai wa Kamati. Aidha, natambua na kuthamini mchango wao adhimu katika utekelezaji wa shughuli za Kamati.

Ni wazi kwamba, bila weledi na ushirikiano wao, Kamati isingetimiza kwa ufanisi shughuli zake katika kipindi chote cha uhai wake. Kwa heshima kubwa naomba niwatambue kwa majina yao kama ifuatavyo:-

1. Mhe.Jasson Samson Rweikiza, (Mb),Mwenyekiti
2. Mhe. Mwanne Ismail Mchemba(Mb),M/Mwenyekiti
3. Mhe. George Malima Lubeleje(Mb),

4. Mhe. Ruth Hiyob Mollel(Mb),
5. Mhe. Hamad Salim Maalim(Mb),
6. Mhe. Alfredina Apolinary Kahigi (Mb),
7. Mhe. Khamis Ali Vuai(Mb),
8. Mhe. Mwatum Dau Haji(Mb),
9. Mhe. Angelina Adam Malembeka(Mb),
10. Mhe. Ahmed Juma Ngwali(Mb),
11. Mhe. Khalifa Mohammed Issa(Mb)
12. Mhe. Waitara Mwita Mwikwabe (Mb),
13. Mhe. Saada Mkuya Salum (Mb),
14. Mhe. Margaret Simwanza Sitta(Mb),
15. Mhe. Esther Alexander Mahawe(Mb),
16. Mhe. Innocent Sebba Bilakwate(Mb),
17. Mhe. Zachariah Paulo Issaay (Mb),
18. Mhe. Salum Khamis Salum(Mb),
19. Mhe. Josephine Tabitha Chagula(Mb),
20. Mhe. Venance Methusela Mwamoto(Mb),
21. Mhe. Maida Hamad Abdallah (Mb),
22. Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri(Mb),
23. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu(Mb),
24. Mhe. Hamoud Abuu Jumaa(Mb),
25. Mhe. Saed Kubenea (Mb).

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai, kwa ushirikiano wake kwa Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake. Vilevile, namshukuru Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, na Ndg. Angelina Sanga, Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Kamati, kwa usimamizi mzuri wa Shughuli za Kamati, na hivyo kuiwezesha Kamati kutimiza kazi zake ipasavyo.

Mwisho lakini si kwa umuhimu wake, napenda kuwatambua na kuwashukuru Makatibu wa Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa, Ndg. Chacha Timasi Nyakega, Ndg. Victor Leonard Mhagama na Ndg. Eunike Donati Shirima, na Wasaidizi wa Kamati Ndg. Mariam Ally na Ndg. Kokuwaisa Gondo, ambao wamekuwa msaada mkubwa sana kwa Kamati katika kutekeleza shughuli zake hadi kukamilisha Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza kwa kina shughuli zilizotekelizwa na Kamati, uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli hizo, maoni na mapendekezo ya Kamati, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa liipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Jasson Samson Rweikiza, Mb

MWENYEKITI

KAMATI YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA

8 Februari, 2018

MHE. MOHAMED O. MCHENERWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante Mwenyekiti, hoja imetolewa na imeungwa mkono. (*Makofi*)

Hoja hizi tatu mtazijadili kwa pamoja jioni ya leo kwa muda huo huo, lakini leo kidogo itakuwa sio dakika 135, itakuwa dakika 90 tu. Nitawataja watakaoanza saa 11, watatu wa kwanza.

Nisome Miongozo ya Spika wa kwanza, Mwongozo wa Spika ulioombwa na Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba (Mbunge) kuhusu kutokuridhika na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa swali lake la nyongeza. Majibu hayakutolewa, ninavyofahamu yalitolewa na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje ya Nchi na Jumuiya ya Afrika Mashariki lakini nadhani tutalisahihisha hilo. Kwenye maelezo ya ndani limekaa vizuri lakini kwenye *cover* tutalisahihisha hilo maana hizi ni *permanent records* za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, katika Kikao cha Saba cha Mkutano wa Kumi cha tarehe 7 Februari, 2018 Mheshimiwa

Peter Joseph Serukamba (Mbunge) aliomba Mwongozo wa Spika, kwa kutumia Kanuni ya 46 ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba hakuridhishwa na majibu yaliyotolewa kwa swali namba 96 hususan sehemu (a) na (b) la swali hilo.

Katika Mwongozo huo Mheshimiwa Serukamba (Mbunge) pamoja na mambo mengine alieleza kuwa jawabu liliilotolewa linahusu *feasibility study* (upembuzi yakinifu) ambao sio utafiti. Mheshimiwa Serukamba (Mbunge) alieleza kuwa nanukuu; "ameulizwa tafiti anasema upembuzi yakinifu wa barabara. Upembuzi yakinifu wa barabara haujawahi kuwa utafiti, ni *process* ya kujenga barabara."

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kupokea Mwongozo huo, nilijibu kuwa nitatoa uamuzi hapo baadae. Swali la msingi namba 96 liliulizwa na Mheshimiwa Daniel Nicodemus Nsanzugwanko (Mbunge) ambaye yeye mwenyewe hakuwepo, swali lake liliulizwa na Mheshimiwa Balozi Kamala ambaye aliridhika na majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Hivyo, sio sahihi kwa Mbunge ambaye hakuuliza swali la msingi kudai kuwa majibu yaliyotolewa hayaridhishi wakati Mbunge mwenye swali ameridhika na majibu hayo.

Waheshimiwa Wabunge, hata hivyo, baada ya kupitia taarifa Rasmi za Bunge *Hansard*, nimeridhika kuwa majibu ya Naibu Waziri kwa swali namba 96 sehemu ya (a) na (b) aliyatoa kwa usahihi.

Katika majibu yake Naibu Waziri alieleza kuwa taarifa za kitafiti hususan katika hatua za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa miradi ya kikanda inayotekelezwa kwa pamoja ambayo ni Mpango wa Uendelezaji wa Mtandao wa Barabara na Reli wa Afrika Mashariki. Tafiti za kuandaa sera, mikakati na sheria pia nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zinashirikiana katiak tafiti za mbegu. Madawa ya mimea na mifugo, usalama wa chakula na udhibiti wa magonjwa ya wanyama na mimea.

Waheshimiwa Wabunge, majibu hayo yanaridhisha kulingana na swali namba 96 liliyoulizwa. Hakuna mahali popote ambapo Naibu Waziri alieleza kuhusu upembuzi yakinifu wa barabara kama ambavyo Mheshimiwa Peter Serukamba (Mbunge) alivyoeleza katika Mwongozo wake. Huo ndiyo Mwongozo wa Kiti ambaao umetolewa tarehe 8 Februari, 2018.

Mwongozo wa pili uliombwa na Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul, Mbunge wa Manyara Mjini kuhusu kutokuridhika na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa swali lake la nyongeza.

Waheshimiwa Wabunge, katika Kikao cha Saba cha Mkutano wa Kumi kilichofanyika tarehe 7 Februari, 2018 Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul (Mbunge) aliomba Mwongozo wa Spika baada ya kutorodhishwa na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa swali lake la nyongeza kutokana na majibu ya swali la msingi namba 86 la Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa.

Waheshimiwa Wabunge, bila hata kuingia kwa undani kujadili majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa swali la nyongeza la Mheshimiwa Pauline Gekul (Mbunge) naomba niwarejeshe kwenye Mwongozo wa Spika wa tarehe 13 Septemba, 2016 kuhusu maswali ya nyongeza na hapa mnisikilize. Wewe mwenye swali la msingi umeuliza unataka sasa ujibiwe, umeuliza maswali ya nyongeza.

Mwongozo wa Spika ni kwamba kiti hakiwezi kujikita kuridhisha maswali ya nyongeza ya papo kwa papo kupata majibu ya ufasaha. Ni maswali ya msingi tu ambayo kiti kinaweza kuelekeza yajibiwe tena kwa usahihi. Hivyo, ni mwongozo wa Kiti kwamba Mheshimiwa Pauline Gekul (Mbunge) kama hakuridhishwa na majibu ya Naibu Waziri Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa swali lake la nyongeza alete swali la msingi kuhusiana na suala hilo. Huo ndiyo Mwongozo wa Kiti ambaao nimeutoa leo tarehe 8 Februari, 2018. Hayo ndiyo majibu yangu kwa upande wa miongozo.

Sasa nimesema kwa leo kwa sababu ya muda tumekula sana muda wetu kwa sababu ya miongozo mizuri tu na muhimu. Tutaanza na Waheshimiwa Wabunge wafuataao, na ni dakika tano, tano, hakuna biashara nyine hapa! (*Makofi*)

Tunaanza na Mheshimiwa Taska Mbogo, atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Mollel na Mheshimiwa Daniel Edward Mtuka kwa mtiririko huo na wengine sasa watafuata. Tunafuata uwiano huo huo, watatu watakuwa CHADEMA, wawili watakuwa CUF na kumi upande wa mkono wangu wa kulia. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo nasitisha shughuli za Bunge kwa mchana huu hadi saa 11 jioni.

(Saa 07.23 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi saa 11:00 Jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae, Katibu.

NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:

HOJA ZA KAMATI

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo na
Kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2017

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria
Kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2017

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za
Mitaa Kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2017
(Majadiliano yanaendelea)

MWENYEKITI: Ahsante, niliwataja wachangiaji wetu wa kwanza lakini naambiwa Mheshimiwa Taska Mbogo ana majukumu mengine, kwa hiyo namtambua Mheshimiwa Jumanne Kishimba.

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii nichangie hoja zilizoletwa na Kamati yangu ya Katiba na Sheria na Sheria Ndogo. Naomba nianze na Kamati yangu ya Katiba na Sheria naomba nimpongeze Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa jinsi alivyoshirikiana na sisi kwenye Kamati yetu na kuweza kutuwezesha sisi kufanya kazi yetu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ila ninayo maoni machache ambayo ningeomba kuyachangia. Nilikuwa naomba Kitengo cha Maafa kilichoko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu Serikali ijaribu kukiongezea fungu ili kiweze kuwafundisha wataalam mbalimbali wa maafa mbalimbali kama vile kuogelea (*divers*). Tunayo mifano mingi sipendi kukumbushia mambo ya zamani lakini tuliwahi kupata matatizo huko nyuma meli ya MV Bukoba ilipozama ilikaa chini kule muda kama wa wiki moja nafikiri kama tungekuwa na *divers* wazuri wale watu wangeweza kuokolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba kitengo hiki kiongezewe nguvu na ikiwezekana zile sehemu zenye maziwa kama vile Ziwa Victoria, Nyasa, Tanganyika hao *divers* wawe *based* kule na pia kingeweza kufundisha wataalam wa zimamoto. Hilo ndio lilikuwa ni ombi langu kwenye Kitengo cha Maafa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo napenda niende ukurasa wa 14 wa wasilisho la Kamati ya Katiba na Sheria. Niipongeze Bodimpya ya NSSFkwanza kwa kulichukulia suala na kuwasimamisha kazi wale wote waliofanya ubadhirifu pale *NSSF*. Lakini sasa niombe hatua zaidi zichukuliwe kwa sababu kumsimamisha mtu kazi tu haitoshi na kwa sababu pia tunayo Mahakama ya Wahujumu Uchumi, Mahakama ya Mafisadi ambayo imeanzishwa lakini haina kesi, itakuwa ni vizuri kama watu hawa wakapelekwa kwenye hiyo mahakama ili iweze kujulikana kama kwamba walifanya huo ubadhirifu au hawakufanya. Na ukiangalia Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kipengele

namba 107 kinatuambia kwamba mahakama ndio mamlaka ya mwisho ya utoaji haki. Kwa hiyo, kwa kuwapeleka mahakamani haki itatendeka itajulikana kama walifanya ubadhirifu au hawakufanya huo ubadhirifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kuongelea suala la *The Law Reform Commission* ambayo iko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kamishna hii ipo lakini cha kushangaza zipo sheria nyingi nyingi ambazo zina matatizo hazibadilishwi kwa mfano Sheria ya *Traffic*, hii sheria bado ina faini za miaka ya nyuma sana ambayo iliachwa na wakoloni wetu watawala wetu. Kwa mfano, sheria hiyo ya *traffic* unaweza ukakuta mtu anagonga gari lakini anapokwenda mahakamani pale akikiri kosa faini ya mwisho ni shilingi 50,000.

Mimi nadhani hii kamisheni ingefanya kazi yake ili iweze kuzichukua zile sheria zote ambazo zina matatizo iweze kuzirekebisha kwa sababu inawezekana wakati wanazitunga zilikuwa zinafaa wakati huo kuwa na faini ya aina hiyo lakini sasa miaka mingi ilikwishapita na nchi zimeendelea na mambo yamekuja mengi. Sasa huwezi ukakaa na faini ambayo imetungwa toka mwaka 1963 bado unatoza faini hiyo hiyo. Nilikuwa naomba hiyo sheria iweze kurekebisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine hii kamisheni nilikuwa naomba ijaribu kurekebisha sheria...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante hiyo Kamishna ya kurekebisha sheria haiko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu iko chini ya Wizara ya Katiba na Sheria.

Tunaendelea Mheshimiwa Amina Mollel.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo na nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na moja kwa moja kwa sababu dakika ni chache niende kwenye kile nilichoandaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 13 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema kwamba watu wote wana haki sawa mbele ya sheria na Mtanzania ye yote hapaswi kuchukuliwa kama mhalifu mbele ya sheria mpaka atakapotiya hatiani na mamlaka husika ambayo ni mahakama. Vilevile Ibara ya 107 inasema kwamba inatambua mamlaka pekee yenye haki na wajibu wa utoaji haki ni mahakama ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimenukuu vipengele hivi na hasa nikienda katika Wizara ya Katiba na Sheria ambayo ndio inayohusika na marekebisho ya sheria mbalimbali na mimi nitazungumzia Sheria ya Usalama barabarani (*Road Traffic Act*) ambayo ni ya zamani sana ya mwaka 1968 na moja kwa moja naomba nizungumzie kero iliyopo ambayo imekuwa sasa hivi ni kero kubwa sana inayosababishwa na askari wa usalama barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyo sema Ibara hiyo ya 13 na 107 lakini niulize tu na wakati Mwenyekiti wa Kamati husika atakapokuja hapa pengine atusaidie sisi ambao kwa namna moja au nyininge mambo ya sheria siyo sana. Ni mamlaka gani hasa ambayo inamruhusu askari wa usalama barabarani pamoja na kwamba taratibu hizo zipo lakini nataka kufahamu ni sheria gani ambayo inamruhusu anaposimamisha tu gari moja kwa moja kudai leseni? Vilevile hapo hapo kuanza kuandika *notification* kutokana na vitu mbalimbali ambavyo ameviona?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano hivi sasa na hata ukiangalia katika Jiji la Dodoma hebu watusaidie ni sheria gani ambayo inamtaka dereva asimame wakati wowote anapofika kwenye *zebra crossing*. Kwa sababu ni busara tu kwamba anapofika kwenye *zebra crossing* kama kweli kuna watu ambao wanavuka pale barabara sawa

Iakini wakati mwingine hakuna hata mtu anayevuka barabara na anapopita katika eneo hilo moja kwa moja tayari askari anamsimamisha na kumwandikia faini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio hilo tu askari anapofika kitu cha kwanza anaomba leseni. Sasa mtusaidie sisi ambao hatujui sheria na Watanzania wengine wote kwamba ni sheria gani ambazo zinamfanya askari wa usalama barabarani kujichukulia sheria yeye na kuandika faini na wakati mwingine mtu anaandikiwa makosa mpaka manne, matano na hasa anapokuona kwamba kwa namna moja au nyingine wewe kidogo unauelewa wa sheria anachukulia kama ni kisasi na ndipo hapo anapoandika makosa mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano mtu anakwambia washa taa kwa mchana hivi jamani tuna haja kweli ya kuwalazimisha watu kuwasha taa na kama hiyo taa labda ina matatizo tayari moja kwa moja hapo hapo anakwandikia *notification*. Tumeona hapa kama nilivyosema hizo Ibara ya 13 na 107 vyote hivyo angalau basi mamlaka zinazohusika ndizo ambazo zinapaswa kuhakikisha kwamba makosa hayo yanafanyiwa kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa sababu sheria hizi ni za muda mrefu sana tunaomba mabadiliko ya sheria yaletwe na kama Serikali bado inaona kwamba kuna wakati mgumu au kuna kigugumizi tuombe basi mwenyekiti wa Kamati husika, kwa sababu na wao pia kwa mujibu wa sheria zinamruhusu kufanya hivyo waahirishe na kuleta kwamba vile ambavyo vinahitaji kufanyiwa marekebisho ili...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea Mheshimiwa Mtuka atafuatiwa na Mheshimiwa Kishimba.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makof*)

MHE. DANIEL E. MTUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Niende moja kwa moja kwenye hoja kwanza niwapongeze wawasilishaji wetu Wenyeviti wa Kamati zote tatu kwa maana ya sheria ndogo, huduma za jamii pamoja na katiba na sheria. Niseme kidogo kuhusu kwa nini tunatunga sheria? Tunatunga sheria kwa ajili ya kuleta utengamano katika jamii pia kulinda haki za watu wote na hasa wanyonge. Hii ni tafsiri tu ya mtu ambaye yuko mtaani sio msomi lakini kwa ujumla hiyo ndio tafsiri ya sheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Magufuli amekuwa makini sana katika kuzingatia utawala wa sheria, ni mwepesi sana. Tumeona hapa kila tunapopitisha sheria mara moja anazisaini kwa sababu anataka kwenda kuzifanya kazi ili kuendeleza huu utawala wa sheria. Pia amekuwa mkali sana Mheshimiwa Rais hasa kwenye sheria hizi ndogo, ukichelewa kutunga kanuni ninyi watu ambaa mmepewa mamlaka ya kutunga kanuni hizi Mheshimiwa Rais amekuwa mkali sana. Mmeshuhudia hivi karibuni sheria nyngi ambazo zimetungwa ambazo hazijawekewa kanuni Mheshimiwa Rais amekuwa mkali sana.

Mheshimiwa Mweyekiti, kwa utangulizi huo labda niseme tu mafupi kuhusu sheria ndogo. Nizungumzie tu umuhimu wa sheria ndogo. Sheria ngogo ni muhimu sana, ni sawasawa na sheria mama zile ambazo zinatungwa. Huwezi ku-*apply* sheria mama kama hujatunga kanuni, haiwezekani, itakuwa *dormant* ndio maana Mheshimiwa Rais amekuwa mkali kwamba tumetunga sheria hii mbona hamjaniwekea kanuni ili niweze kutekeleza sheria hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika uchambuzi wa mimi ni mmoja wa wajumbe wa Kamati hii ya Sheria Ndogo, katika uchambuzi wetu tumegundua mambo mengi sana ambayo tunesomewa hapa. Tathmini yangu karibu *asilimia* 50 ya sheria ndogo ambazo zimekuwa zikipita kwenye kamati yetu kwa kweli zina makosa. *Sample* hii naipeleka kwa nchi nzima kwa ninyi mliokasimiwa mamlaka haya ya kutunga kanuni kwa mujibu wa Ibara ya 97 naomba sana muwe makini kwa sababu mnapokuwa mnafanya makosa kwenye

utungaji wa kanuni hizi zinakwenda kujeruhi wananchi, zinakwenda kuumiza watu. Kwa mfano tumeona ushuru wa mazao, kwa mfano mzuri hapa mwezi Julai wakati Waziri wa Fedha anasoma hotuba yake ya bajeti alisema mazao ya biashara ushuru utozwe asilimia tatu na ya chakula asilimia mbili lakini kuna Halmashauri bado zinatoza mpaka asilimia tano. Hii ni mbaya sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeletewa hapa tumejaribu kuangalia tumeshauri ikiwezekana wakati mwingine wapewe adhabu hawa wanaosimamia vitengo hivi vinavyotunga hizi kanuni zinaumiza wananchi wazingatie haya maoni. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizitake tu mamlaka kwa ujumla zote Wizara zote, *agencies* zote na mamlaka zote ambao wamekasimiwa mamlaka haya ya kutunga hizi kanuni wawe makini sana. Tumeona mfano wa hiyo Sheria ya Nzega ile ya Hifadhi ya Mazingira ni ya ajabu sana, unazungumzia Ziwa Tanganyika wewe upo Nzega. Mita 60 kwamba m-preserve mita 60 msilime ndani ya mita 60 kutoka ukingo wa ziwa, hii ni mbaya sana.

Mimi ningekuwa Mheshimiwa Waziri ningekuwa nimeshampa adhabu huyo ambaye alikuwa amesimamia kutunga hii sheria ndogo, hii ni mbaya sana inaonyesha watu wanaumia sana hasa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hii *copy and paste* watu hawasomi, hizi sheria zinapita maeneo mengi sana lakini mpaka waziri analetewa kusaini kitu kama hichi ni ajabu sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache naunga mkono hoja zote tatu nashukuru sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako. Mheshimiwa Jumanne Kishimba atafuatiwa na Mheshimiwa Mwanne Mchemba.

MHE JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nitaenda moja kwa moja kwenye Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri yangu ilipata hati safi kwenye ukaguzi wa *CAG* vile vile kwenye mwenge tulikuwa washindi wa pili au wa tatu. Lakini kitu cha kushangaza ripoti ya Mkaguzi wa Ndani wa Halmashauri inaonyesha tuna upotevu wa zaidi ya milioni 200 na zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa najaribu kujuliza hapa kwamba inawezekanaje tuna hati safi kwenye mwenge tumekuwa wa pili au wa tatu lakini mkaguzi wa ndani kwenye ripoti ambayo ninayo hapa anaonyesha tuna upotevu wa zaidi ya milioni 200 na zaidi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi Mkurugenzi wetu wa Halmashauri ameendelea kuwaburuza Madiwani kwa kutumia ubabe kiasi ambacho ameweza kuidhinisha ujenzi wa jengo la mamalishe lenye thamani ya shilingi milioni 200. Jengo hili kwa gharama ya shilingi milioni 200 lina mapato ya shilingi 120,000 kwa mwezi. Kwa hiyo faida ya kurudisha jengo hili litachukua zaidi ya miaka 200. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa namwomba waziri atakapokuwa anafanya majumuisho ajaribu kuangalia kama Serikali inakopa pesa, pesa hizo hizo milioni 200 ilizokopa kwenye mabenki ya ndani kwa riba ya asilimia kumi yenye we italipa milioni 20. Ni vipi imeipatia Halmashauri ikajenga jengo la milioni mia mbili itapata *return* baada ya miaka 200 na itapata shilingi milioni 1.4 kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha ubadhirifu huo unaoendelea kwa hao watu wanaitwa wateule wa Rais, Mkurugenzi huyu mpaka leo amekataa kutoa *statement* za benki, Mkuu wa Wilaya hawezi kumhoji, TAKUKURU hawezi kumhoji, Mkuu wa Mkoa hawezi hata sisi kamati ya fedha amekataa na kichekesho hapa ninapoongea anaendelea kupiga machinga wote wa Kahama. Namshukuru Mkuu wa Polisi amekataa kutoa polisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mji wetu wa Kahama watu walioajiriwa hawafiki watu 200, na mji ule una watu zaidi ya laki tano, ni kweli watu hawa watafanya shughuli gani? Hata hivyo Mheshimiwa Rais alisharuhusu machinga na watu wa kawaida waendelee na shughuli zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri Jafo wakati anafanya majumuisho ajaribu kutueleza tutafanya nini au tushitaki wapi sisi? Maana hatuna sehemu yoyote ambayo tunaweza kulalamikia. (*Makofi*)

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Enhee, nani taarifa? Subiri kidogo Mheshimiwa Kishimba.

TAARIFA

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, *wabheja* (ahsante) sana.

Nilitaka nimpe taarifa kaka yangu Mheshimiwa Kishimba, Baraza la Madiwani lina nguvu na wajibu pale ambapo Mheshimiwa Kishimba na wewe ni Mjumbe katika Baraza hilo, mnao uwezo wa kujigeuza kama Kamati. Nilitaka nikusaidie kwa sababu taarifa hizi za Mkurugenzi kuwa mbabe juu ya kuwapiga machinga na akinamama wanaofanya biashara Kahama ninazo.

Kwa hiyo, nilikuwa nakuomba nikupe taarifa kuwa toa ombi kwa Mheshimiwa Jafo, jambo hili ni la dharura, ili aweze kufika Kahama hata Jumamosi ashughulikie jambo hili linakera watu, *wabheja* (ahsante) sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kishimba.

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naipokea hoja yako vizuri nafikiri Mheshimiwa Jafo uko hapo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli sisi ni Wabunge, lakini mtu ambaye anasema ye ye ni mteule anapojaribu kuwa-*disturb* watu waliokupigia kura yanatupa sisi wakati mgumu sana. Tunajaribu kila namna kutafuta pesa kutoka kila kona, ili tusaidie watu wetu, lakini mtu anafika anakataa au ana-*misure* hizi pesa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tuna ongezeko la wanafunzi kwenye kidato cha kwanza zaidi ya asilimia 200; kwenye darasa la kwanza tuna ongezeko la asilimia 200 pia, tuna upungufu wa matundu 2,000 ya choo, lakini Mkurugenzi huyu amechukua pesa hizo milioni 200 amepeleka kwenye jengo la mama lishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hivi ninavyoongea Mheshimiwa Jafo ulipokuwa Naibu Waziri ultioa agizo kwamba, wakati Wabunge wako Bungeni Kamati za Fedha zisikae, lakini ye ye anaitisha Kamati ya Fedha kesho, ameongeza shilingi milioni 40 tena kupeleka kwenye jengo hili kwa ajili ya kuweka vigae. Kwa hiyo, naomba sana mtusaidie maeneo haya ni maeneo ambayo yanatupa matatizo makubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia tu naomba Mheshimiwa Jafo na Mheshimiwa Kakunda kwa kuwa mlifika Kahama mtufikirie sana suala letu la Manispaa. Ni kweli mji wetu umekua, mmeuona kwa macho na matatizo tuliyonayo. Mkitusaidia Manispaa itatusaidia vile vile kwa tatizo la barabara ambalo kwa sasa ni tatizo letu kubwa. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Mwanne Nchemba atafuatiwa na Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub.

MHE. MWANNE J. MCHEMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hotuba zote mbili za kamati tatu, lakini nijikite kwanza kwenye Kamati yangu ya Utawala na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa iliyotolewa na Kamati yangu ni sahihi na ninaipongeza na ninaunga mkono.

Kazi yangu leo sasa hivi hapa ni kuiboresha tu au kukazia yale ambayo yamo kwenye taarifa yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende haraka haraka, hivi karibuni Kamati yangu ilikwenda ziara Mkao wa Iringa, lakini niiombe Serikali, miradi mingi ambayo ilianzishwa na Serikali kwa miaka iliyopita ikamilishwe kwa haraka iwezekanavyo. Kwa mfano tulipokwenda Iringa kwenye Wilaya ya Kilolo tulikuta kuna mradi mkubwa sana wa Serikali amba o pesa zake nyingi zimetumika, lakini kwa bahati mbaya pesa iliyobaki ni kidogo, lakini Serikali haijatoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nizungumzie tu hivi, Hospitali ile ya Wilaya Mheshimiwa Jafo anajua jinsi ilivyaoanza, ni hospitali ya mfano, ina maghorofa manne, inajengwa kwa shilingi bilioni 4.4; ndiyo gharama ya ujenzi na inasimamiwa na TBA, lakini ukiangalia jinsi inavyosuasua inasikitisha, kwa sababu sisi kama Kamati tulisema hivi, ile hopsitali iwe ya mfano kwa nchi nzima. Hii ni kwa sababu kuna makadirio mengine ambayo ni ya hospitali hizo za Wilaya zinatumia zaidi ya shilingi bilioni 10 na 15, lakini hawa niwapongeze sana Halmashauri ya Kilolo kwa kazi nzuri waliyoifanya. Kamati zote zimeenda, watu wa Hazina wameenda, Hazina Makao Makuu wameenda, Hazina Mkao wameenda, wamethibitisha kwamba yale majengo yako vizuri na gharama yake inaridhisha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niiombe Serikali na najua Serikali ina azma nzuri na ina matarajio mazuri ya kuhakikisha wananchi hawapati tabu kwenye huduma ya afya, lakini niiombe Serikali ihakikishe inapeleka pesa haraka sana za wakandarasi, imeathiri. Eneo lile hospitali ile kama ingekamilika ingehudumia wananchi wengi sana ukizingatia na jiografia ya Iringa ilivyo kwa kweli, wananchi wanateseka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine ambalo tulikuwa tumeomba kwenye Kamati yetu ni kwamba Wizara ya TAMISEMI itusaidie kutoa waraka wa ujenzi amba o utazingatia mazingira magumu au utazingatia walemavu/mahitaji maalum. Kwa sababu kuna maeneo mengi

wanajenga majengo ya Serikali lakini kwa bahati mbaya hawazingatii mahitaji maalum. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ambalo mimi nimeliona pia ni kwamba, wanapojenga nyumba, madarasa wanapojenga hawazingatii kutoa waraka wa sera ambayo itasaidia ujenzi wa matundu ya vyoo. Sasa hivi wanaongeza kujenga madarasa, lakini matundu ya vyoo hayapo, ujenzi wa nyumba za walimu haupo, ujenzi wa nyumba za madaktari haupo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba sana, namuomba Mheshimiwa Jafo, ni msikivu na Serikali yangu ya Awamu ya Tano ni sikivu, itusaidie kwa hilo ili angalao tuweze kwenda sambamba na mahitaji ya Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nilikuwa nataka nimuombe Mheshimiwa Mkuchika Waziri wangu, samahani nakutaja jina lakini Waziri wa Utumishi, nafasi ambazo ziko wazi baada ya uhakiki wa vyeti *fake* kwa kweli Serikali ingeangalia upya, ili iangalie namna ya kujaza hizo nafasi upande wa madaktari, upande wa walimu, hakuna kinachofanya kwa sasa hali ni ngumu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningeiomba Serikali iangalie jinsi ya kuweza kuhakikisha kwamba, *EGA* badala ya kuwa wakala awe na mamlaka kamili ili kuhakiki takwimu za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka kuomba pia kuhusu *TARURA*, kwa sababu tunaenda haraka haraka. *TARURA* sasa hivi inafanya kazi nzuri, lakini inafanya kazi kwa kusuasua.

Nilikuwa naishauri, kama walivyosema Kamati yangu, kwamba sasa ipewe 50 kwa 50, *TANROADS* wapate 50 na *TARURA* wapate 50 kwa sababu, barabara za vijijini zimeharibika sana na Kamati yangu inakwenda mpaka vijijini barabara hazifai, madaraja hayafai, masika hii hakuna njia...

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, hotuba zote. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Jaku atafuatiwa na Mheshimiwa Alfredina Kahigi.

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nisikupotезee muda, mimi nitahitaji maelezo maana nikichangia itachukua muda mrefu, nitahitaji maelezo kwenye mambo kama manne Mheshimiwa Waziri. Nikupongeze tu juzi nilikuona katika sherehe za Siku ya Sheria Duniani na ulihimiza sana Mheshimiwa Waziri, mahabusu sheria ya kesi zao zile haraka, hebu tueleze kuna tatizo gani Arusha kule watu wana miaka sita mpaka leo wanachunguzwa nini? Kesi mpaka leo au kunatakiwa ushahidi wa Kinyamwezi mpaka ukamilike? Watu wanateseka, wana familia zao, wana watoto, wengine wanataka kuthubutu kuachwa, hebu tueleze tatizo ni nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kumejitokeza tatizo hivi sasa Zanzibar watu kuchukuliwa wakaja kushitakiwa huku Bara, je, Zanzibar hawana Mahakama? Hawana wanasheria? Tatizo gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, na sheria inavyosema unapokamatwa ndipo unapohukumiwa. Leo sijaona mimi mtu kakamatwa Pakistan akaletwa Tanzania, kakamatwa Mascut akaletwa huku, hebu tueleze utaratibu gani wa sheria huu, ukoje? Mimi si mtaalamu wa sheria, lakini haya mambo yanajitokeza sasa hivi na yanazidi kuendelea, keshokutwa usije ukanichukua mimi ukanileta huku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini na lingine nikuombe, hebu katika hiyo orodha ya mambo ya Muungano, na hii Mheshimiwa Chenge ulikitunga wewe kitabu hiki ukiwa Mwanasheria mwaka 2005. Kuna orodha hii ya mafuta na gesi, mali pamoja na mafuta yasiyochujwa na matokeo ya mafuta aina ya petroli na aina nyingine ya mafuta, limo humu

na sheria hii ilivyoelezwa, angalia Ibara ya 64 Mwanasheria Mkuu na Waziri wa Katiba na Sheria; "*Endapo sheria yoyote iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi inahusu jambo lolote katika Tanzania Zanzibar ambalo liko chini ya mamlaka ya Bunge, sheria hiyo itakuwa ni batili na itatanguka na pia endapo sheria yoyote itakayotungwa na Bunge inahusu jambo lolote ambalo liko chini ya mamlaka ya Baraza la Wawakilishi, sheria hiyo itakuwa ni batili na itatanguka.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ni vichekesho, kwa hiyo bado tuna mtihani wa mafuta Zanzibar. Pamoja na jitihada zilizochukuliwa, niwapongeze Marais wote wawili, lakini bado, na ulijibu hapa, ulimjibu Mheshimiwa Juma Ngwali kuwa bado mafuta ni tatizo. Hebu lipate kuliondoa ili Muungano ulete sura nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na llingine, mara nyingi waislamu wamekuwa wakiahidiwa Mahakama ya Kadhi humu ndani hebu tueleze imefikia wapi? Hata katika Katiba Iliyopendekezwa na wewe ulikuwa ni Mjumbe katika Tume ya Warioba, hebu tuelezeni juu ya Mahakama ya Kadhi nayo ina mambo matatu, ndoa, mirathi na talaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wamekuwa wakilalamikia suala hili, na hili Bunge hili ukifuata *Hansard* limezungumza ndani wakati wa Mheshimiwa Mizengo Pinda kuwa, utaratibu fulani utaletwa, lakini mpaka leo? Imekuwa kama mtoto wa kuku anayetaka kunyonya, kesho, keshokutwa mpaka anakuwa kuku, maziwa hayaoni. Hebu tuelezeni lini utaratibu huu utaletwa wa Mahakama ya Kadhi? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Waziri ulikuwa Mjumbe katika Tume ya Warioba na waislamu wengi walizungumzia suala hili. Kuna mambo ya ndoa, talaka na kuna mambo ya mirathi, hebu tuendelee na utaratibu wa kulieleza suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nisikupotezee muda. Naomba nafasi hii umpe mtu mwengine achangie dakika zilizobaki. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Alfredina Kahigi atafuatiwa na Mheshimiwa Vedasto Ngombale.

MHE. ALFREDINA A. KAHIGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuongea machache. Mimi nitazungumzia kuhusu mambo ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyekiti wangu Profesa Ibrahim Lipumba, mchumi duniani pamoja na baraza lake, naahidi sitamuangusha Mheshimiwa Lipumba. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu, katika Kamati yetu ambayo tumekaa kuna Wilaya 64 ambazo zinakosa Hospitali za Wilaya, mojawapo ni Wilaya yangu ya Bukoba Vijiji hatuna Hospitali ya Wilaya.

MBUNGE FULANI: Unasoma eeh?

MBUNGE FULANI: Hospitali ya Wilaya!

MHE. ALFREDINA A. KAHIGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Bukoba Vijiji...

MBUNGE FULANI: Hakuna anaposoma.

MHE. ALFREDINA A. KAHIGI: Hao waache tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Bukoba hawana hospitali ya wilaya, wanatembea mwendo mrefu au wanalipa gharama za kwenda kutafuta matibabu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo gharama ambazo wanalipa wanakuwa hawakuzipanga kusudi waweze kwenda kutibiwa huko. Kama wangekuwa na hospitali katika wilaya yao wasingepata usumbufu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iwaangalie kwa jicho la huruma iwajengee Hospitali ya Wilaya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Wilaya ya miaka mingi sana. Wilaya ya Bukoba ni Wilaya ya miaka mingi sana, Wilaya zote ambazo ziko katika mkoa wetu zimetokana na Wilaya hiyo, lakini yenyewe haina hospitali. Watu wengine kwa kukosa hela za kwenda kwenye hospitali za *private* wanakunywa dawa za mitishamba ambazo hazina vipimo vyovoyote, wengine wanakufa, naomba Serikali iliangalie. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini namshukuru Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo, lazima nimseme jina, pamoja na Naibu wake na wataalam wao, ni watu wenye moyo mkunjufu. Hili suala tumeliongelea na wameliona na wameahidi kutusaidia katika bajeti hii ambayo tutakaa waweze kutuweka katika *list* hiyo, nawashukuru sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka huko, kwa kuwa, dakika ni kidogo niizungumzie Ofisi ya Utumishi. Ninamuunga mkono Rais wangu Profesa...

(Hapa baadhi ya Wabunge walishangilia)

MHE. ALFREDINA A. KAHIGI: Ninamuunga mkono Rais wangu Mheshimiwa Dkt. Magufuli, kazi aliyofanya siidharau ya kutumbua, kazi ya kutumbua na iwe endelevu, ni kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo ninawasikitikia madereva ambao walitumbuliwa. Madereva mimi najua ujuzi wao, leseni zao, kama wanajua kusoma na kuandika, hivyo ndivyo vinavyowafanya wawe na kazi lakini maskini ya Mungu wametumbuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara hiyo iwaangalie sana watakaokuwa wanaajriwa wawaangalie wasiwe wanawafukuza. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache naunga mkono hoja. Ahsante. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante, haya, tunaendelea, Waheshimiwa ninaomba utulivu Bungeni. Mheshimiwa Vedasto Ngombale, atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Mmasi. Ngombale hayupo eee? Mheshimiwa Ester Mmasi.

MHE. ESTER M. MMASI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia mchango wangu mdogo kulingana na uwasilishwaji wa Taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo, lakini pia na uwasilishwaji wa Kamati ya Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaenda mbali napenda kuipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu chini ya uongozi wa Mheshimiwa Jenista Mhagama pamoja na Mheshimiwa Mavunde kwa kazi yao nzuri ya kuweza kufanya majukumu yao yakawa na tija hata kwa sisi Wanakamati wa Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wajumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo tulikuwa na malalamiko mengi ya muda mrefu. Na malalamiko yetu yalikuwa ni Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina furaha ya pekee kusimama katika Bunge lako hili Tukufu kutoa pongezi za dhati kwa Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kweli wameutendea haki mhimili huu wa sheria. Ninaomba jambo moja lifanyike. Ni dhahiri kwamba tumempata Mpiga Chapa wa Serikali ambaye anakaimu kwa nafasi yake, Bwana Kaswalala. Bwana Kaswalala amefanya mambo mengi, ameleta *reforms* nyingi, ametengeneza *retention strategies*, lakini ameleta mabadiliko kwa muda mfupi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bwana Kaswalala mpaka leo anakaimu. Hata hivyo pamoja na suala hili la kukaimu ambalo tumeona kimantiki halileti tija kwa mtu ambaye tunamuona ana uwezo katika nafasi hii tukashindwa *kum-*confirm**. Kwa hiyo, ni ombi langu kwa Wizara hii, ni ombi langu kwa Ofisi hii tuweze *kum-*confirm** Bwana Kaswalala kwa sababu ukiangalia Sheria za Utumishi wa Umma *provision*

ni *three months* tofauti na hapo mtu ame-*qualify* tunampa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la mitambo mibovu kwa Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali. Tukipata mitambo imara ndio namna pekee ya kuweza kutunza siri na kuhifadi nyaraka za Serikali. Tunaiomba ofisi husika iweze kumsaidia Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali ili aweze kujikimu kupitia mitambo ya kisasa na aweze kufanya kazi ambayo sisi tunamuagiza kama Bunge Tukufu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo masuala ambayo mimi ninapenda nyaongelee. Kuna suala la ucheleweshwaji wa utungaji wa sheria ndogo. Juzi Mheshimiwa Kemilembwe wakati ana-*wind up report* yake, lakini pia hata leo nafikiri nimemsikia Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mazingira, ali-*cite* Sheria ya Wanyamaporii ya mwaka 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi linanisikitisha sana. Sheria ya Wanyamaporii ya mwaka 2009 mpaka leo hatuna kanuni ndogo zinazoongelea ushoroba. Ninapoongelea kutokuwepo kwa kanuni ndogo tayari ni mzigo mkubwa kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe takwimu zifuatazo, kutokuwepo kwa utungaji wa Sheria hii Ndogo ya Masuala ya Ushoroba imeleta madhara yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka mmoja kuanzia mwaka wa jana mwezi wa kwanza mpaka mwaka huu tumekuwa na vifo vya Watanzania 484 kwa nchi ya Tanzania, lakini pia tumekuwa na hasara hekta 42,000 kwa nchi ya Tanzania ambayo inaitaka Wizara ilipe fidia ya shilingi bilioni moja kwa madhaifu haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi sote ni Wabunge, tukiwa Bungeni hapa tulisikia tembo wamekatisha, anapita anaenda *UDOM*. Ninajiliza tunahitaji nini? Je, tembo hawa waingie hapa ndani ndipo tujue madhara yanayotokana na sheria hii? Inasikitisha sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapoongelea ucheleweshaji wa utungaji wa sheria hii, mamlaka inayohusika na masuala mazima mipango miji imeshindwa kuzingatia taratibu na hatimaye hizi *corridor* za wanyama zimekuwa zikitumika na kubalishwa matumizi, na hata leo hii tunakuwa na majengo makubwa.

Mimi ninaomba serikali tujifunze kwenye ujenzi wa Jengo la *TANESCO*. Tumejenga kwa *billions of money*, pesa za Watanzania baada ya siku mbili tunashusha ghorofa. Tujifunze kwenye hili ni lazima tuweze kutunga sheria hizi ili tuweze kuondokana na mizigo isyo ya lazima kwa serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitapenda niongelee suala zima la ushiriki wa wanakamati kwenye masuala ya kuisimamia serikali yetu. Ukitosha Ibara ya 63(2) inasema; "*Bunge itakuwa ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka, kwa niaba ya wananchi, kusimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaombe kwa masikitiko makubwa, Kamati yangu ikiwa tulipata safari ndefu tukasafiri kwa muda mrefu nafikiri ilikuwa safari haikuzidi dakika kumi kwa sababu tulikoka jengo la Bunge hapa tukaenda pale Sabasaba nakumbuka...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. ESTER M. MMASI: Mheshimia Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa na ninaomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Haya, tunaendelea, Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, atafuatiwa na Mheshimiwa Ruth Mollel.

MHE.KHALIFA MOHAMED ISSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu pia kwa kunijalia kupata fursa hii ili kuchangia hoja tatu hizi zilizoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mjumbe wa Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa. Kwa sababu ya muda nitaomba nijikite katika taarifa hii/katika hoja hii ya Kamati yangu na nitakwenda kidogo tu kuchangia habari ya Mfuko Maalum huu wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfuko huu wa *TASAF* hapana ubishi kwamba umewakomboa wanyonge wengi kwa Serikali ya Muungano pamoja na Serikali ya Zanzibar. Mfuko huu umesababisha kuwapatia wale watu wa Kaya ya masikini walau milo yao mitatu kwa siku, lakini pia imeweza watoto kwenda shule, lakini pia kwenda *clinic*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata katika ripoti yetu katika kamati yetu imekuwa ikieleza mara kwa mara kwamba Zanzibar mfuko huu umekuwa ukifanya vizuri kuliko hata Tanzania Bara. Na kama Wajumbe sisi tulipata fursa mara nyingi tu kutembelea sehemu mbalimbali na mashuhuda wakawa wametoa ushahidi kuonekana kwamba mfuko huu umewasaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kidogo ambalo ni dosari na nilitaka Mheshimiwa Waziri wetu aweze kulijua, kwamba Zanzibar mfuko huu upo, lakini ni kama vile makao makuu unapeleka pesa kule lakini hawafuatilii utelekezaji wake mzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tulipata fursa ya kutembelea Shehia moja ya Kilindi iliyoko Wilaya ya Chake Chake, Mkoa wa Kusini Pemba. Pale wananchi wenyewe waliibua mradi wa kuzuia maji ya bahari yasiingie katika mashamba yao na mradi ule ukakubaliwa na ukatengewa pesa za kutosha. Hata hivyo jambo la kusikitisha na haitakiwi maana si lazima uwe mchunguzi wa kada ya *CAG* ndipo

uweze kuweza kujua *value for money* pale. Tuta lile lilikuwa na urefu wa mita 125; lakini tuliambiwa limejengwa kwa shilingi milioni 47. Kwa hesabu za haraka haraka unaweza kuona kila mita moja, basi imejengwa kwa zaidi ya shilingi 350,000. Sasa hapo unaweza kuona tu kama *value for money* haiwezi kupatikana hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiondoka hapo, sisi kama Wabunge, mimi kwa bahati nzuri pia katika shehia yangu ambayo imo katika jimbo langu na ndiyo shehia mimi mwenyewe naishi hapo kuna mradi kama huo wa tuta la kuzuia maji ya bahari yasiingie katika makonde/mashamba ya watu, lakini mimi kama Mbunge sijawahi kushirikishwa wala kuambiwa kama kuna mradi kama huo. Kwa hiyo, tungeomba walau na sisi tukapata fursa ya kushirikishwa tukajua miradi ambayo ipo katika shehia zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine ambalo limenikwaza sana, kama nilivyosema mwanzo miradi hii ikifika Zanzibar labda haina uangalizi mzuri. Tulikwenda tukatembelea ujenzi wa shule ya sekondari Muyuni mwaka jana. Shule ile ilijengwa hafla sana na takribani kwa zaidi shilingi 120, lakini...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako, tunaendelea Mheshimiwa Ruth Mollel atafuatiwa na Mheshimiwa Zacharia Issaay.

MHE. RUTH H. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii yakuchangia kwenye hoja iliyoko mezani. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Utawala Bora na Serikali za Mitaa na naunga mkono hoja ambayo imewasilisha hapo mezani na ninawapongeza wote ambao wamewasilisha hoja zao hapa mezani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitajikita katika maeneo mawili. Katika lile zoezi la vyeti *fake* kuna watumishi

kama 11,696 ambao walitolewa kazini na kati ya hao 3,301 wametoka Serikali za Mitaa. Kwa sababu hiyo sasa upungufu wa watumishi katika Serikali za Mitaa umeruka kuanzia asilimia 51 mpaka asilimia 54 ambayo ni karibu watumishi 57,700.

Sasa ningependa kujua Mheshimiwa Waziri wa Utumishi kuna mkakati gani wa kuhakikisha kwamba serikali za mitaa zinapata watumishi ili kupunguza matatizo katika yale maeneo ya *social services*? Hilo la kwanza,

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, pia tungependa kujua nini hatima ya hawa watu ambao wamekutwa na vyeti *fake*? Najua kweli wamevunja sheria lakini wengine wamekutwa na haya maswahibu karibu wanastaafu na wameitumikia nchi hii kwa muda wote. Je, nini hatma yao? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili linahusu wale walitolewa waliomaliza darasa la saba ambao alishindwa kuendelea mpaka *form four*, kwa utaratibu wa kawaida hawa watakuwa wamestaafishwa. Tungependa kujua, je, serikali ina mpango wa kuwalipa mafao yao kwa sababu wamestaafishwa? Naomba Mheshimiwa Waziri akija atueleze nini hatma ya watumishi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni la mabasi ya mwendo kasi. Serikali imeanzisha huu mradi ambao ni mzuri ilianza vizuri, na lakini sasa hivi hali si nzuri. Si nzuri kwa sababu mabasi yanakuwa machache wakati wa *peak hours* watu wanaskumana kugombe ndani ya basi; na lengo la huu mradi liliikuwa ni kufanya usafiri uwe rahisi maana yake kama tunafuata kweli *rappid transport* kama ilivyo katik anchi za wenzenetu basi hilo haliwezi kukaa muda mpaka lijae kama daladala. Inatakiwa watu wasafiri wakiingia hao hao walioingia wanaondoka linakuja basi lingine, linakuja basi lingine. Lakini mpaka sasa hivi huduma zimedorora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungependa kujua Serikali ina mkakati gani katika kuboresha huo usafiri wa mabasi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, inahusu karakana ya haya mabasi ya mwendo kasi. Inashangaza kwamba Serikali imewavunja wananchi waliokuwa kwenye Mto Msimbazi, nyumba zao zikavunjwa. Hata hivyo ajabu ni Serikali yenewe inajenga karakana ya mwendo kasi katika Mto Msimbazi. Mafuriko yalipokuja mwaka 2017/2018 lile eneo lilifurika, zile ofisi zilifurika maji mabasi yalikuwa kule ndani, vyombo vikaharibika mabasi yakaharibika na kuisabisha Serikali hasara kubwa. Je, Serikali itakuwa na mpango gani sasa kuona kwamba hatua zinachukulia ili kuepusha tena majanga mengine mvua nydingi zitakaponyesha katika lile eneo la Bonde la Msimbazi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *ten percent* katika Halmashauri zetu. Halmashauri nydingine zimekuwa zinafanya vizuri. Lakini Halmashauri zingine zilikuwa hazitengi ile asilimia 10 inayotakwa kwa ajili ya wanawakena vijana maeneo mengine wamefanya vizuri, maeneo mengine hawajafanya vizuri. Tunapendekeza, kama ilivyosemwa katika taarifa yetu, kwamba ingekuja sheria ambayo italazimisha Halmashauri ziweze kutenga hiyo asilimia 10 ya vijana na wanawake ili wananchi waweze kujiweka katika makundi na kuchangia katika uchangia katika maendeleo yao.

T A A R I F A

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mollel; hebu kaa kidogo.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante nilikuwa napenda tu kumpa taarifa dada yangu kwamba katika hiyo asilimia 10 hivi sasa ni asilimia nne kwa wanawake, asilimia nne kwa vijana na asilimia mbili kwa watu wenye.

Kwa hiyo nafahamisha Wabunge wote kwamba ni hivyo na si asilimia tano kwa wanawake na asilimia tano kwa vijana. Kundi la watu wenye ulemavu ni asilimia mbili sasa, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Mollel malizia.

MHE. RUTH H. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nne na nne jumlisha na mbili ni kumi, ahsante.

MWENYEKITI: Tunaendelea, Mheshimiwa Zakaria atafuatiwa na Mheshimiwa Omary Mgumba.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Naomba nichukue nafasi hii kwanza kuipongeza Serikali Baraza la Mawaziri na wataendaji wote Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina mambo machache, kama ambavyo waheshimiwa wajumbe wenzangu wamezungumza kuhusu Wakala huyu wa Barabara Vijijini, naomba Serikali katika bajeti inayokuja ije na utaratibu wa kubadilisha hizi sheria za mgao wa fedha kwenye Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi za *TARURA* hazitoshi zilizokua zinatolewa. Kama ambavyo tunaona kwenye Wilaya tulizotokana na Halmashauri tulizotoka daraja la korongo moja halitoshi kwa fedha ambayo anapewa *TARURA*, sasa kwa kuwa maeneo ya vijijini yamekuwa na ongezeko kubwa na vyombo vya usafiri na mahitaji makubwa ya mtandao wa barabara tungeomba basi Wizara yetu na hata Serikali waone umuhimu wa eneo hili la wakala huyu *TARURA* kuongezewa fedha za mfuko wa barabara zinazomilikuwa na Serikali za Mitaa maeneo ya mijini na vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni eneo la ahadi za Rais. Mheshimiwa Rais sasa tuna miaka miwili na zaidi tangu uchaguzi mkuu umepita. Alihaidi ahadi nyingi za bara bara katika maeneo mengi ya vijijini. Kwa mfano katika jimbo langu la Mbulu Mjini alihaidi barabara ambayo haipo kwenye mtandao wa *TANROADS*. Sisi Wilaya tukasubiri *TANROADS* atakuja kutekeleza hiyo ahadi ya kilometra tano ya lami. Kumbe barabara alizoahidi sasa hivi mmiliki na msimamizi na mtekelezaji ni *TARURA*. Kwa hiyo, nimuombi Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI akija wakati anatoa

mrejesho aone umuhimu wa kuona barabara zile ambazo zimeahidiwa na Mheshimiwa Rais kwenye mtandao wa barabara ambao *TARURA* atahudumia kwenye bajeti hiituanze utekelezaji wake, kwa maana ya kuzitengea fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ajira, Serikali ilikuwa na nia njema ya kutaka kuajiri pengine nafasi kama 50,000 hivi katika mwaka wetu huu ambao umebaki miezi minne. Basi hata kabla ya mwaka huu kuisha tuone ni namna gani nafasi kadhaa zitaajiriwa ili kupunguza hii *gap* kubwa ya mahitaji makubwa ya ajira. Tuna nafasi nyingi kwenye Serikali za Mitaa hasa za Watendaji wa Vijiji, Watendaji wa Kata, walini na wapishi na watu mbalimbali ambao ni kada mbalimbali katika nafasi za ajira. Kwa hiyo, nafasi hizi zingeajiriwa hata sehemu ili kupunguza ukubwa wa tatizo hili kama illivyo sasa hivi na hali hii itasaldia ni kwa namna gani walau tunapata watu ambao watakuwa watenda kazi katika Mamlaka za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la upelekaji wa fedha za mradi ya maendeleo. Nilikuwa namuuliza Mkurugenzi wa kwetu, fedha hadi sasa kiasi kilichopelekwa ni kidogo sana nilikuwa naomba basi fedha za mradi ya maendeleo hata kwa hii robo iliyobaki ipelekwe kwa kiasi kizuri ili kupunguza hali hii ya ukosefu wa fedha za miradi ya maendeleo kwenye ngazi za Halmashauri. Kwa sasa tuna mahitaji ya miradi ambayo tumeahidi kwa wananchi lakini bado hatujapata nafasi ya kupeleka fedha kwa kiasi kizuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa sekta ya miundombini kwa ajili ya ujenzi holela mijini, katika Kamati yetu tulikuwa tumependekeza Serikali ione umuhimu wa kuandika waraka kwa Serikali za Mitaa kwenye Halmashauri ili na wale Maafisa Mipango Miji na Wakurugenzi wadhibiti ujenzi holelea unaoendelea kwenye maeneo ya miji yetu ili kuepuka gharama kubwa ya uvunjaji wa majengo hapo baadaye. Kwa vyovoyote vile nimuombe Mheshimiwa Waziri, nampongeza sana Mheshimiwa Jafo, Wakurugenzi wanapokuja kwenye Kamati yetu safari hii waje na utaratibu

wa kiasi gani walitoa fedha za asilimia 10 ya akina mama kwa mwaka huu wa fedha ili tuone ni kwa namna gani jambo hilitunalozungumza muda mrefu limetekelezwa kwa kiasi na linaweza kuwa na dira nzuri katika utekelezaji ule wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mahakama, tumekuwa na mahitai makubwa ya mahakama, tumekuwa na hali ngumu ya wananchi kufuata huduma ya mahakama mbali. Tutafute ni namna gani walau kwene tarafa tunakuwa na mahakama, kwa hivi sasa zinaemewa zaidi ya kilomita kama 50... (*Makofi*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako Mheshimiwa Omari Mgumba atafuatiwa na Mheshimiwa Haonga.

MHE. LEAH J. KOMANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti naonge kwa niaba ya Omari Mgumba, nitachukua nafasi yake, nakushukuru.

MWENYEKITI: Unasemaje?

MHE. LEAH J. KOMANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naomba niongelee mwenendo wa maduhuli katika Halmashauri zetu. Ni dhahiri kwamba Halmashauri za Wilaya, ufanisi katika ukusanyaji wa mapato umekuwa wa kusuasua, Halmashauri katika mikakati yake ya kukusanya mapato imekuwa ikionesha lakini changamoto wanayoipata ni kutokuwa na sheria ndogo na sababu ya kutokuwa na sheria ndogo wamekuwa wakisema kwamba sheria zinacheleweshwa kusainiwa TAMISEMI. Hivyo nitoe wito TAMISEMI iwashe kusaini sheria ndogo ili ufanisi wa mapato uongezeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilifuta baadhi vyanzo vya mapato ambazo vilikuwa kero katika bajeti ya mwaka

2017/2018 na ninaamini Halmashauri pamoja na Serikali Kuu zilifanya mapitio katika bajeti zao. Lakini cha kusikitisha Halmashauri zinaendelea kutoza mapato kwa vyanzo vilivyofutwa. Kwa mfano Halmashauri hiyo hiyo ina ushuru wa pamba imepunguza asilimia mbili, kwa hiyo inatoza asilimia tatu, lakini Halmashauri hiyo hiyo inaendelea kutoza chanzo kilichofutwa kwa mfano kusafirisha mifugo ndani ya Wilaya. Ukumuuliza mkurugenzi kwa nini anafanya *double standard* anasema hana mwongozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Mkurugenzi asitumie kigezo alichotumia kuteremsha ushuru wa pamba akatumia hicho hicho kigezo kutoza ushuru wa kusafirisha mifugo. Hapa tunawaonea wananchi wetu na tunawaweka katika matabaka. Kwa hiyo ninaomba Wizara husika ilete miongozo ili halmashauri ziweze kurekebisha sheria ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.
(Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Pascal Haonga atafuatiwa na Mheshimiwa Musukuma.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na mimi niweze kuchangia, lakini naomba niseme kwamba nitachangia hii kamati Utawala na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita sana kwenye suala la utawala bora. Taifa letu kwa mara ya kwanza tumeshuhudia kwamba hakuna Utawala Bora katika Taifa letu. Wapo viongozi walipandishwa vyeo baada ya kutuhumia na rushwa, kwa mfano aliye kuwa DC pale Arumeru na leo ni RC Mkoa wa Manyara, amepandishwa cheo licha ya kwamba alituhumiwa kwa rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushahidi ulipelekwa TAKUKURU, viongozi wetu...

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

MWENYEKITI: Ngoja upawe taarifa.

TAARIFA

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, chombo pekee kinachoweza kuthibitisha ni nani alikutikana na tuhuma na rushwa. Aidha, ni chombo cha uchunguzi TAKUKURU lakini Mahakama ndiyo yenye kauli ya mwisho ya kuthibitisha kwamba mtu huyu anatuhumiwa na rushwa. Kwa hiyo nilipenda nimfahamishe ndugu yangu Mbunge *form one* nimpe taarifa maana mwenzangu ni Mbunge *form one*. Wazungu wanasema *a journey of thousands miles start with a single step*. Kwa hiyo wewe unahatua moja una safari ya hatua...

MWENYEKITI: Muda Mheshimiwa.

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Kwa hiyo taarifa yangu ilikuwa ni kwamba jua taratibu za kisheria, za kikatiba, kikanuni na hata utamaduni wa taifa letu.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Kwani ni mkuu wako, si ukae?

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Haonga.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine kulumbana na watu ambao kwanza hawajui mambo ya nchi yanavyokwenda, siwezi kulumbana naye ngoja nimuache tu, wakati mwingine acha wafu wazikane wao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiongozi anatuhumiwa kwa rushwa, ushahidi umeshapelekwa, Mbunge Nassari amepeleka ushahidi pale TAKUKURU, TAKUKURU wanachunguza anakuja kupandishwa cheo anakuwa RC. Hiki ni kitu kibaya sana katika Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utawala bora katika taifa letu umekuwa ni msiba mkubwa sana. Leo tutakumbuka aliyekuwa Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Wilson Kabwe

alituhumiwa tena jukwaani na Paul Makonda ,Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, yule bwana kaachishwa kazi, kwa sababu ya kutuhumiwa tu. Leo mtu alikuwa *DC* ushahidi upo umepelekwa TAKUKURU muda haujafika si mrefu anapandishwa kuwa Mkuu wa Mkoa. Taifa hili hakuna utawala bora na awamu hii utawala bora uko likizo na jambo hili hatuwezi kulivumilia hata kidogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu bomoa bomoa isiyofuta sheria. Leo wote tunafahamu kwamba kaya zaidi ya 1000 zilibomolewa pale Dar es Salaam, lakini kaya hizi zimebomolewa wakati kesi iko mahakamani. Leo mahakama inadharauliwa na mhimili mwingine, huu hauwezi kuwa ni utawala bora na tuheshimu mihimili hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wamekopa fedha benki, kuna watu ambao wamefariki kwa sababu nyumba zao zimesha bomolewa, hawana mahali pa kuishi, Taifa hili linaenaelekea wapi? Awamu ya Tano imetufikisha pabaya sana kwenye utawala bora, hatujawahi kushuhudia haya siku za nyuma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nikuhusu kuzuia mikutano ya hadhara ya vyama vyaya siasa. Unapozua mikutano ya hadhara ya vyama vyaya siasa na nikopongeze sana Mwenyekiti, hii katiba, wewe Mwenyekiti kipindi hicho ulikuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali hii; ukisoma Ibara ya Tatoo ya katiba yetu Ibara ya Tatoo Ibara Ndogo ya Kwanza inasema; "*3.-(1) Jamhuri ya Muungano ni nchi ya kidemokrasia na ya kijamaa, isiyokuwa na dini, yenye kufuata mfumo wa vyama vingi vyaya siasa.*" (*Makofii*)

Mheshimiwa mwenyekiti, ukisoma pia Sheria Namba Tano ya mwaka 1992 ya vyama vyaya siasa inazungumzia shughuli ya vyama vyaya siasa ni pamoa na kufanya mikutano ya hadhara. Leo Rais wa nchi amezuia mikutano ya hadhara, ameikanyaga kanyaga Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ameiweka pembeni. Hakuna utawala bora, kama unaweza leo ukaweka Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania pbeni. Hali hii ni mbaya sana hatuwezi kuivumilia. Na niombe viongozi tulio...

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Ngoja ngoja kidogo taarifa.

T A A R I F A

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti nilitaka nimpe taarifa Mjumbe anayechangia, Mchungaji Msigwa, mionganoni mwa sifa tulizonazo sisi viongozi wa dini ni kuwa na hekima na busara. Naomba nitoe taarifa yangu kama ni nzuri utaipokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya naomba nimpe taarifa mchangiaji anayeendelea sasa hivi, kwanza nchi hii inafuata Katiba na Sheria na ndiyo maana leo uko humu unaongea. Moja ya vitu ambavyo vimukufanya wewe upate fursa ya kuyasema hayo unayosema ni utekelezwaji wa sheria ambayo imekuingiza humu ukapata fursa ya kusema hayo unayoyasema. Kwa hiyo, mimi nilitaka nimpe taarifa mwenzangu kwamba nchi hii inafuata misingi ya Katiba na sheria kwa sababu hata yeye yuko humu kisheria. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Haonga.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: *Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu ni mjinga kabisa kwa sababu wakati mwingine haitakiwi kupambana... (Kicheko) [Maneno Haya siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Haonga! Mheshimiwa Haonga!

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, utulivu...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tupe nafasi!

MWENYEKITI: Nitakutaja wewe Mheshimiwa

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tupe nafasi tumjibu huyo.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu Bungeni, Mheshimiwa Haonga kwa heshima zote naomba ufute kauli yako.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nifute kauli yangu, lakini ajifunze kuwa na adabu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kufungia vyombo vya habari vinavyoikosoa Serikali. Leo vyombo vya habari vinafungiwa, tumeona magazeti yanafungiwa, gazeti la Mwanahalisi limefungiwa, Raia Mwema imefunguwa, Tanzania Daima ilifungiwa, utawala bora uko wapi? Kama leo vyombo vya habari vinavyoikosoa Serikali, vinavyoishauri Serikali, vinafungiwa, Taifa hili liko pabaya zaidi kwenye suala la utawa bora. Leo *Bunge Live* limefungiwa, hakuna *Bunge live* wote tunafahamu kwamba Bunge ni mkutano wa hadhara. (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea Waheshimiwa tunaendelea Mheshimiwa Nchambi.

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nimpe taarifa mdogo wangu hapo...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nchambi.

MHE. SULEIMA M. NCHAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachangia.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nchambi, nimekupa nafasi ya kuchangia.

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti nipo kwenye orodha ya kuchangia, samahani unajua, kwanza kabisa nataka niwafahamishe Waheshimiwa Wabunge wala msishangae, wajinga wameendelea kuwepo ili wafanye wenyewe akili waendelee. (*Makof*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, baada ya kusema kauli hiyo ili kumrekebisha mwenzangu naomba sasa nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii inayosemwa haifuati utaratibu, sheria ama Katiba, jambo hili ni la kushangaza sana. Yapo mambo ya msingi ambayo Rais wa Awamu Tano ameyaainisha kama dira katika Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja mwaka huu na mwaka jana na awamu hii ya Rais John Pombe Magufuli ni awamu ya kazi. Mimi nashindwa kuelewa, mambo mengine ni ya kushangaza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mzee wao, mshauri wao wa chama chao amekwenda Ikulu kumpongeza Rais kwa kazi nzuri anayoifanya. Kama Mzee Lowassa amekwenda Ikulu kumpongeza John Pombe Joseph Magufuli, jambo la kwanza ana ainisha bayana kuwa Katiba ya nchi hii inafuatwa ndiyo maana anampongeza, lakini ana hakika sheria za nchi hii zinafuatwa ndiyo maana anampongeza. Utekelezaji wa llani, kwa maana ya kuwasaidia wanyonge na maskini wa Taifa hili kazi hiyo inafanyika. (*Makof*)

Msheshimiwa Mwenyekiti, maneno haya hata kanga yapo na mimi niwashukuru sana akina mama wana hekima

na busara, maneno haya huwa wanayavaa katika kanga zao tena nyuma kwa chini kabisa, kwa hiyo ndiyo maneno anayoleta mheshimiwa hapa wala tusishanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti...

MHE. KHATIBU SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

MWENYEKITI: Taarifa.

T A A R I F A

MHE. KHATIBU SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa muongeaji anayeongea kwamba huyo anayemwita mshauri na kiongozi wetu pamoja na kumpongeza Rais kama alivyosema, lakini pia aliombwa kujunga na Chama cha Mapinduzi na alikataa, kwa taarifa aliyoitoa mwenywewe.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nchambi endelea.

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naomba niendelee na michango yangu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, taifa hili lilipokuwa limefika na kufikishwa na watu wachache waliokuwa wakishawishi miradi mizuri na mikubwa, mfano mradi wa reli, kwa kipindi kirefu Serikali ya Chama cha Mapinduzi, ilitaka kutekeleza miradi mikubwa lakini watu wachache walikuwa wakishawishi watu juu ya mambo madogo sana, awamu hii wamefeli. Reli inajengwa, waliobomolewa ni watu ambao walikuwa wanakaa katika maeneo inayotakiwa kupita reli kisheria.

Leo hii hawa hawa baada ya muda watakuja kuwaambia wananchi 2019/2020 kwamba wao ndio waliopiga kelele *standard gauge* imejengwa hao ni wadandiaji wa treni, na wanaidandia treni kwa mbele wala tusiwe na mashaka nao safari hawatafika wanakokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo na mimi nilikuwa na michango michache sana.

Jambo la kwanza, naomba tutumie fursa, dada yetu Leah amesema ya maduhuli, Halmashauri zetu hizi zina minada mizuri kule katika Halmashauri, kwa mfano, Halmashauri yangu ya Kishapu, mimi ninaomba sana Mheshimiwa Waziri Jafo nikushauri ndugu yangu, tuna mpango mzuri sana Kishapu wa kutanua ile minada yetu na kuifanya minada ya kimataifa, tunakutana na kikwazo cha minada iliyoko sasa, iko chini ya Wizara ya Mifugo, tukienda kuomba minada ile tunaambiwa kuna madeni machache yanalipwa. Kishapu tuko tayari kulipia deni letu kama wanadaiwa ili tuachiwe ile minada na sisi tutanue *own source* zetu za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe sana Mheshimiwa Naibu Waziri na Mheshimiwa Waziri, hoja hii ni yenu TAMISEMI ongeeni na Wizara ya Mifungo mtupatие mnada wa Muunze na minada mingine. Sisi watu *sharp* tuitanue ile miradi iwe *sharp* na iweze kuingizia mapato makubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Chama cha Mapinduzi imefanya kazi kubwa sana na kwa kweli katika dini yetu sisi waislamu tunasema *Faa-mma biniimati rabbika fahaddith* na tuzisimulie neema za Mungu zilizokojuu ya ardhii. Neema iliyoko Tanzania kwa Serikali ya John Pombe Joseph Magufuli sio ndogo. Serikali hii imeleta miradi ya ndege zetu wenye we tunajenga reli ya kisasa, tunapanua bandari, tunajenga barabara, tumeleta Makao Makuu Dodoma ili Watanzania wote wanapohitaji huduma za Serikali waweweze *ku-connect...* (*Makofii*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Lema.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na ninaomba niwakumbushe Wabunge

wote kwamba hili ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wabunge ndio watunzi wa sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wabunge ndio watunga sera za maendeleo ya taifa hili. Unapokuwa na chombo kama hiki na mizaha ya ajabu ajabu kama inayoendelea, *this is the very serious humiliation for this country. (Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kutoa pole kwa Mheshimiwa Spika, nafahamu yuko India kwa ajili ya *check-up* na matibabu na vilevile Mheshimiwa Lissu ambaye na yeye yuko Ubelgiji kwa ajili ya matibabu. Mheshimiwa Spika anatumia fedha za Bunge za Serikali kwa ajili ya matibabu na Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Lissu tumeendelea kuumkusanya fedha mitaani kwa vikopo naye vilevile ni Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *double standard* inayoendelea katika taifa hili, kwamba Mbunge wa Chama cha Mapinduzi anaweza akatibiwa na Serikali, akatibiwa na Bunge, Mbunge anayetokana na upinzani, *Chief Whip* aliyepigwa risasi Dodoma hawezi kutibiwa na Bunge wala hajapelekewa shilingi mia moja na Bunge. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bob Marley ana wimbo unasema *only time will tell*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema, Mheshimiwa Lema nakusihu ujielekeze kwenye hoja zilizo mbele yetu.

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Katibu naomba uchunge muda wangu.

T A A R I F A

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mimi nilikuwa naumwa na Wabunge

wote, nilitaka nimpe taarifa ndugu yangu Lema; tunainurance ambazo tumekatiwa. Sikupata taabu ya kutibiwa kwa sababu ninayo *insurance* yangu, niliwasilisana na ofisi huko nilikokwenda, kama ni Tanzania ama sehemu yoyote nilitibiwa. Labda wenyewe hawana mawasiliano na Ofisi ya Bunge, kwa hiyo kama hawana mawasiliano *obvious* hawezikutibiwa, nawashauri na nampa taarifa wawasiliane na Ofisi ya Bunge *officially*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema.

MHE. JOHN W. HECHE: Mwenyekiti hana adabu huyu anacheza na uhai wa mtu hii ni *issue* ya uhai wa mtu, hii ni *issue* ya maisha ya mtu.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata
utaratibu)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Heche naomba utulivu, nisikilize tusibishane...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata
utaratibu)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa, Mheshimiwa Heche, Waheshimiwa Wabunge, naomba tusiongozwe na nyoyo zetu naomba tuongozwe na vichwa vyetu, naombeni sana Waheshimiwa Wabunge, na ndiyo maana nilikusihii Mheshimiwa Lema kule unakotaka kwenda utaanzisha mambo ambayo si sahihi. Changia hoja tu hizo tatu kama utapenda twenda vizuri, ahsante.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajadili Taarifa ya Utawala Bora Katiba na Sheria. Kuna *Chief Whip* wa *Opposition* kapigwa risasi, kifungu namba 24(1) cha Sheria cha uendeshaji wa Bunge kinaeleza ni nani anapaswa kuwa *responsible in case* Mbunge amepata matatizo, na kama sitaweza kujadili maslahi ya Wabunge si Lissu peke yake ya Wabunge wote akiwa ameumia ama hajaumia, niko tayari nisiwe Mbunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sisi ni Wabunge hatuwezi kujadili maslahi ya Wabunge, huyu anasimama anaongea mzaha...

MWENYEKITI: Ongea na kiti.

MHE. GODBLESS J. LEMA:... kuna mtu amepotea mpaka leo anaitwa Ben Saanane, kuna watu wanapotea, haya ni mambo yanahusu utawala bora, katiba na sheria, na haya mambo ni ya msingi kuliko madaraja kuliko lami. Uhai wa mtu mmoja unazidi kilometa bilioni moja za lami, haya mambo tukiyajadili kwa miyo ni msingi imara kwa sababu kuna watu wamepotea, kuna mtu ameumia, yuko hospitali tunapojadili hatuwashutumu tunataka mrudi kwenye *sense*, mjue kwamba tunajadili damu za watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo sababu nikasema Spika ni Mbunge, anatibiwa na hela ya Serikali, Lissu ni Mbunge anatibiwa na nani hata tunamchangia fedha? Nataka tulirudishe Bunge kwenye *sense*, kwamba yuko ndugu yetu anaumia, wewe umempiga risasi, si wewe? Kama Bunge tuongee, haya si kuyajadili kwa miyo, tena tuna hekima kwamba tunaendelea kujadili huku tunalia na tunafanya sala ingekuwa ni nchi nyingine watu wangeweza kuingia barabarani kwa sababu kuna mtu ameumia. Tunajadili mambo haya anaibuka mtu tu kama mrembo huko pepepepe! Wewe! Wewe! Wewe! (Makofi)

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, muda wako umekwisha, ahsante sana.

MHE. GODBLESS J. LEMA: *(Hapa alizungumza bila kutumia kipaza sauti).*

MWENYEKITI: Hapana hapana, nimeshakataa, mimi dakika tano tu Mheshimiwa.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nina dakika kumi tu.

MWENYEKITI: Alaa, wewe ndiwe unaongoza shughuli hii, kaa tu Mheshimiwa.

Mheshimiwa Lema, nadhani yawezekana wakati mimi natangaza hukuwepo, wote hawa wanaochangia ni dakika tano, tano tu. Nilisema leo biashara hiyo ya kulalamika haipo dakika tano tu. Kwa hiyo, muda wako umekwisha...

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: (*Hapa alizungumza bila kutumia kipaza sauti*).

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa haupo kwenye orodha hapa. Unasimama aaaa hatuendi hivyo Bungeni hatuendi hivyo Bungeni, hapana

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo basi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa wewe ni mzoefu sana, ni hivi, utaratibu, kaa basi. Wachangiaji nilisema hivi kwa uwiano wetu wa vyama, uwakilishi humu ndani ya Bunge CUF wawili, CHADEMA watatu, CCM kumi; wewe ndiye ulikuwa unahitimisha, Mheshimiwa Lema unahitimisha idadi ya watatu upande wa CHADEMA, kwa hiyo muda wako umekwisha, dakika tano.

MHE. GODBLESS J. LEMA: (*Hapa alizungumza bila kutumia kipaza sauti*).

MWENYEKITI: Wewe umemaliza muda wako usibishane na mimi. Mheshimiwa mimi ndiye ninayeongoza shughuli hii. Tunaendelea, sasa tunaenda tunaelekea upande wa Serikali, muda si rafiki, angalieni. Nitawapa

Mheshimiwa Ikupa Alex dakika tatu, Mheshimiwa Jafo dakika tisa. Mawaziri wote dakika tisa, najua naumiza lakini na mimi nalinda muda wangu. Dakika tatu Mheshimiwa Ikupa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WZIRI MKUU, WENYE ULEMAVU:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, kwa ajili ya muda naomba niende haraka haraka nikiwapongeza Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati zote mbili za Sheria Ndogo pamoja na Kamati ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niongelee kidogo kuhusiana na hoja ya Kamati ya kutokuwa na mafungu ya moja kwa moja kwenye Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya kibajeti kwa ajili ya maendeleo ya vijana pamoja na watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba ikumbukwe kwamba masuala ya watu wenye ulemavu pamoja na vijana ni mtambuka, kwa maana kwamba yapo ambayo yanayoshughulikiwa moja kwa moja na Ofisi ya Waziri Mkuu, lakini pia yapo yanashughulikiwa na Ofisi ya Mheshimiwa Rais, TAMISEMI, na pia Wizara ya Afya pamoja na Wizara ya Elimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo Ofisi ya Waziri Mkuu sasa hivi inaendelea na zoezi la kukamilisha uundwaji wa Mfuko wa Taifa wa Watu Wenye Ulemavu. Mfuko huu utasaidia sana watu wenye ulemavu kwa kuwa mambo mengi ambayo yanahusu watu wenye ulemavu yatakuwa *solved*, ikiwa ikiwa ni pamoja na tafiti za watu wenye ulemavu, pia mambo ya elimu pamoja na mafunzo kwa watu wenye ulemavu, mambo pia ya ruzuku za vyama vya watu wenye ulemavu na mambo mengine ambayo yanahusu mambo ya ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba katika Ofisi ya Waziri Mkuu kuna Idara ya Maendeleo ya Vijana, idara hii ina mfuko wa vijana na mfuko huu unasaidia sana kwa habari ya mikopo ya vijana ambao wanafanya biashara mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukisema vijana ni pamoja na kundi la watu wenyewe ulemavu, kwa hiyo hii hoja ni ya msingi na kwa ufupi wake nimeitolea ufanuzi kwa jinsi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haraka haraka tena kulikuwa na hoja kwamba Serikali itenye fedha kwa ajili ya Baraza la Ushauri la Watu Wenyewe Ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba Serikali inaendelea kutenga fedha kwa ajili ya Baraza la Ushauri la Watu Wenyewe Ulemavu na hivyo limeendelea kufanya vikao vyake vya kuishauri Serikali kama ambavyo Sheria Namba 9 ya mwaka 2010 ya Watu Wenyewe Ulemavu inavyoelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kulikuwa kuna masuala ya utengwaji wa bajeti ya watu wenyewe ulemavu pamoja na vijana. Kama ambavyo nimeeleza hapa mwanzoni ni kwamba Serikali imeendelea kutenga fedha ingawa....(*Makof*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango wako, Mheshimiwa Kakunda.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mchango wangu ni katika maeneo matatu kwa kifupi kabisa ni kwamba nazipongeza sana Kamati zote kwa jinsi ambavyo wameandaa kazi zao na jinsi walivyowasilisha taarifa zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa elimu ya msingi na sekondari hii changamoto ambayo imeletwa na elimu msingi bila malipo tunahitaji wote kushirikiana. Tunahitaji kuhamasisha wananchi waendelee kuchangia ujenzi wa madarasa, ujenzi wa nyumba za walimu, mabweni, mabwalo, maktaba pamoja maabara, Serikali peke yake

haiwezi kuachiwa jukumu hilo maana mahitaji ni makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kuhusu agizo la Serikali kuzitaka Halmashauri kutenga ...

(Hapa baadhi Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Waheshimiwa naomba utulivu Bungeni.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu agizo la Serikali kuzitaka Halmashauri kutenga asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na Vijana, imezungumzwa kwamba hakuna sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukirejea chimbuko la Mfuko wa Vijana ulionzishwa mwaka 1993 ulianzishwa chini ya kifungu cha 17(1) cha Sheria ya Hati ya Idhini ya Malipo na Ukaguzi (*Exchequer in Ordinance*) Sura ya 439. Kwa hiyo, inatakiwa tu labda kama ni marekebisho tufanye marekebisho badala ya kusema kwamba hakuna kabisa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambalo ningependa kuchangia ni kuhusu maji vijiji. Ninaomba kuwasihii Waheshimiwa Wabunge, pamoja na utekelezaji unaoendelea ambao mzuri kasi zaidi itaongezeka kupitia Wakala wa Maji Vijiji, nadhani mambo hayo matatu yanatosha yawe mchango wangu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kakunda nakushukuru sana kwa mchango wako, Mheshimiwa Jafo dakika tisa.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuzipongeza Kamati zote kwa hoja iliyowasilishwa leo Bungeni hapa na ninaomba nikiri wazi hapa kwamba

sisi hapa jukumu letu kubwa ni kupokea michango ya Wabunge kwa maeneo mbalimbali kwa lengo la kuboresha Wizara yetu au Serikali kwa ujumla wake tuweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru Kamati ya TAMISEMI na Kamati ya Sheria Ndogo. Mheshimiwa Mwenyekiti ninafahamu fika wewe ndiye mwenye dhamana ya Kamati ya Sheria Ndogo na maelekezo yako ya aina mbalimbali yameweza kutusasidia katika utekelezaji wa majukumu yetu. Hata hivyo tutaendelea kuboresha yale ambayo yamebainishwa hapa na Waheshimiwa Wabunge hasa katika suala zima la zoezi la kusaini sheria ndogo. Wataalam wanazipitia ili kuondoa makosa ambayo yamebainika na hatimaye tufanye maamuzi kwa ajili ya kuzisaini tupate sheria ndogo zenye kukidhi mahitaji ya wananchi katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni mbalimbali yametolewa hasa katika suala la ujenzi wa *Strategic City Project*. Kuhusiana na mradi huu niishukuru sana Kamati ya TAMISEMI, imefanya kazi kubwa sana katika maeneo mbalimbali. Wamekwenda maeneo Jiji la Tanga, wametembelea hapa Dodoma kwa ufupi, lakini na maeneo mengine na tumepata mchangwo wao kwa kadri iwezekavyo, kwa kweli wamefanya kazi kubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachukua ushauri kuhusu ujenzi wa mifereji. Tukumbuke mradi huu sawa sawa na ile miradi mingine mitatu mikubwa tuliyo nayo. Mradi wa karibuni shilingi billioni 840, ambapo tunajenga katika miji yetu hii. Tuna Mradi wa *DMDP* wa milioni 660 na Mradi wa *UGSLP* karibuni milioni 800 vilevile ambapo katika sehemu hii tunachukua maoni ya Kamati, kwamba kipaumbele kikubwa ni lazima tuhakikishe kwamba tunatengeneza mifereji katika maeneo yote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwahakikishie kwamba katika mradi huu jambo hili tunalichukulia kwa nguvu zote licha ya mifereji pia tunaweka taa za barabarani

kwa ajili ya wakati wa usiku. Hali kadhalika katika maeneo mbalimbali tunajenga na madampo ya kisasa ili kuiwezesha miji yetu iwe miji rafiki sambamba na ununuaji wa mitambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja inayohusu huduma ya afya, naomba nishukuru sana na nishukuru Kamati kwa kiwango kikubwa. Katika mpango wetu wa kuboresha vituo vya afya 205 hivi sasa zoezi lile linaenda vizuri. Hata hivyo nafahamu kwamba changamoto ya afya hatuwezi kuimaliza kwa siku moja, lakini Serikali imeweka uwekezaji mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru mama yangu mama Kahigi alipongeza Wizara hii kwa nguvu zote na kutoa changamoto katika Hospitali ya Bukoba Vijijini. Mchango wako mama Kahiji sambamba na Mzee wetu Mbunge wa Bukoba Vijijini; ndiyo maana kwa sababu mlikuwa hamna Hospitali ya Wilaya tumepeleka ujenzi vituo vya afya pale Katoro na Kashanje kwa lengo la kwamba huduma za upasuaji ziweze kufanyika katika eneo lile. Hata hivyo Halmashauri ya Bukoba Vijijini tumeiweka katika mpango wa ujenzi wa zile hospitali 64 katika Wilaya ambazo hazina hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo jambo hili sasa hivi lipo katika kipaumbele chetu; eneo hilo tutalipatia huduma ya afya kama tunavyokusudia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa zaidi kama nilivyosema kwamba Kamati ya TAMISEMI imefanya kazi kubwa sana hasa ushauri wa meneo mbalimbali; si wa Bunge tu lakini hata nje ya Bunge tukiwa katika vikao vya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri wazi kwamba walivyotembelea kule Kilolo waliona hospitali ya mfano ya Wilaya ya Kilolo, na mimi tu niseme kwamba nimetoa maelekezo na tutaendelea kutoa maelekezo kwa Mkurugenzi nini afanye ili hospitali ile ya mfano iweze kukamilika ili sisi sote tujivunie tumefanya jambo kubwa la mfano katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja iliyohusu mabasi ya mwendo kasi, kwamba ratiba imebadilika. Naomba niwahakikishie kwamba ofisi yetu inafanya kazi kubwa sana; kwa sababu mradi huu leo hii katika Bara la Afrika ndani ya miaka 13 baada ya utoaji wa tuzo maalum Afrika sisi Watanzania tumekuwa watu wa kwanza katika miaka 13 tumeweza kushinda mwaka huu. Tarehe 9 JAnuari wa kwanza Tanzania imetunukiwa tuzo hii maalum kwa mradi wa mwendo kasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo mradi huu una changamoto yake kubwa kama mama Ruth Mollel alivyosema na ndiyo maana kila siku tunaendeleza uboreshaji na ndiyo maana sasa hivi kuna *tender* imetangazwa lengo kubwa ni kwamba tuweze ku-*meetzile specification* za *World Bank* ambazo katika agreement yatu tumekubaliana kwamba tuwe na *service provider* ambao mkataba wao tunadhani ndani ya mwezi wa tano inawezekana tukaenda mahala pazuri zaidi kuhakikisha kwamba tunapata *service provider*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu hii ni awamu ya kwanza lakini tunajumuisha awamu zote sita; tutakuwa na watoa huduma vizuri zaidi kuondoa shida kubwa ya mabasi yaendayo kasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu eneo la karakana pale Jangwani ni kweli na Wajumbe wa Kamati wanafahamu, mmelitembelea pale, changamoto ile ni kubwa. Ndiyo maana katika mpango wa muda mfupi kuititia Mradi wa *DMDP* tumepeleka fedha kwa ajili ya survey, na sasa hivi wataalam wanafanya *survey* kuondoa lile tope na bonde lote ili kulibadilisha Bonde la Msimbazi ili mvua inaponyesha maji yote yaelekee kwenda baharini.

Hata hivyo katika *backup strategy* nimetoa maelekezo kwa wenzetu wa *DART* kwamba mabasi yale yote yaache kulala pale eneo la Jangwani yaende kulala eneo la Gerezani ambako kuna eneo limetengwa ili kuepusha gharama nyingine ambazo zinaweza kujitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu jambo jipya lolote lazima lina changamoto yake kubwa, lakini changamoto hii tunaendelea kujifunza na kufanya marekebisho makubwa hatimaye tuweze kupata fursa kubwa sana kuhakikisha nchi yetu inaenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Kamati ya TAMISEMI na ushauri wenu mmetoa mlipotembelea ukarabati mkubwa wa shule kongwe Tanzania, tunachofanya ni ukarabati wa kwanza kihistoria. Tunakarabati shule 89 tunatumia takribani shilingi bilioni 89 na kazi hii kubwa inafanyika na Kamati imeendelea kushauri japokuwa kuna baadhi ya wakandarasi walitukwamisha *especially TBA*.

Hata hivyo tumetoa maelekezo ili kwamba miradi hii yote ipate mafanikio makubwa na shule zetu kongwe zirudi katika ubora wake ule tunaokusudia. Hatimaye tupeleke elimu bora kwa vijana wetu na sisi kama Watanzania tujivunie kwamba katika mamlaka zetu za Serikali sasa shule zetu za Serikali zinatoa huduma bora kwa vile vijana wana mazingira rafiki ya kujifunzia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna inayohusu *TARURA*. Nishukuru Kamati imetufundisha mambo mengi sana. *TARURA* ni chombo kipyra na hivyo tunapaswa kukilea kuanzia sasa. Sasa hivi ndiyo kwanza kama mtoto anaanza kukaa chini, ana miezi sita. Wabunge mnafahamu eneo hili sasa ninyi mna *ownership* kubwa sana katika *TARURA*. Leo hii ukiwa Mbunge wewe ndiye msemaji mkubwa sana wa *TARURA* katika Wilaya yako. Yaani ndiyo maana ninasema kwa Wabunge kwamba kuanzishwa kwa *TARURA* inakuwa kama kipa katoka wewe Mbunge unadhamana kubwa ya kukielekeza chombo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba niseme, na ninyi mmeona changamoto kubwa ya kifedha, kwamba mgawanyo ni wa asilimia 30 naomba hili kwa sababu ni suala la Wabunge wote tutalijadili hapo baadae kwamba nini kifanyike ili kuufanya wakala huu uweze kusimama vizuri. Hata hivyo jukumu letu kubwa kupitia *TARURA* sasa tunataka

tuhakikishe kwamba tunaimarisha miundombinu yetu ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hasa kujali *value for money* na ubora wa kazi.

Mheshi, wa Mwenyekiti, ni imani yangu kubwa kwamba tutashirikiana kwa pamoja, wakala huu utaweza kutimiza wajibu wake kwa sababu mwisho wa siku jambo hili litaleta faraja kubwa kwa Watanzania. Hii ni kwa sababu huko chini ndiko mazao yanakozalishwa wananchi maskini wako huko. Nina imani miundombinu hii tutaiimarisha, na tutahakikisha kwamba katika maeneo mbalimbali wananchi wanapata huduma vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepewa dakika tisa, japokuwa nina hoja nyigi sana za kujadili, niseme kwa ujumla na nikuhakikishie kwamba sisi ambao tuna jukumu kubwa sana la kuhakikisha katika Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa tunafanya kazi kubwa ya kutosha tumejjipanga. Kamati nawaombea sana ili Mungu asaidie muendelee kutushauri. Lengo kubwa ni kwamba Wizara hii iweze kufanya vizuri na wananchi wapate huduma vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana ninaomba kuwasilisha, lakini naunga mkono hoja zote zilizowasilishwa hapa. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Profesa Kabudi dakika tisa utafuatiwa na Mheshimiwa Mkuchika.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nichukue fursa hii kuzishukuru sana Kamati zote kwa taarifa nzuri walizoziwasilisha. Jukumu letu sisi ni kupokea mapendekezo yote yaliyotolewa na kamati hizo pamoja na Wabunge waliochangia.

Nichukue fursa hii kuishukuru sana Kamati ya Katiba na Sheria kwa mchango mkubwa iliyoutoa hasa wakati tulipokuwa tunakabiliwa na kuitisha sheria zile muhimu kwa ajili wa ulinzi wa rasilimali na mali zetu za asili yaani sheria ya

*The Natural Wealth and Resources Permanent and Sovereignty Act 2017*Act No. 5 of 2017, *The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-Negotiation of Unconscionable Terms) Act No. 6 of 2017*na *The Written Laws Miscellaneous Amendments Act No. 7 of 2017.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wa Kamati ulikuwa mkubwa sana na ndiyo maana kama wote tunakumbuka *schedule of amendment* iliyoletwa na Kamati ilisaidia sana kuboresha sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo nishukuru sana mchango uliotolewa kuhusu utungaji wa kanuni. Ni kweli kabisa sheria zikitungwa zinahitaji kanuni ili ziweze kutekelezwa na moja ya sheria ambayo ilihitaji kanuni hizo ni mabadiliko ya Sheria ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuhimiza ukamilishaji wa Kanuni za Madini na kazi hiyo ilikamilika na nimshukuru sana Waziri wa Madini ingawa alikuwa katika likizo ya uzazi yaani *maternity leave* aliweza kupata nafasi ya kurudi na kuweza kuzitia saini kanuni zote tarehe 9 Januari, 2018.

Pia nimshukuru sana Katibu Mkuu Kiongozi ambaye na yeye kwa mujibu mamlaka aliyopewa chini ya Sheria ya *Executive Urgency* aliweza kutia sahihi amri mbili za kufuta baadhi ya mamlaka ambazo zimeondolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikubaliane na Mheshimiwa Daniel Mtuka, Mbunge wa Manyoni Mashariki kwamba kuna umuhimu wa kuimarisha ubora wa utungaji wa sheria ndogo na utungaji wa kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamini kabisa mabadiliko yaliyoanza kufanyika katika ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali yataongeza ufanisi katika utungaji wa sheria na kanuni ndogo ndogo. Ni eneo ambalo linahitaji kufanyiwa kazi zaidi na nina imani chini ya Mwanasheria Mkuu mpya wa Serikali Dkt. Adelardius Lubango Kilangi tutaongeza ufanisi wa kuitia

sheria na kuzifanya ziwe bora zaidi na baada ya muda mfupi mabadiliko zaidi katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali yatafanyika ili kuhimiza na kuimarisha ufanisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue pia nafasi hii kusema kwamba inapokuja kwenye maswali ambayo yameulizwa na Ndugu Ayoub Jaku namwomba tu kwamba maswali yake yote hayo aliyoauliza yaje Bungeni kwa kanuni za kawaida za Bunge, kwa sababu hapa tunajielekeza katika taarifa iliyotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue pia nafasi hii kuishukuru Kamati kwa maelezo iliyotoa kuhusu kazi kubwa inayofanywa na mahakama. Ni kweli kabisa mahakama zinakabiliwa na upungufu wa Mahakimu na Majaji lakini Serikali iko katika hatua ya kukamilisha upekuzi wa wale wote wamependekezwa kuwa Majaji au Mahakimu ili kuhakikisha kwamba tuna Majaji au Mahakimu ambao hawana tuhuma za ujisadi, hawana tuhuma za rushwa, lakini pia ni waadilifu na wanaoweza kutekeleza majukumu yanayotakiwa kwa ufanisi na weledi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa nieleze kuhusu suala la makosa mbalimbali na faini kuwa chini. Hiyo ni moja ya changamoto na ambazo zinafanyiwa kazi na Tume ya Kurekebisha Sheria, ni kuona ni mfumo gani utumike utakaotusaidia kuhakikisha kwamba faini haziwi chini baada ya muda mfupi kutokana na thamani ya fedha ya Tanzania kushuka. Kwa hiyo, maeneo yote hayo yanafanyiwa kazi ili uhakikisha kwamba faini zitaendana na hali ya mabadiliko ya kiuchumi nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala zima la utawala wa sheria na utalawa bora. Ningependa kuwashakikishia Watanzania wote kwamba taasisi zote na mihimili yote inayohusika na utawala bora inafanya kazi inavyotakiwa. Moja ni Mahakama za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwepo Mahakama ya Rufani ina uhuru kamili, inafanya maamuzi na maamuzi yake yanaleshimiwa na nchi. Kwa hiyo Watanzania wowote au wananchi wowote ambao

wanaona haki zao zimeminywa wanao uhuru kamili chini ya Katiba kwenda mahakamani na mashauri yao kuamuliwa na daima Serikali imekuwa inaheshimi maamuzi ya mahakama kwa jinsi yanavyokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imekuwa inafanya kazi nzuri ya kuelekeza maeneo gani ya utawala bora na haki za binadamu yafanyiwe maboresho ili kuboresha zaidi. Kwa hiyo, naishukuru sana Kamati ya Katiba na Sheria kwa maoni na miongozo mbalimbali waliota kusaidia kuboresha hali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, duniani kote daima utawala bora, utawala wa sheria na demokrasia ni mambo yanayohitaji daima kufanyiwa kazi ili kuyaboresha. Leo nimesafiri na Balozi wa nchi moja ya Ulaya na nilimkumbusha kwamba mpaka leo tunavyozunguza nchi ya Switzerland katika baadhi ya maeneo ya nchi ya Switzerland wanawake hawaruhusiwi kupiga kura na hii ni nchi ya Switzerland, lakini mpaka leo wanawake hawaruhusiwi kupiga kura, wanaopiga kura ni wanaume tu. Nchi za Ulaya mpaka leo kwa daraja lile lile na cheo kile kile mwanamke analipwa chini kuliko mwanaume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Wabunge, Wabunge Wanawake wanalipwa chini kuliko Wabunge Wanaume sihalalishi, lakini nataka nieleze kwamba kila nchi ina changamoto. Wabunge Wanawake hawa wangekuwa kwenye baadhi ya nchi za Ulaya wangepokea mshahara mdogo kuliko Wabunge Wanaume.

Kwa hiyo, changamoto hizi za kuboresha demokrasia daima zipo na Taifa lolote haliwezi kusema limekamilika ni lazima liendelee kuboresha. Kwa maana hiyo tunapokea michango yote iliyotolewa yenye lengo la kuboresha demokrasia yetu na haki za binadamu ili tuweze kuwa na hali bora zaidi bila kubeza hatua kubwa ambayo Tanzania imepiga katika demokrasia, Tanzania imepiga katika haki za binadamu, Tanzania imepiga katika usawa wa wanaume na wanawake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba pia kuunga mkono hoja iliyotolewa. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Profesa kwa mchango wako. Tunaendelea Mheshimiwa Mkuchika dakika zako tisa, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Jenista naye dakika zako tisa.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hasa maeneo yanayohusu Wizara yangu ya Utumishi na Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Kamati ambayo tumefanya nayo kazi, Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa, imetuongoza vizuri mlaka miwilli hii. Mwenzangu aliyenitangulia wameshirikiana naye vizuri na mimi nilipofika nimepata ushirikiano katika miezi hii minne ambayo nimefanya nao kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushukuru kwa pongezi zilizotolewa na Kamati kwa vyombo vitatu vinavyofanya kazi katika Wizara yangu, kwa maana ya *TASAF*, *MKURABITA* na *Mfuko wa Rais wa Kujitegemea*. Kamati inakubali kwamba wanafanya kazi nzuri, wanaomba tu ikiwezekana wawezeshwe ili waweze kufanya kazi nzuri zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kwa upande wa *TASAF*, kwamba tupo *TASAF* Awamu ya *Tatu*, utekelezaji tumefikia walengwa asilimia 70, bado walengwa asilimia 30. Tunafanya utafiti sasa kuijandaa kwa utekelezaji Awamu ya Pili ya *TASAF* ya *Tatu* na lengo la Serikali ni kuwafikia walengwa wote ili Watanzania wote wanaohitaji msaada wapate kusaidiwa na *Mfuko wa TASAF*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lilikuwepo swali hapa kuhusu ajira ya wataalam, ilizungumzwa wataalam katika afya, lakini

kwa sababu Bunge hili hushughulika na ajira kwa watumishi wote, ningependa kusema yafuatayo kuhusu ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua kuwa zoezi la uhakiki wa watumishi limeleta upungufu wa watumishi wa kada mbalimbali ikiwemo watumishi wa kada ya ualimu na afya, Serikali imetoa vibali vya kuajiri watumishi 15,000. Hao 15,000 tumekwishwa waajiri katika hao 4,000 wako afya, 4,000 wako elimu na hasa elimu ya sekondari kwa walimu wa sayansi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshatoa ikama iliyoidhinishwa kwa mwaka 2017/2018 ambapo jumla nafasi zilizokubaliwa 52,436 wanatarajiwa kuajiri, tulikuwa tunaziba pengo la wale ambao wametolewa kwa ajili ya vyeti *fake*, sasa tunataka kuingia katika mchakato wa ajira zile 52,000 ambazo zillikwisha idhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka niseme, nimesikia hapa ndani na baadhi yao wameniandikia vikaratasi, kwamba zipo Halmashauri zahanati imefungwa au kituo cha afya kimefungwa kwa kukosa muhudumu.

Mimi naomba endapo kuna mtu yejote, Mbunge au mwananchi yejote anayenisikia ambako katika Halmashauri yake zahanati imesimama kwa kukosa muhudumu nipewe taarifa, tutamuajiri mara moja ili huduma za afya ziweze kuendelea. Maeneo mengine tunaweza tukasubiri, lakini kwa afya ya binadamu hatuvezi tukaendelea kusubiri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, limegusiwa hapa suala la utawala bora na mimi ni Waziri wa Utawala Bora. Nisingelipenda kubishana sana, lakini nataka niseme hivi, utawala bora maana yake nini? Utawala bora maana yake ni watu kuishi katika jamii kwa kufuatana kwa sheria na taratibu walizokubaliana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Tanzania sheria na taratibu walizokubaliana zinatoka hapa katika Bunge, kwa hiyo mtu anayekwenda kinyume na yanatoka hapa katika

Bunge huyo anakwenda kinyume na Utawala Bora na anapaswa ashughulikiwe kwa sababu anakwenda kinyume na sheria za nchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nataka niseme, magazeti ya leo kama mmesoma *Daily News* wameandika, gazeti la Habari Leo wameandika, kiswahili wameandika lile la kiswahili Tanzania yang'ara katika utawala bora, tumeambiwa katika nchi za Afrika Mashariki, Tanzania ni ya kwanza; Rwanda wanatushinda katika *fighting corruption* wao wa kwanza, sisi wa pili, lakini ile utawala bora ikiunganishwa, akina Mpango mnasema uchumi shirikishi, Tanzania ni ya kwanza katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno hayo yanaungwa mkono na TWaweza, maneno hayo yanaungwa mkono na *Transparent International*, maneno hayo yanaungwa mkono na REPOA, maneno hayo yanaungwa na *World Economic Forum*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi naomba yale mambo yetu mengine si vizuri tukalumbana. Mimi sikuona mahala, nimefatilia na bahati kipindi hicho pia nilikuwa Waziri wa Utawala Bora, sikuona mahala aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Arumeru katiwa hatiani na Mahakama ya nchi hii. Kwa hiyo, unavyosimama hapa ukasema kapewa *promotion* mtu ambaye ametenda kosa hili, hili, hili nchi hii chombo peke yake chenye mamlaka ya kutafasiri sheria ni Mahakama, hakuna mahala yule mtu ametiwa hatiani. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengine ambayo yamezungumzwa hapa ni kuhusu bomoa bomoa. Siwezi kujibu yote, lakini nataka niseme tunataka kutengeneza reli *standard gauge*, tunataka kupeleka barabara iwafikie watu, nyumba yako ipo barabarani tuiache? Mimi nasema Serikali hii haina *double standard*, nyumba za watu binafsi zilizoko barabarani zimevunjwa, sasa hivi jengo la TANESCO mali ya Serikali linavunjwa. Linavunjwa kwa nini, kwa sababu liko

barabarani. Hii Serikali haina *double standard*. Habari ... (*Makofî*)

MHE. KASUKU S. BILAGO: Taarifa Mwenyekiti, taarifa Mheshimiwa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Nakubali, wewe utakuwa taarifa ya mwisho, muda si rafiki kwetu, endelea

TAARIFA

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilikuwa naomba kumpa taarifa mzungumzaji anayeendelea kwamba haya anoyozungumza ya Arumeru na DC aliyekuwa Arumeru aliyoyafanya Arumeru yanajulikana. Hivi kununua Madiwani kwa pesa za umma ni utawala bora? Naomba nimpe hiyo taarifa. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mkuchika endelea.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jinsi nilivyobobea katika siasa sikusudii kubishana naye, nakusudia niendelee tu kujenga hoja niliyokuwa naijenga. Yeye hakai Arumeru, mambo ya Arumeru hayajui. Mwenyekiti Mao Tse Tung anasema *no research, no right to speak*, anajua hao Madiwani wameingiaje? Hivi mimi inanihusu nini hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka nimalizie katika hilo suala la utawala bora. Mmegusia katika habari ya kufungia magazeti, nataka niseme hivi, katika utawala wa nchi hii hakuna *vacuum*, Sheria ya Magazeti ya mwaka 1976 ilikuwa inampa Waziri kufungia magazeti, baadae tumebadilisha Sheria katika vyombo vya habari kuna *committee* inayoitwa *Content Committee*, wale wanafuatilia kama gazeti au redio au luninga imekwenda kinyume wanamshauri Waziri Kamati (*Content Committee*) wanamshauri Waziri kwamba hawa hapa wamekwenda

kinyume na sheria za nchi, Waziri anachukua sheria, hatukurupuki tu hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ile Sheria ya Vyombo vyatulikuja tukairekebisha, tukaipitisha hapa. Kwa hiyo mimi nataka niseme kwamba suala la *good governance* (utawala bora) ni kuishi kwa kuzingatia sheria za nchi ambazo tumekubaliana katika jamii. Inawezekana wewe ultaka sheria iwe hivi, iwe hivi, bado hujawa na *majority*ya kutunga sheria, fuata wale walio wengi walivyotunga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, palikuwapo na hoja kwamba watu wanakaimu muda mrefu bila kudhibitishwa. Nataka kusema kwamba ultolewa mwongozo unaosema kwamba kabla hujamkaimisha, kabla hujamfukuza, wasiliana na Utumishi, Utumishi watambue kule kukaimu kwako ili utakapokuwa unaomba kwamba yule adhibitishwe liwe lisiwe jambo jipyaa kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine watu wanakaimishwa bila Utumishi kuhusishwa, watu wengine wanafukuzwa hata bila Utumishi kupewa taarifa. Tunaomba tu kwamba taratibu tu zifuatwe na taratibu zikifuatwa sisi tukiletewa majina hata kama ni upekuzi tunasimamia na zoezi linaenda kwa jinsi ambavyo limekusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dada yangu pale Mollel kauliza maswali mawili ya msingi sana. Tunawafanyaje darasa la saba wale? Tunafanyaje wale ambao tumewafukuza kwa sababu ya vyeti *fake*? Niseme lile la vyeti *fake* na hilo la watu wa darasa la saba; Serikali imekaa na *TUCTA* (Chama Huru cha Wafanyakazi), ni mambo ambayo tumezungumza, tunaendelea kuzungumza nao, tumepeana muda ili jambo hili tuweze kulimaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka niseme lile la vyeti *fake*, Serikali ilishasema kwamba kama mtu wakati wa kutafuta ajira alipeleka vyeti *fake* na yeye akaingia mkataba na Serikali maana yake mkataba wake ule ni *null and void*. Maana mwajiri alimtaka apelike cheti ambacho ni sahihi,

cheti ni halali. Yule ambaye aliyepeleka cheti *fake* maana yake mkataba nao ni *fake*. Swali linakuja je, unamu-award mtu ambaye ana cheti *fake*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TUCTA* wameiomba Serikali na Serikali imeshasema, kama ni kuwashitaki wale wangeshtakiwa na *TAKUKURU*, wangeweza kushtakiwa na Kanuni za Utumishi, Serikali imetoa msamaha. *TUCTA* wametuomba kwamba tunaomba Serikali iwe na jicho la huruma kwa hawa watu wa darasa la saba, kwa hawa watu wa vyeti *fake* na Serikali inalifanya kazi jambo hilo, muda utakapofika Serikali itatangaza uamuzi wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sjui nimebakiwa na dakika ngapi, maana yake mambo yapo mengi ambayo yalikuwa...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, naounga mkono hoja ya Kamati tunazozijadili, ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jenista Mhagama

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru, na mimi nianze kwa kuwapongeza sana hasa Kamati mbili, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, lakinivilevile kwenye muktadha wa mjadala wetu wa leo niwapongeza pia Kamati ya Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza sana Wajumbe wa Kamati hizi mbili kwa kweli wamefanya kazi

kubwa sana katika kuishauri Serikali na wametekeleza majukumu yao sawasawa. Kwa hiyo kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba niwapongeze sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko hoja kadhaa zimejitokeza katika Kamati hizi zote ambazo zimesoma taarifa na mimi nianze kwanza kwa kuunga mkono hoja ya Kamati hizo zote mbili ambazo zinairuhusu Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme jambo la kwanza limezungumzwa suala kuhusu Baraza la Vijana. Ninaomba nichukue nafasi hii nitoe taarifa kwenye Bunge lako Tukufu, wote tunakumbuka mwaka 2015 tulipitisha Sheria ya Kuunda Baraza la Taifa la Vijana katika nchi yetu ya Tanzania. Lengo letu kubwa ilikuwa ni kuwaunganisha vijana wote wawe pamoja, kuondoa itikadi zao za kisia na kuwafanya wawe wazalendo kwa nchi yao ya Tanzania. Vilevile kuwafanya vijana wa Taifa hili la Tanzania waelewe umuhimu wao wa kuwepo katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge, baada ya sheria ile kupita, tayari kanuni za kuanzisha Baraza hili zimeshakamilika. Hata wewe Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kikao cha leo nakumbuka Ofisi ya Waziri Mkuu ilishakuja mbele ya Kamati yako ili kupertia kanuni zile na kuziweka sawa sawa na sasa muda si mrefu, uundwajiwa wa Baraza la Taifa la Vijana utaanza kupertia ngazi mbalimbali kama sheria inavyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge vijana wote, tutakapofika nafasi hiyo sasa ya uundaji wa Baraza la Vijana la Taifa watoe ushirikiano kwa Serikali kusudi kazi hii iweze kufanyika vizuri. Kwa hiyo, katika suala hilo tunakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Sheria Ndogo imetuelekeza Serikali na kwa kweli tumekuwa Ofisi ya Waziri Mkuu tukitekeleza jukumu la kisheria la kuweka mezani sheria

ndogo zote ambazo zimekuwa zikiandaliwa na kuitishwa na mamlaka mbalimbali za Serikali ikiwemo Wizara mbalimbali. Tumekuwa tukipokea maoni ya jumla yanayohusiana na sheria hizo ndogo zote katika nchi yetu ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Sheria Ndogo imefanya kazi kubwa, imepitia sheria nydingi sana ndogo katika nchi yetu ya Tanzania. Mimi niseme kama Serikali na taasisi zake itaendelea kufanya vizuri katika kutunga sheria ndogo katika nchi yetu ya Tanzania, ni kwa sababu Kamati ya Sheria Ndogo imebaini makosa na imeturekebisha katika maeneo mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nichukue nafasi hii kuliahidi Bunge lako Tukufu kwamba tutazingatia maoni na ushauri wa Kamati ya Sheria Ndogo katika kuhakikisha kwamba sheria ndogo zitakazokuwa zinatumika katika nchi yetu ya Tanzania zinaendana na sheria mama na zitakwenda kutenda haki katika kusimamia sheria mama katika nchi yetu ya Tanzania. Kwa hiyo, maagizo ya Kamati ya Sheria Ndogo tumeyapokea na tutayapeleka Serikalini kwa ajili ya utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lilzungumzwa suala lingine kuhusu *NSSF*. Waheshimiwa Wabunge ninaomba niwaambie, sisi kama Serikali hatujafumba macho kuhusu suala la *NSSF*. Kamati ya *PAC* ilishasoma taarifa yake hapa ndani ya Bunge, na mimi niliwaamba kwamba pamoja na shughuli inayoendelea ndani ya Serikali ya kuimarisha *NSSF*, tumeimarisha Bodi na hivi juzi tumeunganisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, lakini tunesema *NSSF* tabakia kuwa mfuko kwa ajili ya *private sector* na kwa ajili ya sekta isiyo rasmi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa moja kwa moja Serikali inaona jukumu kubwa la *NSSF*. Ninaomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge tunaendelea kuyatupia macho yale yote yaliyojiri kwenye *NSSF* na tumeiagiza Bodi kuhakikisha kwamba inasimamia ipasavyo na inatenda haki katika

kushughulikia masuala yote yaliyojitokeza kwenye *NSSF*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge, jambo hili sisi tunalishughulikia vizuri na msiwe na hofu. Lengo letu ni kuhakikisha fedha za wanachama zinabaki kuwa salama, na vilevile Mfuko wa *NSSF* ambao uhai wake unafika mpaka mwaka 2085 uendelee kuwa mfuko ambao una maisha marefu ya kuhudumia Watanzania. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge niwahakikishie kwamba tupo imara na tutafanya kazi hiyo vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumzwa suala la ajira katika nchi yetu ya Tanzania na hasa kwa ajili ya vijana. Mwaka 2014 tulifanya utafiti wa hali ya nguvukazi katika nchi yetu ya Tanzania, na tuligundua kwamba Watanzania takribani milioni 25 ndio nguvukazi ya taifa katika nchi yetu. Lakini asilimia 56 ya hao Watanzania milioni 25 ni vijana. Tulijitahidi pia kuangalia ujuzi wa hawa vijana je, unaendana na soko la ajira katika nchi yetu ya Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria inafahamu tulipokwenda kwenye Kamati tuliwaeleza baada ya utafiti huu, Ofisi ya Waziri Mkuu ilandaa programu tano za kuhakikisha tunakuza ujuzi wa vijana ili waweze kuajirika katika miradi mbalimbali kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafurahi kukuambia kwamba kwa taarifa tulizonazo sasa mwaka 2015/2016 katika nchi yetu ya Tanzania ajira ambazo ziliikuwa zimetengenezwa nchini ziliikuwa ni ajira 390,676. Mwaka 2016/2017 ajira zilitengenezwa katika nchi yetu ya Tanzania zimeendelea kuongezeka mpaka kufikia ajira 421,803.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta inayoongoza kwa kutoa ajira kwa wingi ni sekta binafsi, sekta inayofatia ya kutoa ajira kwa wingi ni sekta ya miradi ya maendeleo. Kwa hiyo, tunajitahidi kusimamia miradi ya maendeleo ili kukuza ajira katika nchi yetu ya Tanzania. Ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mchango wako. (*Makofii*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. RHODA E. KUNCHELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na mapitio ya hoja za Kamati za Sheria Ndogo zinazopitishwa na Halmashauri zetu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko changamoto chache ambazo kimsingi zinasumbua walipa kodi na kupitia TAMISEMI, kwanza ni ushuru wa maegesho za Halmashauri ya Mji lengo ni kutoza faini kwa maegesho holela na wamiliki wa vyombo vya moto wamekuwa wakitozwa faini hizo shilingi 50,000 na mmiliki akishindwa kulipa anapelekwa mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faini hizi kupitia sheria hizi ndogo usimamizi wa pesa hizi TAMISEMI (kupitia Wizara ya Katiba na Sheria). Je, Serikali haioni kuwa sheria hii ni kandamizi kwa sababu Halmashauri nyingi hazijatenga maeneo ya kutosha ya maegesho hayo hususani mijini? Na je, wananchi wana uelewa kiasi gani kuhusu faini hizi na je, hamuoni kwamba ni Serikali yenye we ilitakiwa itengeneze mazingira ya maegesho makubwa ili uonevu huu usiendelee?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria zilizopitishwa na Halmashauri zetu kupitia makanyagio ya ng'ombe katika minada yetu nchini ushuru huu kwa wafugaji unawakandamiza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfugaji anasafiri kutoka Tarafa moja kwenda nyingine umbali wa kilometra 40 mfano kutoka Karema mpaka Mpanda Ndogo mfugaji anaende mnadani, anapoingia getini analipa ushuru auze/asiuze analipa ushuru na ng'ombe wanaposafirishwa kutoka katika minada katika mageti wanalipa tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii haiko sawasawa maana kuna ushuru mwingi kwa wafugaji na inawaumiza wafugaji. Serikali ilione hili ili angalau wafugaji hawa

wawekewe mfumo wa kulipia mifugo yao kwa mara moja na sio ushuru wenyewe usumbufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushuru wa kutupa taka, sheria mama na sheria ndogo zote zinalenga kuisaidia jamii kuzifuata sheria hizi kupitia mamlaka zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nasisitiza kupitia sheria hii ni nzuri kwa maana ya kutunza mazingira kwa katika hali ya usafi. Je, Serikali imeweka mazingira gani kabla ya kutunga sheria hizi? Serikali ione haja ya kuhakikisha wananchi wanapata elimu ya kutosha na kupatiwa vifaa vy'a usafi halafu utekelezaji wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia sheria hizi ndogo Serikali iangalie upya mazingira ya afya kwa shule za msingi ambazo hazijakidhi vigezo. Mfano sheria inasemaje kwa shule za msingi ambazo watoto wanatumia tundu moja la choo na ni shule za msingi za Serikali, ni kwa nini mazingira haya magumu yako wazi Halmashauri ipo? Sheria inasemaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwazi wa sheria na semina kwa Madiwani katika Halmashauri nchini, kwa kuwa Madiwani wengi hawana elimu ya kisheria na wao ndio watunga sheria katika Manispaa na hivyo kupitia kukosa weledi wa kisheria inapelekea Madiwani kutunga sheria kandamizi. Je, Serikali inasimamia vipi kuhusu semina kwa Madiwani wetu kuhusu masuala ya sheria?

MHE. MARY D. MURO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze na kuunga mkono hoja iliyopo mezani juu ya Taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo iliyowasilishwa vizuri na Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Bunge liwe macho juu ya sheria zozote inapotokea zinakinzana na Katiba ya nchi au inapokinzana na uhalisia wakati wa utekelezaji nikimaanisha sheria inapokuwa haina maslahi kwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeshauri sheria ya umri wa mtoto wa kike kuolewa itoe uangalizi wa sheria hii kwani watoto wa kike sasa hivi wanabalehe mapema, hivyo, naishauri Serikali iangalie kwani sasa hivi ina mchanganyiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kuleta muswada wa sheria kuhusu mwanamke kuwa na haki ya kumiliki ardhi ya familia, sio kama ilivyo sasa ambapo haiko hivyo.

MHE. LUCIA M. MLOWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kuhusu uwasilishaji wa Sheria Ndogo Bungeni; kwa kuwa kuna sheria ndogo ndogo ambazo zina dosari, naishauri Serikali kuleta hapa Bungeni na kufanya marekebisho hapa Bungeni kwa mfano; Sheria ya Vyombo vy'a Usafiri ambayo inatumika kwa vyombo vyote vy'a usafiri kuanzia bodaboda hadi magari makubwa. Kama ni kulipa faini wote wanalipa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Sheria ya Ndoa inayoruhusu watoto chini ya miaka 18 kuolewa ibadilishwe na kuweka umri wa kuolewa uwe miaka 18 na siyo chini yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naiomba Serikali ilete marekebisho ya Sheria ya Ardhi ambayo itawaruhusu wanawake kumiliki ardhi kuliko ilivyo sasa kwamba ni wanaume tu wanamiliki ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Tunaanza na watoa hoja, tutaanza na Makamu wa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, Mheshimiwa Ngeleja, kila mmoja dakika 15, si lazima umalize dakika 15.

MHE. WILLIAM M. NGELEJA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine tena ahsante

sana kwa kunipa fursa hii. Kama ambavyo umeridhia nifanye kazi hii kwa niaba ya Kamati yako unayoiongoza ya Sheria Ndogo naomba nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufikia mahali hapa tulipofikia na hasa katika uhai wa Kamati yetu chini yako wewe.

Pili naendelea kuwapongeza na kuwashukuru sana viongozi wetu wa Bunge tukiongozwa na Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti kama kawaida. Tunaendelea kuwashukuru sana Wabunge wenzetu kwa ushirikiano ambao wametupa na hadi kufikia mahali hapa, taarifa yetu imechangiwa na baadhi ya Wajumbe kwa kadri ambavyo muda umeruhusu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu tu nitambue kwamba walioopata nafasi ya kuchangia kwa kuzungumza ni Mheshimiwa Daniel Mtuka, Mheshimiwa Ester Mmasi, na kwa upande wa Serikali Mheshimiwa Mwenyekiti umemsikia Mheshimiwa Profesa Kabudi, Mheshimiwa Jenista Mhagama pamoja na Mawaziri kwa ujumla waliozungumza kwa kuchangia katika taarifa hizi tatu ambazo zimewasilishwa.

Ninatambua mchango wa Mheshimiwa Ikupa, Mheshimiwa Kakunda hao ni Naibu Mawaziri lakini Mheshimiwa Waziri Jafo, Mheshimiwa Mkuchika wote hawa hakuna hata mmoja ambaye amepinga taarifa ya Kamati hizi na sisi kwa sababu ni sehemu ya Kamati hizi tatu tunatambua mchango wao tunasema ahsanteni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapofanya majumuisho pia tunakuwa tunajielekeza kwenye kile ambacho Serikali imezungumza. Kwa sababu pamoja na kwamba sisi tunafanya majumuisho ya taarifa hizi, lakini kwa kweli hoja nyingi ambazo Waheshimiwa Wabunge na sisi sehemu ya Kamati tulizozitungumza ufanuzi wake umetolewa kuitia Waheshimiwa Mawaziri wakati wanachangia, na ndio utaratibu. Kwa hiyo, tunawapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri kwa kurahisisha kazi hii, na mimi naamini kazi hii haitafika dakika 15 kama ambavyo Mheshimiwa Mwenyekiti umesema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sisitize tu kwamba alichomalizia kukisema Mheshimiwa Jenista, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu ni kweli kabisa Kamati yetu imekuwa ikifanya kazi ya uchambuzi, na asubuhi tulizungumza kwamba kwa kipindi cha mwaka mmoja tumefanya uchambuzi wa sheria ndogo 404. Katika sheria hizo 404 sheria 180 zilionekana kuwa na dosari ambazo zilihitaji marekebisho. Sasa ukipiga mahesabu ya haraka hizo sheria 180 maana yake unazungumzia asilimia 44 *point* kadhaa kuelekea kwenye asilimia 45.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii maana yake ni nini, kwa huu mfumo ambao tunao wa utungaji wa sheria ndogo kwa sababu hizi zinatungwa na mamlaka mbalimbali za Serikali, maana yake ni kwamba hizi ni dosari ambazo tumezibaini wakati zimeshaanza kufanyiwa kazi. Ukitaka kwenda zaidi unasema mpaka wakati ambapo tumependekeza marekebisho na Serikali ikafanya marekebisho yaliyofanywa baada ya Kamati kubaini na Waheshimiwa Wabunge kuridhia maana yake ni kwamba madhara hayo yameshawaumiza wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumbe ndiyo maana tunasisitiza kwamba Serikali iendelee kuimarisha vitengo vyta sheria katika mamlaka mbalimbali na umakini wa utungwaji wa hizi sheria ndogo ili tupunguze hiyo fursa ya kuwa na dosari katika sheria zetu ndogo na hivyo kupunguza kabisa ikiwezekana kumaliza kabisa kuwaumiza wananchi kabla ya hizo sheria ndogo hazijafika Bungeni kwa utaratibu na mfumo tulionao sisi wa utungaji wa sheria ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaishukuru sana Serikali kwa kukubali, lakini kwa dhati kabisa kwa niaba yako Mheshimiwa Mwenyekiti naendelea kuwapongeza sana Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yetu kwa muda waliojitolea. Kwa sababu kama wasingekuwa makini tusingeweza kubaini hii asilimia 45 ya dosari zilizomo katika Sheria Ndogo 180 kati ya sheria 404 tulizozifanyia kazi katika kipindi hiki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nataja waliochangia kwa kuzungumza pia natambua mchango wa maandishi wa baadhi ya Wabunge wenzetu waliopata fursa hiyo; wa kwanza ni Mheshimiwa Rhoda Kunchela ambaye amechangia kwa maandishi na amezungumzia kasoro zinazopatikana katika baadhi ya Sheria ndogo, lakini pia Mheshimiwa Mary Deo Muro tunakushukuru kwa mchango wako wa maandishi, pia Mheshimiwa Lucia Michael Mlowe, hawa ni wale ambao walichangia kwa kuandika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa sababu Serikali imekubali kwamba inaridhia maoni na ushauri wa Kamati; na kwa sababu maoni na ushauri huu tumezungumza kuitia taarifa yetu na hatimaye tumependekeza Azimio la Bunge kwenye maeneo ambayo tunapendekeza yakafanyiwe marekebisho naendelea kusitiza kwamba Serikali ifanye hivyo kama tullyiyoshauri kwamba kabla ya Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge la Jamhuri wa Tanzania tutakapokutana hapa hasa kwenye kamati, Serikali iwe imefanya jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea tena kusistiza kwa Bunge na Watanzania kwa ujumla, kwamba Sheria ndogo hizi zina umuhimu wake. Mheshimiwa Profesa Kabudi Waziri wa Katiba na Sheria amesema, wakati anaunga mkono hoja na mchango wa Mheshimiwa Daniel Mtuka kwamba hizi sheria ndogo ama kanuni zinapochelewa kutungwa zina athiri na wakati mwingine zinakwaza utekelezaji wa sheria mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni tumeona Sheria ya Madini kwa namna ambavyo ilikuwa imesimama utekelezwaji wake kwa sababu ya kanuni hazijatungwa kwa sababu ya sheria ndogo hazijatungwa, kwa hivyo ni muhimu sana sana kwamba kanuni ndogo zitungwe ama sheria ndogo zitungwe mapema kadri inavyowezekana na ziwashirishwe Bungeni ili tupunguze ile ya kurekebisha dosari ambazo zinaweza kupatikana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hapo sisi kama Kamati kwa niaba yako tunapokea pongezi zilizotolewa na

Waheshimiwa Wabunge wakiwemo Waheshimiwa Mawaziri kwa Kamati yako na Kamati zingine, lakini pia na sisi tunasisitiza nje ya taarifa hii nje ya yale ambayo tumeyaazimia kama sehemu ya maazimio na ambao tunaomba Bunge lilitidhie Mheshimiwa Jenista Mhagama kama Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye eneo la ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali tunashukrani na pongezi zetu za dhati kwa kazi kubwa mliyoifanya. (*Makofii*)

Sisi tunaofanyia kazi eneo hilo tumeona mapungufu yaliyokuwepo kwenye miaka ya nyuma, lakini baada ya kufanya mabadiliko hasa kwenye Mtendaji Mkuu na timu na kuipanga timu upya katika hicho kitengo ama hiyo Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali tumeona mabadiliko makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunakwenda mbele kidogo, kama Wajumbe wa Kamati kwamba kwa sababu aliyepo sasa anakaimu; na kwa sababu anafanya kazi kubwa sisi kazi yetu ni kutoa maoni na kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitajali sana basi iongeze kasi ya mchakato ama kumthibitisha ama kumteua *CEO* ambaye ataisimamia hiyo idara ili maamuzi yote yafanyike. Kwa sababu tunafahamu kwamba kuna tofauti kubwa ya kuwa kaimu na kuwa mwenye mamlaka kamili. Kwa hivi sisi tunatoa mapendekezo yetu na ushauri wetu kwenu kwamba mlifanyie jambo hilo maamuzi ili kazi iendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wajumbe kwa ujumla, ukifuatailia taarifa zetu utakuta kwamba mambo tunayoyosisitiza yenye kasoro kubwa moja ni yale ambayo yanakiuka misingi ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kasoro ambazo zinahusu ukiukwaji wa sheria mama, sheria ndogo ambazo zinatungwa na sheria nyengine za nchi, lakini pia yapo masuala ya kiuhariri na kiuandishi, pia ukiukwaji wa haki za binadamu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunasema haya yote yanatokana tu na umakini, kukiwepo na umakini yote haya

yatabainika. Ndiyo maana nasisitiza tena kwa mara nyingine kwamba sisi kama Kamati tulipenda sana Kamati hii na tukafikia hatua ya kuomba kwa sababu tumefurahishwa na jinsi ambavyo changamoto zinazokuja mbele yetu na tunavyozifanyia kazi inaonekana ni jambo la heri sisi tuendelee kuwepo pale. Mheshimiwa Mtemi utakapokuwa una toa mwongozao wako wa mwisho pamoja na kwamba wewe ndiyo *Presiding Officer* leo, lakini kwa nafasi yako unayo nafasi pia ya kufikisha ujumbe na kuthibitisha haya ninayoyasema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kwa mara nyingine tena yale ambayo yamejitokeza kwenye taarifa ya Kamati zetu na baadhi ya wachangiaji waliochangia hasa wa maandishi yanayohusu Kamati ya Katiba na Sheria nitayaifikisha mahali pake. Yako mapendekezo ya kwenye marekebisho ya Sheria Ardhi na Sheria ya Ndoa; lakini kwa mazingira tuliyonayo naamini kwamba hayo ni masuala ambayo yanahitaji muda zaidi na kufuata utaratibu unao kubalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naliomba tena kwa mara nyingine Bunge lako Tukufu liliridhie yale tulipendekeza, tulioyatolea maoni na kutoa ushauri na hatimaye tukapendekeza kwamba Bunge liazime kama ambavyo taarifa yetu rasmi tulivyoiwasilisha inavyosomeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na kwa hatua hii naomba kutoa hoja kwa mara nyingine, ahsante. (*Makofi*)

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Hoja imetolewa na imeungwa mkono, ahsante sana Mheshimiwa Ngeleja, Makamu wa Mwenyekiti wa Kamati. Sasa nitaitoa hoja hiyo muiamue, nitawahoji wanaoafiki Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo pamoja na maoni na mapendekezo yake sasa yapitishwe kama maazimio ya Bunge.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)
(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo
Kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2017 ilipitishwa na
Bunge)*

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kwa dakika zisizozidi 15.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kwa mara nyingine.

Pili niwashukuru Wajumbe na Wabunge wote wa Bunge lako la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao wamechangia kwa namna moja ama nyingine kufanikisha taarifa yetu hii ya mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea wachangiaji saba ambao wamezungumza mbele ya Bunge lako Tukufu, na wachangiaji wawili walituletea michango yao kwa maandishi. Kimsingi michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge ni michango ya kawaida ambayo binafsi ninaamini kabisa kwamba wanaunga mkono Taarifa ya Kamati. Nimshukuru sana Profesa Kabudi kwa niaba ya Serikali pamoja na Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Ikupa na wote kimsingi wameunga mkono hoja za Kamati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo baadhi ya mambo ambayo yameibuka nayo ni kuhusu watuhumiwa kutofikisha katika Mhakama ya Mafisadi ambayo imezungumzwa na Mheshimiwa Taska Mbogo lakini pia ukiukwaji wa Ibara ya 13 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kwa askari polisi kukusanya faini kwa kutoza faini

na kuwalazimisha wale wanaowakamata kutokana na makosa mbalimbali ya *traffic* kulipa faini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia makosa mbalimbali ambayo hayajaainishwa kwenye Sheria ya Makosa Barabarani kutozwa faini na polisi wa usalama wa barabarani ambayo inakiuka Ibara ya 107 kama ambavyo Mheshimiwa Amina Mollel ameizungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Daniel Mutuka amempongeza Mheshimiwa Rais kusaini sheria mbalimbali ambazo zimetungwa na Bunge lako hili tukufu pamoja na Mheshimiwa Jaku ambaye yeye alizungumzia kuhusu kesi za mahabusu kukaa muda mrefu Mahakama, vilevile pia kwamba inakuaje kosa linatendeka Zanzibar na mshitakiwa unaletwa Tanzania Bara kushtakiwa. Pia amezungumzia kuhusu Mahakama ya Kadhi pamoja na kuhusu kipengele cha mafuta na gesi ili kuridhia Zanzibar nao kuwa na haki katika jambo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mmasi pia amezungumzia kuhusu Ofisi ya CPD, Mheshimiwa Zacharia amezungumzia kuhusu mabadiliko ya Sheria ya Barabara ambayo imezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nianzie Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mahakama ya Mafisadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Bunge lako hili Tukufu ambalo lilitanya marekebisho ya Sheria Namba Tatu ya mwaka 2016 na kutunga Sheria ya Mafisadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni jukumu la Mahakama kwa kuwa Mahakama ndiye mwamuzi wa mwisho kabisa katika utoaji haki kamati yangu inaendelea kuikumbusha Serikali kwamba wale wote waliothumiwa ni vyema wakafkishwa mbele ya mahakama. Kwa kuwa ni lengo la Serikali na lengo la Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupigania ujisadi pamoja na rushwa

basi ni vema wale wote walishitakiwa kwa makosa mbalimbali ambao hawajafikishwa mahakamani waweze kufikishwa mahakamani ili Mahakama itoe tafsiri na kuamua kesi ambazo ziko mbele yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Susan Lyimo amezungumzia kuhusu mabadiliko ya Sheria ya Ndoa. Labda niseme tu kwamba kwa kuwa kesi hii inayohusiana na masuala haya ipo Mahakamani na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali nakumbuka siku moja, mbili zilizopita amelizungumza jambo hili naomba na mimi kwa kutumia Sheria ya Kinga na Madaraka ya Bunge nisilzungumze kwa sababu nitakuwa nakiuka matakwa ya sheria husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Mheshimiwa Mary Muro Deo naye alituandikia akizungumzia kuhusu uchelewashaji wa kesi mahakamani. Kwa kuwa taarifa yangu imejieleza kwa kina kuhusu sababau za msingi za ucheleweshaji wa kesi mahakamani ninaomba Serikali ijielekeze katika utekelezaji wa maagizo ambayo Kamati yangu imetoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kuhusu suala la changamoto za Muungano kuhusu masuala ya mafuta na gesi, jambo hili kwa kuwa liliwahi kujadiliwa kwenye Kamati yangu, nimkumbushe tu Mheshimiwa Jaku kwamba jambo hili tayari lilihushughulikiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunatambua kwamba hii ni sehemu ya changamoto kubwa zilizoibuka wakati wa mjadala wa Katiba Mpya, lakini tunatambua kwamba Serikali yetu kuititia Wizara ya Muungano tayari ilishatoa maelekezo kwa Wanasheria Wakuu wa Serikali wote kutoka Tanzania Bara na Tanzania Visiwani kukaa na kutunga sheria kuona utaratibu mzuri wa kuweza kutatua jambo hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze sana Bunge lako tukufu kwani mwaka 2015 tayari imetunga Sheria ya Mafuta na Gesi. Sheria hii imekwenda kufuta sheria iliyokuwepo ya Mafuta na Gesi ya mwaka 1984 sheria ambayo ilikuwa haiitambui Zanzibar katika mchango wa kuchunguza lakini

pia kushughulika na masuala ya mafuta na gesi. Kwa hiyo, jambo hili tayari limeshashghulikiwa kwa kutokana na changamoto iliyokuwepo na tayari mchakato huu umeshasha fanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Taarifa, taarifa, taarifa
Mwenyekiti

MWENYEKITI: Nani huyo?

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mimi Mheshimiwa Chenge.
(*Kicheko*)

MBUNGE FULANI: Wewe Chenge?

MWENYEKITI: Haya.

TAARIFA

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Mwenyekiti, sijakataa lakini maandishi kitu muhimu ndio ushahidi, mtu anafungwa kwa maandishi, liondoshwe humu katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano hili suala ili lilete sura nzuri ya Muungano. Vilevile suala linalopitishwa na Baraza la Wawakilishi halikubaliki katika Bunge hili kwa mujibu wa Katiba yetu hii.

MWENYEKITI: Haya ahsante umeeleweka, haya.

MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kuwa jambo ambalo ndugu yangu analizungumza lipo katika Nyongeza ya Kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninatambua kwamba mabadiliko ya katiba ndiyo yatakayoweza kuliondo jambo hilo katika sehemu ya Muungano, lakini kwa hatua iliyopo sasa Serikali tayari imeshalifanya kazi na ndiyo maana Bunge lako hili tukufu lilitunga Sheria ya Mafuta

na Gesi mwaka 2015 na kupidishwa mbele ya Bunge lako tukufu. Pia ninazo taarifa kwamba Zanzibar tayari pia wanayo Sheria ya Mafuta na Gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na mchakato wa watuhumiwa kuhamishwa kutoka maeneo mbalimbali kule Zanzibar na kuletwa hapa Bara, nimuombe ndugu yangu ajielekeze katika Ibara ya nne ya Katiba ambayo inaizungumzia jambo hili. Pia sitaki kwenda mbele sana huko kwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria atayatolea ufanuzi masuala haya iwapo utayaleta mbele yake, niombe tu kuhitimisha hoja yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza kwa kina shughuli zilizotekelawa na Kamati, maoni na mapendekezo ya Kamati naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa liipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kama Maazimio ya Bunge hili. Naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante hoja imetolewa na imeungwa mkono.

Sasa nitaitoa kwenu Waheshimiwa Wabunge muiamue, hoja ya Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria pamoja na maoni na mapendekezo yake sasa yapidishwe kama Maazimio ya Bunge.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)
(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria
Kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2017 ilipitishwa na
Bunge)*

MWENYEKITI: Maazimio yamepitishwa na Bunge.

Tunaendelea sasa ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Jasson Rweikiza.

MHE. JASSON S. RWEIKIZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGЕ YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru tena kwa fursa hii ya kuhitimisha taarifa yangu, lakini pia niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati yangu ya Utawala na Serikali za Mitaa kwa kazi kubwa sana walioifanya tulioifanya pamoja ambayo imetufikisha hatua hii ya sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipayende kutoa shukrani kwa Wabunge wote waliochangia na waliosikiliza taarifa hii tangu asubuhi kwa umakini mkubwa. Wabunge waliochangia taarifa yangu wako jumla 19. Wa kuandika wako Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Zaynabu Vullu, Mheshimiwa Ester Mahawe, Mheshimiwa Albert Obama, Mheshimiwa Lucia Michael Mlowe, Mheshimiwa Omary Mgumba, Mheshimiwa Mary Deo Muro, Mheshimiwa Sebastian Kapufi, Mheshimiwa Ester Matiko, Mheshimiwa Angelina Malembeka, Mheshimiwa Rhoda Kunchela na Mheshimiwa Waitara Mwita na Wabunge saba wamechangia kwa kusema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri na Mheshimiwa Naibu Waziri George Kakunda, Mheshimiwa Waziri Selemani Jafo na Mheshimiwa Waziri George Mkuchika kwa majibu waliyoyatao wakijibu hoja za Wabunge ambao kwa kweli wamejibu kwa ufasaha na kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongezee kwenye mambo kadhaa machache ambayo yametajwa katika michango ya Waheshimiwa Wabunge niliowataja, la kwanza ni MKURABITA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, MKURABITA ni mpango mzuri sana ambao unasaidia wananchi wanyonge kurasimisha biashara zao na mali zao, ardhi, lakini MKURABITA ina hela

kidogo sana, ukiangalia kwenye bajeti inapata mgao kidogo sana. Kwa hiyo, kwa kweli nipende kusisitiza kwamba ni vizuri Serikali ikaangalia kuongeza bajeti kwenye MKURABITA kusudi kazi ya MKURABITA iweze kuonekana kwa manufaa yanayokusudiwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na la pili, kwenye MKURABITA kusisitiza kwamba hati miliki za kimila zikubaliwe na mabenki. Kuna baadhi ya mabenki ambazo zinazikataa hati miliki hizi kwa sababu ile ardhi ambayo juu yake kuna hiyo hati miliki ya kimila haiuziki. Sasa niseme kwamba ni vizuri Serikali ingefanya utaratibu ili ardhi hiyo ikaweza kuuzika kama mkopaji ata-*default*, na ikiwa hivyo benki zitakubali kutoa mikopo kwa hati miliki hizi. Haki miliki hizi ziwe na manufaa kwa wananchi wanyonge waweze kukopa na kujijendeleza kiuchumi lakini pia kuondoa migogoro ya ardhi katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni *TASAF*. *TASAF* nayo imefanya kazi nzuri sana kwa miaka iliyokuwepo; *TASAF* ya kwanza, *TASAF* ya pili, leo ya tatu. *TASAF* ya kwanza na ya pili zilijenga barabara nydingi, zilijenga madaraja kadhaa, zilijenga shule, madarasa na kadhalika. *TASAF* hii ya sasa inaweka mkazo kwenye kaya maskini sana, na kwa msaada wa *TASAF* kaya nydingi zimeweza kupata chakula kizuri, milo miwili kwa siku, milo mitatu kwa siku. Watoto wameweza kwenda kliniki na kwenda shule kwa ufashaa. Kwa hiyo, niiombe Serikali iongeze mchango wake kwenye *TASAF*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu tulionao imetoea shilingi milioni 750 kati ya lengo la bilioni tatu; ni kidogo lakini si haba. Ni robo ya lengo la Serikali kutoa lakini si haba sana. Kwa hiyo, waongeze jitihada ya kutoa fedha kusudi na wale wafadhili waweze kuongeza fedha *TASAF* iweze kuendelea kutuneemesha Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo limeongelewa na Wabunge wengi kwenye michango yao ni asilimia 10 kutoka Halmashauri kwenda kwenye wanawake

na vijana. Jambo hili limekuwa gumu kwa sababu Halmashauri zinafanya kwa hiari, hazilazimiki kutoa asilimia 10, hakuna sheria inayowalazimisha kwamba watoe asilimia 10, tano kwa vijana na tano kwa wanawake. Tunasisitiza kwamba sheria ingetungwa ili Halmashauri hizi zilazimike kutoa michango hii kwenda kwa wanawake na vijana. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni *TARURA*. *TARURA* ni mamlaka au wakala changa sana ina miezi michache imeanzishwa lakini imefanya kazi nzuri sana. Kazi nzuri imeonekana, barabara nydingi za vijiji na mijini zimeanza kujengwa. Hata hivyo inapewa mgao kidogo sana kutoka *Road Fund Board*, asilimia 30. Kwa kweli hiki ni kiasi kidogo mno. Ina Halmashauri 185 barabara zote za Halmashauri za vijiji na za mijini. Kwa hiyo, ni kwakweli ni jambo jema kama walivyosema wabunge kiasi hiki klongezwe ili kusudi *TARURA* iweze kufanya kazi ambayo inaonesha ufanisi mkubwa. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi hewa walipunguzwa kutokana na vyeti hewa na vyeti Ifake wameathiri sana utendaji kazi Serikalini hasa kwenye afya na madereva. Kama walivyosema Wabunge madereva walikuwa na uzoefu mkubwa, lakini wana vyeti *fake*, basi nitoe wito kwamba wengine waajiriwe, waajiriwe wa kutosha kusudi upungufu huu uliojitekeza hata kwenye afya uweze kuondolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya afya amesema Mheshimiwa Kahigi na Waheshimiwa wengine, kuna Wilaya hazina Hospitali za Wilaya. Halmashauri 64 hazina hospitali za wilaya. Hizi halmashauri 64 Mkoa wa Katavi wote hauna hospitali hata moja ya Wilaya. Mkoa wa Kagera wote, Kagera ina Wilaya name hauna hata wilaya moja yenye hospitali ya Wilaya. Kwa kweli ni vizuri sana kama alivyosema Mheshimiwa Jafo tulimsikia, ametoa ahadi kwamba fedha zitatengwa na itajengwa Hospitali ya Wilaya kule Bukoba moja au mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya elimu imezungumziwa sana na Waheshimiwa Wabunge mbalimbali, lakini mimi niongelee jambo moja kwenye sekta ya elimu. Ukosefu wa vyoo kwenye shule za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna shule nyingi hazina vyoo, hili ni jambo la fedheha kubwa sana. Jana liliongelewa jambo la taulo za wanafunzi wa kike, mimi nasema la vyoo ni kubwa zaidi, kwa sababu la linahusu wasichana na wavulana, wanakwenda wapi? Serikali iweke bidii na jitihada kubwa sana kujenga vyoo. Ni bora nyumba za walimu zikasubiri, shule mpya zisijengwe ili zilizopo zipate vyoo watoto wapate mahali pa kujisitiri, vijengwe vyoo vya kutosha. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na nchi hii imeendelea na kupiga hatua. Barabara nyingi zimejengwa lami, tunajenga barabara za juu pale TAZARA na Ubungo, tunajenga reli ya umeme (*standard gauge*) lakini hatuna vyoo mashulenii, ni jambo la aibu, fedheha na adha kubwa kwa wanafunzi. Hili lingetiliwa mkazo kusudi liweze kutatuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Serikali ikitia nguvu akisema Raís kwamba liishe linaisha. Rais amesema madawati likaisha, tatizo la madawati limekwisha. Kwa hiyo, nafikiri hata Mawaziri wanaohusika na sekta hii ya elimu wakazanie suala la vyoo mashulenii na liondolewe matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maji vijijini ni tatizo kubwa sana. Leo asubuhi nimesikia miongozo humu ndani kuhusu maji vijijini. Waheshimiwa Wabunge wamesimama wote wanalamika kuhusu maji vijijini. Juzi alisema Naibu Waziri wa TAMISEMI kwamba kuna fedha shilingi bilioni 156 kwenye akaunti ya maji vijijini, lakini kitu kinachopungua ni wakala; wakala hauzaanza kusudi huduma hii iweze kutolewa kwa vijiji. Nisilitize kwamba ni vizuri kama wakala huu angeanza mara moja kusudi ishughulikie adha ya maji vijijini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kwa ufupi niombe tena Bunge lako Tukufu liazimie kama taarifa yetu ilivyosema na ninaomba kutoa hoja. (*Makofî*)

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante, hoja imetolewa na imeungwa mkono tunawashukuruni sana.

Sasa nitaitoa muiamueTaarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa pamoja na Maoni na Mapendekezo yake sasa yapitishwe kama Maazimio ya Bunge.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)
(Hoja Iliamuliwa na Kukubaliwa)*

(Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa Kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2017 Ilipitishwa na Bunge)

MWENYEKITI: Taarifa hiyo pamoja na mapendekezo yake yamepitishwa rasmi kama Maazimio ya Bunge hili na hapo ndio tunafika mwisho kwa shughuli zetu za leo, kwa maana ya kuhitimisha hoja hizi tatu tulizozianza asubuhi. Niwashukuru sana Wenyeviti waliowasilisha hoja hizi, ninyi Waheshimiwa Wabunge mliopata nafasi ya kuchangia kwa kusema na kwa maandishi mmechangia vizuri sana, tumemaliza vizuri. Ni Maazimio ya Bunge, kwa taratibu za Ofisi ya Katibu wa Bunge tutayafikisha rasmi Serikalini yakafanyiwe kazi kwa haraka iwezekanavyo yote katika ujumla wake. Lakini mimi niseme tu kwa sababu ya Uenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo, nirudie aliyosema Mheshimiwa Makamu wa Mwenyekiti, hizi ni sheria za nchi ndio maana tunaiomba sana Serikali iwe na uharaka wa kuyafanya marekebisho katika sheria hizo na kuleta Bungeni marekebisho ili zisiendelee kuumiza watumiaji waliolengwa na sheria hizo kwa sababu ya makosa au dosari zilizoonekana. Hilo ndilo la msingi sana.

Nina tangazo hapa la wageni wa Mheshimiwa Suleiman Nchambi ambao ni Ndugu Godfrey Mwita, Ndugu Baraka Shemahonge, Ndugu Michael Mahenge, Ndugu Rahman K. M. A, Ndugu Radhakrishna Barahman, eeh hatari Ndugu Mohamed Ali, Ndugu Abdallah Ali, wako wapi? Aah mko hapo karibuni sana. Hili jina la tano Ndugu Radhakrishna Barahman. (*Makofii/Kicheko*)

Samahani sana kama nimelikosea kulitamka lakini ndio hivyo nimejitätidi kidogo. (*Makofii*)

Sasa asubuhi katika kipindi cha maswali niliombwa Mwongozo lakini kwa upande wa mwongozo wa Mheshimiwa Bashe Serikali ilikuwa imetoa njia ya kutokea na mimi nikasema nadhani twende huko huko.

Hata hivyo nikasema itapendeza kama jioni Serikali itatoa taarifa tu kwa Bunge na Taifa ili wasikie kwa yale ambayo Serikali na Mheshimiwa Mbunge wa Nzega Mjini wamekubaliana kuhusiana na hali ya maji pale.

Kwa hiyo, nimpe muda Mheshimiwa Waziri wa Nchi kama mlivyojipanga mseme kidogo, ahsante na karibu.

MAJIBU YA MWONGOZO

**Mwongozo wa Mheshimiwa Hussein M. Bashe Kuhusu
Ukosefu wa Maji katika Mji wa Nzega kutokana na
TANESCO Kuikatia Umeme Mamlaka ya Maji ya
Mji wa Nzega**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE,
KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Serikali na kwa niaba ya Mawaziri ambao tulitoa ahadi mbele ya Bunge lako tukufu kwamba tungekutana naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba tulitekeleza agizo la Kiti na ahadi ya Serikali na tumefanya kikao na Mheshimiwa Bashe kushughulikia suala ambalo lilikuwa limejitokeza mbele ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mlivyokuwa mmetuagiza, kwamba jicho letu lisiangalie eneo hilo moja tu, jicho letu liangalie maeneo mengine yote. Ninafurahi kuliambia Bunge lako tukufu tumefanya hivyo na utekelezaji wa maagizo ya Serikali katika kuhakikisha kwamba tunatatua tatizo ambalo lilikuwa mbele yetu linalowakabili wananchi katika maeneo mbalimbali limeanza kutatuliwa na maeneo mengi wametupigia simu kwamba sasa wameanza kupata maji na tatizo limekwisha. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tumbakiza mawasiliano kidogo ya maandishi ya barua kwa sababu hatukuwa tumeelewana katika eneo moja ama lingine katika Halmashauri ya Mji wa Nzega. Hata hivyo jambo hilo limesharekebishwa na tunaamini kwamba mji ule wa Nzega sasa tatizo litakuwa limetatuliwa na hivyo tunaomba Wabunge waendelee kuwa na amani, Serikali imefanya kazi yake na tutaendelea kutekeleza wajibu wetu.

Tunaomba Waheshimiwa Wabunge waendelee kuipa ushirikiano Serikali hii ya Rais Dkt. John Pombe Magufuli Serikali sikivu, Serikali ambayo imekuwa ikitekeleza shughuli zake na kuhakikisha kwamba wananchi wa Tanzania wanaondolewa kero zao kwa wakati unaotakiwa. Ahsante. (*Makof*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu kwa maelezo yako. Hivi ndivyo inavyotakiwa kwa upande wa Serikali, maana ukiona hali kilio cha Waheshimiwa Wabunge iwe ni kwenye maji, kwenye afya, kwenye nini mnaingia haraka mnasaidia kujibu ile kiu ambayo Wabunge wanayo. Niwashukuruni sana kwa hilo na naendelea kusema kwa sababu tunaona hali ya maji changamoto ni kubwa. Mimi sitaki kuwachochaea au kuwahamasisha Waheshimiwa Wabunge, mnajua tuko kwenye mchakato wa kuelekea kwenye Bunge la Bajeti. Tuone tutapima yale ambayo tulipatia Serikali nafasi ya kuyafanya na ahadi zake katika sekta ya maji *thenmtashauri* baada ya hapo ni nini kifanyike kama tunadhani baada ya ahadi hizo hatukufikia kile tulichotarajia wote.

Lakini kwa taarifa mliyoona ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha ule uamuzi wenu wa Shilingi 50 kwa lita ya Mafuta ndio umetusaidia sana kwenda vizuri kwenye sekta hiyo muhimu. Kwa hiyo, tuendelee kuona njia nzuri zaidi ya kuboresha sekta ya maji nchini, ni changamoto kubwa sana. (*Makofi*)

Sasa sina tangazo lingine baada ya kusema hayo, sasa naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho siku ya Ijumaa, saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.35 Usiku Bunge liliahirishwa hadi siku ya Ijumaa,
Tarehe 9 Februari, 2018 Saa Tatuu Asubuhi)*